ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
33.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
34. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
35.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
36. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete

37.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
43.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
44.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
45.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
46.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
47.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
48.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
49.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
50.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
51.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
52.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
53.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
54.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
55.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
56.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
57.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile

59.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

60.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

61.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

65.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

66.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

69.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

70.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

71.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

76.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 01Julai, 2013

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Naibu Spika,(Mhe. Ali Abdalla Ali) Alisoma Dua

TAARIFA YA MHE. NAIBU SPIKA

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaanza kazi yetu pana tangazo moja hapa. Tangazo hili linahusu mechi tuliyocheza jana baina ya Baraza letu la Wawakilishi na wenzetu wa SUZA. Baraza la Wawakilishi lilishinda magoli matano na SUZA magoli mawili, wafungaji wa magoli hayo ni Mhe. Ussi Jecha Simai (Messi) wa Baraza la Wawakilishi, kafunga magoli mawili na mtendaji wetu Khamis Hamad kafunga magoli mawili na goli la mwisho lilifungwa na mtendaji wetu Hassan Shairi.

Kwa ushindi huo sasa timu yetu imeingia nusu fainali na siku ya kucheza tunaomba twende sote tukashangirie. Baada ya tangazo hilo, naomba katibu tendelee.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2013/2014. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Ussi Jecha Simai (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria): Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha hati mezani ya muhtasari wa Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC): Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudhibiti na Kuchunguza Hesabu za Serikali na Mashirika, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC), kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaendelea katika orodha yetu ya wachangiaji, jumla ya wachangiaji walioomba ni 34 na mpaka hivi sasa kumebaki wachangiaji 19 na wa 20 ni Mwanasheria Mkuu. Kwa hivyo, tunawaomba wale wote watakaopata muda wa kuchangia tutautumia muda wa mchana tu kuanzia asubuhi hadi mchana, jioni tutamuita Mhe. Waziri kwa majumuisho na kupitisha vifungu.

Kwa hivyo, ningeshauri katika kuchangia tusirejee, wengine hutumia mbinu wakasema aah! Najazia nyama tu pale pa mwenzangu, au mimi nakazia tu. Sasa hiyo kukazia na kujazia nyama kidogo muifanye *aste aste* ili tuweze kuchangia sote 19 na jioni tumpe nafasi Mhe. Waziri ya kutosha, ili kusikiliza majibu ya hoja zenu. Kwa hivyo, baada ya maelezo hayo naomba sasa nimpe nafasi ya mwanzo kwa dakika 20, anayeweza dakika 10 itakuwa nzuri zaidi, au dakika 15 itakuwa vizuri zaidi, lakini dakika 20 ndio mwisho wetu.

Kwa hivyo, tunamkaribisha Mhe. Saleh Nassor Juma na baadae Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa hai na kutupa uwezo wa kuja hapa Barazani tukiwa wazima wa afya.

Aidha Mhe. Naibu Spika, mimi binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo langu la Wawi, kwa heshima kubwa tunamuomba Mwenyezi Mungu aijaalie afya ya Mzee Madiba (Mzee Nelson Mandela) irudi na iimarike.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, naomba moja kwa moja niende katika hoja iliopo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, kama tutaangalia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika ukurasa wa 46 ibara 135 inaiita Tanzania kuwa ni nchi ya vyama vingi vya siasa. Na vyama hivi kwa mujibu wa sheria hii ni vya kitaifa, vinatakiwa vianze kazi Mtambwe mpaka Kigoma, vifanye shughuli kuanzia

Kukuu mpaka Ujiji Kigoma, bila ya matatizo ilimradi wanafuata sheria za nchi.

Kwa mnasaba huo Mhe. Naibu Spika, ikiwa chama chochote cha siasa kitatimiza masharti yake na usalama wa nchi, basi kina haki ya kuendesha shughuli zake popote katika nchi hii bila ya kuingiliwa Mhe. Naibu Spika. Kwa masikitiko makubwa, sisi vile vile tumo katika Baraza hili kwa kupitia vyama vya siasa, watu 10 tu wametajwa na Rais pamoja na Mwanasheria Mkuu ni watu 11. Lakini sote tunapitia kwenye vyama vya siasa kwa mujibu wa sheria namba 5 ya mwaka 1992.

Mhe. Naibu Spika, nalazimika kuleta utangulizi huu kwa sababu kama tutafanya mchezo na kupinda hii sheria namba 5 ya mwaka 1992, basi itatugharimu sana. Kwa sababu kujenga kuleta amani ni kazi kubwa sana, lakini kuvunja ni mara moja.

Mimi nachukua fursa hii Mhe. Naibu Spika, kabla sijaenda kwenye mchango wangu, nimpongeze Mhe. Rais Mstaafu Mhe. Aman Abeid Karume pamoja na Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi CUF Maalim Seif Sharif Hamad, ambaye kwa sasa ni Makamu wa Kwanza wa Rais, kwa kuweza kuleta amani na utulivu katika nchi hii kwa kupitia muafaka.

Aidha, naweza kufanya makosa makubwa sana kama sikutumia fursa hii kuwapongeza wale walioshiriki katika muafaka huu na wamo humu, akina Mhe. Ali Mzee Ali, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Mansoor Yussuf Himid na kadhalika. Kwa kweli wamejitahidi sana na katika hili nachukua fursa hii kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Wawi tunawapongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani hii habari Mwenyezi Mungu aliyotupa tusiilevye levye. Mhe. Naibu Spika, unapomzuia mtu asifanye shughuli za siasa ni kukiuka katiba, sheria namba 5 ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1992. Mimi niliambiwa kuna watu hawataki muafaka nilikuwa siamini. Lakini kuanzia juzi niliamini pale ambapo Katibu mkuu mmoja wa chama cha siasa ambaye kwa sasa ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa visiwa hivi, pale alipokataliwa kufanya mkutano katika uwanja wa Kitope. Mimi nilishtuka sana.

Mhe. Naibu Spika, ikiwa serikali yetu hatukuwa makini, hususan kwa hii hoja ambayo Waziri wetu leo ndio tunaijadili hoja yake, yeye ndiye anayeshughulika na mambo ya mikoa, ikiwa hayuko makini na wakuu wake wa mikoa, basi anaweza kuhatarisha amani wakati wowote katika nchi hii. Inasikitisha sana, kuambiwa Mkuu wa Mkoa anamzuia Katibu Mkuu wa chama cha siasa ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais asifanye

mkutano eti viwanja wenyewe hawataki, alaa! Basi hapa panafanyika mikutano ya vyama vya siasa, kwa sababu kiwanja cha Gombani sisi tuna haki miliki, nyinyi mna haki miliki katika kiwanja cha Gombani kongwe, mna haki miliki katika kiwanja cha Kibirinzi. Haya basi kama si chama changu, nikisema kisifanye mkutano kitafanya pale? Mimi nadhani tuwe makini sana

Mhe. Naibu Spika, nimeamua kusema hivi kwa sababu wakuu wako wa mikoa Mhe. Waziri wana matatizo, wanaweza wakatuhatarishia amani wakati wowote. Sasa nikisema Mwenyekiti na Mwenyekiti wa CCM taifa asimamie mkutano wa Gombani kongwe mpaka niuliwe. Nikisema Katibu Mkuu wa CCM asifanye mkutano Gombani kongwe mpaka niuliwe, amani itapatikana hapo kweli, ni tatizo na ni uadui.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa siamini kama kuna watu ambao hawaitakii mema nchi hii, lakini kuanzia jana nimeamini. Naiomba sana serikali itusaidie, naamini Mhe. Naibu Spika, wanaofanya hivi watakuwa hawajui maana ya utulivu na amani katika nchi, basi namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa sababu ni mwana taaluma na aliyebobea kabisa awaelimishe au watakuwa ni wajinga. Mimi sina vya kuwafanya, lakini serikali isiwaachilie tu wakafanya ujinga, au watakuwa maadui wa nchi hii hapo sasa. Kama ni maadui basi hapo sasa!

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani tusirudi tulipotoka, tusikubali kurudi tulipotoka Mhe. Naibu Spika, tunatoka mbali. Mimi sitoathirika, lakini nyinyi mnaopita na magari huku mkipewa ulinzi. Mimi siathiriki kwa sababu nitakuwa narudi tu kule kule nimeshakuzoea, nikifungua mgongoni huku mimi nina alama ya kupigwa. Lakini kuna watu hapa wana ulinzi na kadhalika, watapata matatizo sana. Mimi jela nimeshakaa, nitakuwa nakwenda jela kwa mara nyengine tu, mtakaoathirika zaidi ni nyinyi. Kwa hivyo, tulindeni amani hii na utulivu uliopo tusirudi tulikotoka, kwa sababu kujenga utulivu na amani ni kazi kubwa zaidi, tukiichafua leo basi tunaweza kufika hata miaka 50 hatujafika hapa tulipokaa.

Baada ya maelezo haya Mhe. Naibu Spika, sasa naomba niende kwenye hoja. Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Usajili wa Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Katika ukurasa wa 32 ibara ya 86. Mhe. Naibu Spika, mimi juzi niliwaombea posho nyeti wapewe hawa, kwa sababu ya mionzi niliwaombea posho nyeti wapewe hawa watu wa vitambulisho kutokana na kazi zao wanazozifanya.

Lakini Mhe. Naibu Spika, katika watu wanaokuvunja moyo na watu ambao hivi sasa hawana imani na Wazanzibari wenzao ni hawa hapa watu wa vitambulisho. Mhe. Naibu Spika, ukiacha blaa blaa ambazo tunapewa humu.

Wakati mwengine Waziri anakuambia hivi, kumbe ni kinyume. Vitambulisho Wazanzibari hawapewi.

Mhe. Naibu Spika, hivi ninavyokuambia kwa mujibu wa taarifa zilivyokuwa nyingi, ni zaidi ya watu 800 wameshakamilisha masharti huko, lakini vitambulisho hawapewi. Kwa mujibu wa sheria za vitambulisho mtu ikiwa hana kitambulisho, basi ashtakiwe. Sasa mimi namtaka huyu mkuu wa vitambulisho atayarishe jela na atuoneshe ni ofisi gani aliyoifungua na hiyo jela ya kuwaweka iko wapi? Kwa sababu umati uliopo ambao haujapewa vitambulisho hawana jela ya kuwaweka, sasa Mheshimiwa tusibabaishane bwana.

Mhe. Naibu Spika, tatizo la vitambulisho sisi tunajua ni tatizo la kisiasa, ni mtaji wa kisiasa wa chama cha siasa. ? Na katika hili mimi nawashauri CCM, rafiki yangu Mangula aje awaambie watendaji wake huku Zanzibar, naishauri Serikali ya Zanzibar kwamba kama tatizo walikuwa hawapewi vitambulisho kwa sababu ya siasa, basi wasilete uchaguzi tu, walete sheria ya ku *-declare mornachy* katika nchi *Wallah* tutaipitisha sisi.

Mimi nakuhakikishia Mhe. Naibu Spika, tuko hapa Wazanzibari walio wengi vitambulisho ni kwa kuwabagua, ubaguzi huu tutakwenda nao mpaka lini? Eti kwa sababu ya kukifurahisha chama cha siasa tu, hili ni tatizo Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo, tusizibague damu zetu, nchi ngapi zina usulutani zinaishi na zina uchumi mzuri. Saudi Arabia wana ufalme, Oman wana ufalme, basi na Zanzibar mkitaka muwe wafalme basi tuwekeeni sheria tubadilishe sheria hapa, lakini tusiwanyanyase kabisa. Kuwanyima Wazanzibari walio wengi vitambulisho ni kuwabagua na huu ni ubaguzi uliobobea sana.

Kwa hivyo, aidha mulete ufalme kuwe hakuna uchaguzi, lakini kama ni vitambulisho muvitoe na ikiwa hamkuvitoa vitambulisho mpaka tarehe 01 mwaka 2015, basi mimi nawashauri sana katika kuleta amani kwenye nchi msilete ubaguzi, mkileta uchaguzi mwaka 2015 bila ya Wazanzibari walio wengi kupata vitambulisho, basi mtakuwa mmehatarisha amani na nyinyi mtakuwa mas-ul, kwa sababu hatutokubali hili.

Jengine Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 60 mpaka 64 amezungumzia Baraza la Mji wa Chake Chake. Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa jadweli hili ni kwamba Baraza la Mji wa Chake Chake linakusanya karibu milioni 83. Haya sio makusanyo makubwa, lakini vile vile sio madogo. Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana kwamba Baraza la Mji wa Chake Chake wao wanageuka kama vile jeta, wao wapelekewe tu lakini kutoa inakuwa tatizo. Katika mambo haya ya kukusanya kodi, maana yake lipa nikupe, pokea mafao na wewe peleka maombi leo kwa watu.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa wakati nazungumza Baraza la Mji wa Chake Chake kuna tatizo la kwamba kodi wanakusanyiwa wananchi. Kwa mfano madereva, kila dereva anapoegesha gari kwenye sehemu za maegesho analipa shilingi 500, kila siku ya Mungu yeye gari yake akiweka mule Chake Chake analipa shilingi 500, ya abiria nafikiri imezidi. Lakini hizi zisizokuwa za abiria ni lazima kwenye maegesho ulipe shilingi 500. La kusikitisha Mhe. Naibu Spika, hiyo sehemu yenyewe ya maegesho hapana. Sehemu iliopo ya maegesho ni pembezoni mwa barabara, abiria huku wanateremka na huku magari mengine yanapita, wanaweza kufanya ajali wakati wowote. Mhe. Naibu Spika, sasa ile thamani ya kodi ya wananchi haipatikani.

Mhe. Naibu Spika, katika Mji wangu wa Chake Chake, nawashauri jambo moja. Wasipokusanya kodi za sehemu ya maegesho ya magari hadi pale watakapowapatia wananchi sehemu ya kujenga hiyo sehemu ya maegesho, kwa sababu ni tatizo. Wako wanaolipa maegesho, lakini hiyo sehemu ya kuegeshea gari hapana. Wewe ukisimama barabarani, unachukuliwa pale pale uende ukalipe. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anieleze ni lini katika Mji wa Chake Chake utakuwa na maegesho rasmi ya gari.

Mhe. Naibu Spika, Mji wa Chake Chake wafanyabiashara wote hapa sokoni tumewaondosha pale juu kwenye soko la zamani, tumewateremsha Qatar. Kule Qatar wameteremshwa wakati hakuna miundombinu, wafanyabiashara ni wengi, wauza tungule, vitunguu, samaki, ilimradi wote wananunua pale

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, bado dakika tano.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika la kusikitisha hata maji pale hapana. Kwa hivyo, uwezekano wa kupata magonjwa ya miripuko ni mkubwa. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa, anieleze ni lini pale Qatar patatayarishwa miundombinu, ili kuhakikisha kwamba miundombinu iliopo inalingana na idadi ya wafanyabiashara waliopo. Je, ni lini pale Qatar patajengwa na sio kuzibwa zibwa yale magunia tu, pajengwe soko ili lilingane na hadhi ya Mji wa Chake Chake na wala sio jaa kama lile liliopo sasa hivi.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende katika vikosi. Napenda kuchukua fursa hii kwanza kuvipongeza vikosi vyetu hivi, kwa kweli vinafanya kazi nzuri pamoja na mapungufu madogo. La kusikitisha Mhe. Naibu Spika, ni kwamba hawa wapiganaji wetu wana matatizo kidogo.

Kwa mfano, hawa ndugu zetu wa kikosi cha Zimamoto pale Bandarini. Sehemu waliopewa ni finyu sana, kiasi ambacho hawana ofisi ni sehemu ndogo tu, hiyo hiyo ndio ofisi, ndio kighala ilimuradi ni tatizo sana. Kama

kuna sehemu ambayo hiki kikosi chetu cha Zimamoto na Uokozi ni sehemu ya bandarini, kwa sababu bandarini wataalamu wanaita ni *extra high hasard place*. Kwa hivyo, panahitaji matayarisho makubwa, kwa kijisehemu walichokipata pale hawawezi ku-*set* hata mitambo yao ya kompyuta, sio ile Zimamoto ya zamani, lakini wanatakiwa *well and scientific equiped*, kile kijiofisi hakiwatoshi. Kwa hivyo, naiomba serikali ihakikishe kwamba pale wanawasaidia angalau sehemu ya kutosha waweze kufanya kazi zao vizuri hawa vijana wetu.

Aidha, tunaliomba Shirika la Bandari litoe mashirikiano na hawa vijana ili wapate sehemu nzuri zaidi waweze kujitanua kuweka *network* zao vizuri. Huu ni ulimwengu wa sayansi na teknolojia, kijipande kile walichonacho hawawezi hata ku-*set* mitambo ya kisasa katika ku-*monitor* ajali, hilo ni jengine.

Mhe. Naibu Spika, Zimamoto waliopo hapa uwanja wa ndege kile kijisehemu walichopewa sio pazuri, kwa sababu ili waweze kufanya kazi zao vizuri hawa lazima ni pale ambapo *possibility* ya *accident* inaweza kutokea, Mwenyezi Mungu atunusuru. Wewe unaweka sehemu ambayo ndege inamalizikia kutua, lakini *possibility* ya *accident* ni katika ku-*take flight na landing* wawekwe sehemu hiyo kwenye lile eneo ambalo wataweza ku-*monitor* ule mwenendo wa ndege zetu.

Mhe. Naibu Spika, nije katika KMKM. Mhe. Naibu Spika, KMKM wanafanya kazi za ziada, na kwa kweli ni kikosi cha kukiimarisha sana, kwa sababu sio kwa mujibu wa kazi zao tu, lakini hata kwa sisi wananchi wa kawaida. Kile kikosi ndio kinachoshughulika na mambo ya kutuokoa bandarini, kutusaidia katika maafa. Lakini vifaa vya uokozi hawana vya kutosha.

Mhe. Naibu Spika, kuna chombo wanakiita kitaalamu kimeshanishinda, lakini kuna chombo ambacho mtu akipata ajali baharini inabidi aingizwe kwenye chombo hicho ili aweze kupata matibabu, lakini hicho chombo kimekufa na hakipo.

Jengine Mhe. Naibu Spika, jengine vile vifaa vya kuzamia havitoshi

Mhe. Naibu Spika: La kumalizia hilo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Nimalizie tu kwa kuomba kwamba wapatiwe *lifting bags*, hizi ni begi ambazo kama meli inapata ajali yanatiwa upepo halafu meli inazuka, hawa hawana, tukisaidieni kikosi chetu.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa Vyuo vya Mafunzo, niwapongeze kwa kuanza kuondoa mitondoo. Hawa jamaa wamejitahidi sana sasa, kwa sababu wanajenga vyoo vya ndani. Nawaomba hili zoezi la kujenga vyoo vya ndani liendelee na lisimalizikie hapa Unguja tu na wapeleke mpaka Pemba, ili hii mitondoo vijana wetu waendelee kuepukana nayo. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, suala la kwenda haja ni la faragha na kutumia mitondoo sio faragha na haki ya faragha ni haki ya kikatiba ya mwananchi. Kwa hivyo, wajitahidi kuondosha mitondoo ndugu zetu hawa. Nawapongeza kwa kuanza kupunguza mitondoo katika magereza haya.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, wana ardhi ya kutosha ya kufanya kilimo na wanajitahidi sana kufanya kilimo ndugu zetu hawa wa Chuo cha Mafunzo. Lakini tunaomba miradi ile ya umwagiliaji ya serikali waonekane hawa, serikali haiwaoni miradi wanapeleka sehemu nyengine tu. Hebu wapelekeeni Chuo cha Mafunzo muone mambo.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, nitakapopata maelekezo ya kutosha kuhusu vitambulisho, upatikanaji wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, nitakapopata maelezo ya kutosha jinsi hawa Wakuu wa Mikoa wanavyoingilia demokrasia ya nchi hii na kudhibiti watu kufanya mikutano yao, nikiridhika basi nitapitisha hoja hii, ahsante *(Makofi).*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, ama baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Allah Subhanahu Wataalla aliyeniwezesha hapa kusimama na kuvuta pumzi zake alizoniazima ambapo wakati wowote anaweza akazichukua. Pia nitakuwa sio mwingi wa fadhila kama sikukushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa jinsi unavyoendesha vikao hivi kwa heshima na taadhima.

Mhe. Naibu Spika, nianze kuvishukuru vikosi vya SMZ pamoja na vikosi vya Muungano kwa kazi wanazozifanya, pamoja na changamoto zinazowakabili ikiwemo kilio cha maslahi kutokana na ukali wa maisha. Jambo la msingi wakumbuke mwanzo wa safari ni hatua moja, panapo majaaliwa maliasili ya gesi na mafuta pindipo ikipatikana wakati wowote mtatononeka na kupata maslahi mazuri kwa nchi hii. Namuomba Mhe. Waziri mwenye dhamana hiyo, kikao kinachokuja mchakato huo watuletee haraka.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwenye kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri kumpongeza kwa kuwasilisha vizuri kwenye ukurasa wa 5 wa kitabu chake. Mhe. Waziri amemtaja Jemedari Hayati Mzee Karume kuwa alikuwa ni Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ni sahihi kabisa.

Mhe. Naibu Spika, historia ya nchi yetu tusiogope kuiweka kwa usahihi. Mzee Karume Mola amlaze mahala pema peponi amina, alikuwa Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Tusione aibu kuisema na kujisifia.

Baada ya utangulizi huo mfupi Mhe. Naibu Spika, nije katika fungu nambari 17 Jeshi la Kujenga Uchumi JKU, kifungu nambari 145,000 mapato mengineyo. Mhe. Naibu Spika, mapato haya hayajaelezwa ni ya aina gani mimi sielewi hii, mengineyo ndio chanzo cha aina gani cha mapato. Lakini labda mimi fikra zangu na akili zangu niagulie labda lile baa la JKU ndio lililochangia mapato haya.

Mhe. Naibu Spika, kuna biashara ya baa pale Makao Makuu ya JKU, bila shaka pengine hayo ndio mapato mengineyo na kama ndio miongoni mwa mapato hayo, basi Mhe. Waziri atakuja kuthibitisha hapa baa ile Mhe. Naibu Spika, kama ni sehemu ya mapato basi ni tatizo, imekuwa mtihani.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wa Saateni walikuwa wakilipigia kelele kwa muda mrefu kuhusu baa ile na hakuna walichokipata mpaka muda huu, limekuwa likiwaudhi wananchi na kutokana na ufinyu wa eneo lile Mhe. Naibu Spika, wananchi walikuwa wanalalamika na tulikuja kusema hapa kwa sababu hiki ndio chombo chao, na askari wetu pale wanatakiwa wawe imara masaa 24, leo kuwawekea baa mule ndani ni mtihani. Mhe. Waziri utakapokuja hapa nataka unieleze baa ile ni lini utaiondoa na wananchi wa Saateni wananisikia hivi sasa au vyenginevyo nitazuia fungu.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Naibu Spika, katika kilio cha masheha. Kwa kweli masheha imekuwa ni kikwazo kikubwa kwa wananchi kupata haki zao Kikatiba katika maeneo ya fuatayo:-

(a) Haki ya kupiga kura;
(b) Haki ya ukaazi;
(c) Haki ya kupata huduma za kijamii;
(d) Haki za kufanya kazi kihalali na
(e) Haki ya hifadhi za heshima na utu.

Mhe. Naibu Spika, wakati masheha wetu wakati wanapochaguliwa wengi wao elimu zao ni ndogo tena kwa ushahidi na tumekuwa tukiyazungumza kila leo. Kwa mfano, hapa nataka ku-*declare my interest*, kwa sababu nilikuwa nikipiga kelele sana na Sheha wangu wa Shehia ya Mchangani wa Mji Mkongwe anafanya kazi kwa ubaguzi na ukitizama Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi pamoja na Katiba ya Zanzibar zote zinakataza, sasa sijui tumemkosa nini sisi? Mengine hayawezi kusemeka Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri sheha huyu imekuwa ni kizingiti na serikali iliwahi kumsimamisha kazi kutokana na utendaji wake mbovu na baada ya muda ikamrejesha tena na hivi sasa watu wanapata shida nikiwemo mimi mmoja. Kwa mfano, wanakuja watu wa chanjo pale hanipi hata taarifa, imekuwa yeye amepewa nguvu gani ya kujiimarisha pale, kwa sababu tukifuga maradhi yatakuja kutuua.

Mhe. Naibu Spika, Sheha wa Shehia ya Mchangani nitahitaji maelezo ya kina, mpaka mtu mzima akilia basi ujue kuna jambo, kwa sababu miongoni mwa watu wavumilivu mimi Mhe. Naibu Spika mvumilivu sana, na kwa bahati nzuri tu Mwenyezi Mungu ameniumba mwanamme na ningekuwa mwanamke ningekuwa nimeshakufa kwa UKIMWI Mhe. Naibu Spika, kwa sababu sijui kukataa na huo ndio ukweli ulivyo.

Nikiendelea Mhe. Naibu Spika, sasa nije kwenye ukurasa wa 62 kuhusu maendeleo ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mwaka 2012/2013. Miradi minane ilikuwa itekelezwe na zilipangwa shilingi bilioni 1.9 na miradi hiyo utekelezaji wake unaonekana kusuasua na kufika mwaka wa fedha miradi iliingiziwa shilingi milioni 672.9 sawa na asilimia 35 kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, miradi hii yote ina umuhimu wake kulingana na uwezo wake badala ya kupanga miradi mingine na kupokea umuhimu mkubwa sana.

Sasa niende kwenye ukurasa wa 65 na mradi huu umeombewa shilingi milioni 256, lakini ukapatiwa shilingi milioni 5.8 kitengo ambacho ni muhimu kwa magereza na hii ni sawa na kununua nyuzi na mikasi tu, *we are not serious* hapa Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, pia hapa naomba kupatiwa maelezo.

Jambo jengine kwenye ukurasa wa 66 na tulilipigia kelele sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili, kwa sababu kuna haki za binadamu zinawagusa, kuna magereza ya watoto na watu wazima kutengenishwa na mradi huu umetengewa shilingi milioni 400, lakini umeingiziwa shilingi milioni 145 kweli tutafika. Mhe. Naibu, naomba nipatiwe maelezo.

Vile vile kuhusu vikosi vyetu vya ulinzi kutumika katika shughuli za ulinzi kwenye taasisi za watu binafsi. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho atusaidie maelezo kuhusu mradi huu umeingiza kiasi gani cha fedha pamoja na kazi za ujenzi zinazofanywa na askari wetu, sababu hawa wanalipwa mishahara kutoka Hazina wakati wanafanya kazi nyengine huku nje.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna kilio chengine cha wananchi wa Mji Mkongwe eneo la Forodhani wale wanaopanga meza. Kwa kweli ada zao wanazolipa kwa muda huu ni kubwa shilingi 90,000/=, yaani ni pima moja tu na hiyo ni ada kubwa kutokana na maisha yetu yanavyokwenda wakati huu.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri ada ile kidogo akaipunguza, kwa sababu wapo watu wengine wameshashindwa na wanaondosha meza na hawawezi kufanya kazi, na lile eneo ni la kihistoria na watalii wakasaidia pato hili, kwani sehemu ile kama itanyesha mvua hakuna sehemu ya kujificha.

Vile vile kuhusu barabara Mhe. Naibu Spika, na swali hili niliuliza mimi hapa Barazani kuhusu kufungwa barabara ya Forodhani, na ukatoa ahadi kwamba kutoka Msikiti wa Ijumaa kwenye ule mti mpaka nyumba iliyokuwa ya Kulelea Watoto eneo lile litakuwa wazi, lakini imefanywa hivyo kwa muda wa siku tatu tu na baadaye ikarejea tena vile vile.

Kwa kweli jambo la kushangaza hivi sasa kuna magari mazito yanapita pale na njia inafunguliwa na kuna Wazanzibari wengine hawana haki ya kuitumia. Mhe. Naibu Spika, suala hili Mhe. Salmin Awadh Salmin amelizungumza kwa urefu tena kwa kina suala hili. Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika wakati atakapokuja kufanya majumuisho atusaidie maelezo kidogo.

Mhe. Naibu spika, kuna eneo jengine la Gongoni hivi sasa wananchi imekuwa hatari wanaweza kupoteza maisha yao hasa watoto wadogo. Sehemu yenyewe ni kutoka kwenye *Club ya Small Simba* kuna mtaro kutoka Gongoni mpaka Kikwajuni kwenye Benki ya *FBME*. Kwa kweli mtaro ule ni hatari na vile vibakuli au visanduku tayari vimeshaanza kufumuka hivi sasa.

Kwa hivyo, nahitaji maelezo kutokana na msingi ule unaotoka *Club ya Small Simba* mpaka Benki ya *FBME*, kwa sababu ni hatari kwa watoto wadogo wanaocheza pale na ule hauhitaji hata msaada. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja anisaidie maelezo kwamba msingi ule utatengenezwa lini, kwani kuna watoto wadogo wanacheza mule.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu Soko la Mji Mkongwe marikiti. Wananchi pale wanaotoa huduma wanachangia, lakini eneo la kuchinjia kuku mwaka jana nililipigia kelele na nikaambiwa litaezekwa na wala hakuna hatua iliyochukuliwa na watu hawa wanalipa na wanavujiwa kwenye kipenu pale.

Sasa niende kwenye ukurasa wa 55 Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU). Mhe. Naibu Spika, JKU inaendelea na miradi ya kuimarisha kufuga kuku, ng'ombe

wa maziwa na mayai, kuna ununuzi wa vifaranga 2000 vya nyama na 1000 vya mayai pamoja na ng'ombe wawili wa maziwa.

Mhe. Naibu Spika, naweza kusema hatuko *serious* kwa sababu mradi kama huu anaweza kuufanya mtu mmoja. Hivi leo unanunua ng'ombe wawili wa maziwa na leo tunategemea kuku kutoka Brazil au Tanzania Bara, nadhani ni vyema tuwe *serious* kwenye hii miradi au nyanya tunategemea zitoke Tanzania Bara.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anisaidie maelezo ya kina na hapo ndipo nitakapounga mkono hoja hii. Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa nafasi tunampa Mhe. Salim Abdalla Hamad baadaye Mhe. Panya Ali Abdalla na ajiandae Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru asubuhi hii kupata nafasi ya kuchangia machache katika hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya wakati naomba moja kwa moja nianze na Baraza la Manispaa au usafi wa maeneo kadhaa ya Mji wa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, kwa bahati mbaya mpaka hivi sasa hali ya usafishaji hasa wa Mji wa Zanzibar bado iko mashakani, tena uko mashakani kiasi ambacho na wala si vibaya kusema kuwa Mhe. Waziri labda watendaji wake wameshindwa kufanya kazi ipasavyo. Kwa mfano, juzi tumeshuhudia kuwa taka zinatupwa mpaka skuli wakati hili ni jambo baya sana.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, afanye kila inavyowezekana, ili mji huu pamoja na sehemu nyengine usafi wake uimarike kwa masaa 24, ili wenzetu wanaotembelea katika mji huu uwe ni kielelezo kama miji mingine ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, katika mji huu ni mwezi wa pili huu tunapopita tunawaona wafanyabiashara wadogo wadogo wanavyoadhibiwa. Kwa kweli tunajua serikali yetu kwa kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa makusudi inahimiza watu wajiajiri, wajitafutie riziki, wapunguze umasikini na waweze kujiendesha. Kwa maana hiyo, wenzetu kwa kujitafutia maisha wanafanya biashara hizi ndogo ndogo na wanafanya katika mji, kwa sababu ndiko kwenye wanunuzi wengi, ili na wao kuweza kujiendeshea maisha yao.

Mhe. Naibu Spika, nchi hii tunasema inafuata sheria na kuna vyombo vya sheria. Kwa hiyo, sioni sababu kwa nini watu hawa ikawa kila siku wanafukuzwa na askari wanavunjiwa vibanda vyao vya kufanyia biashara, wananyang'anywa na mali zao na wala haijulikani ilipo, wanatiwa umasikini.

Kutokana na hali hiyo, imefikia hadi majeshi yetu, ambayo yenye heshima yanayofanya kazi zake vizuri tena kwa uaminifu wanapewa jina baya la kunyang'anya mali zao, na kwa bahati mbaya hawajaitwa wezi tu na Mwenyezi Mungu asijaalie wakaitwa hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, najua kwamba watu hawa wamewekewa sehemu ya kuuzia biashara zao kule kwenye mikandaa au mikoko kule Saateni, na ninaamini wasingeliweza kuacha soko lao kule na kusambaa katika mji ni kuwa ile sehemu hairidhishi.

Sasa wakati nchi hii ni ya watu si ya mtu na wote ni mamlaka wanatakiwa kuwatumikia watu waone kuwa watu hawakuridhika na kuuza biashara kule kwenye mikandaa. Kwa hivyo, ni wajibu wa serikali kuwatafutia sehemu nzuri kama zilivyo nchi za wenzetu, ili waweze kufanya shughuli zao ipasavyo kuliko kuwanyang'anya mali zao bure wakati wengine mali hizi kuwa wanaazima, yaani wanauza na kurejesha fedha za watu.

Mhe. Naibu Spika, nadhani ni vyema sasa tukae tuangalie kwa sababu kuna kelele kubwa kuwa Soko la Darajani lina adha samaki wanauzwa mpaka barabarani, vumba linanuka, matumbo ya samaki yananuka. Kwa nini hatuiondoi hii adha hapa na wenzetu tukawaweka kule mikandaani na wale watu wakatafutiwa sehemu nyengine wakakaa na kufanya biashara zao vilivyo, nashauri hivyo kwa maslahi yetu sote.

Kwa hivyo, natumia fursa hii kumpongeza na kutoa shukurani mzee wetu ambaye yupo pale Kikwajuni juu kwenye Msikiti wa marehemu Sheikh Nassor Bachu, mzee Ali Salim kwa kazi kubwa anayofanya ya kujitolea yeye mwenyewe pamoja na watu wake waliomfuata katika kufanya usafi wa mji, nafikiri Mhe. Waziri anamjua na mimi napeleka pongezi hizo na ninaomba zitambuliwe. *(Makofi)*

Nikiendela na mchango wangu Mhe. Naibu Spika, niende kwenye suala la Vitambulisho vya Mzanzibari na mimi naomba viendelee kuitwa hivyo, na hivyo na hii ukaazi ni nadharia tu. Mhe. Naibu Spika, tukiangalia ukurasa wa 33 na 34 kimeeleza kwa urefu kuhusu Vitambulisho vya Mzanzibari na huku kuna Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho. Tukisoma kifungu cha 87 cha kitabu hichi naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 87 cha kitabu cha hotuba, kinaeleza hivi:-

> "Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho, imefanya usajili wa Wazanzibari Wakaazi 26,594 waliotimiza masharti ya usajili ikiwa ni ongezeko la asilimia 151 ukilinganisha na idadi ya Wazanzibari Wakaazi 10,578 waliosajiliwa katika mwaka 2011/2012.
>
> Aidha ofisi imetengeneza vitambulisho vipya 18,532 vilivyomaliza muda wake wa matumizi na imetengeneza vitambulisho 5,178 kwa wananchi waliopoteza na walioomba kufanyiwa marekebisho halali ya taarifa zao binafsi".

Mhe. Naibu Spika, kuhusu haya marekebisho halali ya taarifa zao binafsi hapa naomba nipate maelezo.

Vile vile tukiangalia kifungu cha 92 ukurasa wa 33 wa kitabu hichi, naomba kunukuu kidogo.

Kifungu cha 92(1) kinaeleza hivi:-

> "Ofisi ya usajili wa Kadi za Utambulisho inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-
>
> (i) Kuwasajili Wazanzibari Wakaazi waliotimiza masharti kwa mujibu wa sheria na kuwapa vitambulisho;".

Mhe. Naibu Spika, kwanza tuanzie hapo. Kwa kweli kazi hiyo inaendelea na inatendeka kwa Jimbo la Mkwajuni na Nungwi, na taarifa tuliyoipata kwa Mkurugenzi wa *Organization* na Chaguzi wa Chama cha Wananchi *CUF*, akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*, pia ni Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake ni Mhe. Omar Ali Shehe.

Kwa hivyo, baada ya kufanya utafiti wa uhakika aligundua kuwa katika Jimbo la Nungwi kuna wananchi wasiopungua elfu nne na nane ambao hawa wanavyo vyeti vya kuzaliwa, umri wao ni zaidi ya miaka 18 na hawa wamekataliwa kuandikishwa, na ametuthibitishia juzi kuwa ameandika barua na kumpelekea Mhe. Waziri anayehusika pamoja na majina ya watu hao kuonesha kuwa ni uthibitisho kamili.

Katika Jimbo la Mkwajuni kule kuna wananchi wasiopungua 328 wenye vyeti vya kuzaliwa na umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea na pia hao wamekataliwa. Mhe. Naibu Spika, katika jimbo hili pia kuna wananchi wasiopungua 71 waliofikia umri wa miaka 18 wameshajisajili pamoja na kupiga picha na kadhalika tokea miezi mitatu iliyopita na mpaka leo hawajapewa vitambulisho vyao.

Sasa Mhe. Naibu Spika, kama tunavyoona kuwa kitambulisho ni haki ya kila Mzanzibari ndio maana kikaitwa Kitambulisho cha Mzanzibari. Kwa hivyo, ikiwa mtu ametimiza masharti kama haya na ikawa hakuandikishwa. Kwa kweli hali kama hii inatia wasi wasi kuwa Mhe. Waziri anafanya kwa makusudi kabisa kuleta ubaguzi katika nchi hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tukifungua Katiba ya Zanzibar ukurasa wa 7 kifungu cha 12 sehemu ya kwanza ndogo na sehemu ya tano, kwa ruhusa yako Mhe. Naibu Spika, naomba niisome.

Kifungu cha 12(1) na (5) cha Katiba ya Zanzibar kinaeleza hivi:-

12(1) "Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria.

12(5) Katika kifungu hichi neno "kubagua" maana yake ni kutimiza haja kwa watu mbali mbali kwa kutegemea utaifa wao, kabila, jinsia, ulemavu, mahala walipotokea, muelekeo wao kisiasa, rangi au dini, ambapo watu wa aina fulani wanaonekana kuwa ni dhaifu na duni au wawekewe vikwazo na pingamizi, ambavyo wale watu wa aina nyengine hawawekeani au wanapewa fursa au faida ambayo hawapewi watu wa aina nyengine".

Mhe. Naibu Spika, hapo ndio mwisho wa kunukuu na hii ni Katiba ya Zanzibar ambayo tumeitunga wenyewe kwa kutaka usawa. Sasa leo ikiwa Mhe. Waziri anapelekewa orodha ya majina kama hivi mpaka leo hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na wakati kuna wengine wanasajiliwa *Wallahi* Mhe. Naibu Spika huu ni ubaguzi wa dhahiri tena wa kisiasa. *(Makofi)*,

Katika ukurasa wa 32 kifungu cha 88 naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 88 cha kitabu cha hotuba kinaeleza hivi:-

> "Naomba kutoa taarifa kuwa sheria Nam. 7 ya mwaka 2005 iliyofanyiwa marekebisho kuwa sheria Nam. 14 mwaka 2012, ili kuruhusu kupewa vitambulisho maalum kwa wageni wanaoishi Zanzibar. Utaratibu wa kutoa vitambulisho umekamilika na serikali inategemea kuanzisha rasmi utoaji wa vitambulisho hivyo katika mwaka ujao wa fedha 2013/2014.

Mhe. Naibu Spika, sheria ndio hii ambayo imefanyiwa marekebisho, lakini sio kila kifungu ambacho kimefanyiwa marekebisho, kuna baadhi ya vifungu viliachwa vile vile. Kwa mfano, kifungu Nam. 6 ambacho kimeandikwa Mhe. Naibu Spika, naomba kunukuu kwa kiingereza.

> Kifungu Nam. 6 kinaeleza hivi:-
>
> > "*Duty of the Director of Regisration*, wajibu au kazi za Mkurugenzi wa Uandikishaji wa hivi vitambulisho".

Sheria hii inasema hivi: "*Subject to the province of the act and directives of the Minister that the director shall register every Zanzibari resident in the Zanzibar who had attend the age of eighteen years and above*".

Mhe. Naibu Spika, maana yake kwa ufupi ni kutokana na toleo kama lilivyo na maelekezo ya Waziri, sasa huyu mkurugenzi ataandikisha kila mzanzibari mkaazi katika Zanzibar aliyetimiza miaka 18 na kuendelea. Kwa maana hiyo, lazima Mhe. Waziri kuna mdogo wake anafuata kifungu Nam. 6 cha sheria hii.

Kutokana na sababu za kudhalilisha na kuvunja haki za binadamu, kuleta ubaguzi katika nchi hii, ambayo ina utulivu. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria afanye kila inavyowezekana afanye marekebisho kwenye kifungu hichi yaondolewe, ili tusimuache Mhe. Waziri akakitumia anavyotaka yeye mwenyewe, ambayo ni kwa maslahi yake binafsi na wala si kwa maslahi ya nchi hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, unazo dakika tano.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu kuhusu masuala ya ubaguzi. Katika nchi hii askari wote hawatakiwi kujiingiza katika siasa, na nchi hii kila mtu ana haki ya kuajiriwa wakati ametimiza sifa na kumkosesha kuajiriwa wakati ametimiza sifa kama wengine ni ubaguzi.

Mhe. Naibu Spika, katika kupita kwangu nilikuta hati ya kiapo ya Jeshi la Ulinzi KMKM, na hii karatasi hii niliuliza na nikaambiwa kuwa karatasi hii inahusiana na usaili wa uajiri, yaani vijana wapoajiriwa KMKM huwa wanaulizwa maswali na yote huwa yanatoka kwenye fomu hii, na kutokana na fomu hii mtu anapata au anakosa maswali yenyewe ni 9 Mhe. Naibu Spika. Lakini swali la 9 ambalo liko kwenye ukurasa wa pili Mhe. Naibu Spika naomba kunukuu kidogo.

1. Je, wewe ni mwanachama wa CCM?
2. Halafu tena nambari yako ya kadi?

Mhe. Naibu Spika, ikiwa fomu ndio zile zile na Mhe. Waziri akitaka nitampelekea kwa masharti aniletee mwenyewe maana nitakwenda kuiazima nilikoipata. Kwa maana hiyo, ile fomu ndio zile zile basi hii inaonesha kwamba bado upo ubaguzi tena wa dhahiri hata katika kuwaajiri vijana wetu. *(Makofi)*

Sasa ninaloomba Mhe. Naibu Spika, kile kifungu Nam. 9 kinachouliza uanachama kifutwe moja kwa moja, ili kuwe na usawa katika ajira, kwa sababu nchi hii ni ya wote si ya chama cha siasa wala si ya mtu binafsi. Kwa kweli hata serikali kwenye Katiba inasema kuwa ni ya wananchi wenyewe. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, umalizie dakika 20 tayari.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia kuna jambo moja naomba nipatiwe maelezo kwa vile wakati hatuna na ninasikitika kwamba muda umekuwa mdogo ni kwamba hapa Jamhuri *Garden* kuna mradi ule wa kufurahishia watoto nasikia imo kwenye mamlaka ya Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tunataka kujua mradi ule asili yake nini? Mradi wa nani? Unafanya kazi vipi na serikali inafaidika vipi?

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache nashukuru naomba kukaa kitako. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe. Sasa nafasi tunampa Mhe. Panya Ali Abdalla na baadaye Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na Mhe. Mlinde Mabrouk Juma.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai na kuweza kukutana hapa asubuhi hii.

Pili nichukue fursa hii kukushukuru wewe ambaye umenipatia nafasi hii.

Vile vile nimshukuru na nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na watendaji wake wote ambao wametuletea bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaanza mchango wangu nataka niseme neno moja ambalo nalikumbuka alituwaidhi Komandoo Dkt. Salmin Amour Juma. Mhe. Naibu Spika, alisema kwamba "ukichokozwa usichokozeke na ukipigwa kofi kulia basi geuza kushoto". Kwa kweli maneno au mawaidha haya tutaendelea kuyazingatia tukijua tunadumisha amani ya nchi yetu
. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, sasa napenda nianze mchango kwenye ukurasa wa 32 ambao unaeleza kuhusu Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho. Mhe. Naibu Spika, mimi niseme zoezi la daftari limeanza kwetu Kaskazini juzi tarehe 29 Juni, 2013 na mimi nilikuwa miongoni mwa watu waliotembelea katika zoezi hili.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na juhudi zote, pamoja na elimu yote ambayo tunayoitoa kwa wananchi wetu pamoja na mapungufu ambayo wenzangu wanayasema, lakini bado kuna kazi kubwa ya kuelimisha wananchi wetu. Kwa kweli mimi nimepita na nimeshuhudia baadhi ya matukio kwamba wananchi wetu hawana elimu ya kutosha.

Kwa mfano, wamekwenda juzi katika zoezi lile la kujiandikisha na wengine wamekwenda na zile *pass* za uraia, yaani hawajui hata kile kinachoendelea, wamefika pale na *pass* za uraia kwa ajili ya kuandikishwa na wapo wengine hawana zana hata moja, lakini wamekwenda kujiandikisha. Sasa kwa namna kama hii huwezi kuandikishwa kwenye daftari. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Naibu Spika, naomba sana sisi viongozi tuchukue juhudi ya kuelimisha wananchi wetu, inaonekana bado elimu haijawafikia wengi. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye Idara Maalum. Kwanza napenda nichukue fursa hii kuvipongeza vikosi vyetu vyote vya SMZ kwa kazi kubwa wanazozifanya na majukumu waliyonayo ya kuiweka nchi yetu katika hali ya usalama mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, hii ni bajeti ya tatu tangu mimi niingie katika Baraza hili na kila wakati tulikuwa tukisema sana kwa kumuomba Mhe. Waziri kama askari wetu wanahitaji kuboreshewa maslahi yao pamoja na makaazi na ofisi

zao kwa jumla, ingawa tunaona humu Mhe. Waziri ameeleza. Lakini nimuombe sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba askari wetu bado wanaishi katika nyumba duni ambazo hazilingani na wala hazina hadhi na wao.

Kwa hivyo, niiombe sana serikali kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba iendelee kuwatafutia makaazi pamoja na ofisi ziwe nzuri kwa ajili ya kufanyia kazi zao, vyenginevyo tutakuwa tunawalaumu askari wetu labda hawafanyi kazi ipasavyo, lakini kumbe hata vitendea kazi hawana vya kutosha.

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda nimuulize Mhe. Waziri ni kwa nini kwanza askari wa KMKM ambao wako karibu sana na mimi nawaona sana mambo yao.Kwa nini bado wanaendelea kupokea mishahara yao katika kambi yao, hawapokei benki kama wanavyofanya watu wengine. Hii pengine ingeweza kuwaweka na wao angalau wanaweka salio kidogo kujiwekea akiba. Lakini kama unampa mtu pesa zake zote inawezekana akatumia zote bila ya kujiwekea akiba yoyote.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimuombe tena Mhe. Waziri pale tulipo Mkokotoni inaonekana kuna bandari, na ile bandari nimesema mara nyingi inakuwa kwa kasi kikubwa. Halafu kuna kisiwa ambacho watu wanavuka mara kwa mara. Nimuombe sana Mhe. Waziri, kuzingatia kuwaongezea boti KMKM wa pale. Ukizingatia kunajitokeza matokeo mbali mbali na wale wao ndio wanaopigiwa simu mwanzo kuweza kukimbilia katika matukio. Nakuomba sana Mhe. Waziri kulingana na ile bandari iliyopo matokea mengi huwa yanajitokeza na KMKM huwa wanataka kusaidia lakini wanashindwa kutokana na zana.

Mhe. Naibu Spika, pia niende katika askari wa Zima Moto, tulifanya ziara Kisiwani Pemba, tukafika *Airport*, tuliona mazingira yao na wao hayaridhishi, hata zile nguo za uokozi haziridhishi. Na hivyo ndio jumla ya vitendea kazi. Kwa hivyo nikuombe sana Mhe. Waziri kulizingatia hili, wale watu wapatiwe vifaa, wapatiwe magodoro yaliyokuwa mazuri ili waweze kulala mahala pazuri. Lakini pia nichukue fursa hii nimshukuru Meneja wa Uwanja wa Ndege kwa kuwatengenezea Ofisi yao ikawa katika hali nzuri.

Mhe. Naibu Spika, katika kitabu hiki nimeona kuna kiwanda cha ushoni *Zanzibar* Q*uality Tailoring*). Mimi nataka kukuuliza kiwanda hiki kipo wapi na kinashona nini, maana mimi sikijui kilipo.

Mhe. Naibu Spika, niende ukurasa wa 38, nichukue fursa hii kuipongeza sana serikali kwa ujenzi wa Ofisi za Mikoa na nyumba za viongozi ambazo wamejaaliwa kuzipitia katika ujenzi huo. Naipongeza sana serikali na

naishukuru. Ofisi zile zimehamiwa lakini bado hazijamaliza, kwa hiyo serikali pia izingatie kuyamalizia majengo yale ili yawe katika hali nzuri.

Mhe. Naibu Spika, niiombe sana serikali kwamba fedha wanazoingiziwa Wakuu wa Mikoa niseme zinakuwa ndogo na hazifikii yale malengo ambayo wamejipangia kuweza kupata fedha zile, kuweza kutimiza malengo yao. Kwa hivyo nikuombe sana Mhe. Waziri, tujitahidi *OC* hizi ziweze kupatikana ili Mikoa iweze kufanya kazi zake vizuri. Tunaelewa Mikoa ina kazi nyingi, tukikosa kuzifikisha fedha hizi katika malengo, tuelewe kama na kule malengo vile vile tuliyojipangia hayatimii.

Mhe. Naibu Spika, niende kidogo katika Baraza la Manispaa. Mimi nichukue fursa hii kwanza kuipongeza serikali, huwa sisemi labda tunalaumu tu lakini tunapongeza. Lakini bado juhudi kubwa inataka kuchukuliwa. Wafanyakazi wanajitahidi kuweka usafi, lakini bado kuna vitu vinakosekana. Nikisema pamesafishwa lakini hapana *dust bin* la kuwekwa pale paliposafishwa maana yake kwamba mtu ataweza kutupa taka tena vile vile baada ya muda mdogo pale paliposafishwa hapataweza kuonekana kama kweli pamesafishwa.

Niiombe serikali basi iweze kuweka zile *dust bin* katika sehemu ili tayari sisi tukiwa na taka tuwe na pa kutupa. Hii itaweza kutujenga kusimamia ile sheria, bila ya kuweka hivyo huwezi kusimamia kwa sababu itakuwa bado wananchi wanasumbuka hawajui taka waweke wapi. Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri na zoezi hili hata tungechukua padogo padogo tukaanza kuona kweli tunaweza tukafanikiwa, si lazima labda tukatamba katika mji wetu, lakini tukapasimamia pahala padogo tukaweza kufanya usafi na tukaona mafanikio, basi tunaweza kupata nguvu ya kuendelea na kwengineko.

Mhe. Naibu Spika, wenzangu hapa wamegusia *parking* lakini na mimi nataka nizungumze kuhusu *parking* za magari. Mhe. Naibu Spika, nimuomba Mhe. Waziri, zile *parking* kuziboresha kuwa nzuri. Kwa sababu mtu anapolipa fedha yake anategemea aweza kuona kitu kinakwenda vizuri. Naomba *parking* zile ziboreshwe na ziko vibaya vibaya, kwa hivyo ziweze kukaa vizuri ili mtu anapo- *park* gari yake pasiwe na mazonge mazonge.

Mhe. Naibu Spika, mimi baada ya kusema hayo nichukue fursa hii kuipongeza sana serikali kwa juhudi zake na naiombea heri iweze kupitisha bajeti zake zote za mawazira ili wananchi wa Zanzibar waweze kufikia katika mafanikio makubwa. Baada ya kusema hayo naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, nakushukuru.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia mawili matatu kwa vile wenzangu wengi wameshayazungumza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kuniamsha salama nikafika leo katika Baraza letu hili tukufu na ukanipa ruhusa ya kuchangia. Mimi nianze ukurasa wa 28 unaohusu Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nchi za Nje.

Mhe. Naibu Spika, hapa Mhe. Waziri niseme kati kati ya kifungu alisema kuwa idara ina jukumu la kuwatafuta na kutambua na kuwashajihisha Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi ili kuchangia, kujenga uchumi mzuri na kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, niseme ni kweli namuunga mkono Mhe. Waziri. Lakini vile vile kati ya hivyo kuwatafuta na kuwatambua sio suluhu tu na kuwajua ni wangapi Wazanzibari waliyekuwepo nje na kuwajua pia Wazanzibari hawa wana uwezo wa kuchangia katika nchi yao au hawana uwezo wa kuchangia. Kwa sababu wengi wao huondoka hapa kwa kudandia tu na wanapofika kule huwa mtu hata nguo ya kuvaa huwa hana, na wakati mwengine anakuwa mtu anataka kurudi kwao lakini hana uwezo wa kurudi. Ningemuomba Mhe. Waziri aliangalie sana kwanza ni kuwatambua na pia katika kuchangia wajue kwamba hawa wanao uwezo wa kuchangia.

Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa wa 62 Miradi ya Maendeleo ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwenye kifungu kidogo kinachosema kwamba Mradi na Uimarishaji wa nyumba za viongozi na nyumba za serikali. Mhe. Waziri hapa alisema matengenezo ya Ikulu ya Mkoani yapo katika hatua za mwisho kwa kukamilika. Tuseme Mhe. Naibu Spika, pamoja na matengenezo ya Ikulu ya Mkoani lakini bado viongozi wetu hatujawatafutia nyumba za kukaa. Kwa sababu Ikulu ya Mkoani ni Ikulu ambayo haistahili kukaa kiongozi yeyote ambaye ni wa juu kama mfano ni Rais. Ikulu ile sasa hivi imeingiwa na mmong'onyoko wa ardhi ambao unamong'onyoka na nyumba zile ambazo zimepasuka zinakarabatiwa. Ambayo ni nyumba ya kiongozi mzima na kiongozi wa juu kweli Mhe. Naibu Spika, kiongozi kama huyu tutamuweka kama pale.

Mhe. Naibu Spika, kwamba Mhe. Waziri atafute na serikali pamoja itafute kiwanja ambacho kitajengwa nyumba za kile na za kisasa na nyumba iliyo nzuri ya Mhe. Rais wetu, hii ni kumdhalilisha Mhe. Rais. Nyumba ile pale haifai kwa kukaa kiongozi wetu.

Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa wa 65 unaosema mradi wa Kiwanda cha Ushoni *(Zanzibar Quality Tailoring Limited)*. Naomba kidogo ninukuu hapa.

"Mhe. Spika, Mradi wa "Zanzibar Quality Tailoring Ltd" uliidhinishiwa TZS. 256.0 milioni na hadi kufikia Machi 2013 mradi huu uliingiziwa TZS 5.8 milioni ambazo ni sawa na asilimia 2.3 ya makadirio ya matumizi na kutekeleza yafuatayo:-

i) Kugharamia shughuli za uendeshaji wa kiwanda hicho kikiwemo ununuzi wa vifaa vidogo vidogo kama vile mikasi na nyuzi za kushonea."

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba TZS. 256 milioni ambazo zimeingizwa TZS 5.8 milioni na hizi walinunua nyuzi na mikasi tu. Hebu Mhe. Waziri atakapokuja anifafanulie vizuri kwa sababu naona sijafahamu. TZS 256 milioni wakaingiziwa TZS 5.8 milioni kwa kununua nyuzi tu na mikasi. Hii Mhe. Naibu Spika, naona kidogo ni tatizo. Halafu vile kwa mwaka wa fedha 2013/2014 mradi wa kuimarisha Kiwanda cha Ushoni kumetengewa TZS. 350.0 milioni utatekeleza kazi zifuatazo.

Ununuzi wa vifaa pamoja na kutafuta mali ghafi za uzalishaji.
Kujenga uwezo wa watendaji na kiwanda

Nataka nimuulize Mhe. Waziri ni kigezo gani kilichotumika Mhe. Waziri kuwa hapa TZS 256 milioni na mwaka 2013/2014 wakatengewa TZS. 250 milioni kinachotendeka Mhe. Waziri hakionekani. Naomba Mhe. Waziri utakapokuja hapa utupe maelezo kamili.

Mhe. Naibu Spika, nije katika Idara ya Vitambulisho na mimi kidogo nichangie kwa kusema Zanzibar ni nchi kama ilivyo nchi yengine. Halafu Zanzibar ina watu wake kamili kuanzia siku moja mpaka miaka mia moja na kuendelea. Hapa Barazani tunatunga sheria kwamba kila aliyefikia umri wa miaka 18 apewe kitambulisho cha Mzanzibari. Isitoshe watu wengine hawana vitambulisho mpaka kwenye redio jana watu wanahojiwa kwamba vitambulisho hawana na masheha hawawapi. Je, Mhe.Waziri nimuulize hivyo hii ni nchi inayotaka watu wake, nchi hii ikoje.

Mhe. Naibu Spika, watu wetu sasa hivi wanapotaka kusafiri wanashindwa hata kusafiri, kutokana kwamba hawana vitambulisho. Kitambulisho ndio roho ya Zanzibar na roho ya kila mtu. Mhe. Waziri naomba maelezo zaidi. Hapa mchangiaji mmoja alisema kwamba vitambulisho katika Ofisi ya Vitambulisho vipo vimerundikana na watu hawajaenda kuvichukua. Mimi

ningeomba Mhe. Waziri akaunda Tume ili kwenda kuvitafuta vile vitambulisho vya watu ambao hawajavipata kwamba ni vitambulisho vya Mkoa gani na Wilaya gani na Shehia gani, kila mtu akajulikana kwamba vitambulisho hivi vipo. Lakini ikiwa ni hivi tu kila siku tunasema vitambulisho vipo na vimerundikana na serikali tunaitia hasara kwa vitambulisho kuvitafuta, hebu Mhe. Waziri aunde Tume kwanza twende tukaviangalie vitambulisho vya Wilaya gani na Mikoa gani vilivyopo.

Mhe. Naibu Spika, nije katika Manispaa hapa ningemuomba Mhe. Waziri huu ni mwezi Mtukufu wa Ramadhani ambao kila mmoja anajitafutia rizki na watu wetu kila moja anategemea na kazi yake anayoifanya. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri kwa Mwezi huu Mkutukufu wa Ramadhani awaachie wale watoto wetu ambao wanauza biashara pale ili wauze kwa kujitafutia rizki zao za Ramadhani zilizo za halali. Lakini ikiwa tunawapiga vita wale sasa hivi tunawategemeza wapi, watakwenda kuiba wale ambao rizki iliyokuwa sio ya halali na Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani. Ningelimuomba Mhe. Waziri awaachie kwa mwezi huu wa Ramadhani watafute rizki zao zilizo za halali ili waweze kula na watoto wao.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

Mhe. Mlinde Mabrouk Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi asubuhi hii kupata fursa ya kuchangia mawili matatu katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais.

Mhe. Naibu Spika, mimi napenda kuanza katika ukurasa wa 6 pale Mhe. Waziri alipotuelezea kwamba kuna Shirika la Miradi inayosimamia Idara Maalum, yaani idara maalum inashughulikia miradi ya vikosi.

Mhe. Naibu Spika, katika Kikosi cha Zimamoto kunaandaliwa utaratibu wa kuweka vifaa vya kuzimia moto katika magari. Ni jambo zuri na limekuja kwa wakati. Lakini kuna usafiri wa aina mbili na wa baharini, vipi kwa upande wa baharini mmejipanga vipi kuhusiana na hili? Kwa sababu kuna wasafiri wengi na ambao wanatumia vyombo vya bahari. Hapa tumejipanga vipi, kama vimo kwenye meli zetu je, vinakaguliwa.

La pili nilitaka kuangalia kidogo katika kikosi cha KMKM. Mhe. Naibu Spika, kwanza nawapongeza maafisa wetu wanne wale waliokwenda kupata mafunzo nchini Uingereza katika kitengo cha *diver,* kwa kweli nchi yetu tumeshuhudia mara nyingi kuwa tunapata majanga mbali mbali hasa ya kuzama kwa meli. Kupeleka wataalamu hawa wanne nina imani watakaporudi watakuja kuwasaidia wale waliokuwepo vikosini. Tuna *experience* ya Mzee wetu mmoja Kipande jina lake halisi simjui natumia hili jina la umaarufu la

Kipande huyu alipata mafunzo nchini Uingereza na leo tunashuhudia kwamba mzee huyu pamoja na kuwa amestaafu lakini anaisaidia nchi hii yeye na vijana wengi ambao wamewafunza na wameweza kuisaidia nchi katika majanga yale yaliyotokea.

Mhe. Naibu Spika, katika jeshi hili hili la KMKM kuna kambi imeanzishwa kule Tumbatu na kunatarajiwa kujengwe mnara. Mimi nilikuwa najenga hoja tu kuhusiana na huu mnara tumeshuhudia hapa na sasa hivi tunasikia maneno mengi kuhusiana na Fungu letu kule Fungu Mbaraka kwamba kuna wenzetu wengine wanasema kwamba ni la kwao. Sasa kama hili ni la kwao je, mnara huu si ingekuwa vyema ukaenda ukajengwa Fungu Mbaraka ambako kuna wengine wanadai kuwa la kwao. Kuliko tukasema tujenge Tumbatu wakati Fungu Mbaraka limeanza kuwa na mgogoro.

Nikiendelea mbele Mhe. Naibu Spika, katika jeshi hili hili la KMKM sasa hivi tunaingia katika miaka 50 na Kikosi hiki kimeanzishwa tangu mwaka 1964. Nilikuwa naomba tu katika sherehe zetu za miaka 50 basi wafikirie angalau kambi moja kumuenzi yule Mkuu wao wa kwanza wa kikosi kile angalau kambi moja kuipa jina kuliko kuwa kama hivi sasa, kuna kambi zinaitwa nasikia Kibwengo *Camp*. Si majina mazuri haya. Basi angalau kambi moja itafutwe tumpe yule mzee wetu ambaye ni muasisi wa kikosi kile kama kuwaenzi ili vijana wanaokuja kuweza kuthamini na kuujua mchango wake katika kikosi hicho.

Mhe. Spika, nataka nizungumzie Idara hii ya Vitambulisho kumekuwa na malalamiko mengi, wengi wanasema kwamba vitambulisho hawajapata au hawapatiwi. Niwaombe kwamba wale wenye sifa kupitia kwa Masheha na Serikali za Wilaya ziwasaidie ili kuondoa haya malalamiko. Inaonekana kuna watu walidanganya haiwezekani kuwa na vitambulisho zaidi ya elfu ishirini, havijaenda kuchukuliwa na wenyewe. Serikali imekaa kimya inaeleza tu vipo vipo. Hawa kama wapo washtakiwe kwa sababu hawa wametia hasara serikali, kadi moja gharama mnaijua, zaidi ya vitambulisho elfu ishirini waachiwe tu hivi hivi, Hii itapunguza ule udanganyifu.

Mwisho Mhe. Spika, nizungumzie kitengo cha GSO hiki ni kitengo muhimu na nawapongeza kwa kutoa mafunzo. Wameeleza mambo mengi ambayo wanayafanya pia kutoa mafunzo kwa waajiriwa wetu. Kwa hivyo kitengo hichi cha GSO ni muhimu katika ajira na pia nawapongeza kwa kugundua wale waliokuwa wanajaribu kuingia katika ajira ili kutunyang'anya ajira zetu hapa ambao wametoka nje ya nchi na kuwaibua na kuwatoa.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii kutoa mchango wangu katika hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti, wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (SW) aliyenijaalia kuwa katika hali ya uzima na afya inaniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu. Pia nampongeza sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa hotuba yake nzuri ambayo inagusa sehemu nyingi.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea moja kwa moja katika mchango wangu kwa sababu muda hautoshi nifunue ukurasa wa 3 katika kitabu hichi ambapo hapa pamejaa mambo mengi. Naomba Mheshimiwa uniruhusu ninukuu, katika pragrafu ya 9 inasema hivi:

SHABAHA YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

Mheshimiwa Spika, Shabaha kuu ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni:-

i. Kudumisha amani, ulinzi na usalama,
ii. Kufanya vijana wawe na maadili mema na mtazamo wa kujiajiri wenyewe,
iii. Kustawisha haki za wanafunzi waliohalifu sheria,
iv. Kutoa huduma bora kwa jamii,
v. Kuimarika kwa maendeleo ya Zanzibar"

Mhe. Naibu Spika, katika kuchangia hapa panatosha, unaweza ukaogelea unavyotaka. Lakini kwanza nianze na mambo ya kudumisha amani, ulinzi na usalama. Kwa kweli ukiangalia katika eneo hili na ukiangalia na hali ya Zanzibar sasa hivi ilivyo, kudumisha amani na usalama hoja ni kwamba amani na usalama vimetuweka mijini na vijijini. Vitendo vya uporaji, ubakaji vinaongezeka Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia katika mazingira yetu Zanzibar inapoteza hata maadili yake ya kuaminiana. Kwa sababu sasa hivi hata mtu mwenzake hamuamini. Kutembea usiku ni matatizo. Ukiangalia vijana wanaoingia katika makundi yaliyokuwa hayahusiki ambayo yanavunja amani. Kwa mfano Mheshimiwa tukiangalia vijana wetu hasa vijana wa kiume wamepoteza muelekeo.

Huwezi kumkuta mtu kijana wa Kizanzibari mwenye maadili mema akawa amevaa suruali ambayo akiinama au akitembea inanyururika, ni matatizo. Huwezi kumkuta kijana wa Kizanzibari amesuka nywele, haya ni matatizo na sio maadili yetu. Sasa tumlaumu nani? Wa kulaumiwa ni sisi wenyewe wasimamizi. Hili Mheshimiwa tusipoliangalia litatupeleka katika hali mbaya sana ya Zanzibar. Kwa sababu tukiangalia wanaofanya hivyo ndio hao wanaotumia madawa ya kulevya na wanaofanya kila kitu. Wewe mwanamme mzima unakwenda kusuka nywele, mwanamke afanye nini, aibu.

Mhe. Naibu Spika, tunamuomba Mhe. Waziri katika kusimamia maadili haya pamoja na sote wazazi basi tusilipeleke katika wimbi hili huko tunakoelekea. Ni matatizo makubwa sana yatatufika siku hadi siku tutazalishavijana ambao kuwa hawezi kufanya kazi ambao wanafanya mambo machafu kabisa katika nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, tukiendelea hapo vile vile tumesema vijana wajiajiri wenyewe na hili ni jambo zuri. Kwa sababu wote hatuwezi kupata kazi za serikali, lakini tukijiajiri wenyewe kuna nyanja mbali mbali za kujiajiri. Nchi hii inakwenda kwa mujibu wa sheria, tungejiwekea sisi wenyewe. Kuna mambo ya Mahakama na kuna mambo ya fursa nyingi sana za haki za mwananchi. Tukiangalia vijana waliojiajiri wenyewe pale sehemu ya Darajani kwa kupata rizki ya kula na watoto. Lakini jambo la kusikitisha kama wamekwenda kinyume na utaratibu waliowekewa sio kuwatumia nguvu kupita kiasi.

Vijana wale wanataka elimu ya kutosha ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi. Lakini leo anathubutu askari wa nchi hii, sijui tuwaite vipi. Maana kama ni askari unayejiamini huwezi kwenda na ninja au masoksi umevaa katika uso, wakifika pale wanapora mali za wananchi na wanazitia magarini. Lakini kwa heshima kubwa mimi Mzee Waziri Mwinyihaji Makame ni Mzee wangu kabisa Mhe. Naibu Spika, sitaki asemwe vibaya. Kwa sababu kuna msanii mmoja anasema *mtu mzima huzima hauachi ukawaka*. Sasa yeye ni mtu wa busara kweli kweli asiuache ukawaka. Ninachochelea miye ni jambo moja kwamba askari wakianza kurushiana mawe na wananchi hii nchi tunaipeleka kubaya. Ni kuwafundisha katika utundu kabisa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kulisema hilo basi naomba sana Mheshimiwa anayo haki ya kuzungumza na wananchi wake, ni wananchi wake mpaka kufikia Uwaziri ni kuwa ametoka mikononi mwa wananchi. Kwanza ana haki ya kukaa nao na akawaelimisha zaidi pamoja na sisi tukasaidia. Lakini hakuna haki mtu kuvaa mavazi ambayo hayahusiki akaja pale Darajani akafukuza wananchi, *Wallahi* tumeshuhudia kijana mmoja pale kapigwa rungu hii! Na katika kukimbizana mmoja akagongwa na vespa, ni tatizo. Mtu atakuwa

anapita na shughuli zake lakini kutokana na vurugu lile ikasababisha mtu aliyekuwa hana hatia akaumia kama hivyo. Tunaomba tusifikie huko katika nchi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nikija katika ukurasa wa 32, Idara ya Vitambulisho na hapa nataka nitanabahishe sana, usifikirie kwamba tunapenda kurudia rudia tu, lakini pahali pakiwa na tatizo ni lazima liguswe na lisemwe, na hapa ndio pahali petu pa kusemea hatuna penginepo. Hapa ndio chombo cha kuwasemea wananchi, hatuna pengine.

Mhe. Naibu Spika, nasema kwa uchungu kabisa, lakini katika ukurasa wa 32, Idara ya Vitambulisho hapa nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, alituahidi ziara na ameifanya ziara na watendaji wote amewaita pale. Wakuu wa Mikoa, Masheha, Afisa wa Vitambulisho, Wakurugenzi wote walikuwepo na tuliona rundo zima la vitambulisho. Lakini Mheshimiwa mpaka hivi nazungumza hapa nataka kukwambia watendaji wako bado wana matatizo makubwa kuhusu hapa, kila siku utalaumiwa wewe wakati wewe unafanya vizuri lakini hawataki kufanya vyema wao.

Mimi mwaka 1995 nilikuwa Diwani lakini nilikuta sheria inayohusu serikali za mitaa katika mambo ya Madiwani. Sheha ili awe mzuri awe anapendwa na wananchi wake. Lakini ninakuhakikishia kwamba sasa hivi hakuna hata Sheha mmoja anayependwa na wananchi wake, kwa kutotoa huduma vizuri, wanatoa huduma kwa upendeleo. Ninakuhakikishia wanatoa huduma kwa upendeleo na *wallahi* kama hawatoi huduma kwa upendeleo haya leo yasingekuwepo tunayoyazungumza hivi sasa. Tunaomba tujirekebishe bila ya hivyo tutakuwa tunasema tu hapa, tukiondoka hapa basi jambo limekwisha. Wananchi wote wana matumaini na chombo hiki, wananchi wote wana matumaini ya serikali ya Umoja wa Kitaifa lakini tunapotizama yale tunakuja kusema hapa hakuna hata kitu kimoja kinachoshikwa, tusilifanye Baraza letu kama la Zee Comedy ikawa vichekesho tu tusifikie huko, tukisema kitu kitekelezwe wananchi wajue Baraza linafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa naomba kama kutakuwa na utafiti wa kutosha basi tulikuja pale siku ile Mheshimiwa Waziri tukakwambia kuna wananchi waliopiga kura mwaka 2000 mpaka 2005 hawa walikuwa na haki ya kupiga kura lakini baadae wakaachwa solemba. Wana vitambulisho vyao vya kupiga kura kwa nini watu wasipewe vitambulisho ni tatizo. Mheshimiwa tunawaomba hawa waliopiga kura 2000 na 2005 wapewe vitambulisho, mimi siamini kama wote wenye vitambulisho kama wanavyo vyeti vya kuzaliwa. Kuwa wengine wana vyeti vya kuzaliwa wengine hawana, tufanye *research* tunaweza tukaligundua hilo.

Tumesema kuna sababu kama mtu hawezi kupewa kitambulisho kama hajafikia umri wa miaka 18, awe ni mzanzibari mkaazi wapo watu wa aina hiyo. Hivi mimi ninaweza sijafika umri wa miaka 18 kuna watu wanaonizidi mimi hawana vitambulisho na ndio hawa tunaowazungumza, walipiga kura lakini 2010 hawakupiga kura. Tulikuletea Mheshimiwa hawa.

Tunaomba Wizara yako hii ifanye kazi ya kutosha katika kufanya utafiti hatusemi tu kwamba Mwakilishi aliyekuja hapa aseme abwate ovyo! Tatizo bado lipo na *wallahi* ukiliondoa leo kama utasemwa na mtu tena hapa. Na mimi nathubutu kusema naona vibaya kusemwa mtu mzima kama wewe kwa jambo hili nataka tufanye jambo lifikie mwisho haya mimi niulizie kuna woga gani? Kwa nini wananchi wasipate vitambulisho ni woga gani, tusiwe waoga.

Mhe. Panya kazungumza hapa kama mtu kaja na kadi ya uraia huyu hakupeleka kadi ya uraia kwa sababu hajui anajionesha kama ni mzanzibari halisi huko nilikotoka kwa sababu ana kadi ya uraia huo usumbufu anaoupata. Anaonesha hii kadi ya uraia kama mimi ni mzaliwa hapa lakini *wallahi* kwa utashi tu kabisa mtu ananyimwa hivi hivi akiona. Jambo hili kama halimo katika kisiasa tusingepata ugumu huo lakini haiwezekani kabisa limo katika mambo ya kisiasa.

Mheshimiwa tusifike huko tuna haki sawa sawa. Zanzibar ni yetu na hatuna pengine pa kwenda popote isipokuwa hapa Zanzibar. Sote tumesema hii katiba haijabagua na ina misingi mizuri tu haijabagua kitu, kila mtu ana haki mbele ya sheria na hatabaguliwa. Lakini leo tukifika kwenye watendaji hapa watu wanabagua hivi hivi.

Mheshimiwa nije katika vikosi vyetu ukurasa 52 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo. Hawa ni vijana wetu na ni wazuri, wanafanya kazi vizuri, na ndani ya Baraza hili tumewasikia sana katika kufanya kazi ya kuzuia magendo hasa katika zao letu kubwa la kipato cha taifa karafuu. Lakini je, na wao tumewawekea misingi mizuri? Jibu ni kuwa hapana. Mheshimiwa hawa mishahara yao ni midogo sana, tunaomba askari tukiwapa mishahara inayowakidhi haja watafanya kazi vizuri na kutosha lakini mshahara ukiwa mdogo mtu anaingia katika majanga mengine.Tulifikirieni hili tusiwatume tu, tuwatume halafu wakidhi na watoto wao, hawa ni watoto wanataka kusomeshwa kila kitu. Wewe mtu unamlipa mshahara ndani ya mwezi kila siku anatumia elfu tano hazikidhi haja ni tatizo.

Mheshimiwa vikosi hivi hivi vya KMKM hawa hata wakipata uhamisho posho lao la uhamisho hawapati wanatusikitikia. Mimi ninao kituoni kwangu

Kojani wapo hawa tunawaona hali zao zilizokuwa duni. Kwa hivyo tuwaangalie kwa jicho la huruma.

Nikitoka hapo Kikosi cha Zimamoto, kikosi hiki Mheshimiwa na wao wanafanya kazi za vizuri lakini kwa kuzingatia. Mimi awamu iliyopita nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, nilitembelea pale uwanja wa ndege na bajeti iliyopita tuliwazungumzia hawa lakini leo mwenzangu hapa amesimama kawazungumzia.

Bi Salma kawazungumzia vizuri kwa sababu yumo katika kamati hiyo, lakini hakujarekebishwa chochote tulichokizungumzia mwaka jana kilichopita hapa. Kwa hivyo wale watu pale uwanja wa ndege wana makaazi mabaya sana pale mvua ikinyesha wanakuwa katika tabu kubwa kabisa. Kwa hivyo na wao tuwaangalie kwa jicho la huruma vitendea kazi zao haviridhishi. Vitanda vyao halikadhalika kwa hivyo tuwaangalie kwa jicho la huruma.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea katika mchango huu mazingira ya mji wa Zanzibar takriban na Pemba yake ni mazingira machafu. Tumesema ukiona mambo yamezagaa, uchafu umekithiri. Mimi naomba Mhe. Waziri afanye ziara siku nyengine atembee kwa miguu kuangalia hali ya mandhari ilivyo inatisha.

Nakuzungumzia jumba namba saba nyumba za maendeleo ninazungumza tena na leo hebu jaribu kupita usipite barabarani tu, pia nyuma ya jumba lile upite uangalie hali ilivyo uchafu umekithiri na si hapo tu. Halafu vijana tunajisaidia ovyo ovyo mikojo imetapakaa mji unanuka harufu mbaya kwa hivyo Mheshimiwa tuliangalie wasimamizi wetu wanopewa kusimamia wasimamie kwa vyema ili mji wetu uwe safi.

Mji wetu unakaribisha watalii, sasa mtalii akija hapa asome uchafu. Jambo la kwanza anazungumzia usafi kama atazungumzia utakuwa mvuto na wengine wanakuja na serikali inapata. Lakini leo ukiambiwa utakwenda kutalii lakini mji mchafu kama huu haipendezi.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu umenipa fursa hii, nami ninakushukuru sana naomba niwapishe wenzangu ili waje wachangie na wao watoe mawazo yao lakini Mheshimiwa hapo kwenye vitambulisho nakuomba mzee wangu Mwinyihaji ukija hapa unipe la kushika. Wazee wangu wale ambao walipiga kura 2000 na 2005, 2010 hawakupiga kura hapa Mheshimiwa uniweke wazi ndio niku-*support* katika hii hotuba yako. Ahsante sana ninakushukuru.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Mhe. Naibu Spika, na mimi ninashukuru kwa sababu nilikuwa sina tamaa kwamba nitapata kusema chochote katika

mpango huu wa Ofisi ya Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi lakini bahati nzuri nimebahatika na mimi kupata fursa ya kusema machache ninashukuru kwa hilo.

Mhe. Naibu Spika, mimi mara nyingi huwa nina masuala ninajiuliza huwa ninasikitika na pengine huwa ninashangaa lakini mwisho huwa ninajiuliza kuna nini hapa kwetu Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, miaka 2 au mmoja uliopita nyuma Jamhuri ya Watu wa China ilitupa ufadhili, na ufadhili huu uliwawezesha watendaji wetu wakiwemo mawaziri na watendaji wakuu wa serikali kuelekea nchini China. Na imani yangu kwamba wale wenzetu walituita kule twende tukaangalie jinsi gani walikotoka na jinsi gani walivyofikia. Kwa vile tunayo macho basi nina imani kwamba tulikuwa tunaona walichokifanya.

Kwa ujumla Mhe. Naibu Spika, ni kwamba wenzetu wamefikia hatua kubwa sana katika mambo ya usafi na wao walituita twende tukaangalie jinsi gani wanaweka usafi kama huo. Lakini mimi kinachonishangaza ni kwamba watu wale waliokwenda kujifunza wamerudi sijui hawakuona, sijui hawakufahamu kwa sababu ni masikitiko makubwa. Kwa sababu ukienda barabarani mbali na kauli ya Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa nchi hii kwamba ng'ombe wasionekane bado wanaonekana, mbuzi wanaingia katika maduka, madimbwi ya maji hujui upite wapi? Na ukienda lile soko kuu sijui harufu ngapi zilizochanganyika pale. Sasa hatuoni Mhe. Waziri.

La kushangaza ukiambiwa kwamba aa leo ushasema maneno kama haya hapa basi Waziri na watendaji wake atakimbilia kuwaondosha wale watu wa Jua kali hatokimbilia kuondosha ule uchafu pale marikiti aa! Watakimbilia kuondosha wale watu wa Jua kali Mhe. Mwenyekiti hebu wapeni fursa na wao wapumzike wapumue, waachieni! La msingi ni kuondosha uchafu sio kuwaondosha wale watu wa Jua kali. Nia ya kukaa pale ni kutafuta ajira kama ilivyo katika malengo ya Wizara hii kwamba vijana kuwapatia ajira ile ni moja kati ya ajira. T

umekwenda kujifunza tukirudi tuyatekeleza hayo, wale vijana hatuna sababu ya kuwaondosha. Tulikuwa na malengo ya kujenga *Babylon in Zanzibar* na ndio iliyokuwa sababu ya kuwahamisha wale kila leo mara hapa mara hapa lakini naona huu ni mwaka wa pili sijui huo mpango wa kujenga hiyo *babylon* upo au umefikia wapi? Kama haupo tuacheni na wao wapumue watafute riziki, tunaelekea katika mwezi wa Ramadhan isiwe tena kupigishana mbio tu watalii tu watalii wanatushangaa, wakija pale wanaona kuna nini kumbe anaondoshwa raia wa nchi hii ati akatafute sehemu nyengine akae kapewa na nani hiyo sehemu nyengine. Mhe. Naibu Spika, hiyo si busara.

Mhe. Naibu Spika, jengine ninalotaka kulizungumza ni suala la *diaspora*, imekuwa ni maneno ya kwenye vitabu huu sijui ni mwaka wa tatu kila siku tunasema *diaspora*, *diaspora* wenzetu walioko nje waje watusaidie katika kujenga uchumi wa nchi hii, lakini kinachoendelea Mhe. Naibu Spika, sikioni. Kuna ofisi ambayo labda kila mwaka tunaiingizia fedha lakini kinachofanyika mimi sikioni. Lakini viulize labda nimuulize Waziri ninachokijua ni kwamba suala la uraia ni suala la Muungano, na katika bajeti hii hotuba hii tulielezwa kwamba aliyekwenda kuonana na Wazanzibari walioko Oman ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Kikwete. Sasa linaandaliwa vipi hili suala la *diaspora* linaratibiwa vipi? Linaratibiwa kwa Zanzibar kwake na Tanganyika kwake, au ilinaratibiwa kwa pamoja sisi tuko katika njia gani. Kwa sababu raia bado ninawahesabu wa Muungano.

Sasa sisi tukisema Zanzibar tunataka *diaspora* tunaungana na wale wenzetu tunakwenda moja kwa moja au tunakwenda Zanzibar kama sisi peke yetu na walioko Tanganyika na wao wanakwenda peke yao. Lakini kama ni hivyo kwa nini suala hili alisimamie Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na tusisimamie sisi wenyewe kwenda huko nchi za nje tukatafuta hao Wazanzibari. Lakini jengine je, kama tutakwenda nje tutawatafuta hawa tukawaambia Wazanzibari na hawa Watanganyika hatutakuwa tunabagua kuwaweka raia wa nchi moja makundi mawili tofauti hawa Wazanzibari na hawa Watanganyika?

Mhe. Naibu Spika, niendelee kidogo katika suala la GSO, Mheshimiwa moja katika kazi zake kitengo hiki ni kuangalia wafanyakazi watakaoingia kazini katika utumishi wa umma kwa mara ya kwanza. Lakini pia na wale ambao wapo kazini. Cha kushangaza na hiki mimi sikijengei imani hata kidogo ni kwamba kitengo hiki sijui kwa yule mfanyakazi anayetaka kuajiriwa leo wanakuwa wanamuangalia nini. Ninachofahamu kwamba linapotoka tangazo kwamba anaambiwa tangazo linatoka anatakiwa mtu aje na shahada yake ya masomo baadae aje na kitambulisho chake cha aidha ni Mzanzibari mkaazi au la. Sasa akishapeleka hivyo ina maana huyu hatakiwi kuchunguzwa jengine. Kinachozidi zaidi ya hapo kama utakwenda *beyond that* ina maana Mhe. Naibu Spika, utakuwa una-*practice apartheid*.

Sasa mimi nasema kwamba hiki kitengo kwa wale waajiriwa wa mwanzo basi kisiwachunguze. Kwa sababu sisi tumempa mtu kitambulisho kwamba wewe ni raia mkaazi wa nchi hii tena tunamtilia wasiwasi nini? Kama cheti cha kuzaliwa siku hizi tunakwenda kufanya mambo ya *scanning* kwenye kompyuta yoyote unaangalia nini, matokeo yake tunawakosa wataalam. Kwa sababu tunakwenda zaidi ya hapo na sisi hatutakiwi kwenda zaidi ya hapo, tukifanya hivyo *human right* haikubali, mambo ya haki za binaadam.

Sasa mimi ninamuomba Mhe. Waziri angalau hebu aje anipe matokeo watakapofanya utafiti na sisi ajenge mazoea ya kuja kutwambia kwamba Idara fulani kwa mfano Baraza la Wawakilishi limetangazia nafasi za kazi matokeo yalikuwa haya hapa, aje atuoneshe tuone na sisi turidhike. Si hivyo mimi siridhiki na utendaji wa kitengo hiki, kwa sababu wanachokiangalia ni kinyume cha haki za binaadam. Lakini zaidi ya hayo ni kwamba kitengo hiki pia kinawachunguza watu ambao tayari wako makazini je kuna ripoti zozote zile ambazo tayari wanazo na wanaweza wakatupatia kwamba idara fulani wafanyakazi fulani walikuwa moja, mbili, tatu na anastahiki kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

Mhe. Naibu Spika, labda niingie katika sehemu nyengine ye kadi za vitambulisho. Kila mmoja hapa Mhe. Naibu Spika, amezungumza kwa anavyojua yeye mwenyewe na hii ndio sifa ya lugha. Kwa sababu lugha Mhe. Naibu Spika, wataalamu wanasema, *a selection and combination of words.* Yaani kuchagua kutoka moja ukasema sio moja ukasema mbili, halafu ile mbili ukasema aa naiweka na hili yaani unachagua neno unayaunganisha ndio lugha. Kwa hivyo wengi wanakuja hapa kila mmoja anasema vyake. Na Mhe. Waziri na yeye ni hivyo hivyo anakuja hapa anatwambia hivi, anatwambia hivi kwa sababu lugha ya Kiswahili ni lugha yetu. Lakini kiujumla katika sehemu hii kuna matatizo. Mhe. Waziri anatumia sababu ya kwamba kuna vitambulisho vingi havijachukuliwa, anayekuwepo nje kama hajafika mahkamani hata kama ana kosa hajashtakiwa huwezi ukamuhukumu.

Tunachomuomba kwamba hawa waliokuwa hawajapata ndio awape vitambulisho, na wapo na orodha tunazo. Hii ya kutwambia kuna vitambulisho 20,000 kuna vitambulisho vingapi achane nayo awatafute kama ni Kiongozi wa nchi hii na ni haki yao awapatie basi hao waliokuwa hawajachukua afanye bidii. Mhe. Waziri wa Katiba aliandaa utaratibu wa vyeti vya kuzaliwa akawa anakwenda katika Wilaya anawatafuta wale ambao hawajachukua anawaambia nani ni huyu hebu nani hajaandika huyu anawapatia. Kwa nini na wao wasichukue *initiative* kama hiyo akaona kwamba hii ni haki na mimi kama ni Waziri ninayesimamia kitengo hiki, leo haoni aibu kuja hapa akatwambia tu kuna vitambulisho 20,000 havijachukuliwa maana yake nini? Maana yake wewe kama ni Waziri hakikisha kwamba vimechukuliwa watafutwe wapewe wenyewe haki zao au haki ile adai nani.

Mhe. Naibu Spika, ninamuomba Waziri afanye bidii kama vipo awapatie wenyewe na waliokuwa hawajapata basi afanye bidii kwamba kila mmoja aliyepo katika nchi hii ampatie haki yake. Waliosoma historia za Marekani wanajua kwamba hivi sasa ni taifa moja lililoimarika lakini wanajua fika kwamba taifa lile lilipigana vita vya wenyewe kwa wenyewe; *civil war*. Na

moja katika sababu zinazosababisha taifa lile kupigana *civil war* ni kudharauliana. Waliokuwepo Kaskazini walijiona wao ni bora zaidi kuliko waliokuweko Kusini. Kwa hivyo dharau hizo zikawafanya wa kusini na wao waone aa kwa nini na sisi tumo katika taifa moja watunyanyase na watudhalilishe kama hivi. Matokeo yake wakaingia katika vita vya wenyewe kwa wenyewe. Lakini matokeo tunayaona kwamba hivi sasa ni taifa moja lililoungana na lina nguvu kubwa duniani sasa itafikia wakati mtu atakujaona ee! Kwa nini na mimi niliyemo katika nchi hii haki yangu ni hii kwa nini siidai katika njia nyengine ambayo naweza kuifanya. Lisifike hilo hili ni tatizo na Mhe. Waziri anajua na atakapokuja hapa atatumia lugha yake anayoijua yeye lakini bado ni tatizo ukweli ni huo asikubali asikubali, afanye bidii raia wa nchi hii tuwatambue kwa hicho kitambulisho kilichowekwa na serikali.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kwa mradi wa shamba la mfano la pamoja la Bambi. Shamba hili kwa kumbukumbu yangu mwaka jana tulizuia fedha zisitumike mpaka tupate maelezo. Mwaka huu zinaombewa tena milioni mia mbili na hamsini. Mimi nimuulize Mhe. Waziri tulivyoelezwa mradi wa shamba la mfano la pamoja kwamba je hawa ambao tunashirikiana nao wao wanachangia nini katika shamba hili ni utaalamu pekee ni fedha au ni nini.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninakushukuru.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Naibu Spika, na mimi ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii angalau niseme mawili matatu, lakini kwanza Mhe. Naibu Spika ninakupongeza wewe binafsi kwa maelekezo yako na Wajumbe wameyafuata. Maana yake mimi nilipopeleka sikuwa na tamaa kama ningefikwa leo lakini Wajumbe wamekuwa wanafuata yale maelekezo yako ya kusema zile *point* zao chap chap ili wasitumie muda mwingi, na hilo limenisaidia na mimi kupata nafasi ya kusema na mimi nitafanya hivyo hivyo tukijaaliwa.

Mheshimiwa nataka nianze na ukurasa wa 38 kuna mamlaka ya serikali za Mikoa na naomba ninukuu kidogo ili niweze kufahamika wakati nitakapokuwa ninatoa hoja yangu. Imeelezwa hapa Mamlaka ya Serikali za Mikoa zimepewa jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa maagizo ya serikali katika maeneo yao ya utawala, uratibu na kutekeleza maagizo ya serikali katika maeneo yao ya utawala hilo ndio jukumu lao la msingi.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya awamu hii ya Dr. Shein Wakuu wa Mikoa walikuwa ni wanasiasa na wewe ni shahidi huko tunakotoka hakukuwa na mazingira mazuri tulikuwa tukivutana sana katika mambo ya kisiasa. Na

katika hili nataka niwashukuru Mhe. Dr Karume Rais Mstaafu na Mhe. Maalim Seif kama Katibu Mkuu kwa wakati ule kukubaliana kuiondoa jamii yetu katika uhasama wa kisiasa. Lakini unajua jambo ukiliweka akilini sana mara nyengine linasababisha ulemavu fulani na ndio maana tukawa mara kwa mara tunamkumbusha Dr. Shein kwamba hawa Wakuu wa Mikoa hebu fanya mabadiliko tena wabadilishe, kwa sababu sasa hivi ni watendaji si wanasiasa tena lakini hawa waliopo ni wale wale ambao kwanza walikuwa wanasiasa sasa hivi wameondolewa kwenye siasa ni watendaji, lakini wana zile nongo nongo za kisiasa wanafanya kazi si za kwao tena.

Sasa mimi naomba sana kupitia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi naomba kupitia kwake nimpe salamu Mhe. Dr. Shein kwamba alirithi nchi ikiwa tayari imepata utulivu, alhamdulillahi mwaka wa pili au tunakaribia mwaka wa tatu sasa hivi tunaendelea katika hali nzuri sana kwa kweli kila mmoja anasifia hilo. Na ndio maana tunawataja waasisi wa haya makubaliano kwa ajili ya kujipongeza wenyetu na sote tulikuwemo humu tukaamua kuyakubali yale tukayapeleka kwa wananchi yakakubalika.

Sasa tunaendelea vizuri, sasa mimi nadhani wasitokee watu wakataka kuturudisha kule tunakotoka, hii jamii jamani wazanzibari ni watu wa aina yake ni visiwa viwili lakini tuliochanganyika sana. Ukiendelea kumchochea huyu ili amhasimu huyu utakuwa unafanya dhambi kubwa sana maana unagombanisha watu wa familia moja namuomba sana Mhe. Waziri anifikishie salamu zangu kwa Dr. Shein naomba umwambie Dr. Shein na hili hata Dr. Karume aliwahi kufanya, tulipokuwa tunaandaa makubaliano na katika kura za maoni kuna baadhi ya Wakuu wa Wilaya walikuwa bado wako kule kule kwenye siasa, Dr. Karume kachukua hatua.

Ninamuomba sana Dr. Shein kama kuna mtu anataka kuturudisha tulikotoka amchukulie hatua amuweke kando, watu wapo wengi wa kufanya kazi za Wakuu wa mikoa. Watu wako wengi sana walio na sifa za kuwa wakuu wa Wilaya asituwekee watu waliokuwa na ulemavu ndani ya akili zao watatuhangaisha sana. Tunataka tupige hatua mbele sio kuendelea kuhasimiana kila siku Mhe. Naibu Spika.

Baada ya utangulizi huo sasa naomba niingie kwenye serikali za mitaa ambayo imeelezwa katika ukurasa wa 67, nayo pia naomba ninukuu kidogo Mhe. Naibu Spika. Kwamba serikali za mitaa ndio muhimili mkubwa wa utekelezaji wa majukumu ya serikali katika lengo zima la kuhakikisha yanakuwepo maendeleo endelevu katika nchi yetu, hilo ni jukumu la serikali za mitaa. Sasa hoja yangu hapa na ukiangalia katika makabrasha na vitabu alivyotuletea Mhe. Waziri ukitaja serikali za mitaa anazungumza kwanza

Baraza la Manispaa, Mabaraza ya Miji, Halmashauri hizo ndio serikali za mitaa.

Sasa mimi nilikuwa ninajiuliza ikiwa serikali za mitaa jukumu lake ni kuisaidia serikali ndio muhimili mkuu wa utekelezaji wa majukumu ya serikali, sasa Sheha nafasi yake ni ipi? Maana yake tulikuwa tukiuliza mbona Sheha na Diwani kazi zao zinaingilianaingiliana. Tukaambiwa aa Sheha anatekeleza majukumu ya serikali ni taasisi ya serikali ni taasisi ya serikali kule chini. Lakini kwa mujibu wa maelezo haya ya ukurasa wa 67 jukumu hili ni la serikali la mitaa ambayo ni halmashauri kuna madiwani mabaraza ya miji kuna madiwani. Kwa hivyo unakuta kama kuna *duplication* ya kazi kati ya Sheha na hizi serikali za mitaa. Sasa hoja yangu mimi nilikuwa nadhani ngazi hii ya masheha tuiondoshe isiwepo kabisa kwa sababu kuna ngazi ya madiwani ambayo ndio serikali za mitaa zinatekeleza majukumu yale yale ya Sheha hakuna haja ya kuwa na *duplication*. Na pamoja na hayo sasa tatizo linatokea mara nyingi nimewahi kusema masheha tunaowachagua hawa-*qualify* kuwa masheha kwa maana ya masheha.

Maana yake Sheha Mhe. Naibu Spika, tulikuwa wadogo sisi lakini tunakumbuka kulikuwa na masheha wale wa zamani wale, wale masheha walikuwa wakichaguliwa watu maarufu sana katika mitaa, watu wenye kuheshimika, watu wanaojiheshimu, watu waadilifu.Siku nyengine hata ukisikia mtu ni Sheha pengine ni Imamu wa Msikiti huyo anaheshimika ndani ya jamii. Leo Masheha wetu hawachaguliwi kwa misingi hiyo, unamkuta Sheha kuswali haswali eti ni Sheha anawatawala waislamu wote wanaosali katika mji wake, unamkuta Sheha ni very *corruptive* maana yake tatizo katika nchi, mla rushwa mkubwa, anabinya haki za watu, sasa wanasababisha *conflicts* katika jamii.

Mhe. Naibu Spika, mara nyingi huwa napenda kutoa mifano wa wale masheha wangu kule Jimboni. Kuna Masheha kule jimboni wazuri kweli kweli, *very polite*, unajua kwamba huyu kwa kweli anafanya kazi ya usheha, lakini kuna Masheha wengine wanarundika mas-*scandals* kila siku. Kuna Sheha kule Kilindi sitaki nimtaje kwa jina nadhani Mhe. Waziri anamjua hata kwa sura huyu ni *corruptive*.Nimeshawahi kushtaki kesi nyingi za Sheha yule na leo nakupa nyengine. Kwanza Sheha yule kuna mradi wa upandaji miti, zikatolewa milioni 60 zimo ndani ya kitabu nimeziona, kenda katafuta wanawe wawili watatu pale wakaenda wakapanda mivinje mitano halafu wakatoa ripoti kwamba wameshapanda mivinje ya milioni sitini, nimekwenda kuikagua siioni, pesa kala na nimesema humu.
Mhe. Naibu Spika, kuna mradi ule wa mashua zile, kila kijiji kilitakiwa kupata mashua. Bahati nzuri sana Shehia ya Kilindi ikapata mashua mbili, kitu ambacho ni adimu sana, mara nyingi kila Shehia inapata mashua moja.

Ile Shehia ya Kilindi ni kubwa ina vijiji vingi, kachukua mashine zote mbili kawapa jamaa, mimi nilikuwa najua watu wa Kilindi wananung'unika mbona sisi hatukupata hatukupata, mimi nikakataa maana huwa sizingatii sana, nikaja nikacheki kwenye vitabu kumbe imo, tukaitafuta hii mashua iko wapi kawapa watu saba jamaa zake.

Leo watu wa Tundauwa wananinung'unikia, tena na tulikuwa na ahadi na Mkuu wa Mkoa kwenda kule kushughulikia matatizo ya watu wa Tundauwa, wananiambia sasa Sheha anashirikiana na aliyekuwa Diwani sijui nani wanaanza kuuza ardhi, jambo ambalo Serikali imeelekeza sana kwamba Masheha wasijishirikishe katika migogoro ya ardhi, leo Sheha anauza ardhi za watu kule.

Mhe. Naibu Spika, kuna Afisa Tawala nilimkuta hapa nikamwambia bwana Sheha wako ana matatizo akaniambia hiyo habari siijui, sasa habari ndio hiyo, anauza na hili naomba sana Mhe. Waziri lifanyie utafiti nataka maelezo ya kina ana *authority* gani Sheha yule kwenda kuuza ardhi za watu.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ni Idara ya Vitambulisho ambayo iko ukurasa wa 37. Idara ya vitambulisho ilianzishwa kisheria na kazi zake zinatakiwa zifanywe kwa mujibu wa sheria na ni Idara ya Kiserikali. Ni Idara ambayo inatakiwa itoe huduma sawa kwa wananchi wote, sasa mara nyingi Idara hii imekuwa ikinung'unikiwa sana sana, na mimi nathubutu kusema kwamba Idara hii badala ya kufanya au kutoa huduma kwa ajili ya jamii nzima, sasa inatoa *service* kisiasa zaidi. Kwa sababu wanaotakiwa kusajiliwa ni Wazanzibari lakini bahati mbaya kuna Wazanzibari wengi katika nchi yetu hawajasajiliwa na wenzangu wamesema humu kuna wengine walikuwa tayari wamesajiliwa lakini sasa wamefutwa, sababu ni vyeti vya kuzaliwa.

Mhe. Naibu Spika, vyeti vya kuzaliwa vina tatizo kubwa katika nchi yetu sasa. Kwanza Masheha ndio waliokuwa wanaipa *qualification* za kuwa hichi kitu kinafaa au hakifai.Tukasema sema Mhe. Waziri, akachukua juhudi kubwa sana ya kuwaambia Masheha si kazi yenu, kazi yenu ni kumtambua huyu mtu anayeomba kitambulisho ni mtu wa Shehia yako au la, wewe tia *comment* hizo, Masheha wakaacha.

Kwa hivyo sasa cheti kinakaguliwa kule Idara ya Vitambulisho. Lakini kinachotokea kule ni kwamba hakuna cheti ambacho ni *qualified*, kila cheti kinachopelekwa kule, basi kuna wataalamu kuliko wale Maafisa wa kule vizazi na vifo kule kwa Mrajis. Hawa Maafisa walionao hawa watu wa vitambulisho basi wana uwezo zaidi wa kufanya *analysis* ya cheti kuliko wale watu wenyewe wanaohusika na usajili wa vizazi na vifo, hata cheti kiwe vipi, ukienda kule utaambiwa cheti hichi ni feki, cheti hiki sijui kina hivi, hakina

hivi, almuradi watatia kila sababu mpaka watu washindwe kupata haki yao ya vitambulisho.

Na unapomzuia mtu haki yake ya kitambulisho unafanya kosa la jinai, maana sheria ya vitambulisho inataka kila mtu apate haki yake ya kupata kitambulisho, lakini huyu anatafuta visababu vyake vya kisiasa unamzuia mtu kupata haki yake.

Mhe. Naibu Spika, ushahidi juzi sikuwepo lakini nasikia Mhe. Salma aliutoa na huu naukumbuka kwa sababu Mhe. Salma alituonesha vyeti vile ndani ya kikao na Waziri alikuwemo na Mkurugenzi wa Vitambulisho alikuwepo na akatueleza historia ya vile vyeti vyake, kwamba kavipeleka kwa Waziri. Waziri akavikagua kwa kadiri ya uwezo wake Waziri wa Katiba na Sheria akamwambia hivi vyetu ni sahihi, lakini hebu vipeleke kwa Mrajis, akavipeleka kwa Mrajis wa Vizazi na Vifo ambapo kwa vyovyote vile atakuwa ana-*access* ya kujua kwamba kitu hiki ni sahihi zaidi kuliko mtu mwengine yoyote. Mrajis aka-*comment* vyeti vyako ni sahihi havina matatizo.

Mhe. Salma akavitoa akapewa Mkurugenzi wa Vitambulizo pale akawapa watendaji wake wakamwambia vyeti hivi vina matatizo, sasa ikiwa Mrajis wa Vizazi na Vifo akafika pahala akasema vyeti havina matatizo, leo anatoka mtu wa Vitambulisho anasema vyeti vina matatizo, hivyo mwenye dhamana ya kujua cheti kina matatizo au hakina ni nani? Sasa kwa misingi hiyo ikiwa yule ni Mheshimiwa unavyosema kwamba angalau mtu anafumba fumba moja wakati wa kumpatia huduma yeye, lakini kuna wale wasiokuwa Waheshimiwa hali zao zitakuwaje? Kwa maana hiyo kuna watu wengi sana ambao wanastahiki kupata vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi lakini hawapati kwa misingi ya namna hiyo.

Mhe. Naibu Spika, unapomzuia mtu kitambulisho maana yake kwanza unapinga sheria yako mwenyewe, maana sheria inakutaka umpe kitambulisho sasa humpi unavunja sheria ya kwanza. Sheria ya pili unamnyima haki yake ya kikatiba, kwa sababu ni kupitia kitambulisho kile ndio atapata kuandikishwa katika daftari la wapiga kura, kwa hivyo unafanya makosa mawili; unavunja katiba, unavunja sheria. Sasa mimi nadhani natoa hoja moja tu, kwamba ikiwa hii ndio hali ya Mkurugenzi wetu mimi nadhani hafai aondolewe kabisa kabisa. Awekwe atakayekuwa muadilifu afanye kazi kwa mujibu wa sheria sio afanye kazi za kisiasa.

Na katika hili mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, kwa sababu kuna hoja nyingi, ukiwaambia hao kuwa kitambulisho hatupati wanakwambia kama kuna vitambulisho vingi tu kule watu hawaji kuchukua, mimi walinipa orodha nina

watu elfu moja na nne katika jimbo langu kwamba wamekuja wakapigwa picha hapa vikatayarishwa hawakuja kuchukua, nimewatafuta Jimboni mwangu siwaoni hata watu hamsini sijapata, Sasa ikanijia kwa nini inakuwa hivi.

Mhe. Naibu Spika, dhana yangu ni kwamba kuna watu wameandikishwa vitambulisho vya bandia mule na ndio maana hawajitokezi wenyewe kuja kuchukua maana hawapo. Sasa kwa misingi hiyo naomba kutoa hoja kwamba sasa tuunde kamati teule tukaichunguze Idara ya Vitambulisho, tukalikague buku, tukachunguze na vitambulisho ambavyo wanavyo havijawahi kuchukuliwa ni vingapi, na wenyewe ni akina nani tuone kwamba ni Wazanzibari kweli, Mzanzibari kweli kuwe na kitambulisho chake yuko tayari kutoa laki nzima apate kitambulisho leo asiende kukichukua, wasitudanganye bwana. Sasa naomba tuunde kamati Mhe. Bi. Panya kasema hapa kwamba kuna watu wanakwenda kwenye daftari nafasi ya uraia ile ya zamani, sasa aende na ipi na ndio aliyokuwa nayo, kitambulisho hana hapewi na ile ni haki yake ya kupiga kura asiende nafasi na pasi ya uraia aende na nini, atakwenda na pasi ya uraia, atakwenda na leseni ya gari, atakwenda na vitambulisho vyengine tele, si anataka haki yake bwana.

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, naomba nizungumze na Ofisi za Wilaya, na hili ninataka nimwambie Waziri. Ofisi zake za Wilaya ndizo sasa zilizopewa jukumu la kuandika vyeti vya kuzaliwa. Tuna wasi wasi sasa kwamba ofisi hizi zinafanya sivyo na kuna mwananchi mmoja mimi alinipa habari, akanambia kuna Sheha mmoja kaenda Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Chake Chake, alipofika akakuta rundo la vyeti vyingi, ni kawaida ya Masheha wakifika pale hujaribu kuchakua chakua mle kwenye vyeti, ili kama kuna raia wake vyeti vyao vimo mule basi huvichukua kwa kuwasaidia kazi akawapelekea. Sheha yule katafuta kapata vyeti viwili, akajua kwamba hawa ni watoto wa fulani, kwa hivyo akawachukulia vyeti vyao, akaenda zake nyumbani. Sokoni akamkuta mzee wa wale watoto, akamwambia bwana mkubwa nina vyeti vya watoto wako wawili naomba uje nyumbani uchukue. Yule mzee akashangaa akasema hawa watoto anaonitajia vyeti vyao ninavyo nyumbani, lakini akamuitikia alitaka kujua mwisho wake lile, akamwambia sawa nitakuja kwanza akakimbilia nyumbani akaenda akaangalia pale anapohifadhia vyeti vya wanawe hivi vyeti havipo kweli hapa, akacheki vyeti pale viko vya watoto wale wale, akasema ah! Hivyo Sheha ana vyeti vya nani ngoja niende, alipokwenda akapewa tena vyeti vya wanawe wale wale wawili ambapo nyumbani anavyo, lakini vimechapishwa tena, tena si watoto wachanga ni watoto wa kuzaliwa siku nyingi, akavichukua vile vyeti, sasa akajiuliza kulikoni kuna nini na Sheha alimwabia hivi vyeti viko vingi mie nachagua chagua ndio napata hivi viwili ninavyovijua viko vingi hivi.

Mhe. Naibu Spika, mimi hapa ninapata wasi wasi, na napata wasi wasi kwa sababu aliyenihadithia hili ana uzoefu wa jambo jengine, ana mwanawe yupo hapa Unguja kama sikosei Jimboni kwa Mhe. Hamza, wakati wa uchaguzi yule mtoto alipata misukosuko kidogo, wakati aliyekuwepo pale kituoni liliitwa jina la yule mtoto, sasa kwa sababu yule wakala yule mtoto ni jirani yake anamjua vizuri, aliposikia lile jina akashtuka akamtizama usoni, alipomtazama usoni siye yule, ni mtoto mwengine tena wa kibara akawaambia wale viongozi pale huyo jina hilo si la kwake na wala si fulani huyu, musije kutumia jina la mtu mwengine, lakini waliokuwa wakilinda kituo pale wakampisha pisha wanataka kufanya fujo hivi na hivi akawaambia basi muacheni apige kura lakini nakwambieni huyo siye na nina hakika mwenyewe hapa atakuja na baada ya sala ya adhuhuri yule mwenyewe halisi akaja na kitambulisho chake cha kupigia kura kamili kuja kupiga kura yake.

Alipofika akajitambulisha pale akapeleka kitambulisho chake wakaangalia kwenye *list* wakamwabia kura yako imeshapigwa, imeshapigwa vipi na mimi ndio ninakuja sasa hivi. Sasa wakala akawaambia nilikwambieni mwenyewe atakuja, akamwambia mama nenda zako ukalale, jina lako keshapewa mtu mwengine wa kibara keshapiga kura nenda zako ukalale, yule mtoto akalia siku tatu, hakupata kupiga kura yake.

Mhe. Naibu Spika, kilichopo ni nini, kilichopo kumbe hivi vyeti hivi vinavyotayarishwa huku halafu wanaandikwa watu kwenye madaftari ya kupigia kura na pengine wanapewa *instruction* kapigeni mapema ili wenyewe halisi wakija kura zimeshapigwa, nikasema hili ni tatizo kubwa sana hili. Ndio nikasema Wakuu wa Wilaya sasa kuna haja sana, na hii ninamuomba sana Mhe. Waziri tena sio peke yake akishirikiana na Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Idara yake ya Vizazi na Vifo, wafuatilie vyeti wanavyovitayarisha Wakuu wa Wilaya ni vyeti halisi? Isije wanafoji vyeti halafu wanatuletea matatizo, tumechoka matatizo jamani kwa nini hatuwezi kwenda kisheria.

Naomba sana Mhe. Waziri, hilo lichukue Wakuu wa Wilaya wana matatizo na kuna haja ya kuangalia upya je jukumu hili la kugawa vyeti bado waendelee kuachiwa wao au lirudi vizazi na vifo tukapige foleni kule kule.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naendelea ku-rese*r*ve kusema kuwa siungi mkono hoja hii mpaka kwanza nisikilize *response* ya Mhe. Waziri, Ahsante.

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Bismillahi Rahmani Rahim. Mhe. Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake wa kutufikisha hapa leo na mimi nikapata bahati ya kuchangia. Mhe. Naibu Spika, kwanza

nampongeza Waziri, kwa hotuba yake hii nzuri ya bajeti yetu ya mwaka 2013/14.

Mhe. Naibu Spika, mimi nikianza na mchango wangu mdogo tu, kwanza niko hapa katika ukurasa wa 3 ibara ya 9 sehemu ambayo inaitwa kwamba kustawisha au kuwafanya vijana wawe na maadili mema na mtazamo wa kujiajiri wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, kuna kujiajiri wenyewe na kuajiriwa. Sasa kwa bahati Zanzibar vijana wengi wanaojiajiri wenyewe na kazi za kujiajiri wenyewe Zanzibar kwa ruhusa yako naomba nizitaje hapa ili tuzielewe.

Mhe. Naibu Spika, kazi ya kwanza ya Zanzibar kujiajiri ni uvuvi, pili kilimo, ya tatu biashara ndogo ndogo na biashara zenyewe kuuza samaki, vitambaa, maandazi, machungwa, miwa, mihogo ya kuchoma, samaki wa kukaanga, hizi ndio kazi za kujiajiri wenyewe Zanzibar. Kazi za kuajiriwa ni kazi za maofisi, kama vikosi, majeshi na mengineyo, kazi hizi kama huna *diploma* huzipati, kwa hivyo kazi zinazopatikana za kujiajiri wenyewe ni hizi nilizozitaja hapa hizi hazina *diploma* wala hazina cheti wala madarasa makubwa.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, kwa vile nchi yetu ya Zanzibar haikuwa na mipango miji, kwa mfano tukichukua Matemwe tukajenga kila kitu pale soko tuweke pale, marikiti kubwa tuweke pale, hospitali tuweke pale hiyo hapana. Kwa mfano tukija Chumbuni tulijenge soko kubwa pale, tujenge Skuli pale, tujenge hospitali pale yaani mahitaji yote yako pale hapana. Lakini tokea ukoloni tunavyojua sisi soko kubwa la Zanzibar ni Darajani, anayetoka Matemwe anakimbilia Darajani, anayetoka Pemba Darajani, kwa hivyo kazi zote hizi hapa mkondo wake pale Darajani.

Kwa hiyo tukiwachukulia hawa vijana hawa wote wanaofanya biashara pale wamefuata mkondo wa watu, sasa lazima Serikali pale iwafikirie kwamba pale ndipo panapo biashara kubwa, angalau kama ingelikuwa tumefanya mipango miji ya kuweza wananchi wote kwa mfano kuna mtaa mmoja kule Nyarugusu, lingejengwa soko kubwa kule pia hospitali au skuli nafikiri watu wote wasingekuja Darajani, lakini Darajani ndipo pana soko kubwa. Sasa Serikali lazima iwafikirie vijana wale ili kuwapa motisha ya kukuza biashara zao, wakuze vipi pale Darajani sio kuwapiga bunduki, haisuluhishi, bunduki haisuluhishi mwananchi kutofanya biashara isipokuwa utamuumiza na utamvunjia maslahi na utamtia hasara.

Mhe. Naibu Spika, tuchukulie mfano mwananchi ameshakwenda Dubai maana sasa hivi tunakimbilia Dubai au China. Hebu tukaangalie kule Dubai

wenzetu mnapokwenda kuwafuata kule Dubai wamefanya vipi mpaka sisi tunatoka hapa kwenda Dubai au tunakwenda China, kwa nini sisi tujiulize kwa nini tunafuatia vitambaa China, kwa nini tunafuatia makopo, vijiko Dubai. Sasa tunasema tuna miaka 50 kesho kutwa ya Mapinduzi ya Zanzibar, wenzetu kwa kila inapofika miaka 10 wanafanya sherehe kuonesha maendeleo yao kwa vile vitu ambavyo wamevitengeneza wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, ukisema kwamba mimi nimeendelea kwa kutengeneza vitu vya nchi za nje hujaendelea, utengeneze vitu uoneshe vitu uoneshe kila mwaka au kila baada ya muda tumefanya vijiko, leo vijiko hapa hatuna, bado tunawafukuza vijana waliokwenda kuchukua vijiko kwa kuweka Darajani. Kwa hivyo ninaiomba Serikali tuwajengee mipango miji ili waweze kuuza biashara vijana bila ya kupata matatizo, tunawatia hasara vijana.

Mhe. Naibu Spika, mtu anakwenda kununua machungwa pakacha mbili Mwanakwerekwe anazileta Darajani, sasa pakacha mbili zile hapa kwetu masikini bado hatujawa na sindano za kuzuia uzazi bado watu wanazaa mpaka watoto kumi, watoto kumi aendeshwe na pakacha mbili zile. Anakuja Manispaa mara ya kwanza anachukua shilingi mia, wa pili anachukua shilingi mia mpaka anamaliza pale washakuja Manispaa kuliko watano wanachukua pesa za pakacha mbili.

Mhe. Waziri, hili jambo lazima lifikiriwe Zanzibar linawaumiza vijana mpaka sisi, kwa sababu na sisi tunategemea vijana wale wapate pesa watulishe. Sasa ikiwa pale pakacha zinachukuliwa na Manispaa, pakacha mbili achukue huyu, anakuja usiku hana chochote, anazipanga anasema du! Pakacha mbili zile nimenunua shilingi elfu tano, Manispaa kachukua ngapi, polisi kachukua ngapi mpaka anafanya hesabu anazikuta zote zimechukuliwa na polisi.

Mhe. Naibu Spika, ninakuja maandazi, kina mama wengi wa Zanzibar ajira zao ni maandazi, samaki wa kukaanga, na huku Serikali inasema inawapa mkopo wa JK na AK na nani, wakati samaki wa kukaanga wale wanachukuliwa na Manispaa wote analipa vipi, atawalipia kitu gani, ndio utaona Mhe. Spika, mikopo mingi Wazanzibari inawashinda kulipa kwa sababu biashara zao haziendi. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri hili jambo lifikiriwe sana, jambo linaumiza vijana, vijana wanaumia wanakula hasara, biashara wanakwenda kuchukua Dubai si kudogo, China si kudogo, China mbali, Dubai mbali, tena wanatumia kwa dola, dola moja sijui ukivunjisha sijui unapata elfu moja na ngapi sijui.

Mhe. Naibu Spika, hili jambo linatuumiza sana hapa Zanzibar, linatuumiza, vijana wanaumia, vijana badala tuwape njia za kujiendesha biashara kama uko uwezekano sasa hivi ikiwa tunaona kwamba mji utaingia uchafu basi

tuwajengee sehemu ambazo zinazofaa. Na kama hatuna sehemu zinazofaa za kuwajengea biashara watafanya wapi, kule pinda mgongo hakutambulikani hakuna hata pa kukaa na kila siku vijana wanazidi, pinda mgongo kushajaa, sasa kule pinda mgongo hata nafasi hapana, watakwenda wapi itabidi waende Darajani. Darajani ndiko kunako mkondo wa watu lazima wafuate pale na pale sasa hivi anakwenda Manispaa, anakwenda Askari anapiga bunduki, watakwenda wapi. Sasa hivi hii tunayosema hapa kwamba kuwajengea maadili basi mimi naona hatuwajengei maadili mema, kwa sababu itabidi wengine wasuke nywele wakatafute maadili watafanya nini? Maadili mema hayatakuja madhali sisi vijana hawana fursa ya kufanya biashara wanazojiajiri, tujenge au tuwajengee maadili ya biashara zao wauze kwa uhuru, sisi Serikali kazi yake kubwa itoe zile kodi zake kama kutwa moja shilingi mia tatu ili Serikali ipate kodi, lakini kijana anakwenda kuweka biashara pale, anakwenda kunyang'anywa tutakwenda wapi.

Namuomba turegeze kamba kwa vijana ili vijana wapate maendeleo, nguvu zetu sisi ni vijana, Serikali sasa hivi imeshakuwa na vijana wengi na ajira sasa hivi hakuna, sasa vijana hawa ndio wameshakuwa wanajiajiri, uvuvi ni ajira yao, kilimo ni ajira yao, biashara ni ajira yao, kuuza samaki ndio ajira zenyewe hizo kwa Zanzibar hakuna tena. Kutokana na ajira hizi ndio vijana watapata kutononoka, lakini vijana ikiwa leo wataekewa mtutu wa bunduki hawatononoki na tutakuwa hatuna maadili mema.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda kwenye ukurasa wa 53 *Diving Section,* Mhe. Naibu Spika, hii *Diving Section* ni kazi ya kuhami maafa kwa vile vyombo vinavyozama baharini, kwa hivyo vijana hawa Serikali lazima iwatunze, iwanunulie vifaa, tena iwatizame kwa hali ya juu. Kwa sababu Zanzibar ni nchi inayozungukwa na bahari, na kila wakati meli zetu hizi zinapata misukosuko, kwanza meli zetu ndogo, meli zetu zinaletwa Zanzibar ni ndogo na bahari yetu ni kubwa na wakati inapochafuka bahari tunaziona meli zetu. Kwa hivyo serikali ijitahidi kuweka vyombo vya kuweza kuokoa watu kwa mara moja, vyombo vya kuokolea hatuna, madeni tunayo lakini vyombo hatuna, zana za kuokolea hatuna. Kwa hivyo, niiombe serikali kupitia wizara, vijana wawekewe zana za kutosha na za uhakika.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuheshimu muda wako natilia mkazo sana tena sana vijana wenye kuuza biashara wasinyanyaswe, hakuna ajira hapa kama sio hizi kwa Zanzibar za kujiajiri wenyewe. Ahsante Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa na mimi nafasi ya kuchangia machache, nilikuwa tayari nimeshapeleka mchango wangu kwa maandishi lakini kwa vile nimepata muda naona bora nizungumze mwenyewe ili iingie kwenye *hansard*.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na watendaji wake jinsi alivyowasilisha hotuba yake hii.

Pili, naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Naibu Spika, mimi moja kwa moja nataka niende kwenye ukurasa wa 44 kifungu 144 kwenye Mkoa wa Kaskazini Pemba. Kabla sijaendelea na kutoa mchango wangu naomba nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa ufuatiliaji wake mzuri kwa shughuli mbali mbali na miradi ya serikali ikiwemo miradi ya barabara.

Mhe. Naibu Spika, hapa kwenye ufuatiliaji huu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba miongoni mwa miradi mingi waliofuatilia ikiwemo afya, elimu pia kuna na mradi wa barabara. Sasa hapa wenyewe walitaja kwamba wamefuatilia mradi wa barabara Wete/Gando na Wete/Konde. Mhe. Naibu Spika, katika ujenzi wa barabara hizi kuna kilio kikubwa cha wananchi wetu, kilio ambacho kuna wananchi wameharibikiwa na nyumba zao ambao hawakuwemo katika *list* za kuvunjwa nyumba zao katika upitishaji wa barabara. Lakini zimevunjika kwa sababu ya kupita vile vifaa vizito vya utengenezaji wa barabara hizo zimebomoka nyumba nyingi. Wananchi hao wanapokwenda kudai wanajibiwa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano watalipwa baada ya barabara kukamilika.

Mhe. Naibu Spika, umalizikaji wa hiyo barabara ya Wete/Gando na Wete/Konde unakatisha tamaa. Kwa nini niseme hivyo? Kwa sababu hata mkandarasi ameshaondoka kutokana na matatizo mbali mbali. Sasa naomba nimuulize Mhe. Waziri katika ufuatiliaji wao wa shughuli mbali mbali wameliona suala hili la watu wanaolalamikia majumba yao kuporomoka? Kama wameliona wameishauri nini serikali kuu kuhusu suala hili ili wananchi wetu wapate pahala pazuri pa kustirika. Kwa sababu mtu akikosa nyumba ni mtihani, mtu anajenga nyumba hiyo zaidi ya miaka minane haikamiliki, haitimii, sasa leo nyumba imeshakamilika inavunjika lakini malipo yanakuwa ni mtihani. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anifahamishe hilo.

Eneo jengine ambalo nataka kuchangia Mhe. Naibu Spika, ni Baraza la Mji wa Wete. Baraza la Mji wa Wete kuna mambo mawili, la mwanzo tulisikia kuna mfadhili Mhe. Naibu Spika, aliyefadhili utanuzi wa Soko Kuu la Mji wa Wete.

Suala hili ni la muda mrefu tumelisikia muda mrefu soko linataka kutanuliwa. Kwa sababu kama alivyozungumza Mhe. Abdi Mossi kwamba kuna watu

wanaotoka Makaani, Ole, watu wote wanakimbilia Darajani na watu wa vijiji vyote vya Wilaya ya Wete na vijiji vyengine wanakimbilia Wete kwenye soko kuu kutafuta rizki kwa kuuza biashara zao, lakini lile soko bado ni dogo halitoshi. Na tulisikia kama kuna mradi huu wa utanuzi wa soko hili. Sasa namuomba Mhe. Waziri anijuilishe mfadhili yule ni kweli amepatikana, ni mfadhili kutoka wapi na pamekusudiwa kutumiwa kiasi gani cha fedha ili kushughulikiwa soko lile na wananchi wetu wapate kujiajiri wenyewe wasisubiri ajira za serikali ambazo ni ngumu kupatikana.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine katika hilo hilo Baraza la Mji wa Wete kuna suala dogo nataka nilizungumzie. Kuna aliyekuwa Katibu wa Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake, ambaye alikosa uaminifu katika utendaji wake. Na hili silikosi kwa kufikiria, kwa kudhania au kwa sababu nimeambiwa na mtu. Suala hili tumelishuhudia wenyewe Kamati za Baraza la Wawakilishi tulipokwenda pale katika kufanya uchunguzi wetu tumeona kwamba katibu yule alitumia pesa kinyume na utaratibu ambazo hazihusu kuzitumia yeye. Ulifikia wakati kuna watendaji wake pale walimfungia milango. Kwa sababu wamechoshwa na zile jeuri zake. Sasa kwa bahati mbaya sana yule mtu baada ya kelele nyingi zilizotokea akahamishwa akapelekwa Wilaya ya Micheweni.

Na baada ya kelele nyingi za watu wenyewe Wilaya ya Micheweni akiwemo Mhe. Subeit Khamis Faki, Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni na wengine walivyosema wao pia hawamuhitaji kule kwa sababu yule mtu ni mharibifu, na katika Halmashauri ya Wilaya iliyokuwa inaongoza kwa ukusanyaji mzuri ni Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni. Sasa baada ya kupelekwa kule na wenyewe wakapiga kelele sina uhakika lakini nasikia kama na kule anataka kuondoshwa. Aidha kwa vile Halmashauri zetu bado za Wete na Mkoani.

Namuomba sana Mhe. Waziri mtu ambaye si muaminifu katika kuharibu mapato ya nchi yetu basi namuomba umuondoshe katika sehemu hiyo na usimpeleke tena katika Wilaya nyengine ili akaenda akavuruga zaidi.

Kuna mifano mingi tu iliyojitokeza, kuna walimu katika baadhi ya vipindi walikuwa wakifanya makosa katika maeneo yao, basi adhabu ilikuwa si kumtoa katika skuli ile ukampeleka kwengine, lakini unamtoa sehemu ambapo ukimpeleka atajua hapa mimi napewa adhabu ili aweze kujirekebisha na ule uharibifu uliotokea. Nakuomba sana Mhe. Waziri katika hilo, aliyekuwa Katibu wa Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake usitupelekee wilaya yetu na sisi hatumhitaji kwa sababu ya uharibifu ule wa kukosa uaminifu na Wilaya ya Mkoani vile vile kwa Pemba nzima, yule mtu mtafutie eneo jengine umpeleke ambalo halina makusanyo, ajue kwamba ule uchungu wa watu kukusanya pesa zinatakiwa zitumike kwa mujibu wa sheria sio ziende mfukoni mwake.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ambalo nizungumze haraka haraka ni eneo la vikosi vyetu. Eneo la uajiri ndani ya vikosi Mhe. Naibu Spika lina utata, wananchi wetu wanalalamika kiukweli kwenye ajira. Kwanza nakuomba Zanzibar ni yetu sote kila mmoja anasomesha watoto wake kwa nguvu nyingi, kwa pesa nyingi, linapotokezea jambo la ajira tusitumie mambo ya kisiasa kwa sababu watu wote ni wetu wenyewe. Wote ni wananchi wetu na wewe ni kiongozi wa watu wote. Kwa hivyo ajira zikitokea tafuta mtu ambaye ana sifa ya kupata ajira ile umpe ajira sio kama apewe huyu, huyu asipewe hilo linasikitisha Mhe. Naibu Spika.

Pia nimesikia tetesi sina uhakika kama ni kweli au si kweli, Mhe. Waziri atanitoa wasiwasi. Nimesikia kwamba kuna baadhi ya Wawakilishi wenzetu wamepewa nafasi tano tano wengine nne za kuajiri vijana wao ndani ya vikosi. Sasa nataka katika hili ututoe wasiwasi kama kweli hilo au si kweli.

Mhe. Naibu Spika, nataka niingie katika suala la vitambulisho kwa sababu vitambulisho ni uhai wa kila mtu, ni maisha ya kila Mzanzibari na ni haki ya kila Mzanzibari, basi kila tutakapopata nafasi tutalizungumza suala la vitambulisho kama lilivyokuwa likizungumziwa suala la *ICU* katika Hospitali ya Mnazi Mmoja likawa kero mpaka *ICU* ile ikapatikana. Kwa hivyo, na sisi tunaomba sana katika suala la vitambulisho msione kama ni kero, tunatetea haki za watu na kila mmoja lazima apate kitambulisho kwa aliyekwishafikia muda wa kupata kitambulisho.

Sasa katika hili Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri kila linapotokea kila suala la msingi hapa basi yeye pia huwa anajibu na anatoa maelezo mengi kuhusu vitambulisho vilivyoko ndani ya mawilaya ambavyo havijachukuliwa. Sasa kama sikosei katika kikao cha Januari Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la Mhe. Ussi Jecha Simai la nyongeza Mwakilishi wa Jimbo la Chaani lililotokana na swali la msingi la Mhe. Saleh Nassor Juma Nam. 78 alikiri kuwa ni kweli kuna vitambulisho vingi ambavyo wenyewe hawajaenda kuchukua lakini ukakiri kuwa ni wageni. Na akakiri pia katika majibu yake kwamba anafanya uchunguzi wa kina kabisa kufuatilia wale ni nani waliokwenda kuchukua vitambulisho vile.

Sasa swali langu kwa Mhe. Waziri, uchunguzi ule umefikia hatua gani na ni watu wangapi waliobainika kama ni wageni, lakini wamekwenda kupewa vile vitambulisho. Kama wamepatikana idadi ya watu wale, je mmewachukulia hatua gani wao kama wao. Na baada ya kuchukuliwa hatua wao je, wale masheha ambao ndio ngazi ya mwanzo kabisa ya kuwapatia watu vitambulisho mtu hawezi kupata kitambulisho kama hajapitia kwa Sheha je, atatwambia nini masheha wale walivyochukua juhudi mpaka wakawapatia

watu vitambulisho wakati si vyao na vikabakia kurundikana ndani ya maofisi ya wilaya kuitia hasara serikali yetu.

Mhe. Naibu Spika, pia nataka niendelee katika ukurasa wa tatu. Mhe. Abdi Mossi hapa alizungumzia kuhusu ajira ndogo kujiajiri wenyewe, sasa mimi nataka niache niingie katika kufanya vijana wawe na maadili mema. Mhe. Naibu Spika, vijana kuwa na maadili mema lazima serikali iwe makini.

Kwa hivyo, wizara yake kwa vile imeamua hapa kuwa hii ni moja ya shabaha ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni kuwafanya vijana wakawa na maadili mema, hapa ajipange Mhe. Waziri. Kwa sababu vijana wetu akitaka asitake maadili yamemong'onyoka, si wa kike si wa kiume. Sasa hebu jamani mfano mzuri unaigwa.

Mimi nakumbuka nilikuwa mdogo lakini nina kumbukumbu zangu, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume wazazi wetu hicho kipindi cha nyuma walikuwa wanavaa nguo fupi hata mtu kuinama kwenye watu hawezi na baada ya kutoa amri na kupiga karantini ya kuvaliwa nguo zile fupi sasa watu walibadilisha wakaanza kushona nguo refu zikaitwa meksi. Sasa kwa nini serikali hailitilii maanani hili wakaadhibiwa hawa vijana wetu wa kiume wanaovaa suruali ncha ya matako na wanawake wanaotembea uchi katika nchi yetu hii ya Zanzibar ambayo maadili ni muhimu. Tutalalamika maadili, maadili, lakini maadili kama hatujakubaliana wazee, viongozi, na serikali kwa jumla basi tutaendelea kuporomokewa na maadili halafu tukasikitika tumevamiwa na wimbi la maradhi, UKIMWI na mengineyo.

Mhe. Naibu spika, namuomba sana Mhe. Waziri katika hili turudini katika kulinda maadili ya nchi yetu na vijana wetu waendelee kuwa vijana wazuri ili tupate maendeleo ya nchi yetu. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kunipa fursa na mimi asubuhi hii ya leo niweze kutoa mchango wangu mchache katika hotuba hii ya bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu (*SW*) kuniwezesha asubuhi ya leo kusimama hapa kuchangia. Pili, Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuwasilisha vizuri hotuba yake na pia nimpongeze kwa ule uungwana wake. Kwa sababu Mwenyezi Mungu unapopata pahala padogo tu basi unatakiwa utoe shukurani, umshukuru Mwenyezi Mungu na umshukuru yule aliyekusaidia. Kama hutatoa shukurani basi utakuwa wewe hutekelezi zile ahadi za Mwenyezi Mungu za kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake.

Kwa hivyo, nimshukuru kwa kutimiza uungwana baada ya kumueleza kwamba Wilaya ya Micheweni mtendaji wa Katibu wa Halmashauri hatuna imani naye na akaahidi kuwa atalifanyia kazi na namshukuru kuwa amelifanyia kazi.

Jambo la pili napenda niipongeze kwanza Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwa ajili ya makusanyo mazuri katika utekelezaji wao wa kipindi kinachomalizia. Mhe. Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni katika makadirio ya kipindi kilichopita ilitakiwa ikusanye shilingi 77 milioni lakini mpaka kufika Machi imekusanya shilingi 65 milioni hivyo karibu imevuka malengo. Sasa nawapongeza sana na nawatakia waendelee na juhudi zao wasije wakawa mgema wakapunguza kasi na nguvu yao.

Lakini wakati huo huo kipindi kilichopita Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni waliahidi kujenga ukumbi wa mikutano uliokuwepo kwenye banda la mikutano kwa Shaame Mata, lakini nimeona kwamba katika kipindi hicho waliidhinishiwa kutumia shilingi 13 milioni kwa ajili ya kujenga ukumbi huo, lakini pesa hizo nimeona katika kitabu kuwa walitumia katika upimaji wa ramani na mambo mengine, kwa hivyo hawakuwahi kujenga. Kwa hivyo, nawaomba sana kama kipindi hiki tunachokwenda nacho bajeti hii wajitahidi sana tuone kuwa ule ukumbi umejengwa.

Kwa sababu unapoazimia kufanya kitu basi umalize kile kitu kukifanya, lakini sio umeomba pesa kwa ajili ya kufanya kitu kile halafu baadae usifanye. Sasa niwaombe sana huyo mtendaji anayekabidhiwa kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni basi ahakikishe kwamba lile suala linaendelezwa.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine nataka nizungumzie Mkoa wa Kaskazini Pemba, na mimi niwapongeze watendaji wa mkoa wetu, Mkuu wa Mkoa pamoja na watendaji wake. Lakini nimeona kuwa wamefanya vikao zaidi ya 15 vya ulinzi na usalama kuhakikisha kwamba katika mkoa wetu kunakuwa na amani, utulivu na ulinzi wao unakuwa mzuri.

Nimuombe Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba nimwambie kama katika mkoa wetu vitendo vya uhalifu vimeongezeka zaidi. Kwa sababu siku za nyuma watu walikwenda kuvamia Hoteli ya Panga ya Watoro, watalii wakatolewa wakawekwa nje watu wakachukua walichochukua wakaenda zao. Karibuni watu walikwenda wakamvamia mtu mmoja Tumbe na wakampora pesa zake na mapanga wakampiga matano, nani juzi tu, tumesikia kwamba kuna mtu kakatwa kichwa katika Wilaya yetu ya Micheweni kijiji cha Finya.

Sasa Mhe. Naibu Spika, naomba pamoja na kuwa nazungumzia Mkoa wa Kaskazini lakini naiomba Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar iangalie kama vitendo vya uhalifu katika nchi yetu vimezidi sana. Kwa hivyo, namuomba Mkuu wa Mkoa alione hilo na kama kuna kuimarisha ulinzi basi uimarishwe.

Nikiondoka hapo Mhe. Naibu Spika, na mimi nataka nizungumzie kidogo alipozungumza Mhe. Abdi Mossi. Mhe. Naibu Spika, serikali yetu kupitia MKUZA imepunguza umasikini kwa wananchi wa kipato na kuwaongezea kipato. Sasa Mheshimiwa katika nchi yetu kuna wasomi na waliokuwa si wasomi, na nchi haiwezi kwenda kwa wasomi watupu lazima wawemo wasomi wafanye kazi na wasiokuwa wasomi wafanye kazi. Sasa wananchi wetu wameitikia wito wa kujiajiri ajira za aina mbali mbali, kama alivyosema wanauza samaki, vitambaa, machungwa, njugu, zote ni biashara na wote hawa wanafanya kazi kwa ajili ya kuwa jioni mtu ajikimu kimaisha na watoto wao.

Leo Mhe. Naibu Spika, wale wanaojiajiri baada ya kuitikia wito wa serikali tunakwenda sasa tukiwabughudhi, tukiwaondoa, tukiwapiga Mhe. Naibu Spika, mambo mengine ni aibu sana na ni aibu sana kwa serikali yetu.

Mhe. Naibu Spika, aibu ya serikali kuvitumia vikosi kuvifanya vikosi vyetu vya SMZ wananchi wa Zanzibar wakose imani navyo ni aibu sana. Haiwezekani vikosi kwenda kwa wananchi wakavaa ninja au wakajitia masinzi ni aibu, Mheshimiwa serikali inafanya aibu. Askari wa serikali halali ambao ni walinzi wa raia na mali zao leo wanakwenda kwa wananchi wako unavaa ninja au wanajipaka masinzi na unakwenda kufanya ulinzi wa serikali halali ni aibu, aibu jamani tunafanya haiwezekani. Vikosi vyetu tunatakiwa tuvifundishe maadili mazuri, leo askari anakwenda kufanya ulinzi kwa raia wake anavaa ninja, wanaovaa ninja Mhe. Naibu Spika ni majambazi, mtu kama anakwenda kufanya ujambazi anavaa ninja au anajipaka masinzi asijulikane, lakini wewe unakwenda kufanya ulinzi kwa raia unavaa ninja jamani aibu gani hii tunayoifanya. Tena Mheshimiwa huwa nayaona mimi mwenyewe sihadithiwi, inatokea matokeo haya niko Darajani mwenyewe nawakuta askari wetu wamevaa ninja.

Mhe. Naibu Spika, tunatakiwa tuwafundishe askari wetu maadili mazuri. Leo unamfanya mwananchi akiona askari wake wa Zanzibar awakimbie badala ya kuwakimbilia. Raia wanatakiwa wawakimbilie askari wao wapate waone leo wanakimbilia kwenye usalama wangu, leo raia anakimbia askari. Mhe. Naibu Spika, mambo mengine ni aibu, vitendo vya uhalifu nchi yetu vimezidi sio pale Darajani tu, sasa hivi ukipita kwenye uchochoro kidogo mara unapigwa kabari, hawa askari wetu kwa nini hatuwatumii kufanya ulinzi wakawalinda wananchi. Ukipita kichochoroni unapigwa kabari unanyang'anywa simu,

mara unaporwa pesa, kweupe mchana. Mheshimiwa maadili yetu ya Zanzibar yameondoka.

Juzi kuna watu walimkodi dereva wa gari akawapeleka kwenye starehe zao Mesi wakaenda Mesi wanarudi saa nane za usiku walimgeuka dereva kufika juu pale Welezo walimwambia simamisha gari toa pesa ulizonazo zote. Jamaa yule katika kujihami akawapa ufunguo wa gari akakimbilia kwenye majumba ya watu, jamani nakufa niokoweni, nifungulieni mlango, hapana mtu wa kufungua mlango kwa sababu maadili yameondoka watu wanaona huyo anayekuja ni mwinzi tu na yeye. Hivi mtu anaonewa bwana, jamaa akapigwa mapanga akahasiriwa vibaya vibaya mno. Leo askari wetu badala ya kuwatumia kwa kulinda wananchi wetu tunawatumia kwa kwenda kupiga wananchi, Mheshimiwa ni aibu mambo mengine. Namuomba Mhe. Waziri mimi ni Mjumbe wa kamati hii ilikuwa sitaki kuchangia lakini mambo mengine yanatufanya tuchangie kwa hasira.

Mhe. Naibu Spika, kila siku mimi nasema tunapokuwa kwenye kamati wale watu wachukuliwe waelimishwe, wafunzwe kazi wanayoifanya wanaisaidia serikali pale kama serikali imejipanga vizuri itakusanya mapato unafikiri kiasi gani cha fedha tutazokusanya kwa siku, fedha ngapi tutazikusanya. Lakini badala ya kukaa tukapanga utaratibu wa kukusanya mapato tukapata mapato zaidi serikalini tunakwenda tukiwatimua tukiwachukulia vitambaa vyao.

Mhe. Naibu Spika, vitambaa askari wanavichukua kisha wanakwenda kugawana. Leo hii tukimuuliza Mhe. Waziri twende akatuoneshe ghala wanayovificha hana, au kama ipo ghala basi twende tukaoneshwe, lakini leo vitambaa vya watu vinachukuliwa, nguo za watu zinachukuliwa wengine washafungua maduka kwa vitambaa vya watu. Kama wanavyosema wengine wanakwenda kuchukua vitambaa China, Burundi, Dubai vikija pale badala ya kuuza askari wanakwenda kuvichukua halafu wanagawana, hawawatendei haki watu. Kama ni mtu kataifishwa kitu kinawekwa kikapigwa mnada na serikali kitu kile kikaenda serikalini, lakini sasa kitu kile kinachukuliwa kinataifishwa ikisha watu wanagawana haya mapato gani yanayopatikana kwa serikali kama wanagawana wao?

Halaf,u Mheshimiwa ni kosa askari kuvaa ninja usivae ninja! Kwa nini wavae ninja hakuna sheria inayoruhusu kuvaa ninja kwenda kunako raia. Halafu pia nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, bado namuomba tena kwa heshima na taadhima akae nao wale watu wawaelimishe kwa utaratibu, wawatafutie sehemu wawaweke wafanye biashara serikali ipate mapato lakini sio wafukuzwe halafu askari wanakwenda pale wanapiga mabunduki. Mimi nipo hivi yanapigwa mabunduki baadae wale watu mtawatoa imani, mkiwatoa imani itakuwa sasa wavaane na askari watupiwe

mawe. Mhe. Naibu Spika cha msingi tunachotaka nchi yetu iwe na amani isiende hivyo, na kama wananchi wajiajiri basi wamejiajiri tuwasaidieni fikra na mawazo, serikali pale iwasaidie kuwapa mapato. Mheshimiwa hilo naliacha nakwenda kwenye suala la vitambulisho.

Mhe. Naibu Spika, suala la vitambulisho watu wakizungumza kila siku hapa hatulalamiki tu watu wanasema kwa kuona kwamba haya mambo yanafanywa. Mhe. Naibu Spika, labda kuna siri fulani hebu tuambiwe hii siri iliyopo kuhusu vitambulisho. Leo tunazungumza na waziri, tunakaa na waziri, tunakaa na Mkurugenzi wa Vitambulisho tunazungumza vizuri tukishaondoka pale wanabadilika, sasa ni sawa sawa na kuwa labda tukishatoka huku wanapewa mafunzo mengine, haiwezekani Mheshimiwa.

Kwa sababu wananchi tunapopiga kelele watu wanaposema kama kuna sheria inayowabana wananchi serikali ikubali kuifanyia marekebisho kwa nini inakataa kuifanyia marekebisho na wananchi ni haki yao. Sasa Mheshimiwa mimi nasema kama wananchi wa Zanzibar kwa sababu sheria inasema kama mtu hana kitambulisho ashtakiwe afungwe mwaka mmoja au atoe faini, na ikiwa tumeshaona hawa wananchi wa Zanzibar waliokuwa wamezaliwa mfano mtoto niliyemzaa mimi ikiwa hana sifa ya Uzanzibari basi achukuliwe akawekwe kwenye kisiwa wahamishwe hapa wakapewe kisiwa chao wakae. Si Wazanzibari hawa hawana haki hapa basi wakawekwe kwenye kisiwa huko baharini wakae baharini.

Lakini leo tunawakosesha watu haki zao kama sheria ina mapungufu na irekebishwe kwani kwa wao zito kurekebisha. Leo Mheshimiwa tuna orodha hizi za majina na huyo Mhe. Waziri keshapewa barua, kuna watu wa Nungwi 408 wana vyeti vya kuzaliwa kila kitu washakamilisha lakini vitambulisho hawapewi, kwa nini na wana vyeti hawa? Kuna watu Pale Mkwajuni watu 307 wana vyeti vya kuzaliwa kamili lakini vitambulisho kuvipata ni uzito, kuna watu wa 71 wa Mkwajuni wana vyeti washapiga picha kila kitu tayari vitambulisho kwa sababu daftari liko wameshindwa kupewa.

Mkurugenzi alitueleza kama wiki mbili watu wapewe sasa hivi ukisema unaambiwa kuna vitambulisho vingi vimekusanyika watu hawajavichukua. Sasa hivi mtu jamani ikiwa kafanya kosa mtu huyo ahukumiwe huyu, kuna watu kama vitambulisho vyao hawajavichukua hawavitaki hao, lakini kuna watu wanaovitaka wana haki na wanakuja hawapewi ndio wanazuiliwa mpaka vichukuliwe hivyo? Ndio sababu mnayotupa kila tukizungumza mnatwambia kama kuna vitambulisho havijachukuliwa sawa, havijachukuliwa lakini hao wanaotaka kuchukua wazuiliwe wao?

Mhe. Naibu Spika, naomba tuwe wakweli na tuwe wawazi, bado hatujawa wakweli wala hatujawa wawazi hapa. Tukija mnatwambia tunalalamika, anayelalamika kapigwa fimbo imempata kama hajapigwa mtu halalamiki, hata mtu akilalamika keshapigwa. Sasa sisi tunalalamika kwa sababu watu wanakoseshwa haki zao hatusemi tu hivi kichwa mchungwa, tukija tunakuja na ushahidi humu, tunasema kwa ushahidi kila siku, lakini tunasema hata tukishasema mnaona wale hawana akili mnakwenda kupanga vyengine, haiwezekani hivi. Mimi nasema kuna mpango maalum haiwezekani.

Hawa masheha wakishaambiwa tukishapanga pamoja labda wanarudi wanawaeleza vyengine, haiwezekani hivi jamani kwa nini hatuambiani ukweli? Mhe. Naibu Spika, kila siku tunapiga kelele suala hili, kama serikali inaona hili suala lina matatizo kwa nini haituletei sheria hapa tukaifanyia marekebisho likaondoka tatizo hilo kila mtu akapata haki yake.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na naomba nimalizie hapo.

Mhe. Salma Mohammed Bilali: Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya na kunipa uwezo wa kusimama mbele ya Baraza hili tukufu leo na kuchangia angalau machache katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba hii. Mhe. Naibu Spika, pia naomba uniruhusu nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutayarisha na kutuwasilishia hotuba hii adhimu ambayo leo hii tunaendelea kuichangia.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa utaratibu wake aliouandaa kwa kuaandaa ufupisho wa utelezaji wa maagizo ya Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu waliyotoa katika Bajeti iliyopita. Utaratibu huu Mhe. Naibu Spika, utasaidia katika kupata ufafanuzi wa mambo aliyoulizwa Mhe. Waziri kwa niaba ya wananchi na wananchi hao wataridhirika kabisa na utaratibu huu na Mhe. Waziri huu ndio Utawala Bora.

Mhe. Naibu Spika nakwenda moja kwa moja katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja. Mhe. Spika, naomba kwa dhati kabisa mimpongeze Mhe. Mkuu wa Mkoa wa kusini pamoja na watendaji wake kwa utekelezaji wao mahiri wa ilani ya Chama cha Mapinduzi katika kuwaondoshea wananchi wa Mkoa wa Kusini kero mbali mbali zinazowakabili kama Maji safi na Salama huduma ya Afya na mambo mengine ambayo ni kero kwa wananchi wa Mkoa wa Kusini.

Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri katika bajeti ya mwaka uliopita hadi kufikia Machi mwaka huu ni asilimia 65 tu ya fedha walizoomba ambazo wamepatiwa. Mhe. Waziri naomba ujitahidi sana katika kuwakamilishia Bajeti zao mapema ili waweze kutekeleza vizuri maagizo ya wananchi na kuwaondolea kero zao mbali mbali ambazo zinakuwa zinawakabili.

Mhe. Naibu Spika, pia niipongeze kwa dhati kabisa Ofisi ya Vitambulisho vya Usajili wa Mzanzibari kwa kazi yao kubwa na nzuri wanayoifanya ya kuwapatia vitambulisho wananchi wa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, pia nitoe ombi kwa viongozi wenzangu kwamba tuwashajihishe wananchi wetu wanapokwenda kuandikisha waende wakavichukue vitambulisho ambavyo bado vinarundikana katika Wilaya zetu, na pia niwaombe wananchi Wazanzibari wote ambao wameshafika umri na wameshaandikishwa wakimaliza taratibu za uandishaji waende wakavichukue vitambulisho hivyo, wasikae tu kulalamika na viongozi pia ni jukumu letu kushajihisha na kwenda kushajihisha katika majimbo yetu na Shehia zetu ni wangapi ambao vitambulisho vyao pale vipo na wao washajihishwe wakavichukue.

Mhe. Naibu Spika, napenda pia kupongeza kwa dhati juhudi zinazochukuliwa na kikosi cha Zima moto na uokozi kwa mkakati wao wa kuboresha huduma zao. Mhe. Naibu Spika, pia nina masikitiko makubwa kwa kikosi cha Zima moto cha *Airport* Pemba.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Mara zote ambazo tunakwenda Pemba tunawakuta vijana wale wako katika mazingira magumu, mabaya hayastahiki vijana kama wale ambao ni vijana wetu askari wetu tunawategemea katika shughuli zetu mbali mbali, lakini mazingira yao hayaridhishi.

Mhe. Spika, naomba ufanye juhudi za makusudi kuwatafutia eneo na pia kuwajengea jengo lenye hadhi ya vijana wale. Mhe. Naibu Spika, naomba sana kwa sababu wakati wa mvua wanakuwa katika hali ngumu, wanapoishi wanalala hapo hapo, jikoni hapo hapo. Lakini wakati wa mvua wanakuwa hawawezi kupika na wakitaka kupanda vitandani lazima waweke matofali ya kufikia katika malazi yao. Mhe. Naibu Spika, naomba ufanye sana juhudi za makusudi ili uweze kuwapatia makaazi bora vijana wetu hawa.

Mhe. Naibu Spika, mwisho nimalizie kwa vikosi vyetu vya SMZ. Mhe. Naibu Spika, nakuomba sana uvitizame kwa jicho la huruma vikosi vyetu hivi vya SMZ vikosi ambavyo tunavitegemea sana katika kutuwekea usalama wa nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, naomba uangalie kwa jicho la huruma katika

kuwaongezea kipato cha mishahara vijana wetu hawa ili waweze kulingana na kazi ambazo wanatufanyia katika nchi yetu hii.

Mhe. Naibu Spika mengi yameshazungumzwa na mimi angalau ilikuwa nitoe mchango wangu mdogo. Kwa hivyo, kwa niaba ya Wanawake wa Mkoa wa Kusini Unguja naumga mkono hoja asilimia mia juu ya mia. (*Makofi*).

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nikushukuru na wewe kwa dhati na mimi kunipa nafasi ya kusema machache sana kwenye hotuba hii ya Mhe. Waziri.

Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri na timu yake ambayo timu mahiri. Niwashukuru pia na Waheshimiwa Wajumbe waliotangulia kuchangia wamefanya kazi nzuri.

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba sana utuvumilie kwa sababu hii ni Ofisi nyeti ya Mhe. Rais. Bahati nzuri kuna mambo yamewekwa hapa kwenye Ofisi hii, nilishawahi kusema mara nyingi ingefaa mengine yakaondolewa hapa kwa sababu hii ni Ofisi takatifu, bahati mbaya hilo halijasikilizwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitaanza na Serikali za Mitaa, kwenye kitabu hichi cha Mhe. Waziri amekiri kwamba ili maendeleo ya haraka na yale endelevu ni kupitia Serikali za Mitaa. Lakini akasema hadi sasa tatizo liliopo ni wataalamu wa kuzisimamia Serikali hizi, kwa kufanya hivyo watakosa kukusanya mapato na matumizi ya fedha kwa nidhamu.

Nilichotarajia hotuba itaendelea kusema kwamba mikakati ipi ya muda mfupi na wakati na ule mrefu, kwa sababu tunataka maendeleo endelevu yametandikwa na Serikali ili kuziwezesha Serikali hizi kufanya kazi zao zilizokusudiwa.

Matokeo yake hotuba imechupa na kutaja makusanyo na mapato najiuliza mimi makusanyo, mapato na matumizi hayatawezekana tena nimesema haitawezekana kufanya hivyo, kwa sababu ya kukosekana wataalamu. Wataalamu hawakutajwa tena pametajwa balaa chungu tele.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri Mhe. Rais amekupa Ofisi yake kwa kukuamini sana na kakupa wataalamu mimi nawaheshimu sana. Lakini yanayoendelea yanakatisha tamaa. Si vyema wala haifai tunaposimama ikawa kila siku tunazungumza hilo hilo, tunafika mahali tunasema ni dharau, tunafika mahali tunasema Serikali inajisifu, jee inastahili hii sifa ya usikivu au kuna watu kwa makusudi wanaitia doa hii Serikali.

Mhe. Naibu Spika, ni lazima tuheshimu lakini tutendee haki za watu, nchi hii si ya mtu fulani wala chama fulani wala taasisi fulani. Nchi hii ni mamlaka ya wananchi ndio wenye madaraka ya kuiweka Serikali yao wanayoitaka wao, kumchagua wanayemtaka wao.

Si masuala mengine ya fursa kuteka mtu nyara akaona ana nafasi ya kufanya mabadiliko hayo hayapo tunakwenda kwa mujibu wa Katiba yetu hii ya mwaka 1984 kuna sheria, kanuni na taratibu tunaziheshimu wenyewe. Mhe. Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo.

Mhe. Naibu Spika, kuna kitabu hichi hii ni taarifa ya Kamati Teule ya Baraza hili. Baraza lililowekwa na wananchi wenyewe tuliomo humu ni watu wazima na tunalipwa na wananchi kuwatendea kazi zao. Moja kati ya hizo ni kusimamia Serikali yao iweze kufanya yale ambayo imeahidi.

Mhe. Naibu Spika, kwa ufupi sana taarifa inaeleza mapungufu kadhaa. Kuhusu Manispaa ya Zanzibar jinsi kwa kuvunja kwake kwa sheria, kanuni. Lakini pia humu mna maelezo ya ubadhirifu wa fedha za umma iliyofanywa na Mkurugezi aliyepita. Mie nawauliza Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hivi *iliyopita si ndwele*?

Mhe. Naibu Spika, namuuliza Mhe. Waziri anayo haki ya kusimama kudai fedha nyengine endapo hizi zilizofujwa na kuharibiwa haijatolewa taarifa yake na Serikali. Jee, anayo haki Mhe. Waziri kusimama mbele ya Baraza hili akadai fedha nyengine ilhali hizi tulizomuidhinishia mwaka uliopita zimevurugwa na mpaka leo hazina maelezo, nataka anijibu hapo.
Mhe. Naibu Spika, pamesemwa kwa hasira na uchungu vitendo vya Askari wa Manispaa. Wale ni Wazanzibari, wale ni binaadamu, wale vijana wanaokaa pale, tunahangaika kuwasaidia wenyewe wanajituma kuepukana na aibu na fedheha na mambo yasiyojuzu binaadamu kuyafanya.

Kwa nini Serikali ifanye kitendo cha kukatisha tamaa. Mhe. Naibu Spika, yale matendo yanayofanywa pale wengine wamechukua hatua mbaya sana na wengine walichukua hatua kubwa nashindwa hata kutaja maana nna hasira sijiwezi namuomba Mwenyezi Mungu anisaidie.
Mhe. Naibu Spika, amechukua mkopo kijana amekwenda alipokwenda kaleta vitambaa vyake wamekuja vyote wamevichukua kesho ni mwezi wa Ramadhani. Mhe. Waziri wewe ndiye *mas-ul* haya ndiyo unayoyasimamia. Mimi nataka majibu tu haya ndio unayoyasimamia?

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri nataka anijibu Manispaa na ubadhirifu anijibu vitendo vile vinavyoendelea kufanywa na askari wako wa Manispaa

kwa vijana wale. Sitaki hadithi ya wapi kule walipokwenda wao kwenye mikeka mibovu wakajenga banda moja wakawapa wanaowataka na wengine wasiwape ikiwa ndio sababu.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni Vikosi vya SMZ. Mhe. Naibu Spika, imani ya Wazanzibari hivi ni vikosi vyao hebu tujiulize ni kweli askari atalishwa mkate mmoja wa boflo mdogo pale asubuhi na kibabuli cha haragwe alipwe mshahara shilingi 140 na hizo hizo akatwe aambiwe kuna michezo, stahili yake hapati, lakini pia ili posho ya nyumba haimo na siku anayopewa anapewa shilingi elfu kumi.

Mhe. Naibu Spika, wale vijana wa KMKM siku za msimu wa karafuu yanayotendeka ili wapelekwe kule Pemba hayajuzu na wanayakubali masharti katika hali ya umasikini mkubwa. Mtu anasamehe mshahara miezi mitano na ndio maana zinakamatwa karafuu majahazi kwa majahazi wenye karafuu hawapatikani. Hivi kweli hatujajiuliza kulikoni ni kwa sababu ule umasikini tunaowalazimisha vijana wale nafasi pekee ya kujisaidia ni ile ya kumsamehe mwenye karafuu wakachukua wao karafuu. Hivi tunawafanyisha kazi halali.

Mhe. Naibu Spika, hii ni bajeti, na kanuni inatulinda na nimeomba mapema ni Ofisi kubwa nakuomba sana. Mhe. Naibu Spika, sisi ni wazanzibari tumekubali wenyewe mfumo gani twende nao, tukakubaliana mfumo wa vyama vingi kwa staili gani, kura moja mtu mmoja atakayeshinda aheshimiwe.
Mhe. Naibu Spika, sitaki niende mbali katika vyama vingi kuna kuvumiliana lakini pia kuna kuheshimiana Wazanzibari wameamua na wakakubaliana kikatiba ni hii Katiba ya Zanzibar atakayeshinda ataunda Serikali lakini Serikali hiyo itaendeshwa kwa mfumo wa Kitaifa. Hivi iweje wengine kujifanya wao ndio wao, mwenye madaraka baada ya wananchi wakawapora wao na wengine hawana haki hiyo? Tendo hilo ni kuonesha dharau.

Si dharau tu ni kuanza kutuletea harufu ya vurugu, mtengemano mpya kama wamezoea hayo wenyewe wamesema basi tunawaomba sana viongozi wa watendaji ambao hawakuridhika na mfumo huu wengi wameridhika waheshimuni. Wale wengi wameridhika kwa hivyo mwanasiasa aliyeiva huheshimu maamuzi ya walio wengi.

Mhe. Naibu Spika, wanafika mahali wanauliza masuala hata hayauliziki. Kwa kumuona mtu huko aliko labda watu wanamtamani wenyewe wamempenda anakerwa na hilo, ni haki ni maamuzi yake. Mhe. Naibu Spika tulipoanza Semina *Zanzibar Beach* Waheshimiwa wako hawa walianza kwa kutoa mifano mingi kukazia yale aliyoyazungumza, Wajumbe wakatoa misemo na

tungo kukazia. Mimi nakuomba muda wangu uliobaki nimalize kwa kumkumbuka marehemu Siti binti Sadi kwa sentensi moja alisema:

" Ndani ya hii dunia mambo matatu kwa mja huwa ni neema kwanza ni uzima, lakini si kitu tatu ni bahati kupendwa na watu, bahati ya mwenzio usiifungulie mlango wazi, hupendwi kama hujajipendekeza, hubahatiki kama hujabahatisha na kitu kile si kile cha kutoa kilichotajwa hapa".

Mhe. Naibu Spika, ni kama kinaa cha moyo huyo ndie Seif Sharif Hamad wale walioiuliza sababu nawajibu haya Mwenyezi Mungu ndie aliyemjaalia. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*).

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia machache katika hotuba hii ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Pia nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote, pia nivishukuru vikosi vya SMZ kwa kazi kubwa za kuimarisha ulinzi katika visiwa vyetu. Pia na taasisi zote zilizo chini ya Ofisi ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais na Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, kama ulivyokwisha kunambia kwamba tutizame wakati na kwa bahati wakati ni kitu muhimu na hasa pale Mwenyezi Mungu aliapa na sura ile ya "*Wal-asri*".

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi niende na ukurasa wa 8 ambapo Mhe. Waziri alisema kwamba Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imekuwa ikiendelea na juhudi za kuimarisha usafi katika Manispaa ya Zanzibar, ambapo utaratibu maalum utaandaliwa kusafisha mji wakati wa usiku kuwezesha mji kuwa safi.

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, wenzangu wameshasema na hasa tukitizama eneo la Marikiti pale kwamba kunatupwa taka, na taka zile zinanuka na ikiwa ni mji wetu huu pale ndio kioo cha mji huu. Kwa kweli, Mhe. Naibu Spika, hili ni tatizo kubwa. Vile vile napenda nichukue nafasi hii kukisoma kifungu namba 22, kinasema kwamba:

> “Baada ya kuonesha mafanikio makubwa mbali ya majaribio ya uwekaji wa taa za barabarani zenye kutumia nguvu za jua ambao ni ufadhili kutoka Serikali ya Jamhuri ya watu wa China”.

Na sasa hivi anataka kuingia mradi wa pili ambao utajumuisha barabara za maeneo mengine ikiwemo pamoja na eneo la jimbo la Amani.

Kwa kweli mimi najiuliza na hapa namuuliza Mhe. Waziri kwa sababu zile taa ambazo zimewekwa maeneo ya kuanzia Darajani hapa kwendea Michenzani zimeshaanza nyengine kuwa hazifanyi kazi. Je. Mhe. Waziri Serikali imejipanga vipi kuwapa taaluma mafundi wetu ili wakiondoka wale mafundi wa kichina iwezekane kuwa jambo hili liendelee. Kwa hivyo, nimeona kwamba pale taa sasa zimeshaanza kuharibika kama taa tatu ukipita maeneo ya Michenzani hazifanyi kazi.

Vile vile Mhe. Waziri kwenye ukurasa kutoka kumi na mbili mpaka kumi na sita hapa ameeleza mengi kuhusu ziara za Mhe. Rais ambayo alionana na viongozi wengi mbali mbali na pia kupata ushauri na fursa mbali mbali za kuzungumza nao. Lakini sasa niulize Serikali inatumia ushauri ule vipi na inazitumia vipi hizo fursa ambazo walizokaa na viongozi mbali mbali.
Mhe. Naibu Spika, pia nikienda kwenye ukurasa namba 17 kwenye hiyo hiyo utangulizi wake Mhe. Waziri amesema kwamba kifungu namba 40 kinasema:

"Ofisi iliendelea kuimarisha Ikulu na Mnazi Mmoja kwa kujenga na kuimairisha jengo jipya linalojumuisha stoo, ofisi katika Ikulu ya Migombani, mashine tatu za vipoza hewa".

Mhe. Naibu Spika, mimi niende katika hili jengo ni kwa kila muda gani ambapo Mhe. Waziri majengo haya yanafanyiwa ukarabati.

Vile vile nikiendelea kwenye ukurasa namba 19 Mhe. Waziri amesema kwamba katika Ofisi ya Faragha hii mwaka 2013/2014 kuna kifungu kidogo cha 4 kujenga uwezo kwa wafanyakazi 6 katika ngazi za Stashahada na ngazi, watatu ngazi ya Cheti. Nimuulize Mhe. Waziri wanawake wangapi na wanaume wangapi.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na ukurasa namba 28 pia Mhe. Waziri amesema Zanzibar imeshiriki kikamilifu katika mkutano wa kikanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuhusu Jumuiya ya Maendeleo ya nchi ya Kusini mwa Afrika *SADC* na Mkutano wa nchi zinazozungukwa na bahari ya Hindi.
Idara kushirikiana na Wizara za SMZ itafuatilia maamuzi ya vikao kwa manufaa ya Wizara ya Mifugo. Lakini vile vile hapa imesema kwamba Ofisi inaendelea kufuatilia hatua za mwisho za kuanzisha Taasisi ya Kiswahili ya Juimuiya ya Afrika Mashariki.

Nimuulize Mhe. Waziri kwamba kuna taasisi nyingi na hasa ile taasisi ya *EACROTANAL* ambayo ilianzishwa miaka ya nyuma huko na sasa hivi sijui kama inaendelea au vipi, lakini nina wasi wasi kwamba kazi zake sasa ziko, lakini sijui hata hao wanachama kwamba wanaendelea kuisaidia. Kwa hivyo,

wamejipanga vipi kuhusu suala hili la kuanzisha jumuiya ambayo inaanzisha taasisi ya Kiswahili.

Vile vile Mhe. Waziri kwenye ukurasa wa 29 kwenye Idara hii ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nje, ambayo ameeleza hapa pamoja na hili la kuanzisha Jumuiya ya Kiswahili. Kuna kifungu 79, naomba nikinukuu;

Kifungu 79

"kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo.

79(1)

Kuhakikisha kuwa Zanzibar inashiriki kikamilifu katika mikutano mbali mbali ya kikanda na kimataifa.

Kuwashajihisha Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii".

Mimi nimuulize Mhe. Waziri serikali huandaa vipi kushiriki kikamilifu katika mikutano mbali mbali ya kimataifa na kitaifa. Namuuliza Mhe. Waziri swali hilo ili niweze kujua.

Mhe. Naibu Spika, nikimalizia niende kwenye suala la wafanyabiashara wadogo wadogo. Zamani kama wenzangu walivyotoa historia hapa. Zamani ilikuwa mfanyabiashara mdogo mdogo ni lazima akapimwe, lazima awe na kisanduku cha kuuzia ile biashara, lakini sasa hivi inaonekana hili jambo limepotea. Kwa hivyo, nimuulize Mhe. Waziri je, suala hili wanalichukulia vipi kwa sasa hivi na hasa tukijua kwamba kuna matatizo mengi ya kiafya.

Vile vile nikienda kwenye hii mamlaka ya serikali za mikoa, kuna udhibiti huu wa wanyama, lakini kuna unyanyaswaji mkubwa wa wanyama. Sijui na hili pia wameliandaa vipi ili kuondoa usumbufu wa kunyanyaswa kwa wanyama.

Pia niende kwenye ukurasa wa 41

Mhe. Naibu Spika: La kumalizia hilo Mhe. Mjumbe.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nimalizie hapa. Mhe. Waziri amesema kwenye kifungu nambari 118 kwamba mwaka 2013/2014 Mkoa wa Mjini Magharibi unatarajia kutekeleza malengo yafuatayo. Kuimarisha kiwango cha utendaji wa wafanyakazi wa Mkoa wa

Mjini Magharibi, kuimarisha hali ya ulinzi na usalama ndani ya mkoa, kuhakikisha jamii yenye afya njema na kuhakikisha maendeleo endelevu ya jamii.

Mhe. Naibu Spika, nimuulize Mhe. Waziri ni kwa namna gani ndani ya hali ngumu ya maisha ya watu wasio na ajira maendeleo endelevu yanapatikana? Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi).*

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Allah Subhanahu Wataala kwa kunijaalia na mimi nikaweza kupata nafasi hii juu ya masikitiko mengi. Mhe. Naibu Spika, katika watu wa mwanzo tarehe 28/06/2013 asubuhi tulioomba, Mhe. Mwenyekiti, aliyekuwepo hapo alisema ana watu 22 na sisi tukaomba muda huo. Lakini hatima yake leo tukafikia kuwa watu wa mwisho wa wachangiaji. Kwa kweli hili ni masikitiko kwa kiasi fulani, tunaomba sana utaratibu ujaliwe sana kufuatwa ili aliyeomba mapema basi haki ile aweze kuipata na mapema, ahsante.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitaanza kwenye mchangio wangu, japokuwa wenzangu wengi wameeleza, mimi nitakwenda kwa muhtasari tu. Katika ukurasa wa 3 kifungu cha 9. Mhe. Naibu Spika, hapa Mhe. Waziri ameelezea mambo mbali mbali katika shabaha ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kuna mambo matano pale ameyaelezea. Katika hayo matano mimi swali langu ni la kwanza na la pili, lakini sio swali.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri anieleze ni vikao vingapi ambavyo alivifanya na maeneo gani aliyowahi taasisi yake kukaa na vijana, kuwapa hizi taaluma na mafunzo ya maadili mema. Ni maeneo gani na ni vijana gani aliyewapa. Lakini pia hawa vijana wanapojiajiri kwa kupitia mitaji yao mbali mbali. Hawa vijana wanakopa pesa benki na mashirika mengine ili kuweza kumudu maisha yao na familia zao.

Je, ni sheria gani inayoelezea vikosi vyetu kwenda kuwavamia vijana hawa na kuwapora biashara zao. Naomba nipate maelezo ya kina ili tuone kwamba wanaofanya vikosi sio tatizo bali vijana ndio wenye matatizo. Naomba ufafanuzi Mhe. Naibu Spika.

Nikiondoka hapo nije katika ukurasa wa 5 kifungu cha 13 kuadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi. Lakini na mimi nieleze kwamba ni kweli baada ya Mapinduzi hadi kufikia mwaka unaofuata tutatimiza miaka 50. Mhe. Naibu Spika, mimi mara nyingi huwa najiuliza, maendeleo ya miaka hii 50 ya dhati kabisa ambayo ni kiyo kwa Wazanzibari nashindwa kuyaona.

Mhe. Naibu Spika, miaka 50 tumeshindwa hata kutengeneza ile *choral* ya kibiriti, hiki ni kilio. Miaka 50 ya uhuru Zanzibar hatuna *choral* ya ujiti wa kibiriti tumeshindwa kutengeneza. Kwa sababu Wazanzibari kwa asilimia kubwa ni wakulima, wakulima wetu wanalima mihogo, ndizi, viazi na mambo mengine. Lakini tumeshindwa kutengeneza hata biskuti ya viazi vitamu au ya ndizi au ya muhogo ndani ya miaka 50.

Kwa hivyo, Naibu Spika, mara hii serikali imekusudia kutumia bilioni moja kwa sherehe ya haya Mapinduzi, lakini hali ya nchi ukitizama badala ya kupiga hatua mbele ya maendeleo ndio kwanza nchi inarudi chini kimaendeleo na wananchi hali zao zinakuwa duni zaidi. Kwa hivyo, naomba mambo haya ni lazima tuyatizame maendeleo ya wananchi wetu. Viwanda ni muhimu, wananchi kuweza kupata ajira ni muhimu, lakini yote haya yamekosekana.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni hawa wana Mapinduzi kila tunavyokwenda historia inakufa. Kweli Rais wa mwanzo ni Jemedari wa Mapinduzi, lakini Waswahili wanasema *kidole kimoja hakiwezi kuvunja chawa*. Kwa hali yoyote ilikuwa kuna waandamizi waliokuwepo chini ya huyu bwana, lakini hawa wote waandamizi wamesahaulika hawatajwi kwenye vyombo vya habari wala kwenye magazeti wala kwenye maeneo mengine yoyote. Kwa hivyo, sisi vijana tuliokuwa hatukuyaona hayo Mapinduzi, tunashindwa kufahamu wapinduzi ni nani na nani. Kwa hivyo, ningeiomba sana serikali hao waandamizi watajwe ili vijana waweze kuwakumbuka na kuwafahamu ni nani wazee hao waliotufikisha katika maeneo haya tuliyonayo. Tusiendelee tu kuiua historia ya Zanzibar na wananchi wetu wakakosa kuijua. Kwa hivyo, ni muhimu sana wazee wetu hawa waliopigana kina Mzee Thabit Kombo na wengine wakaweza kutajwa katika vyombo ili kizazi kilichopo wakaweza kuwafahamu wazee wao wa Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende katika ukurasa wa 52 hadi 61 pale

Mhe. Naibu Spika: Dakika mbili zimesalia.

Mhe. Rufai Said Rufai: Nakuomba sana hata hizo dakika mbili na nusu sitapata, lakini nitajitahidi. Mhe. Naibu Spika, kuna vikosi vya ulinzi. Mhe. Naibu Spika, vikosi hivi kwa Zanzibar tuna vikosi vyetu vitano na hivi vikosi tunashukuru kwamba vinafanya kazi zake vizuri, lakini vimekosa matunzo Mhe. Naibu Spika kuna baadhi ya vikosi hasa hawa ndugu zetu wa chini ukiwatizama katika mavazi yao, chukua kikosi cha Idara ya Chuo cha Mafunzo, wale ambao wanashinda kwenye kazi na wale waliomo katika mafunzo, wafungwa, *uniform* zao zimechachuka hazifai hata kidogo, jasho na viatu. Maana ile hali yake ukimtazama kwa kweli haridhishi *uniform* zao.

Ukitizama katika bajeti, bajeti imepangwa, lakini miaka mitano iliyopita mwaka 2010/2011 na 2011/2012 na mpaka huu mwaka 2013/2014 ndio mara hii wamepangiwa milioni 50, lakini miaka yote iliyopita hakuna chochote kikosi hiki walichofaidika nacho. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, huku ni kukidhalilisha hiki kikosi.

Lakini Mhe. Naibu Spika, vikosi vyengine vyote vilivyobakia wamepangiwa pesa za kutosha kabisa. Naomba Mhe. Naibu Spika, nije kupata maelezo katika kikosi cha Jeshi la Kujenga Uchumi JKU. Mhe. Naibu Spika, nije katika kifungu 211505 sare za kiaskari, *Military Uniform*. Mwaka 2010/2011 ni shilingi milioni 85, mwaka 2011/2012 shilingi milioni 80, mwaka 2012/2013 shilingi milioni 90 na mwaka 2013/2014 shilingi milioni 281,500,000 kwa kweli hili ongezeko linatisha. Naomba kupata ufafanuzi katika kifungu hiki.

Mhe. Naibu Spika, hivi vikosi vyetu ukija katika vivazi vyao, kofia zao zimechacha, hazina maana. Kile kiatu ukikitizama soli yake basi ile soli imegawika chini ni vipande viwili. Kwa kweli hali hii ambayo hivi sasa tuna miaka 50 ya Mapinduzi, lakini vikosi vyetu havifai hata kidogo. Kwa kweli hapa bado hatujajipanga vizuri ni njia moja bado vikosi vyetu tunavidhalilisha, hatujaviwekea utaratibu hali ya kuwa ndani ya vifungu vyao pesa hizi zimeingizwa. Je, pesa hizi zinakwenda wapi. Kwa kweli hili linasikitisha Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, lakini hata ukiangalia kikosi cha KVZ kwa taarifa tulizopata juzi hapa Barazani, ni kwamba tayari wameshaajiriwa watu ndani ya makambi mbali mbali. Lakini KVZ bajeti hiyo iliyopangiwa kama sikosei Mhe. Naibu Spika, pesa yao ni ndogo mno na posho lao hili halijawahi kuongezeka toka mwaka 2010 hadi kufikia leo mwaka 2013, hawa watu wanaajiri na wanaongezeka, lakini kifungu chao hiki hakiongezeki tatizo ni nini, na hawa ni wengi kwa kiasi fulani. Kwa hivyo, hali ya vikosi vyetu sio nzuri na ikipatikana hiyo nafasi ya kutolewa kwenda katika maeneo mbali mbali ndio tukakuta watu wetu wanaporwa na wanachukuliwa bidhaa zao. Kwa kweli huu sio utaratibu mzuri, naiomba sana serikali isimamie inavyopaswa katika kuviimarisha vikosi vyetu hivi vya ulinzi.

Mhe. Naibu Spika: Malizia Mhe. Mjumbe.

Mhe. Rufai Said Rufai: Namalizia Mhe. Naibu Spika, katika Ofisi ya Usajili wa Vitambulisho katika ukurasa wa 32. Wenzangu wamechangia mengi na ni kweli, yote yaliyochangiwa mimi naamini.

Mimi nimuulize Mhe. Naibu Spika. Mhe. Waziri, anasisitiza katika Baraza hili jamani tudumishe sheria, sheria. Sasa sheria hii ni kwa wananchi tu na sisi Wawakilishi sio. Lakini hawa wenye kupewa hizi shughuli wao sheria hii haiwahusu, kama inawahusu kwa nini wakawa hawasimamii sheria. Sasa Mhe. Naibu Spika, ukiyachukua maneno haya yote tunayoyasema yakawa hayafanyiwi kazi ni sawa sawa na alivyotuambia Mwenyezi Mungu kwamba, naomba ninukuu kidogo Mhe. Naibu Spika. Mwenyezi Mungu amesema; "*yaquuluna bialsnatihim maa laysa fiy quluubihim*", wanasema kwa ndimi zao hapa tu, lakini siyo yaliyo ndani ya nafsi zao. Hii inaonesha picha mbaya Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, tunaichukua siasa kwamba siasa uhai wake na mambo yake yote ni hapa duniani, sio kweli. Siasa inakwenda mpaka mbele ya Mwenyezi Mungu. Sasa tunasema mbele ya ndimi na tunafurahi sana hapa, lakini sio kweli ndani ya nyoyo chimbuko liliopo ni kubwa mno na dhahiri linaonesha hali kama hii. Mhe. Naibu Spika, ni lazima tuwe wakweli na tusimamie yale tuliyoyaandika kwa mikono yetu. Kinyume na hivyo, yule unampa haki lakini mwengine unamnyima hapo Mhe. Naibu Spika, itakuwa hatujatekeleza sheria tuliyoiandaa. Ningekuomba sana Mhe. Naibu Spika, wakati umeshaniambia kuwa muda ni mdogo na kuna wenzangu wanataka kuchangia, basi naomba nifikie hapo *Inshaallah* yatakapojibiwa hayo niliyouliza basi nitaweza kuiunga mkono hoja nitakaporidhika. Ahsante.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuweza kunipa nafasi na mimi kuchangia bajeti hii kuhusu maendeleo ya nchi yetu. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi hii tukawa wazima na tukafika hapa kuweza kuchangia sote hadi mimi nikawa mtu wa mwisho kwa leo kuweza kuchangia nafasi hii.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nampa hongera Mhe. Waziri ambaye ametunga kitabu hiki kuweza kutujulisha masuala yote ya wizara zake alizopewa. Kwa kweli nampongeza sana Mhe. Waziri kuhusu suala hili. Kuhusu vitambulisho, kwanza nampa hongera kwa kuweza kutembelea mikoa yote ya Zanzibar kuweza kuwashajihisha wananchi ili waweze kujisajili na kuweza kuvifuatilia vitambulisho vyao na hili lilifanyika, namshukuru sana kwa hili. *(Makofi/Vicheko).*

Mhe. Naibu Spika, wengi wao hawafiki kwenda kuchukua vitambulisho vyao ambavyo walitakiwa kwenda kuchukua. Suala hili kwa kweli wasiwalaumu masheha kuwa wao ndio wanaowasababishia wasipate vitambulisho vyao. Masheha wanafanya majukumu ambayo yamepangwa na serikali na wao ndio wanaoshajihisha shehia ya serikali za mitaa. *(Makofi/Vicheko).*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mpeni raha mchangiaji.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Vile vile namshukuru Mhe. Waziri kuhusu vikosi vyetu vya JKU na JKT. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, vijana wetu wanapokwenda kufanya mafunzo ya JKU na JKT wanakwenda kwa muda maalum ili kwenda kupata mafunzo, wengi wao wanabahatika kupata kazi za ajira hasa kwenye vikosi vya ulinzi, polisi, jeshi na kadhalika, lakini wanapomaliza miaka ile mitatu wakati hawakupata nafasi. Mhe. Waziri naomba uwakumbuke vijana hawa wawezeshwe ili wanaporudi katika vijiji na mitaa waweze kujiajiri wenyewe kwa kuwezeshwa ili wapate misaada na waanze maisha mapya katika vijiji, ili waweze kuondokana na yale matatizo ambayo wengi wao wanajiingiza katika ujambazi na ujangili. Wakiwezeshwa basi tutakuwa na vijana wazuri ambao sio lazima kupata kazi za ajira, ni kwamba wakiwa wamepata fedha za kujiajiri wenyewe huwenda wakapata maisha yao mazuri na wakawa walinzi bora wa taifa hili.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ndugu zetu wa Chuo cha Mafunzo, kwa kweli iko haja ya kupunguza msongomano katika Chuo cha Mafunzo, wanapohukumiwa watu sio lazima kupelekwa Chuo cha Mafunzo kwa miaka hiyo. Wezi ambao wanaiba mazao vijijini sio lazima kwenda Chuo cha Mafunzo kwa wakati huu. Wezi kama hawa wafungwe katika kifungo cha nje, wapewe masheha na askari jamii ili wawawezeshe kwenda kulima mashamba ya wale watu wanaowaibia, badala ya kukaa Chuo cha Mafunzo kama miaka mitatu, basi wamlimie mwenye ndizi ile kwa muda wa miaka mitatu, hapo tutaondosha msongomano katika magereza yetu, kule waende wale wahalifu wanaohalifu nchi yetu hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli Chuo cha Mafunzo iko haja ya kuwezeshwa kwa kila hali, chuo hiki hivi sasa wanalo bwawa la samaki kule Bumbwini. Mhe. Naibu Spika, iko haja wawezeshwe kwa sababu bwawa lile kama watawezeshwa kupewa zana za kisasa kwa kweli wanaweza kuilisha Zanzibar na wao wenyewe wakawalisha wale wafungwa wote, ikawa hatuna haja ya kutumia pesa hata kidogo za serikali. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba ukijali Chuo cha Mafunzo uwawezeshe kuwapa zana za kisasa ili waweze kufanya ufugaji mzuri.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Baraza la Mji kwa kweli baraza hili hivi sasa lina matatizo makubwa sana kuwa wameshindwa kuweka usafi katika mji wetu, wanatutia aibu sana. Kama hii kazi wameshindwa basi ni afadhali wapewe vikosi vile ambavyo vina wastaafu kama vile UMAWA na vikosi vyengine ambavyo vya wastaafu waweze kuujenga huu mji kwa usafi. Na wao kwa vile watakuwa ni wajasiri amali wanaweza wakafanya kazi kwa bidii, wakaweza kuuweka safi mji wetu, ukang'ara na watalii wakaweza kutembea vizuri.

Kama tukienda Mji Mkongwe, basi siku ya pili huwezi kwenda kwa harufu mbaya iliyokuwepo. Naomba Mhe. Waziri suala la Baraza la Mji ulitilie mkazo sana, iko haja wafanye shughuli zao na kama wameshindwa basi wakodishe hiyo nafasi kwa vikosi vyetu vya wastaafu wanaweza kuulinda mji wetu kuwa safi.

Kuhusu kuratibu mikoa. Mhe. Naibu Spika, iko haja iundwe tume maalum ya nchi yetu, kwa vile vijana wengi hawajisajili katika sehemu zao walizozaliwa wanapoishi, wanakwenda sehemu pengine matembezi na hutaka huko wajisajili wakati sio vijiji vyao wala sehemu yao ya kujisajili, kwa kweli wanatia aibu na kwa kuwa vijana wa vijiji vile wanajuana basi inakuwa ngumu kupata vitambulisho kwa sababu sehemu wanazokwenda sio zao.

Mhe. Naibu Spika, sisi Wawakilishi kwa kweli wengi wetu hatukupitia kazi za uaskari, iweje sisi tuwafundishe vikosi au tumfundishe kamanda jinsi ya kumvisha askari kifaa cha kuweza kupambana na adui, wakati mtu anakwenda kuisaliti serikali huyo ni adui, sasa itakuaje tumfundishe kamanda askari wake tumuambie sisi huku raia ambao tuko katika Baraza kwamba kamanda vifaa vya mara hii tuwape askari wako wakapambane na adui, sisi tunajuaje. Kwa hivyo, ina maana tuwafundishe kuwapa vifaa hivyo, basi tuwape nafasi ya kwenda Darajani wakanunue poda na rangi za mdomo wakapambane na maadui, hapo ndio tutakuwa tunawafundisha makamanda. Lakini hatuwezi kuwafundisha makamanda vipi wakapambane na maadui wa nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, huo ndio mchango wangu, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia pamoja na wananchi wangu wa Koani, ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, Kwa kweli muda ni mdogo na ufafanuzi niliokuwa nataka kuutoa ni mkubwa kidogo, lakini hata hivyo nitagusia maeneo machache. Kuna eneo moja ambalo limezungumziwa sana katika Baraza lako tukufu linalohusu vitambulisho. Mimi nadhani Waheshimiwa Wajumbe, twende na vigezo vya kimataifa vinavyohusu ukuaji wa idadi ya watu katika nchi. Nchi yetu ina watu 1,300,000 kwa mujibu wa sensa ya hivi karibuni ambayo imefanywa.

Mhe. Naibu Spika, kikawaida watu wanaofikia umri wa miaka 18 na kuendelea mpaka zaidi ya 100 kama wapo wanaoishi hivyo, basi wanatakiwa wasipindukie asilimia 40 ya *population* ya nchi kwa idadi ya watu waliopo katika eneo hilo. Sasa tukijirejesha katika idadi ya watu ambao wameshapata vitambulisho au vitambulisho ambavyo vimetolewa. Sasa hivi Zan ID kuna idadi karibu 599,300 na zaidi, hii ni zaidi ya asilimia 40. Tuseme pengine hizo

takwimu za kimataifa zinaendana na *one plus two*, kwa sababu wenzetu katika kaya moja kuna idadi ya watoto wawili wanaozaliwa, lakini sisi idadi yetu tunaweza tukasema kuanzia watoto watano hadi tisa, pengine labda ndio imetufikisha kuzidi zaidi ya asilimia 40. Sasa ili tufikie asilimia 50 kwa idadi hii ambayo idara ya vitambulisho imeshatoa vitambulisho, maana yake tunahitaji tupate watu 650,000 lakini sasa tuna watu 599,300, sasa hii 650,000 ni karibu asilimia 50, jambo ambalo katika vigezo vya kimataifa hili halikubaliki.

Sasa mimi nadhani Mhe. Waziri labda aje atupe ufafanuzi ni asilimia ngapi ya Wazanzibari wanaostahiki kupata vitambulisho na idadi ambayo hivi sasa tunayo, na pengine tunaweza tukamaliza haya maneno ya kushtumiana. Kwa hivyo, sisi kama serikali au kama nchi ni lazima pia na vigezo hivi tuvizingatie kama tunataka kuwa wakweli.

Jengine ninalotaka kulisema ni kwamba wako wachangiaji ambao katika kitabu cha Mhe. Waziri kilizungumzia suala la tume ya idara maalum na tume ya utumishi. Ni kweli eneo hili nafikiri mwenyewe Mhe. Waziri atakuja kututhibitishia zaidi katika ukurasa wa 52, kufuatilia ajira na maslahi ya watumishi wa idara maalum za SMZ kwa kushirikiana na tume ya utumishi serikalini. Hapa nataka niseme kwa mujibu wa sheria sio Tume ya utumishi serikalini ni Kamisheni ya utumishi wa umma.

Kwa hivyo, hapa nakubaliana na Mjumbe ambaye amelisema hili kwamba tume ya utumishi serikalini na tume ya idara maalum zote kimamlaka ziko sawa kwa mujibu wa sheria. Isipokuwa kama kushirikiana, wanatakiwa kwa ajili ya kupata maamuzi mengine ya juu, wanatakiwa washirikiane na Kamisheni ya utumishi wa umma.

Jengine ambalo lilizungumzwa sana katika mjadala huu ni maslahi madogo ya watumishi wa idara maalum. Kwanza nataka nimpongeze sana Kamanda Mkuu wa idara maalum, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, huyo ndiye kamanda mkuu wa idara maalum kama vile ilivyo kwa Amiri Jeshi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo, Rais wa Zanzibar yeye ni Kamanda Mkuu.

Nataka nimpongeze kwa sababu kipindi kilichopita alijaribu kuhakikisha kwamba wapiganaji wetu wa vikosi vya SMZ maslahi yao kidogo yananyanyuka na yanakuwa tofauti na waajiriwa wengine wa utumishi wa umma. Hivi sasa azma hiyo bado anaiendeleza. Ninachotaka kulihakikishia Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika, kwamba hivi sasa *salary structure* ya idara maalum ipo kwenye Kamisheni ya utumishi wa umma kwa ajili ya

kupata mazingatio, na kwa sababu kinachofanyika sio marekebisho madogo ya kumfikiria nani apate posho na nani apate nini.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria yetu ile ya utumishi wa umma hata hao kamisheni wanapotaka kubadilisha *salary structure* ya watumishi, inabidi wafanye *consultation* na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora ndipo waweze kufanya maamuzi ya kuweza kumshauri Mhe. Rais. Mimi nina hakika kwa sababu Mhe. Rais yeye ndiye kamanda mkuu, atakapopelekewa ushauri huu basi askari wetu wataweza kunufaika na hili. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, muda wa asubuhi tunamalizia hapa, tunawashukuru Wajumbe kwa michango yao, lakini tunawaomba jioni tufike mapema ili tusikilize majumuisho.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaakhirisha kuna tangazo. Tunaambiwa kwamba ile semina yetu inayohusu Mizozo namna ya kuitatua ipo hapo juu kama ilivyopangwa, mambo yote yametayarishwa msiwe na wasi wasi. Kwa hivyo, tunaakhirisha kikao chetu hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa nafasi tunampa Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora achukue muda mdogo tu na baadaye Mhe. Machano Othman Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, nadhani kuhusu suala la maslahi madogo kwa askari wetu tayari nimeshalitolea maelezo juu ya zile taratibu ambazo zinaendelea katika kuhakikisha kwamba askari wetu wanalipwa malipo stahiki kwa mujibu wa uzito na ugumu wa majukumu yao ya kazi.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo limejitokeza katika Mkutano huu na liliulizwa swali kwa nini kunafanyika ajira ya vikosi. Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar huwa inafanya ajira kufuatia mpango madhubuti wa matumizi wa hizo ajira ambazo zinafanyika. Katika eneo hili la vikosi ajira inafanyika kwa sababu tu ya kuona kuwa askari au idadi ya ajira

ya askari waliopo vikosi vya SMZ ni kidogo na ndipo serikali imeamua kuwaajiri askari hawa.

Kwa mfano, kama tutakumbuka kwenye matukio ya hivi karibuni ambayo yalitokea katika nchi yetu, kwa kweli tulishuhudia ni jinsi gani tulipoamua kutuliza ghasia au serikali ilipoamua kuirejesha nchi katika hali ya utulivu na amani, namna ya askari hao walivyokuwa wakifanyakazi pengine kinyume na ule utaratibu wa binadamu kufanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, binadamu anatakiwa afanye kazi katika kipindi cha masaa 24 kwa masaa yasiozidi manane na halafu unatakiwa upumzike. Lakini tulishuhudia askari hawa wa Vikosi vya SMZ wakiwa wakifanyakazi karibu wiki tatu nzima mpaka walipoona hali imetulizana. Kwa hivyo, kuajiriwa kwa askari katika Vikosi vya SMZ kunatokana na kwamba idadi ndogo ya askari waliopo ndio maana mahitaji na tumeamua serikali tufanye ajira kwa vijana hawa katika Vikosi vya SMZ.

Vile vile tumeshuhudia matukio ya uhalifu na mambo mbali mbali ambayo yanajitokeza, pia tumeshuhudia katika ofisi za serikali kunafanyika wizi kwa sababu ya kuweka askari hawa wanaolinda kwa virungu au bakora. Sasa serikali inataka kuhakikisha kwamba tunawaajiri vijana hawa katika Vikosi vya SMZ, ili tuwe na nguvu kazi ya kutosha katika vikosi vya kuweza kulinda vituo muhimu vya serikali na kulinda mali za serikali katika maeneo tofauti. Kwa hivyo, hiyo ndio sababu ya msingi ya kuona. Lakini jambo jengine ni kwamba askari waliopo wengine wanastaafu kama wanastaafu basi inabidi ipatikane *replacement*, kwa ajili ya ku-*cover* zile nafasi wanazostaafu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia kumeulizwa ni kwa nini askari wastaafu wanaajiriwa kwa mkataba. Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria yetu ya Utumishi wa Umma inaruhusu kumuajiri mtu kwa mkataba, lakini kwa madhumuni ya kutoa mafunzo kwa wale wapya wanaoajiriwa, yaani kutoa uzoefu kwa maana ya kurithisha utendaji au mpango kazi. Kwa hivyo, lazima wawepo watu ambao wanaweza kuwarithisha wale ambao wanaajiriwa katika ajira mpya na hiyo ndio sababu ya kutosha.

Mhe. Naibu Spika, kama mtakumbuka wakati nilipokuwa nikijibu swali tuligundua kwamba katika kipindi hichi cha mwaka huu utumishi wa umma mzima tuliajiri watu wasiozidi 30, sasa wale walikuwa ni maeneo yote ya utumishi wa umma kwa maana Tume ya Utumishi, Idara Maalum, Tume ya Utumishi ya Mahakama, Tume ya Utumishi Serikalini na Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi. Sasa ukenda kwenye mchanganuo basi katika watu

tuliowaajiri 2419 utakutia kuajiri watu 30 wakiwemo hawa askari wa vikosi wastaafu utakutia sio idadi kubwa ambayo tumeamua kuajiri serikali.

Jambo jengine ambalo ningependa kulitolea ufafanuzi ni juu ya suala zima la *scheme of service* ya vikosi. Mhe. Naibu Spika, lazima tukiri kwamba katika kipindi cha muda mrefu mambo haya ya miundo ya utumishi yalikuwa hayafanyiki vile inavyotakiwa. Sasa baada ya kuja Sheria ya Utumishi ya Umma na kila Tume ya Utumishi kupangiwa majukumu yake na moja kati ya majukumu ya Tume za Utumishi ni kupendekeza miundo ya utumishi katika maeneo yao ikiwemo hii Tume ya Utumishi ya Vikosi.

Kwa hivyo, Idara Maalum hivi karibuni imetengeneza muundo wake wa Utumishi na hivi sasa uko Kamisheni unafanyiwa kazi na si muda mrefu katika kipindi hichi idhini ya kutumika kwa muundo huo itatoka, kwa maana hiyo kasoro hii ya miundo ya utumishi ya Idara Maalum itakuwa si tatizo tena kama ilivyokuwa kwenye maeneo mengine ya Tume nyengine za Utumishi wa Umma.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kutoa ufafanuzi kwa upande wa kumsaidia Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, sasa naomba nitoe ufafanuzi juu ya suala la uteuzi wa Wajumbe wa Tume ya Utumishi Idara Maalum na hoja hapa ni kwa nini yupo raia kwenye tume ile.

Katika tume ile kwanza muundo wake kuna mwakilishi kutoka kila Kikosi cha SMZ, ambaye anawakilisha kikosi chake ndani ya tume, Mwenyekiti wa Tume anateuliwa kwa mujibu wa sifa ambazo zimetajwa na wengine wanaingia kwa nafasi zao.

Sasa nilipoiangalia tume yupo kweli raia mmoja, lakini sheria ile haitufungi kuweza kumteua mtu kwa mujibu wa ujuzi na sifa ambazo zimetajwa ndani ya Sheria ya Utumishi wa Umma. Kwa hivyo, Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume ya Utumishi wana sifa ambazo zimeainishwa katika sheria, nafikiri nikiamua kuzieleza hapa tutachukua muda mrefu na nadhani Mhe. Waziri atakapokuja atatoa ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, wajumbe wengine wa tume ile waliomo. Kwa mfano, mwenyekiti ni askari mstaafu alikuwa na cheo cha kanali na baadhi ya wajumbe pia ni askari kutoka kwenye vikosi isipokuwa huyu mjumbe mmoja na wajumbe wengine ambao Mhe. Waziri anawateua ni wastaafu kutoka kwenye vikosi hivi. Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua moja kati ya masharti ya kuwa mjumbe katika tume hizi ni lazima uwe umestaafu.

Nikiondoka hapo sasa nielekee katika Mkoa wa Kaskazini Unjua nimpongeze na nimshukuru sana Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa kusimamia vyema majukumu yake ya kiutawala ndani ya Mkoa wa Kaskazini pamoja na kuzingatia masuala ya utawala bora na kuendesha taasisi kwa mujibu wa kufuata misingi ya sheria na taratibu zilizopo. *(Makofi)*

Lakini nataka nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hasa Marais kwa azma yao tokea Rais Mstaafu Dkt. Salmin Amour Juma Komandoo, ambaye kwa makusudi mazima aliamua kuitangaza Tumbatu kuwa ni Wilaya Ndogo na Kojani pia kuwa Wilaya Ndogo, Mhe. Naibu Spika tumetoka mbali sana. Katika mazingira ya kawaida watu wa Tumbatu lazima tuseme kweli tumetokea mbali. Mhe. Naibu Spika, leo hii Kisiwa cha Tumbatu kuwa na hadhi ya Wilaya Ndogo na nini madhumuni yake? Kwa kweli madhumuni yake ni kusogeza huduma za jamii zinazohudumiwa na watendaji wa serikali karibu na wananchi. *(Makofi).*

Kutokana na hali hiyo, naomba nimpongeze Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja pamoja na serikali kwa jumla kwamba kadri hivi tunavyokwenda wale wataalamu ambao pengine wananchi wa Kisiwa cha Tumbatu walikuwa wakivuka kuja Mkokotoni na maeneo mengine kufuata utawala hivi sasa haifanyiki hivyo, utawala upo kule kule Tumbatu lakini asili ya Tumbatu tokea zamani kulikuwa na utawala wake. Kwa hivyo, Dkt. Salmin Amour Juma Rais Mstaafu kurejesha hadhi ya watumbatu hakukosea. *(Makofi).*

Vile vile nataka niwashukuru Marais wengine wa awamu zote zilizofuata baadaye, awamu ya Sita ya Dkt. Karume ambaye na yeye yako mambo mengi ambayo ameyafanya. Kwanza alihakikisha jengo la Utawala wa Wilaya Ndogo Tumbatu linakamilika. Pili huduma nyingi za kijamii alihakikisha zinasogea karibu. Sasa hizo huduma za jamii ili ziweze kufikia kiwango ambacho kimekusudiwa basi lazima kuwe na sehemu inayoratibu shughuli hizo na sehemu ya kuratibu shughuli hizo ni ile Ofisi ya Wilaya ya Ndogo Tumbatu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nimshukuru Dkt. Ali Mohammed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuona umuhimu wa kuwepo kwa Wilaya Ndogo ya Tumbatu kwa kuwezesha kuruhusu fungu au *sub vote* ya Wilaya Ndogo Tumbatu ya matumizi, kwa sababu unapoweka ofisi basi lazima uweke na kasma ya kuweza kuiendesha ile ofisi. Kwa hivyo, nimshukuru sana Dkt. Shein inaonesha zile juhudi zake tokea ameingia madarakani. Kwanza amewezesha Ofisi ya Wilaya Ndogo Tumbatu badala ya kuwa na watendaji wachache, hivi sasa kuwa na baadhi ya watendaji ambao

watakidhi haja katika kuhakikisha wanatoa huduma zilizokusudiwa kwa mujibu wa matakwa na uanzishwaji wa ile Wilaya Ndogo Tumbatu. *(Makofi).*

Baada ya kusema hayo na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tumbatu nataka niishukuru sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanzia awamu ya kwanza ya mwaka 1964 mpaka awamu hii ya saba. Kwa hivyo, lazima tukiri sisi kama Watumbatu mpaka mwaka 1964 hakuna mtu ambaye anaweza kusoma barua, hivi sasa tunao watu wanazo *PhD* kwenye fani tofauti. Kwa maana hiyo, lazima mimi mmoja kama nitakuwa siyashukuru mapinduzi ya mwaka 1964 *Wallahi* sitawatendea haki watu wa Tumbatu. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, yako mengi zamani tukilala mapema na siku hizi hatulali mapema kwa sababu umeme, maji pamoja na huduma za uzazi zipo na mambo mengineyo na tutaendela. Kwa hivyo, nimshukuru Dkt. Ali Mohammed Shein Mhe. Rais wa Zanzibar kwa juhudi zake hizo za kuendeleza ile azma ya kuwepo Wilaya Ndogo Tumbatu. Vile vile nikishukuru Kikosi cha KMKM kwa kujenga kituo cha askari cha KMKM kule Tumbatu. Kwa kweli kulingana na mazingira ya Kisiwa cha Tumbatu kunahitaji kuwepo kwa vijana ambapo ikitokezea dharura basi waweze kusaidia.

Mhe. Naibu Spika, asubuhi ilizungumzwa habari ya ujenzi wa mnara, ule mnara unaojengwa Tumbatu sio sawa na ule mnara wa kupachikia bendera isipokuwa ni kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano katika utendaji bora wa vikosi vyetu vya SMZ hasa wakati wa kufanya doria. Kwa hivyo, mnara ule hautawasaidia askari peke yao, pia utasaidia wavuvi pamoja na watu wengine ambao wataitumia bahari kwa maendeleo yao kama vile wasafiri na wavuvi na wengine wengi. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tumbatu naiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Machano Othman Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti hii ya Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Pili naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai, uzima na afya.

Tatu tumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake uliotukuka na kuwatendea vyema wananchi wa

Zanzibar. Mhe. Rais wa Zanzibar tangu amechaguliwa mwaka 2010 ameonesha ni mtu muungwana, mkweli na mtendakazi kwa bidii. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amejitahidi sana katika kuandika kitabu mara hii, ameandika kitabu vizuri na ameweka vitabu vyengine vya mafahamisho na ninahakika sisi Waheshimiwa Wawakilishi tutamuelewa na kumuunga mkono katika bajeti yake hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, muda umekuwa ni mwingi na tunataka kumaliza bajeti hii lakini mimi nataka nichangie kama sehemu nne na wenzangu wamechangia, isipokuwa na mimi nataka nitoe maoni yangu.

Jambo la kwanza ni sehemu ya Baraza la Mapinduzi na kwa bahati nzuri na mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi, kwa hiyo nitasema yale ambayo ninayaelewa na kuwatoa hofu baadhi ya Waheshimiwa Wawakilishi kama walivyozungumza. Nadhani alikuwa ni Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwamba fungu na Baraza la Mapinduzi viburudishaji vimepanda sana kutoka milioni 266 mpaka milioni 303.

Lakini mimi namuomba aunge mkono bajeti hii kwa sababu huko miaka ya nyuma Baraza la Mapinduzi lilikuwa likikutana mara moja kwa mwezi, lakini hivi sasa Baraza la Mapinduzi linakutana mara mbili kwa mwezi na kila kikao kimoja kinaweza kutumia siku mbili au tatu inagemea na ajenga ambazo zipo. Kwa kweli hata hizo siku mbili za Baraza basi Wajumbe tunaweza kufika saa 5 au mpaka 7 za usiku. Kwa hivyo, Wajumbe wa Baraza wanafanyakazi na serikali inafanyakazi.

Vile vile kuna vikao vya Makatibu Wakuu vimetoka 12 mpaka 48 navyo hivyo vinatumia fedha karibu milioni 1,500,000/= kwa kikao na Baraza la Mapinduzi ni karibu milioni 4,800,000/=, pia kuna kamati mbili za Baraza la Mapinduzi pamoja na Bango Kitita. Sasa wajumbe wa vikao hivi sio mawaziri peke yao, wanakuja makatibu wakuu, wataalamu wa wizara, wasaidizi wa Mhe. Rais, wasaidizi wa Makamu wa Kwanza na wa Pili, lakini sisi mawaziri tunao madereva yaani watu wengi sana wanakula pale Ikulu.

Mhe. Naibu Spika, kwenye Baraza la Mapinduzi sio kwamba tunakula chakula cha mchana tu, tunakunywa chai asubuhi, tunakula mchana na pengine watu wasiopungua 200 kwa kikao kimoja. Kutokana na hali hiyo, mimi sioni kwamba shilingi milioni 300 ni nyingi kwa kuhojiwa Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, Tanzania leo ina ugeni na tunashukuru sana Mhe. Rais Barack Obama wa Marekani katika nchi tatu alizotembelea Afrika, gharama zake ametumia shilingi bilioni 160 kwa nchi tatu tu za Afrika. Sasa serikali nzima ya Zanzibar, yaani Baraza la Mapinduzi kutumia shilingi milioni 303 naona sio tatizo kubwa.

Mhe. Naibu Spika, bila ya Baraza la Mapinduzi kukutana basi Baraza la Wawakilishi haliwezi kukutana, kwa sababu Baraza la Mapinduzi ndilo linaloandaa miswada, sera pamoja na mambo mengine. Kwa hivyo, nafikiri Mhe. Mjumbe aelewe kuwa hakuna jambo ambalo limezidi katika matumizi hayo.

Pili Waheshimiwa Wajumbe wamezungumzia kuhusu Vikosi vya SMZ. Kwanza nataka niunge mkono kwamba vikosi hivi vimefanyakazi nzuri na vinaendelea kufanya kazi nzuri katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora alizungumza hapa kwamba mwaka jana sote ni mashahidi kwa jinsi askari wetu walivyofanyakazi vizuri katika mazingira magumu na wameweza kuituliza nchi yetu katika hali ya amani na usalama.

Kwa mfano, kuna kipindi wakati wa Mhe. Rais Mstaafu wa Zanzibar Aboud Jumbe Mwinyi tuko Mnazi Mmoja Baraza hili la Wawakilishi, sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuliwahi kufikia hatua na tukaomba uongozi wa juu utupatie silaha ili tutembee na silaha maana tulikuwa tumetawaliwa na woga. Lakini vikosi vyetu vimefanyakazi nzuri bila ya sisi kuwa na silaha. Kwa hivyo, mimi vikosi vyote vitano, yaani KMKM, JKU, Mafunzo, Valantia pamoja na Zimamoto wanafanyakazi vizuri. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, naungana na wale wote waliosema maslahi yao yaboreshwe na kama alivyosema Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwamba ni vyema askari wetu waongezwe maslahi yao na serikali haiwezi kuwaacha mkono. Kwa hivyo, nafikiri ni wajibu wetu Waheshimiwa Wawakilishi tuviunge mkono vikosi vyetu hivi vinafanyakazi nzuri na makamanda wao wanajitahidi kwamba nchi yetu iende salama kwa kushirikiana na askari polisi. *(Makofi).*

Tatu nataka kuzungumzia kuhusu Idara ya Usajili na Kadi za Utambulisho. Mhe. Naibu Spika, hapa yapo maneno lakini ukifuatilia sana lile ambalo tulisema tusilitumie ndilo ambalo linalotumiwa. Kwa mfano, Waheshimiwa Wajumbe wengi wamesema tusitumie siasa katika kuzungumzia vitambulisho, lakini akizungumza mtu unajua kwamba anatumia siasa katika kuzungumzia suala hilo.

Kwa nini nasema hivyo? Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya Waheshimiwa wamelalamika kwamba Kaskazini 'A' Kidoti kuna watu 400 ambao hawajaandikishwa, sasa mtu alijuwaje sio jimbo lake wala wilaya yake. Mhe. Naibu Spika, kwa bahati nzuri humu wengi tunayo majimbo na mimi naona upo utata lakini nitatoa mapendekezo baadaye tufanye nini, ili tulitatue tatizo hili.

Kwanza nadhani idara hii inafanyakazi vizuri lakini tupende tusipende lazima wadanganyifu wapo na sheria ya kupata kitambulisho cha Mzanzibari sio umri peke yake, yaani unatakiwa uwe na umri umefikia 18, uwe Mzanzibari Mkaazi wa eneo na hili pia ndio tatizo kubwa. Tatizo hili linasababishwa na mambo mengi tu, lakini mimi pendekezo langu kwa Mhe. Waziri na kama huko mbele litakaa sawa basi lifanyike.

Mhe. Naibu Spika, nafikiri wakati umefika wa kuzichanganya Idara ya Vizazi na Vifo na Idara ya Usajili wa Kadi za Utambulizi, ili tangu mtu anazaliwa mpaka anaendelea na maisha yake basi ajue, yaani tukiwa na Idara moja ya Vizazi na Vifo ambapo na usajili ni hapo hapo, basi haiwezekani hata siku moja kudanganya katika jambo hili, nafikiri tutamaliza jambo hili. *(Makofi)*
Mhe. Naibu Spika, watu walioandikishwa Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora aliwataja asubuhi karibu laki 590 na zaidi, kwa sababu ukisema watu wanaandikishwa kisiasa unakosea sana. Mimi mpaka Disemba 2012 nilikuwa Mkuu wa Idara ya *Organization* CCM Zanzibar. Kwa hivyo, najua wanachama wa CCM Zanzibar nzima hawazidi 400,000 sasa hawa wengine walipatikana wapi walioandikishwa, waliulizwa. Kwa kweli mimi naamini wanaandikishwa kila mwananchi wa Zanzibar baada ya kuthibitishwa vielelezo kama yeye ni mkaazi halisi wa eneo husika. Kwa hivyo, nawaomba wananchi wenzangu wa Zanzibar hata kama unahamia sehemu basi fuata taratibu za uhamiaji nenda kwa Sheha, chukua barua unakotoka, ishi katika eneo ufike miaka mitatu uone kama hukuandikishwa, nafikiri hili linaweza likakaa sawa.

Mhe. Naibu Spika, jengine kwa haraka haraka ni mikutano ya kikanda. Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, tujitahidi sana kushiriki katika mikutano hii, kwa sababu mikutano ya kikanda ni muhimu sana kwa nchi yetu ya Zanzibar, kwani nchi yetu ni ndogo tena ni ya kisiwa. Vile vile mikutano ya Afrika ya Mashariki tusiache kushiriki, *SADC* tusiache kushiriki pamoja na gharama zake za fedha, lakini kuna umuhimu mkubwa wa kushiriki.

Sasa Mhe. Naibu Spika, nizungumzie suala langu la mwisho hapa tumezungumzia matatizo ya wafanyabiashara wa Darajani na kila Mhe. Mjumbe amezungumza kwa hamasa sana, nilimsikia Mhe. Abdi Mosi Kombo

nilikuwa nje. Mimi naona suluhisho la Darajani litakuja na mipango miji haiwezekani hata siku moja tukatarajia kwamba Darajani tutamaliza tatizo la ajira la wafanyabiashara wa Zanzibar, kwa nini nasema hivyo? Kwa kweli kila mwaka vijana wasiopungua 15,000 wanamaliza skuli na kila mkoa wanamaliza skuli itawezekana vipi watu wote waje Darajani. Mimi nafikiria kwamba kila mkoa, labda pale Serikali za Mitaa zitakapoanza kazi basi tuanzishe Kituo cha biashara cha Mkoa kwa ajili ya kusaidia vijana wetu kupata ajira katika maeneo yao. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, kidogo tuangalie hali halisi ilivyo hivi sasa Mkoa wa Mjini/Magharibi, kuna wananchi wasiopungua 590,000 wakati mwaka 2002 walikuwa wananchi 300,000 karibu mara mbili wamezidi. Kutokana na hali hiyo, Mkoa wa Mjini/Magharibi una idadi ya wananchi wa Zanzibar asilimia 46, yaani katika mikoa yote ya Zanzibar asilimia 46 ya wananchi wanaishi katika Mkoa wa Mjini/Magharibi. Kwa hivyo, wananchi hao wanahitaji maji safi na salama, pia wanahitaji huduma za afya, ulinzi wao pamoja na mambo mengine mengi.

Lakini mikoa mingine ina wananchi ambao hawaongezeki na tukiangalia sensa ya mwaka jana na Mkoa wa Mjini/Magharibi umeongezeka asilimia 4.2 na Mkoa wa Kaskazini Unguja imeongezeka asilimia 3.2, Mkoa wa Kusini Unguja asilimia 2, Mkoa wa Kaskazini Pemba asilimia 1.3, Mkoa wa Kusini Pemba asilimia 1.1.

Sasa ukiangalia utaona kuna mikoa kama watu hawajazaliwa kwa sababu hakuna kinachoongezeka. Lakini kuna mikoa mengine kama vile Mkoa wa Mjini/Magharibi unaona kama watu wamekuja kudondoshwa tu, yaani wamekuwa watu wengi sana. Katika hali kama hiyo kimaendeleo hatuwezi kwenda mbele. Wilaya ya Magharibi peke yake ina watu 390,000 ni kubwa kwa watu kuliko mikoa mingine na mkoa mwengine unaofuatia kwa watu kuwa wengi ni Mkoa wa Kaskazini Pemba ni watu 202,000.

Mhe. Naibu Spika, lazima tufike pahala Waheshimiwa Wawakilishi tuisaidie serikali yetu kuangalia tutafanya nini kupunguza tatizo la ajira kutokana na wingi wa watu. Kwa hivyo, mimi nafikiria Mhe. Waziri pamoja na gharama lakini imefika wakati sasa Mkoa wa Mjini/Magharibi kuwa mikoa miwili ya kiserikali, kwa ajili ya kupunguza hili tatizo kwa sababu Wilaya ya Mjini ina watu 270,000 na Wilaya ya Magharibi ina watu 390,000 ni watu wengi ambao hawawezi kuhudumiwa na mkoa mmoja.

Mhe. Naibu Spika, katika Wilaya ya Magharibi Shehia tu zina watu mpaka 26,000 Tomondo, ukiangalia Shehia 14 za Wilaya ya Magharibi zina watu kuanzia 11,000 mpaka 26,000. Lakini katika mikoa mingine Shehia zina watu

kati 900 mpaka 8,000, kwa hivyo hapa utaona kwamba kuna tatizo la kiutawala na kiwingi wa watu katika Mkoa wa Mjini/Magharibi.

Sasa ukiacha Mkoa wa Dar-es-Salaam, Mkoa wa Mjini/Magharibi ndio unaoongoza kwa wakaazi kwa kieneo, kilomita moja na hivi. Sasa sisi tunaishi karibu watu 2,000 na zaidi kwa kilomita moja. Mhe. Naibu Spika, haya ni matatizo nadhani Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aweze kuyafanyia kazi, ili kupunguza haya matatizo ambayo yanalalamikiwa katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kuunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja na matarajio yangu ni kwamba ushauri waliotoa Waheshimiwa Wawakilishi, basi Mhe. Waziri atauzingatia pia Waheshimiwa Wawakilishi watazingatia juhudi za Mhe. Waziri za wizara hii kubwa na juhudi yake katika ufanisi na maendeleo ya nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie hapo. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, ahsante sana. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe katika michango tumefikia hapo na sasa tunamwita Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ajili ya kuja kufanya majumuisho na baadaye tupitishe vifungu. *(Makofi).*

1/07/2013

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kupata fursa hii mara nyengine tena ya kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu kuja kufanya majumuisho ya michango ya Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali waliopata fursa ya kuchangia hoja yetu hii hapa kwenye ukumbi wetu na wale ambao walichangia kimaandishi. Ni imani yangu kwamba karibu watu wote wangependa wachangie lakini bahati mbaya muda hautoshi. Lakini nashukuru watu waliojitokeza kuchangia ni wengi, jumla ya watu 34 wamechangia hapa ukumbini na wa 5 wamechangia kimaandishi. Kabla sijenda mbele ni vyema nikawatambua mmoja baada ya mwengine na kuwashukuru sana kwa ushauri, mawazo, maelekezo, yote yanalenga katika kujenga. Kwa kweli tumechambua hasa *issue* kubwa ni tisa, lakini ukizigawa hizo *issues* ndogo ndogo basi tutapata kama *issues* 53, yaani hizo 9 ukizigawa undani wake basi inafikia 53.

Mhe. Naibu Spika, haitokuwa rahisi kuzijibu zote, kwa hivyo nawaomba sana Waheshimiwa mnivumilie lakini mimi nichukue kwamba mmetuchangia, mmetuelekeza na maelekezo yenu yote sisi tutayachukua kama kawaida yetu ili tuyafanyie kazi ili tupate ufanisi katika wizara yetu. Si lengo kama pengine sikumtaja mheshimiwa au hoja yake sikuitaja aone kwamba nimedharau. Sikuwa na dhamira hiyo, kwa hivyo naomba sana Waheshimiwa mtuvumilie na nafikiri hotuba ilikuwa masaa mawili pengine michangio tu kwa kuwaridhisha wote labda ungenipa masaa matatu. Lakini isnhaallah hatutofika huko.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba niwatambue wachangiaji nao ni kama wafuatao:-

1. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Asha Bakari Makame
4. Mhe. Omar Ali Shehe
5. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
6. Mhe. Kazija Khamis Kona
7. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
8. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
9. Mhe. Marina Joel Thomas
10. Mhe. Mohammed Haji Khalid
11. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
12. Mhe. Hija Hassan Hija
13. Mhe. Salmin Awadh Salmin

14. Mhe. Salma Muhammed Ali
15. Mhe. Bikame Yousuf Hamad
16. Mhe. Saleh Nassor Juma
17. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
18. Mhe. Salum Abdalla Hamad
19. Mhe. Panya Ali Abdalla
20. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
21. Mhe. Mlinde Mbarouk Juma
22. Mhe. Hassan Hamad Omar
23. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
24. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
25. Mhe. Abdi Mosi Kombo
26. Mhe. Farida Amour Ali
27. Mhe. Subeit Khami Faki
28. Mhe. Salma Mussa Bilal
29. Mhe. Asaa Othman Hamad
30. Mhe. Fatma Mbarouk Said
31. Mhe. Rufai Mohammes Said
32. Mhe. Mussa Ali Hassan
33. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora
34. Mhe. Machano Othman Said, Waziri wa Nchi, Asiyekuwa na Wizara Maalum

Mhe. Naibu Spika, michango kwa maandishi nimeipokea kutoka kwa Waheshimiwa wafuatao:-

1. Mhe. Ashura Sharif Ali
2. Mhe. Mgeni Hassan Juma
3. Mhe. Asha Abdu Haji
4. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa

Mhe. Spika, kama nilivyosema tunawashukuru wote kwa michango mizuri, mizito yenye lengo la kujenga. Kama nilivyoeleza kwa ujumla Waheshimiwa wengi sana wamezungumzia suala zima la:-

1. Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi

2. Maslahi kwa idara maalum za SMZ

3. Manispaa na hasa msongamano pale Darajani, Masoko ya Mjini *vis-a-vis* hali yake hasa Saateni na Darajani, Usafi wa Mji, Vizuizi vya njia ya Forodhani

4. Agizo la kutofanya au kutoingilia kufanya au kuingilia kutofanya mikutano ya kisiasa lililotokea Jimbo la Kitope

5. Pesa za likizo kwa wapiganaji wetu

6. Vifungu vilivyotuna

7. Migogoro ya Ardhi

8. Mikato kwa Maaskari kwa upatikanaji wa *pay slip* na hasa ile *accessibility* ya wapiganaji wetu kuona mishahara yao katika *pay slip* zile

9. Ukataji wa pesa kwa wanamichezo waliokuwepo vikosini

Mhe. Naibu Spika, yote tumejumuisha kwa ujumla haya lakini michango mingi imezunguka humo humo. Naomba kuchukua nafasi hii niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa michango yao mizuri ambayo itasaidia katika utekelezaji wa kazi zetu. Nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote kwa kunisaidia kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe hasa Mhe. Haji Omar na Mhe. Machano Othman Said.

Mhe. Naibu Spika, shukurani za pekee naomba ziende kwa Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa Kuchaguliwa wa Jimbo la Kwamtipura ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi na pia ni Mwenyekiti anayesimamia Ofisi za Viongozi Wakuu, pamoja na Wajumbe wake wote ambao walisaidia sana katika kuipitia bajeti yetu, kifungu hadi kifungu tena kwa umakini sana. Hali hii sisi imetuwezesha kuwa na majibu ya hoja zote ambazo Waheshimiwa Wajumbe wamezitoa.

Mhe. Spika, michango mingi kama nilivyosema imejikita katika pongezi, mapendekezo, maoni, ushauri na kutaka ufafanuzi katika baadhi ya maeneo yakiwemo ya utekelezaji wa shughuli, maagizo na vifungu vilivyokuwemo katika kitabu cha kwanza cha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo kwa mwaka 2013/2014.

Aidha hoja nyengine zilizotolewa ni za Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, Maslahi ya Idara Maalum za SMZ, kama nilivyozungumza hapo awali.

Mhe. Spika, kuhusu utoaji wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, serikali inarudia tena msisitizo wake kwamba kwa mujibu wa sheria kwa kila Mzanzibari mwenye haki ya kupewa kitambulisho, kitambulisho hiki ni

lazima awe nacho. Haki ya kupewa kitambulisho hiki lazima awe nacho. Lazima awe nacho, serikali inaahidi kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba hakuna mwananchi atakayenyimwa kitambulisho hiki kama anazo sifa za kupewa kisheria.

Tunaomba wananchi wote wafuate taratibu zilizowekwa kisheria ili kila mmoja wetu awe na kitambulisho hicho. Kama baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe walivyosema, mimi mwenyewe binafsi nimefanya zoezi maalum Unguja na Pemba kwa kuangalia matatizo yanayozungumzwa juu ya vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, katika ziara hizo niliwashirikisha Waheshimiwa Wawakilishi, Waheshimiwa Madiwani, Masheha na Wakuu wa Mikoa na Wilaya.

Waheshimiwa Wajumbe mtakuwa mashahidi wangu kwamba tatizo kubwa ni kutokufuata taratibu za kisheria na kuna vitambulisho vingi vimerundikana katika Ofisi za Wilaya ambavyo wahusika hawajenda kuzichukua. Naomba niripoti Mhe. Naibu Spika, kwamba baada ya ziara yetu ya Pemba ambapo tuligundua vitambulisho si chini ya 22,000 vilivyorundikana baada ya ziara yetu, basi vitambulisho kama 6,000 tayari vimeshachukuliwa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la maslahi kwa wapiganaji. Naomba kusisitiza kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawapenda wafanyakazi wake wote na inawapenda zaidi wapiganaji wetu na maafisa wetu wa Idara Maalum za SMZ kutokana na mchango wao mkubwa na wa kujitolea kwao katika kulinda amani, usalama na kukuza uchumi wa nchi yetu, zaidi wao ndio walinzi wa mapinduzi yetu matukufu ya Januari 1964. Kwa hivyo tuna kila haki au tuna kila la kufanya ili kuwaenzi na wao wajisikia kweli wanaenziwa nchini mwao.

Mhe. Naibu Spika, serikali imekuwa mstari wa mbele katika kutetea maslahi ya hatma ya vikosi vyetu na ndio maana tukaviweka ndani ya Katiba. Tunaelewa kuwa maslahi madogo na makaazi duni waliyonayo ndio maana serikali imekuwa ikihangaika kutafuta majibu, sio majawabu ya kutatua tatizo hili. Katika kutatua maslahi yao kama alivyozungumza Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora, serikali tayari imeshaanzisha miundo ya kiutumishi ambayo maslahi yao italingana na vyeti vyao na taaluma zao. Hivi sasa muundo huo kama nilivyosema nishawasilisha katika Kamisheni ya Utumishi wa Umma ili iweze kutoa mapendekezo yao kwa serikali na hatimaye kuanza kutumika. Aidha serikali ipo katika mazungumzo na *ZSSF* ili Idara Maalum nazo ziweze kurejeshwa tena katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Mhe. Naibu Spika, katika kulitafutia ufumbuzi suala la makaazi, serikali imeagiza lazima vikosi vyote viandae mpango wa mkakati ili iweze kutoa majibu ya matatizo yao na njia zipi za kuyashughulikia. Chuo cha Mafunzo tayari wameanza kujitayarisha na vikosi vyengine wametenga fedha katika mwaka ujao wa fedha.

Aidha kuhusu posho za likizo za watumishi wa Idara Maalum za SMZ, fedha hizo hutolewa kwa kila anayestahiki kila baada ya miaka miwili na kuthibitisha hilo utaziona fedha hizo zimetengwa ndani ya vifungu vya kila Idara Maalum. Hata hivyo katika suala hili la likizo wenzetu askari wana utaratibu maalum ambao upo tofauti na uraiani, wao sheria inawalazimisha Idadi Maalum ya askari lazima wawepo kazini wakati wowote. Lakini iwapo kuna matatizo nawaahidi Waheshimiwa Wajumbe kwamba nitayafuatilia kama walivyoshauri.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu vifungu vilivyotuna, naishukuru Kamati yako ya Kudumu ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ambayo ilipitia na kuhoji bajeti yetu kifungu kwa kifungu na kupata ufafanuzi ambao umeridhika nao. Naamini Waheshimiwa Wajumbe na wao wataridhika na ufafanuzi ambao tutautoa na hatimaye wataiidhinisha bajeti yetu. Naomba kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwa kila kifungu kilichotuna na kilichopungua kina sababu zake za msingi zilizopelekea kuwa hivyo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu migogoro ya ardhi, serikali za Mikoa na Wilaya zinafanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba migogoro ya ardhi inaondoka kabisa. Hata hivyo nawaomba Waheshimiwa Wajumbe washiriki katika vikao vya ardhi na ambapo matatizo yote ya Mkoa na Wilaya husika huzungumzwa katika vikao hivyo. Kushiriki kwa Waheshimiwa Wajumbe katika vikao hivyo kutawasaidia sana kutatua migogoro hiyo kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu eneo la Darajani ni nia ya serikali kuhakikisha kwamba mazingira ya eneo lile yanaimarika na panakuwa mahali panapovutia kibiashara. Hali ilivyo hivi sasa hairidhishi hasa ukizingatia kuwa eneo lile ndio kioo cha Zanzibar kama Waheshimiwa wengi walivyozungumza. Serikali imepokea mapendekezo mbali mbali ya kuliimarisha eneo lile, ikiwa ni pamoja na kukiondosha kituo cha daladala na kuweka mpango mpya wa kudumu wa matumizi ya eneo la Darajani kupitia utekelezaji wa mradi wa *ZUSP*.

Vile vile serikali inaelewa kuhusu wafanyabiashara wadogo wadogo wanaotafuta rizki zao katika eneo lile. Hivyo serikali itaendelea kuwahakikishia wafanyabiashara hao wanakuwa na eneo zuri la kufanyia biashara. Hivi sasa eneo la Saateni limeshatengwa na linaendelea

kuendelezwa ili pawepo na huduma bora kwa wafanyabiashara wadogo wadogo, pia tunafikiria na maeneo mengine. Lakini pia tuliwaza hata kujenga *Shopping Mall* pale Darajani. Kama nilivyosema tumeshapokea maombi mawili tunayafanyia kazi kuona kama kweli pale panaweza kujengeka kwa hali ilivyo.

Ninachotaka kusisitiza Mhe. Naibu Spika, kwamba Waheshimiwa Wawakilishi sote tuwaelimishe wananchi wetu, wafanyabiashara wetu, ndugu zetu kwamba hakuna anayepigwa kutafuta rizki, lakini tufuate sheria, taratibu ziliopo basi. Haipendezi kutundika biashara katika Skuli ya Vikokotoni kwenye madirisha ya watoto wa skuli au leo kwenye ile njia ya Darajani inayokwenda Vikokotoni wanaiziba njia, wanapanga vitu chini.

Mwenzetu mmoja alizungumza kuhusu China hayapo yale bwana, sisi tumeona, wewe utajenga wapi kitu kama kile. Niliwahi kutoa mifano mingi. Hata Bara wenzetu wao wanatumia nguvu, sisi hatupendi kutumia nguvu wala hatutaki, tunawaheshimu watu wetu wote, tunawaenzi kama wanavyoienzi serikali yao. Kwa hivyo serikali haina nia wala haitokuwa na nia hiyo. Nawaomba sana Waheshimiwa tuwaelimishe watu wetu kwamba wafuate taratibu zilizokuwepo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu alisema kwamba nilisema kwamba wasishindane na serikali. Huo ndio ukweli kwamba mimi naamini kwamba kuna vijana wengine wanafanya kwa makusudi wanasema tuone mtatufanya nini. Lakini sisi hatuko huko, sisi tuko katika kujenga amani, utulivu, umoja, masikilizano katika nchi yetu tujenge nchi pamoja kila mwenye rizki yake atafute, mahala panapokwenda kisheria. Hivyo ndivyo ninavyosisitiza.

Nakuombeni sana Waheshimiwa Wajumbe mtusaidie kwa hili, haitopendeza kuwa-*encourage* kwamba wale wafanye tu mahala hata ambapo hapastahiki. Si vizuri hivyo. Mhe. Naibu Spika, kumradhi basi tuwaruhusu na hapa mbele ya stendi tukawaambia waje wafanyabiashara, maana yake kama hakuna sheria, hakuna taratibu popote tu wafanye biashara, tuwambie waje wapange biashara zao mbele ya uso hapo, utaruhusu Mhe. Naibu Spika. Lazima taratibu tuzifuate.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo ya jumla sasa naomba kutoa ufafanuzi juu ya hoja mbali mbali, kama zilivyowasilishwa na Kamati na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Kwanza kabisa naomba nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Shadia Mohammed Suleiman kama nilivyosema kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Viongozi Wakuu wa Serikali kwa namna alivyowasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi,

kwa umahiri na utulivu na kufahamika vizuri. Uwezo aliouonesha wakati anawasilisha maoni kwa niaba ya Kamati amedhihirisha kwamba yeye ni Mwakilishi makini.

Mhe. Naibu Spika, kama ilivyo kawaida kwamba mimi mwenyewe na watendaji wangu tumekuwa wasikivu sana kwa Kamati na tunachukua maoni na mapendekezo yenu mliyoyatoa yote na tutahakikisha kwamba tunayafanyia kazi. Aidha tunaipongeza Kamati kwa kutusaidia kuiboresha bajeti yetu wakati tulipokutana nao. Pia tunazichukua pongezi mlizotupa na zaidi zimekuja kutokana na ushirikiano wenu katika kipindi hichi kifupi tulichokaa nao. Pamoja na hayo Mhe. Naibu Spika, naahidi kwamba Kamati ushauri wao wa kuimarisha Idara Maalum za SMZ pamoja na kuwajengea uwezo watendaji wa Serikali za Mitaa tumeuchukua na tutaufanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nikiri kwamba mradi wa *ZUSP* umechelewa kuanza. Hii inatokana na matatizo mbali mbali yakiwemo taratibu za manunuzi na masharti ambayo benki ya dunia imeyaweka. Lakini hivi sasa tayari mambo kadhaa yameshachukuliwa hatua kama yanavyoonekana katika kitabu cha hotuba kiambatanisho Nam. 14 ukurasa wa 105.

Plan za ujenzi wa mitaro zipo vile vile kama ilivyoshauriwa hapo awali. Mhe. Hamza Hassan Juma usiwe na wasi wasi hakuna mabadiliko katika *plan* zile, tatizo tumechelewa tu kuanza, hakijabadilishwa kitu. Isipokuwa pesa kwa wakati ule zilivyokisiwa pengine zitapunguka, wameturuhusu kwamba tufanye maombi ya ziada lakini hakuna mabadiliko kuhusu *plan* iliyowekwa.

Mhe. Naibu Spika, suala hili pia amelizunguza Mhe. Salmin Awadh Salmin naomba kumtoa wasi wasi kuanza kwa utekelezaji wa mradi huu. Nakubaliana na ushauri wa Kamati kwamba ujenzi wa ukuta wa Ikulu ya Mkokotoni naahidi tutaujenga katika mwaka ujao wa fedha. Mhe. Bi. Panya pia alizungumza suala hili.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kuwepo kwa *master plan* ya wawekezaji na hasa baada ya wito wa Mhe. Rais, wawekezaji wa Kichina naomba kuliarifu Baraza lako kuwa serikali imejipanga vizuri kwa hilo na watendaji wa mamlaka ya kukuza wawekezaji uchumi, yaani *ZIPA* walikuwepo wakati wa ziara ya Rais na wanayafanyia kazi maagizo yote yaliyotolewa kwa maslahi ya Zanzibar. Kama nilivyosema katika utangulizi wangu nilielezea kuhusu utatuzi wa migogoro ya ardhi na kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe washiriki katika vikao vya Kamati za Maendeleo za Mikoa na Wilaya ili waweze kusaidia kutoa ushauri juu ya utatuzi wa migogoro ya ardhi. Hili ni tatizo letu sote tunaomba tushirikiane. Suala la migogoro ya ardhi pia

lilizungumzwa na Mbarouk Wadi Mussa na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. Baadae nitakuja kuitaja hasa hiyo migogoro yenyewe.

Mhe. Naibu Spika, niliahidi katika kikao kilichopita kuwa tutashughulikia hati miliki za mejengo yote ya Ikulu na nimefanya hivyo kama nilivyosema kwenye hotuba yangu. Hivi sasa hati miliki ya Ikulu ya Mnazi Mmoja tayari imeshapatikana na hati za nyumba nyengine za Ikulu zitatolewa hivi karibuni kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa kupitia mwenyewe Mhe. Waziri. Suala hili pia alilizungumza dada yangu Mhe. Asha Bakari Makame.

Mhe. Naibu Spika, tunaelewa kuwa fedha nyingi zinatolewa na Wazanzibari wanaoishi nchi za nje zinaletwa kwa njia zisizotajika rasmi, ndio maana sasa tunaanda sera ambayo itatoa miongozo ya kurahisisha baadhi ya maeneo na kupunguza gharama zenye mianya ya fedha. Naomba kulitaarifu Baraza lako tukufu kwamba fursa zilizopo katika Jumuia ya *India Ocean Reem* ni nyingi ikiwemo fursa za biashara miongoni mwa nchi wanachama, wawekezaji, wasimamiaji wa rasilimali zilizopo baharini, udhibiti wa majanga, maendeleo ya sekta ya sayansi na teknolojia, uendashaji wa sekta ya utalii na utamaduni. Jumla ya miradi mitatu inayohusiana na uhifadhi wa samaki aina ya jodari, kamba pamoja na majongoo ya pwani, unafuatiliwa utekelezaji wake na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la posho nyeti kwa wastaafu wa kitengo cha Mzanzibari Mkaazi, napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba hoja iliyotolewa na Kamati ya kupatiwa posho nyeti kwa watendaji wa Ofisi ya Usajili na Kazi ya Vitambulisho ni ya msingi na tunaikubali. Hivi sasa watendaji hao wanalipwa posho la shilingi ishirini elfu kwa mwezi, kwa mwaka ujao wa fedha watendaji hao watalipwa posho la shilingi hamsini elfu kwa mwezi. Hoja hii pia ilichangia na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na maoni ya Kamati kwamba pamekuwepo na malalamiko mengi yanayotokana na kuwepo kwa baa zinazouza pombe katika Wilaya zetu. Tatizo hili kwa sasa linafanyiwa kazi na zitaweza kutatuliwa baada ya kukamilika kwa sheria ya vileo. Muongozo wa rasimu ya sheria mpya ya vileo umeshakamilika, hatua inayofuata ni kuwasilisha kwa wadau ili kupata maoni yao na baadae kukamilisha utaratibu wa kupitisha sheria.

Mhe. Naibu Spika, Kamati iligusia suala la wanyama wanaozurura mjini. Kwanza kabisa tunapokea pongezi za Kamati walizotupatia kutokana na jitihada wanazochukua za kuwaondosha wanyama wanaozurura mjini. Hoja hii ya wanyama wanaozurura mjini pia ilichangiwa na Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa na Mhe. Hija Hassan Hija. Kama nilivyoeleza katika hotuba

yangu ukurasa wa 39 aya ya 113, jumla ya wanyama 119 wamekamatwa na wamepelekwa sehemu maalum iliyotengwa. Hadi sasa wanyama 140 wamegombolewa na wamekabidhiwa wenyewe. Wanyama 46 bado wanashikiliwa kutokana na wenyewe kutokufika kuwagomboa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la vitambulisho vya wageni kwa mara nyengine tena naomba kuiarifu Ofisi yako na naomba kuiarifu Kamati kwamba ofisi yangu kwa mwaka wa fedha 2013/2014 itaanza rasmi utoaji wa vitambulisho vya wageni baada ya kukamilika kwa marekebisho ya Sheria Nam. 7 ya mwaka 2005 tuliyoipitisha katika Baraza lako tukufu. Marekebisho haya yanaruhusu kuwapatia vitambulisho wageni maalum wote wanaoishi Zanzibar kwa ruhusa maalum. Mchakato huo wa kuwapatia vitambulisho wageni utafanyika kwa mashirikiano makubwa na Serikali za Mikoa ambapo wageni wanaoishi katika eneo la Nungwi nao watazingatiwa.

Aidha naomba kumuarifu Mhe. Hija Hassan Hija kwamba hadi sasa jumla ya wageni 17 wameshukiwa kupata vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Wageni hao 9 wa Kenya, 1 raia wa Oman, 2 wa Congo, 1 wa Zambia, 3 Msumbiji na 1 raia wa Comoro. Mhe. Naibu Spika, taarifa za washukiwa hao zimeshawasilishwa katika Ofisi za Uhamiaji kwa lengo la kuthibitisha uraia wao. Kwa yeyote atakayebainika kwenda kinyume na sheria ya usajili wa mwaka 2005 atachukuliwa hatua pamoja na kuifuta kadi aliyoipata kinyume na sheria.

Mhe. Naibu Spika, serikali kwa kushirikiana na Idara ya Uhamiaji pamoja na Bodi ya Mapato Zanzibar, itafanya juhudi za makusudi za kuitambua nyumba za watu binafsi ambazo wanaishi wageni. Nakubaliana na maoni ya Kamati kwamba wageni wanaoishi katika nyumba hizi huwa wanaikosesha serikali mapato.

Mhe. Naibu Spika, tunapokea kwa dhati ushauri wa Kamati ya kuimarisha maslahi ya watendaji wa Idara Maalum za SMZ. Serikali imefanya juhudi za makusudi za kutayarisha muundo wa Utumishi wa Idara Maalum za SMZ kama nilivyoeleza katika bajeti kwenye ukurasa wa 50 aya ya 150 ambapo miongoni mwa azma yake ni kuimarisha maslahi ya wapiganaji wa idara hizo. Hili kalieleza vizuri sana Mhe. Haji Omar Kheri. Wafanyakazi wote wa serikali wakiwemo wapiganaji na maafisa wanaruhusiwa kupatiwa *pay slip* za mishahara yao pindipo wanapozihitaji. Hivi sasa wapo baadhi ya maaskari, *pay slip* wanazitumia pale wanapoomba mikopo kwenye mabenki, kwa sababu hawapewi fursa hiyo mpaka ionekana hasa *status* ya mishahara yao.

Waheshimiwa wengi wamelichangia suala hili akiwemo Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Marina Joel Thomas, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe.

Omar Ali Shehe, Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Salmin Awadh Salmin walitaka kusisitiza tu kwamba uwezo wa kuangalia mishahara yao uko wazi, hawanyimwi fursa hiyo ipo tulikuwa tuna matatizo ya kuichapisha kwa sababu ya *volume* ya makaratasi ni kubwa. Lakini kwa maombi mengi mliyotwambia na ushauri mwingi mliotupa basi Waheshimiwa tunaichukua hili japo angalau kila miezi mitatu au miezi sita ichapishe wapewe mmoja moja kila mmoja ajionee mwenyewe. Ushauri wenu tunauchukua ili tutaufanyia kazi, kwa kushirikiana na Wizara ya Utumishi wa Umma na Wizara ya Fedha.

Mhe. Naibu Spika, ushauri uliotolewa na Kamati kwenye kikosi chetu cha Jeshi la Kujenga Uchumi kuendelea kujifunza kwa wenzao wa JKT ya Tanzania Bara, tunaupokea na tutaendelea kuufanyia kazi. Hivi karibuni maafisa wa JKU walikwenda kujifunza kwa wenzao juu ya namna ya kampuni ya SUMA JKT ilivyoanzishwa na ilivyofanya kazi. Elimu waliyoipata wataitumia katika kuanzisha shirika kama hilo hapa Zanzibar. Ushauri huu pia ulitolewa na Mhe. Marina Joel Thomas wakati alipokuwa akitoa mchango wake.

Mhe. Naibu Spika, tunakubaliana na hoja iliyotolewa na Kamati kwamba baadhi ya makaazi wanayoishi wapiganaji wa Idara Maalum ya SMZ hayaridhishi. Ofisi yangu inafanya juhudi za makusudi kutatua tatizo hili na kila mwaka huwa inatengwa bajeti maalum ya kufanyia matengenezo ya makaazi ya maaskari hao. Kazi kubwa imefanyika katika kipindi kilichopita na nawaomba Waheshimiwa Wajumbe, watembelee kuona hatua iliyofikiwa ya uimarishaji wa makaazi hayo.

Aidha Kikosi cha Zimamoto ya Uokozi kinategemea kuanza ujenzi wa Kituo kipya cha Zimamoto katika eneo la Uwanja wa Ndege Pemba katika mwaka ujao wa fedha. Kwa upande wa vyuo vya mafunzo katika bajeti ya mwaka wa 2013/2014 zimetengwa jumla ya shilingi milioni kumi na moja kwa ajili ya matengenezo madogo madogo ya vyuo vya mafunzo vya Pemba. Waheshimiwa wengine waliochangia hoja hii ni Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Wanu Hafidh Ameir na Mhe. Salma Mohammed Ali.

Mhe. Naibu Spika, ushauri wa kamati uliotolewa wa kukipandisha hadhi Chuo cha Mafunzo cha Ubago ili kusaidia msongamano wa wanafunzi katika vyuo vyengine vya mafunzo, tumeupokea na tutaufanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, tunamshukuru Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwa michango yake aliyoitoa na hoja zake kuhusu polisi jamii na Shehia ya Kwaalinatu. Tayari tumeshayashughulikia ipasavyo. Nampongeza sana yeye mwenyewe amekubali ameondoka na Maofisa wetu wamekwenda katika

Shehia wamekutana na watendaji wahusika na sisi tutafuatilia kuona kama haya mambo yamerekebishwa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu fungu la chakula la Baraza la Mapinduzi naomba kutoa maelezo kwamba fedha hizi ni kwa ajili ya kuhudumia gharama za vikao 12 vya kawaida vya Baraza la Mapinduzi, vikao 48 vya kawaida vya Kamati ya Makatibu Wakuu. Vikao vya Kamati vya Baraza la Mapinduzi ni vikao vya kupitia utekelezaji wa Wizara zote za *SMZ* maarufu kwa jina la bango kitita ambavyo hufanyika kila baada ya robo mwaka. Suala hili pia lilizungumzwa na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, naomba kusisistiza kwamba Baraza la Mapinduzi ndio chombo kikuu kinachoendesha Serikali na ndipo maamuzi makuu ya Serikali yanapotolewa. Naomba kumshukuru sana Mhe. Machano alitoa ufafanuzi mzuri juu ya suala hili.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa makubaliano ya vikao vya *Club* za michezo vikosini, askari wote ni wanachama wa timu hizo, hivyo ni wajibu wao kuchangia kila mwezi ili kuimarisha michezo vikosini na sio mpira wa miguu peke yake ila ni michezo yote ambayo huwapa afya njema na ukakamavu askari na kuweza kushiriki vyema mashindano ya kitaifa na kimataifa. Askari na Maofisa wote wanakatwa kwa kuwa wote wanahesabiwa kuwa ni wanachama wa *club* zao za vikosi. Hata hivyo Serikali kupitia bajeti za vikosi na Baraza la Michezo pia huchangia fedha zake pale panapotokea mashindano makubwa ili kuziwezesha timu hizo kushiriki vyema. Hoja hii imechangiwa pia na Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa kweli wanachokatwa ni shs.1,000/= na 2,000/= si zaidi ya hapo, kama kuna zaidi ya hapo tunamuomba mwanamichezo yeyote au mpiganaji yeyote basi atujuilishe na tutafuatilia tuone tunairekebisha kasoro hiyo. Lakini michezo Waheshimiwa ni gharama na *club* zetu nazipongeza kwa kweli ziko mbele katika kutwaa ubingwa kama nilivyosema si mchezo tu wa *football* lakini hata *netball*.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumthibitishia tena Mhe. Mshimba kuwa nafuatilia kwa karibu sana ajira za Idara Maalumu kwa kufanya ziara katika maeneo yote ambayo zoezi hili lilikuwa likiendeshwa na nitaendelea kufuatilia kila wakati. Aidha napenda kumhakikishia kwamba Serikali inawajali sana wazamiaji wetu kwa kuwa natambua wazi juhudi wanazozifanya na mazingira wanayofanyia kazi. Wazamiaji huwa wanapewa fedha za chakula ikizingatiwa kuwa huwa wanahitaji chakula maalumu kutokana na mazingira wanayofanyia kazi, kwa upande mwengine fidia huwa inatolewa baada ya kuthibitishwa na ustawi wa jamii na fedha zimetengwa kwa ajili hiyo. Hoja hii pia ilichangiwa na Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru sana Mhe. Asha Bakari Makame na pongezi zake kwa Mhe. Rais tunazipokea na tutamfikishia, naamini pongezi hizi ameshazisikia huko aliko kutokana na maendeleo ya teknolojia yaliyokuwepo hivi sasa duniani. Pongezi kwa Wakuu wa Mikoa wa Pemba kwa kufanikisha uwashaji wa mwenge nazo tumezipokea na wenyewe wamesikia. Tunashukuru kwa pongezi alizozitoa kwa utengenezaji wa Ikulu ya Mkoani, ushauri wake wa kujenga uzio wa mawe, kuzuia mmomonyoko tunauchukua na kuufanyia kazi ambapo katika bajeti ijayo tayari fedha zake zimeshatengwa. Hali sio mbaya kama labda Waheshimiwa wengine walivyonayo ni kule chini tu barabarani wakati wa mvua nyingi na ile miti ndio dongo limeporomoka, haijafika kwenye jengo bado, jengo liko salama.

Mhe. Naibu Spika, katika hoja yake ya kuimarisha masoko ya Darajani, Mwanakwerekwe, Saateni na Mombasa, tunamuahidi kuwa matatizo madogo madogo yaliyokuwepo tutayatatua katika mwaka ujao ambapo jumla ya sh.20,000,000/= kwa ajili ya soko la Saateni kwa kuweka vyoo na taa na sh. 6,000,000/= kwa ajili ya huduma za maji ya soko la Mombasa na sh.9,000,000/= kwa soko la Darajani kwa ajili ya kuimarisha miundo mbinu katika eneo la wafanyabiashara wa vyakula mama lishe. Ushauri wa Mhe. Asha Bakari wa kuweka *inspectors* kwa kushirikiana na Wizara nyengine tunaupokea na tunamuahidi kwa utaratibu huu wa kuwarejesha mpango ule wa zamani tutahakikisha kwamba tunautimiza mapema iwezekanavyo, na lile suala hasa la kuwapatia *uniform* maalumu.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru sana Mhe. Omar Ali Shehe kwa mchango. Aidha pongezi kwa Mhe. Rais nazo tumezipokea. Maelezo yake kuhusu mkutano wa *CUF* Mkoa wa Kaskazini Unguja yametolewa ufafanuzi mzuri na Mhe. Salmin Awadh, kimsingi Mkuu wa Mkoa wala Mkuu wa Wilaya hawakuzuia mkutano huo kufanyika. Ninafikiri kulikuwa na *breakdown communication*, kilichotokezea ni mgogoro wa umiliki wa kiwanja kile kwa makundi mawili ya wananchi ambao walikuwa wakivutana juu ya uhalali wa umiliki wa kiwanja kilichopangwa kufanyika mkutano wa *CUF* na bahati nzuri hata hivyo vikundi viwili kimoja kilikuwa cha Chama Tawala na kingine ni Chama cha *CUF*. Sasa wao wenyewe walikuwa wanapingana, hali kama hiyo halafu tumchukue Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais tumpeleke nafikiri Mkoa una ziara yoyote ya viongozi wetu Makamu wa Pili, Makamu wa Kwanza, Mhe. Rais, lazima tuhakikishe kuna usalama wa hali ya juu na kuna watu wenye kazi zao za kukagua waende wakaone na unaweza kumwambia Mheshimiwa usiende hilo lilifanyika.

Kwa hivyo Mhe. Makamu wa Kwanza kwa kweli mimi mwenyewe alinipigia simu, amempigia simu Makamu wa Pili na tukamueleza hali ilivyo, tatizo wale wenyewe kiwanja kile ndio walikuwa na mzozo, mikutano mingi *CUF*

wameshafanya Mkoa wa Kaskazini, hakukuwa na tatizo lolote na jana baada kule kuonekana mzozo wamekwenda wamefanya mkutano wao Upenja bugheri hakuna matatizo yoyote, lakini pale tumeshaona pana matatizo tupaepuke, sisi ndio dhima, sisi ndio Serikali kwenda kule unarushiwa madongo haina maana si vizuri. Kwa hivyo hayo tumeyafanya makusudi Mkuu wa Mkoa kaingia hapo baada ya kuona ile hali kule si nzuri. Kwa hivyo tusiwalaumu hawa hawana nguvu ya kuzuia mkutano lakini wao wanaingia kuzuia mikutano kutoa ruhusa kwa sababu ya usalama, hilo ndilo suala la msingi sana.

Mhe. Naibu Spika, hoja hii walichangia Waheshimiwa wengi sana kama nilivyosema lakini ufafanuzi wake hasa ndio huo, hakuna lengo lolote kila mmoja anasema sasa na chama chake, kila mmoja ana sera zake wazinadi kadri anavyoweza kwa mahala bila ya matatizo yoyote, hakuna tatizo lolote, muhimu ruhusa ya pale wenyewe wakubaliane tu basi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu hoja yake ya utambulisho kama nilivyosema namuhakikishia tena kwamba hakuna Mzanzibari mwenye haki ya kuandikishwa atakayenyimwa haki yake. Takwimu zinaonesha kwa mwezi wa Juni, 2013 Wilaya ya Kaskazini 'A', jumla ya vitambulisho 769 vimetolewa na Wilaya ya Kaskazini 'A' na Wilaya ya Kaskazini 'B' jumla ya vitambulisho 219 vimetolewa. Sasa Mhe. Omar Ali Shehe hiyo *list* unayosema ya watu 500 mbona haina tatizo lakini imetokea wapi saa hizi, hilo ndilo suala la msingi. Saa hizi unakuja na *list* ya watu 500 unaniletea mimi Waziri, mimi ndio mwenye dhamana lakini niko ofisini nina watu wangu wa *field* kule, mtu wangu wa *field* ni mwenye kitambulisho, Masheha wao ndio watasema huyu ni *qualify* huyu haja-*qualify* kwa mujibu wa sifa. Sasa hunitendei haki ukinambia Waziri utoe kauli, kauli yangu mimi nilikwambia mwanzo Mhe. Omar, turudi kwa wenye kazi zao Masheha wao ndio wataweka sawa, hanyimwi mtu muhimu tufuate utaratibu, hakuna tatizo lolote. Sasa ukija na *list* ya 500 saa hizi, mimi najiuliza watu 500 hao saa wametokea wapi, kwa nini muda wote wasijitokeze wakapewa, hapa kidogo panatia wasi wasi.

Mhe. Naibu Spika, hoja hii pia ilichangiwa kama nilivyosema na Mhe. Hijja, Mhe.Kazija na Mhe. Mohammed Haji Khalid.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Omar Ali Shehe aliulizia wasi wasi wake juu ya fedha za kuwalipa vijana wapya walioajiriwa katika Idara Maalum za SMZ. Naomba kumuhakikishia kwamba fedha hizi zipo na ajira zinafanywa kulingana na mahitaji ya ajira yaliyojitokeza. Kama alivyoeleza vizuri sana Mhe. Haji Omar Kheir kuhusu hoja yake ya ajira za mikataba namuhakikishia kwamba ajira hizo hufanywa kwa mujibu wa sheria na wale wote wanapewa

mikataba hiyo huwa wana ujuzi maalum ambao bado huwa wanahitajika katika vikosi vyetu. Fomu ya ajira aliyoonesha Mheshimiwa ambayo inataja chama cha siasa, nafikiri anafahamu fomu hiyo ni ya zamani sana wakati wa mfumo wa chama kimoja cha siasa, fomu hiyo hivi sasa haitumiki kabisa na si kweli. Mheshimiwa nitakupa baadae fomu ambayo inatumika hivi sasa, haulizwi mtu chama chako, haulizwi mtu popote, hiyo fomu sijui Mheshimiwa kaipata wapi, kwa kweli ni ya zamani mno, haitumiki hivi sasa, ajira zote zinafanywa kote. Nitaitafuta baadae nitakukabidhi ili uione.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Omar Ali Shehe, pia tunapokea ushauri wake kwamba Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwa waangalifu katika matumizi ya Wizara hiyo na hiyo ndio adhma ya Serikali sio kufuja fedha, lazima tuwe waangalifu naamini Kamati yake wakati wowote itakuwa pamoja nasi kuhakikisha kwamba hili linatendeka.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mhe. Jussa kwa mchango wake pongezi zake kwa Mhe. Rais, Mhe. Karume, Maalim Seif Sharif Hamad Makamu wa Kwanza wa Rais na mimi binafsi pia tunazipokea. Hoja yake kuhusu eneo la Darajani ni kama nilivyoelezwa hapo awali lakini tunasisitiza kuwa nchi inaendeshwa kisheria na taratibu ambazo tunajipangia wenyewe na wanaosimamia sheria hizo ni Serikali na vyombo vyake, hivyo basi kila moja ana wajibu wa kutii sheria hizo na sisi kama Wizara kupitia Baraza la Manispaa tunamuomba sana na hili nimeshawahi kuzungumza mara nyingi kwa Mhe. Mwakilishi tusaidiane tufanye kazi pamoja, yeye ndiye mwenye watu wa Jimbo la Mji Mkongwe, tufanye kazi kwa pamoja, uso wake tu pale akionana Mwakilishi kasimama Mhe. Jussa akitoa kauli itasikilizwa. Kwa hivyo nakuomba sana Mhe. Jussa nimeshawahi kukwambia hili, tusaidiane tuende kama Mwakilishi naamini *image* yako pale itakubalika na wala hakuna msokotano hakuna tatizo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Jussa anataka kujua matengenezo yaliyofanyika kwa nyumba za Ikulu na yale ambayo hayafanyika. Naomba kumueleza kwamba matengenezo yaliyofanyika ni pamoja na kukamilisha nyumba za Migombani pamoja na kujenga nyumba mpya tatu ndani ya eneo hilo ambalo ni *laundry* na majiko makubwa mawili, nyumba hizo ziliezuliwa mapaa na kuezekwa vigae, ukuta pamoja na *canop* nazo zimejengwa upya. Nyumba ya Bwefum iliezekwa paa, matengenezo yalifanywa pia na nyumba za Dodoma. Ikulu Kuu ya Mnazi Mmoja imejengwa *store* mpya pamoja na *laundry* nayo pia imefanyiwa ukarati. Nyumba ya Mkoani imefanyiwa matengenezo makubwa na inatarajiwa kukamilika hivi karibuni, matengenezo yaliyofanyika ni kuisuka upya nyumba hiyo. Ninaomba kumuhakikishia Mhe. Jussa, kuwa yeye ni mjumbe wa Kamati ya Kamati ya Ujenzi namualika na namuomba

tupate wasaa pamoja na Kamati twende tukatembelee na kuona mabadiliko ya nyumba hiyo, tupo tayari kupokea ushauri wake zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba sheria namba 3 ya mwaka 2005 imenipa uwezo na kuweka mipaka ya maeneo ya Baraza la Manispaa, kama unavyofahamu sheria hii sasa tunaifanyia marekebisho kwa mujibu wa sera ya Serikali za Mitaa ambayo tumeshakufanyieni semina na kuiridhia. Hivyo suala la mipaka pamoja na mambo mengine yataekwa vizuri katika sheria mpya ambayo inatarajiwa kuileta katika kikao kijacho cha Baraza. Mhe. Jussa pia alieleza kuhusu maaskari kufanyiwa kazi za ujenzi bila ya kupatiwa ujira. Kwa mujibu wa taratibu tulizoweka askari wanaofanya kazi za uzalishaji huwa analipwa asilimia 20 ya mapato yanayotokana kupitia na kazi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, wakati anatoa hoja zake Mhe. Jussa alitoa kielelezo cha barua cha wito wa askari kwa ajili ya kwenda kwenye mafunzo na akaeleza kuwa wito huo unatolewa kwa upendeleo. Naomba kumuhakikishia kwamba mafunzo ya askari yanafanyika baada ya kuangalia vigezo vingi vikiwemo afya, nidhamu na mambo mengine ya kiaskari na kamwe haifanywi kwa misingi ya upendeleo. Hata hivyo nimeshangazwa sana na kusikitishwa sana kuona barua ya Serikali tena inayohusu Idara Maalum ya SMZ inatolewa ndani ya jalada la siri la Serikali na kukabidhiwa Mhe. Jussa kuionesha hadharani ndani ya Baraza la Wawakilishi. Sisi kwa upande wetu tutafanya uchunguzi wa hali ya juu kabisa tuweze kubaini nani aliyetoa barua hiyo ndani ya faili, hili suala nafikiri lazima tuweke *sense of discipline* ndani ya vikosi vyetu haiwezekani. Mhe. Jussa, wewe uko-*right* kutoa lolote hapa lakini yeye aliyekwenda kuitoa barua ndani ya *file* siri akaiweka hadharani, huyo ni mhalifu kwa kijeshi na sisi tutafanya uchunguzi tuone kwamba hatua za kinidhamu tunazichukua dhidi yake.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimtaarifu Mhe. Jussa na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa kwamba kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti ukurasa wa 68 aya ya 208 kuwa sera za mradi wa shamba la mfano la pamoja Bambi kwa mwaka wa fedha 2012/13 zilizuiliwa na hazikuingizwa kabisa. Kamati ya wataalamu ya kuchunguza uendeshaji wa mradi huu iliundwa kama ilivyoagizwa na Baraza hili tukufu ambapo ripoti ya kamati hiyo imeshakamilika na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi, Mipango ya Maendeleo ndio walitayarisha na kuifanya kazi hiyo. Naomba kusema tu kwamba athari zilizosababishwa kutokana na kutotumika kwa fedha hizo ni kubwa sana pamoja na kuharibika kwa mbegu za nerika tani kumi na nane na mbolea ambayo ilitarajiwa kutumika katika shamba hilo.

Mhe. Naibu Spika, naomba nisome kwa muhtasari hiyo ripoti yenyewe ambayo imefanyiwa kazi na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya

Maendeleo. Ripoti inaitwa ripoti ya utafiti wa uendeshaji wa mradi wa shamba la pamoja kati ya Misri na Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, muhtasari wa ripoti ni *page* moja na nusu tu naisoma haraka sana.

> "Ripoti hii ni utafiti wa uendeshaji wa mradi wa shamba la pamoja la mfano kati ya Misrina Zanzibar kupitia Jeshi la Kujenga Uchumi. Madhumuni ya kazi hii ni kutekeleza agizo la Baraza la Wawakilishi la kufanya utafiti juu ya uendeshaji wa mradi ili kuweza kutoa taarifa kwa Kamati ya Kudumu ya Baraaza la Wawakilishi ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa na kuandalia mustakabali wa shamba kwa lengo la kupata taarifa zinazoonesha kwamba kuna haja ya kuendelea na mradi au la. Njia zilizotumika kukusanya taarifa za utafiti huu ni kufanya mahojiano na watendaji wakuu wa mradi ambao ni Jeshi la Kujenga Uchumi, Meneja wa Mradi na Mhandishi kutoka Misri. Pia Kamati ya Utafiti ilikutana na Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi wa Mradi iliyopo Zanzibar pamoja na kupitia kumbukumbu za mradi zilizopo.

Utafiti wa ripoti hii ulibaini kuwa mradi huu umepokea jumla ya shilingi zipatazo 1,316,363,532/= kwa miaka mitano kutoka SMZ. Katika utafiti huu Kamati imegundua kwamba mradi hauna mtiririko uliowazi wa kimaamuzi, matumizi mengi yamehusisha kiwango kikubwa cha fedha na kuwa matumizi mengi yana kazi zinazoshabihiana bila ya kufuata taratibu za Serikali za matumizi. Aidha, imegunduliwa pia utaratibu wa manunuzi, utunzaji na utoaji wa vifaa haukuwepo. Imebainika kuwa fedha nyingi za mradi zilikuwa zikitumika katika kununua vifaa vya ujenzi na mambo mengine ambayo hayahusiki moja kwa moja na kazi za shamba.

Kwa upande wa uzalishaji jumla ya shilingi zipatazo shilingi zipatazo 50,473,990/= zimepatikana kutokana na mauzo ya uzalishaji kwa kipindi cha miaka 4 kuanzia mwaka 2009/12. Kutokana na utafiti uliofanyika Kamati ya Wataalamu ya kuchunguza mradi imetoa mapendekezo yafuatayo:-

Uwepo mfumo unaofaa wa kifedha wa mradi utakaokubalika na Serikali zote mbili.

- Kuwe na Akaunti itakayoridhiwa na pande zote mbili na Mhasibu wake atakayekuwa na Mamlaka kamili kwa fedha za mradi.

- Uwepo mbadala wa kupata vibarua kutoka vijiji vya jirani.

- Kujenga madarasa ya kufundishia na kumaliza nyumba za wataalamu na kuweka samani.

- Mradi utafutiwe watendaji wenye sifa na uzoefu na kuwa na mkakati wa utekelezaji kulingana na malengo yaliyokusudiwa.

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa yapo mapungufu mengi yanayodhorotesha ya utekelezaji wa mradi na kupelekea uzalishaji kuwa ni mdogo ukilinganishwa na ukubwa wa eneo.Licha ya kuwepo kwa mapungufu hayo inapendekezwa kuwa mradi wa shamba la pamoja la mfano kati ya Misri na Zanzibar uendelee kwa kuwa unaweza kuifanya Zanzibar kuzalisha mboga mboga za kutosha, kukidhi mahitaji ya soko la utalii na watumiaji wa kawaida. Aidha mradi huu utawezesha kuimarika kwa kilimo na kuwa cha kisasa, kilimo cha umwagiliaji maji. Kukuza kipato cha mtu mmoja mmoja na hatimae shamba kuwa kituo kikuu cha utafiti wa mbegu na mazao mbali mbali. Haya yatawezekana endapo mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii yatafanyiwa kazi kikamilifu.

Kwa hivyo mapendekezo haya tumeyapata na sisi tunayafanyia kazi na ndio maana tukaona baada ya marekebisho baada ya sisi wenyewe kutafakari tuombe tena fedha ili tuendelee na mradi huu".

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, naomba Katibu amuoneshe Mhe. Mtando ili azidi kuiona.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Kazija Khamis Kona, namshukuru kwa mchango wake na lazima nimuombe radhi kwa kutomualika katika ziara yangu niliyoifanya Wilaya ya Kaskazini ‘A’ hivi karibuni. Napenda kumueleza kuwa ada aliyoeleza katika kanuni ya shilingi mia tano ipo kisheria, napenda kumueleza kuwa ada hiyo imeelezwa katika kanuni ya sheria namba 7 mwaka 2005 kifungu namba 4.

Mhe. Naibu Spika, Wazanzibari wanaoishi nchi za nje wametoa michango kadhaa kwa maendeleo ya Zanzibar. Kwa upande wa Unguja, Skuli ya Msingi ya Unguja Ukuu imefanyiwa matengenezo makubwa na Wazanzibari wanaoishi nchi za nje Canada, matengenezo hayo yamehusisha ujenzi wa madarasa 13, ofisi tatu moja ya mwalimu mkuu na mbili za walimu wa kawaida, *store* moja na chumba cha *computer* kimoja. Kwa upande wa Pemba Wazanzibari hao wametoa misaada yao katika Skuli za Mitiulaya, Skuli ya Kwale na Skuli ya Ziwani. Aidha Skuli imepokea msaada meza kumi na tatu, viti mia mbili hamsini na mbili, meza kubwa tano na viti thalathini vya ofisi ya walimu, msaada huu umetoka kwa Wazanzibari

wanaoishi Denmark. Skuli ya Ziwani imepokea msaada wa meza 147, viti 242, vyarahani 25 na *computer* 105.

Mhe. Naibu Spika, sekta ya afya kwa upande wa Unguja Wazanzibari wanaoishi nchi za nje hasa kutoka Canada wamechangia vifaa vya matibabu ya meno katika hospitali ya *Cottage* ya Makunduchi. Aidha Wazanzibari walitoa huduma ya matibabu ya meno kupitia *outreach program* katika maeneo ya Matemwe pamoja na kutoa msaada wa madawa katika Hospitali ya Wagonwa wa Akili ya Kidonge Chekundu. Vile vile hivi karibuni tulishuhudia msaada uliotolewa na Wazanzibari wanaoishi Uingereza katika Hospitali ya Jimbo la Kwamtipura, msaasa huo ulihusisha vifaa tofauti vya hospitali na kiti cha kung'olea meno, viti vya kukalia na vifaa vyenginevyo venye gharama ya 50,000,000/=.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Pemba, Wazanzibari wanaoishi nchi za nje wametoa msaada katika hospitali ya Chake-Chake, msaada huo ulihusisha vitanda vinne, meza nne pamoja na mashine sita za kuchunguza mapigo ya moyo.

Mhe. Naibu Spika, takwimu zinaonesha kwamba Wazanzibari wanaoishi na kufanya kazi nchi za nje wanachangia kiasi kikubwa cha fedha ambacho kinasaidia kupunguza makali ya umaskini kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kupitia mpango wa majaribio wa kutumia fedha kwa kutumia wakala wa *world remit* unaotekelezwa na Benki ya Watu wa Zanzibar, kuanzia tarehe 8 Februari mwaka 2013 hadi kufikia tarehe 31/5/2013 jumla ya miamara 284 yenye thamani ya 105,781,470/= ilifanyika, fedha hizi zilitumwa na Wazanzibari wanaoishi Canada, Sweden, UK, German, Norway, Australia, Finland, Island, Netherland, Denmark, Belgium, Zambia na France.

Mhe. Naibu Spika, misaada yote ya kijamii na kiuchumi pamoja na utumaji wa fedha kutoka kwa Wazanzibari wanaoishi nchi za nje itaratibiwa kwa umakini zaidi baada ya kuona sera ya *DIASPORA* ya Zanzibar ambayo itatoa muongozo wa namna ya kuyashughulikia mambo yote yanayohusiana na *DIASPORA*, sera ya *DIASPORA* inatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2013/14.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la soko la Kinyasini, ofisi inaendelea na juhudi ya kuimarisha huduma za kibiashara katika soko la Kinyasini Unguja. Katika kufanikisha hilo ofisi imeweka kifusi gari 21 zenye thamani ya sh.1,950,000/= ili kuzuia maji yanayotuwama katika eneo hilo. Aidha katika kutafuta ufumbuzi wa kudumu ofisi imefanya mazungumzo na mfuko wa

hifadhi ya jamii ili kuboresha soko, hatu iliyobaki ni kupatikana kwa hati miliki ya eneo hilo ili mazungumzo yakamilike na kazi ya ujenzi ianze mara moja.

Mhe. Naibu Spika, nampongeza Mhe. Mwanaidi Kassim kwa mchango wake mzuri, yeye alitaka kujua mmiliki wa nyumba iliyokuwa ikitumiwa kama Ofisi ya Wilaya ya Mjini. Naomba kumuarifu kuwa taarifa zinaonesha kuwa nyumba hiyo ni mali ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Aidha tunakubaliana na ushauri wake wa kuweka mazingira yake mazuri kwa wafanyabiashara wadogo wadogo akina mama.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumshukuru ndugu yangu Mtando kwa mchango wake. Aidha ufafanuzi wake katika vifungu vifuatavyo naomba nivisome. Kasma 220201 chakula na vinywaji, kima cha fedha zilizotengwa ni 303,000,000/= hii ya BLM, fedha hizi ni kwa ajili ya kuhudhumia vikao 12 vya kawaida vya Baraza la Mapinduzi, vikao 48 vya kawaida vya Kamati ya Makatibu Wakuu, vikao vya Kamati ya Baraza la Mapinduzi na vikao vya kupitia utekelezaji wa Wizara zote za SMZ ambavyo hufanyika kila baada ya robo moja ya mwaka.

Mhe. Naibu Spika, kasma nyengine ambayo anataka maelezo ni 220603 ununuzi wa samani yenye thamani ya sh. 17,800,000/=, fedha hizi ni kwa ajili ya ununuzi wa samani ambazo zitawekwa katika ukumbi wa Kamati ya Makatibu Wakuu baada ya kukamilika kwa utanuzi wa ukumbi unaotarajiwa kufanyika hivi karibuni. Kasma nyengine 220702 matengenezo makubwa ya jengo, kima cha fedha sh. 138,306,000/= fedha hizi ni kwa ajili ya matengenezo ya ukumbi wa kamati ya Makatibu Wakuu. Kasma nyengine ni 263078 ushauri nasaha na *HIV sh.*4,000,000/= fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya kupima afya za wafanyakazi kuhusiana na maradhi ya ukimwi pamoja na maradhi mengine kama vile *blood pressure*, kisukari na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, kasma nyengine ni 272108 kusaidia shughuli za kijamii, kima cha fedha zilizotengwa ni 18,000,000/= fedha hizi zimetengwa kwa makusudi kwa kusaidia shughuli mbali mbali za kijamii kwa Waheshimiwa Mawaziri watatu wasiokuwa na Wizara Maalum ambao wapo chini ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kasma nyengine ni 311202 ununuzi wa gari, kima cha fedha ni 50,000,000/= hii ni fedha iliyotengwa kwa ajili ya ununuzi wa gari kwa ajili ya matumizi ya kusambazia nyaraka pamoja na kufuatilia maamuzi na maagizo mbali mbali ya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake.

Mhe. Naibu Spika, kasma nyengine ni kasma 311216 ununuzi wa genereta, kima cha fedha ni 20,000,000/= hii ni fedha iliyotengwa kwa ajili ya genereta

la dharura kwa ajili ya matumizi ya ukumbi wa Kamati ya Makatibu Wakuu. Kasma Ofisi Kuu Pemba, Mhe. Mtando ametaka maelezo ya vifungu 30, ameniandikia karatasi vifungu 30 kutaka maelezo, vyengine viko *straight forward* kabisa lakini sasa ninatimiza wajibu wa kuvisoma kama alivyotaka.

Mhe. Naibu Spika, kasma 0301 Ofisi Kuu Pemba. 220501 vifaa vya kuandikia, kima cha fedha 8,843,000/= maelezo fedha hizi ni kwa ajili kuhudumia Ofisi Kuu Pemba kwa vile ofisi hii ndio kiungo cha Wizara nzima kwa Pemba. Kasma nyengine ni 220504 vifaa vya *computer*, kima cha fedha ni 11,300,000/= fedha hizi ni kwa ajili ya ununuzi wa *software* na *hardware* ambazo zilitakiwa kununuliwa katika mwaka wa fedha uliopita kutokana na kutopatikana kwa fedha hizi ofisi imepanga kununua katika mwaka huu.

Mhe. Naibu Spika, kasma nyengine ni kasma 221105 misaada ya wanafunzi, hii kwa Pemba haipo lakini Mhe. Mtando kaiorodhesha. Kasma nyengine ni 221199 vifaa vya mafunzo kwa Pemba haina bajeti lakini Mhe. Mtando kaiorodhesha. Kifungu chengine ni kifungu 311202 ununuzi wa gari hakina bajeti kwa Pemba, lakini Mhe. Mtando kaiorodhesha. Kifungu chengine ni 311203 ununuzi wa vespa chenye 3,000,000/= itanunuliwa vespa moja. Kifungu chengine 220601 ununuzi wa mapazia ni 7,830,000/= fedha hizi ni kwa ajili ya ununuzi wa mapazia 60 ya Ikulu ya Chake-Chake pamoja na mashuka 20. Kasma nyengine ni 220702 matengenezo makubwa ya jengo kiasi cha fedha ni 33,250,000/= maelezo ni kwamba fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya michoro ya jengo jipya la Ofisi ya Rais- Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kasma nyengine ni 211115 posho la kufundishia, kwa Pemba hakina bajeti lakini Mhe. Mtando kaiorodhesha. Kasma nyengine ni 220105 gharama za usafishaji, Pemba hakuna kifungu hicho. Kasma nyengine ni 220108 huduma za mtandao sh.3,294,000/= hii haikubadilika ni sh.3,294,000/= kwa mwaka huu na mwaka ujao sawa sawa.

Mhe. Naibu Spika, kifungu chengine ni 220201 chakula na vinywaji 15,290,000/= mwaka jana kimeshuka, hizi ni kwa ajili ya mikutano kisheria kama Kamati ya Ukaguzi wa Ndani, mikutano ya kila mwezi ya Maafisa Wadhamini na mafunzo ya ndani yanayoendeshwa na ofisi. Kasma nyengine ni 220203 viburudishaji, kina cha fedha ni sh.7,250,000/= mwaka ujao kimeshuka hizi ni kwa ajili ya mikutano kisheria kama Kamati ya Ukaguzi wa Ndani, mikutano ya kila mwezi ya Maafisa Wadhamini na mafunzo ya ndani yanayoendeshwa na ofisi. Mhe. Naibu Spika, kasma nyengine Mhe. Mtando, alitaka maelezo ni kasma 1101 Utumishi na Uendeshaji, kasma ni 220501 vifaa vya kuandikia, kima cha fedha kilichopangwa ni 24,883,000/=. Maelezo ni kwamba fedha hizi ni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia katika Ofisi ya Mhe. Waziri, Katibu Mkuu, Washauri wanne wa Rais, Idara ya

Uendeshaji na Utumishi, Kitengo cha Uhasibu, Kitengo cha Ununuzi na Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani.

Mhe. Naibu Spika, kasma nyengine ni 220106 gharama za matangazo, fedha yenyewe ni sh.18,280,000/= fedha hizi ni kwa ajili ya matangazo ya Bodi ya Wazabuni pamoja na matangazo ya sheria zote za kitaifa. Kifungu chengine Mhe. Naibu Spika, 220508 ununuzi wa magazeti sh.960,000/=, fedha hizi ni kwa ajili ya ununuzi wa magazeti ya Mhe. Waziri, Katibu Mkuu, Washauri wanne wa Rais, Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Kitengo cha Uhasibu na Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani. Kasma nyengine ni 220418 gharama za umeme ni sh.18,000,000/=, fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya kulipa umeme ambao wastani wa matumizi kwa kila mwezi ni 1,000,000/= ambapo 6,000,000/= zilizobakia zimepangwa kupunguza deni la umeme la ofisi.

Mhe. Naibu Spika, kasma nyengine au kifungu chengine kikubwa ni kasma 0801 Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, hapa Mhe. Mtando, kataka ufafanuzi wa vifungu vitatu. Kwanza kifungu 311202 ununuzi wa gari, fedha iliyotengwa ni sh.60,000,000/=, fedha hizi ni kwa ajili ya ununuzi wa gari moja la Idara. Kifungu chengine ni 311205 ununuzi wa friji, kifungu hichi hakikutengewa fedha. Mhe. Naibu Spika, kifungu chengine ni kifungu 311207 ununuzi wa kompyuta, kima cha fedha ni 10,800,000/= fedha hizi ni kwa ajili ya ununuzi wa kompyuta 5 ambazo zinatakiwa kuwekwa katika ofisi za watendaji wa Idara na kuziondosha kompyuta 5 za teknolojia ya zamani. Kasma nyengine kubwa ni kasma 0701 Ofisi ya Faragha ya Rais, kifungu 220105 gharama za vifaa vya uchapishaji 37,075,000/= fedha hizi ni kwa ajili ya kazi ya uchapishaji wa vitabu mbali mbali vya hotuba ya Mhe. Rais, katika maadhimisho ya miaka 50 ya sherehe za mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, kasma nyengine ni kifungu 220108 hotuba za mtandao. Kima cha fedha ni sh.57,000,000/=, fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya hotuba za *Internet* katika majengo ya Ikulu zote zinazotumiwa na Serikali. Kasma nyengine Mhe. Naibu Spika, ni 220203 viburudishaji ni sh.22,800,000/=, fedha hizi ni kwa ajili ya viburudishaji vya wageni ya Mhe. Rais. Kasma nyengine ni 220505 vifaa vidogo vidogo vyenye jumla ya fedha sh.36,533,000/=. Fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya matumizi madogo madogo yanayojitokeza ofisini kwa Mhe. Rais, na watendaji wa Ofisi ya Faragha. Kifungu chengine ni 220506 vifaa vya usafi ni sh.36,960,000/=, fedha hizi ni kwa ajili ya fedha zote za nyumba za Ikulu ambazo jumla yake ni 11.

Mhe. Naibu Spika, kasma nyengine ni 220603 ununuzi wa samani ni sh.90,000,000/=, ununuzi wa samani kwa Ikulu ya Mkoani na Ikulu Kuu ya Mnazi Mmoja kwa ukumbi wa wageni, nyumba ya Ikulu Mkoani iko tayari

lakini haina kitu, hivyo hasa ndio hizi zilipotengwa pamoja na kuweka sawa baadhi ya samani kwa Ikulu ya Mnazi Mmoja. Kasma nyengine ni 311202 ununuzi wa gari sh.12,890,000/= ununuzi wa gari mpya *canter*. Kasma nyengine ni 311216 ununuzi wa genereta ni sh.40,000,000/=, ununuzi wa genereta *KVA 100* ya Ikulu ya Dodoma. Kifungu chengine ni 220201 chakula na vinywaji, kifungu hiki tayari tumeshakielezea kile cha BLM ni sh.303,000,000/=. Nafikiri maelezo yake nimeshayasoma sidhani haja ya kuendelea tena. Kasma nyengine ni 220603 ununuzi wa samani ni sh.17,800,000/=, fedha hizi ni kwa ajili ya ununuzi wa samani ambazo zitawekwa katika ukumbi wa Kamati ya Makatibu Wakuu baada ya kukamilika kwa utanuzi wa ukumbi unaotarajiwa kufanywa.

Mhe. Naibu Spika, kasma nyengine ni 220702 matengenezo makubwa ya majengo, kima cha fedha kilichopangwa ni sh.138,309,000/=, fedha hizi ni kwa ajili ya matengenezo ya ukumbi wa Kamati ya Makatibu Wakuu. Kasma nyengine ni kasma 263178 ushauri nasaha na *HIV* sh.4,000,000/=, fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya kupima afya za wafanyakazi kuhusiana na maradhi ya ukimwi pamoja na maradhi mengine kama *pressure*, kisukari na kadhalika. Kifungu 272108 kusaidia shughuli za kijamii ni sh.18,000,000/=, fedha hizi zimetengwa makusudi kwa ajili ya kusaidia shughuli mbali mbali za kijamii kwa waheshimiwa watatu wasiokuwa na Wizara Maalum ambao wapo chini ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, hii ni *political vote*, waheshimiwa watatu kila mmoja ni sh.5,000,000,000/=.

Mhe. Naibu Spika, kasma nyengine ni 311202 ununuzi wa gari ni sh.50,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kusambaza nyaraka pamoja na kusaidia maamuzi na maagizo mbali mbali ya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake. Kasma nyengine 311210 ununuzi wa *generator* ni sh.20,000,00/=, hizi ni fedha zilizotengwa kwa ajili ya ununuzi wa genereta la dharura kwa ajili ya matumizi ya ukumbi wa Kamati ya Makatibu Wakuu.

Mhe. Naibu Spika, bado *list* ni ndefu kasma 0301 Ofisi Kuu Pemba, kasma hiyo ni 22051 vifaa vya kuandikia, hii nyengine nimeshazisoma hizi.

Mhe. Naibu Spika, utumishi na uwekezaji kasma 220501 vifaa vya kuandikia ni sh.24,883,000/=, fedha hii ni kwa ajili ya matumizi ya vifaa vya kuandikia katika Ofisi ya Mhe. Waziri na hii tayari pia nimeshaisoma. Kasma nyengine 220106 gharama za matangazo, 220508 ununuzi wa magazeti, 220408 gharama za umeme. Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ununuzi wa gari, ununuzi wa friji, ununuzi wa *computer* kasma 311202, 311205, 311207. Mhe. Naibu Spika, haya mengine Mhe. Mtando, labda anataka maelezo zaidi lakini nafikiri kifungu kinafafanua kwa uwazi kabisa hakuna matatizo.

Mhe. Naibu Spika, kasma ya Ofisi ya Faragha ya Rais, 220105 gharama za vifaa vya usafishaji sh.37,075,000/=, fedha hizi ni kwa ajili ya kazi za usafishaji wa vitabu mbali mbali za hotuba za Mhe. Rais, katika maadhimisho yajayo ya sherehe. Halafu chengine 220108, 220203 huduma za mtandao na viburudishaji.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema …

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, hivyo vifungu umeshavitaja mimi nafikiri unakuwa unavirudia rudia, sasa mimi nafikiri ungeliendea kwengine. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi(OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti wangu, lakini hivi nimefanya makusudi na nilimuomba sana Mhe. Mtando aniandikie hasa hivyo vifungu vyake na kaniandikia na hiyo nimefanya *homework* ya makusudi ya kupitia kimoja baada ya chengine ili kuepuka mabuti yake.

Aidha Mhe. Mtando, alitaka ufafanuzi kuhusu ukurasa wa 20 *paragraph* 46 kitabu cha Mhe. Waziri wa Nchi, nimeeleza kuwa semina mbili zimefanyika ambazo mbali na mambo mengine tulifanya tathmini ya utendaji kazi wa Serikali, semina hizo zimefanyika tarehe 26 hadi 28 Septemba Pemba na tarehe 1 hadi 3 Octoba mwaka jana hapa Unguja. Semina hizo ziliwashirikisha viongozi wa Serikali za Mitaa na Serikali Kuu wakiwemo Masheha, Madiwani, Maafisa Tawala, Maafisa Wadhamini, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Naibu Makatibu, Naibu Mawaziri na Mawaziri pamoja na viongozi wakuu wa kitaifa. Katika tathmini hiyo masuala 12 yalifanyiwa tathmini ya kiutendaji, Mahusiano baina ya viongozi, uwajibikaji wa wafanyakazi, uendeshaji wa majukumu ya kila taasisi, uhamasishaji wa majukumu ya kila mfanyakazi, maadili, sheria na kanuni za manunuzi, ukusanyaji wa mapato, kudhibiti matumizi yasiyokuwa ya lazima, taarifa na ripoti ya Mdhibiti na Mkakuzi Mkuu wa Hesabu, utaratibu wa mawasiliano, utunzaji wa kumbukumbu.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa tathmini hiyo utendaji wa Serikali katika maeneo yaliyofanyiwa tathmini ni kama ifuatavyo. Suala la mahusiano ni baina ya viongozi asilimia 79, uwajibikaji asilimia 80, uhamishaji wa majukumu ya kila taasisi asilimia 62, uhamasishaji wa majukumu ya kila mfanyakazi asilimia 78, ushirikishwaji wa wafanyakazi asilimia 89, maadili asilimia 79, sheria na kanuni za fedha asilimia 88, ukusanyaji wa mapato asilimia 64, kudhibiti matumizi yasiyokuwa ya lazima asilimia 93, taarifa ya

ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu asilimia 85, utaratibu wa mawasiliano asilimia 84 na utunzaji wa kumbukumbu asilimia 75.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mtando, alihoji kitengo cha *GSO* kupitia malengo yake. Kwa kawaida kitengo kinafanya *vetting* kutokana na maoni ya Kamisheni ya Tume ya Utumishi Serikali na Taasisi nyengine za Serikali, hadi kufikia mwezi Mach mwaka huu, kitengo kimefanya upekuzi kwa watumishi 168 lakini kuanzia mwezi wa April hadi sasa kitengo kimeshapokea maombi 60 ambayo yote yameshafanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, migogoro ya ardhi Mhe. Mtando, pia alitaka kuielezea lakini kama ninavyosema nafikiri akifungua *page 45* ya hotuba kifungu 131 kimeelezea hasa migogoro iliyopo katika Mkoa Kaskazini.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mhe. Marina kwa mchango wake, pongezi zake tunazipokea na tunamshukuru kwa maoni na ushauri alioutoa. Naomba kumuhakikishia kwamba Serikali tayari imeshafikiria kuanzisha kikosi maalumu cha ulinzi katika mahoteli. Ushauri wake katika udhalilishaji wa kijinsia na utoro wa wanafunzi tunauchukua, suala la utoro kwa wanafunzi pia limechangia na Mhe. Wanu ambaye alitaka mikoa mingine iige mfano mzuri wa Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mhe. Moh'd Haji Khalid kwa mchango wake, naomba nikiri kuwa hakuna kifungu maalum cha mchango wa *DIASPORA* katika pato la taifa bali michango yao inajumuishwa katika vifungu vya sekta kama afya, ujenzi na elimu. Aidha jumla ya sh.26,800,000/= alizozitaja Mhe. Mohammed hazikutumika kufanyiwa mikutano bali fedha hizo ni makusanyo ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani katika kipindi cha miezi tisa, anaweza kuangalia katika jadweli No. 9 ukurasa wa 66.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mhe. Wanu Hafidh Ameir kwa mchango wake, naomba kumuhakikishia kwamba rai yake ya uaandaji wa vipindi vya Rais kwa njia ya *documentary* tunaichukua. Ofisi yangu tayari imo katika ujenzi wa *studio* ambayo itaweza kufanikisha yote aliyoyashauri Mhe. Mjumbe. Aidha vifaa ambavyo nimevitaja katika hotuba yangu vifaa vya gari la mawasiliano atakalotumia Mhe. Rais Pemba. Kuhusu Ikulu ya Kibweni namuhakikishia Mjumbe kuwa mbovu bali inahitaji kutiwa rangi hasa kutokana na jengo lenyewe hapo lilipo rangi yake huchakaa haraka sana na mara kwa mara linahitaji *re-painting*.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mhe. Hija Hassan Hija kwa mchango wake. Aidha tunazipokea pongezi zake kwa taa zilizowekwa na Baraza la Manispaa na ushauri wake alioutoa tunauchukua. Napenda kumuhakikishia Mhe. Hija

kwamba Serikali inavipenda sana vikosi vyake na itafanya kila jitihada vya kuvienzi. Kuhusu suala la kujiunga na *ZSSF* sio kweli kwamba vikosi hivyo havijaingizwa kutokana na kujulikana idadi yake. Atakumbuka kuwa ulipoanza mfuko wa *ZSSF* mwaka 1998 vikosi viliingizwa katika utaratibu wa mfuko wa *ZSSF*. Hata hivyo kutokana na utaratibu wa kustaafu askari ambapo unalingana na cheo na umri. Hivyo ikaonekana sio rahisi wao kuendelea katika mfumo huo kwa kuwa sio wote wastaafu kwa miaka 55 au 60. Kama nilivyosema hapo awali kwamba Serikali inaendelea kuzungumza na *ZSSF* kurejesha tena suala hilo kwa mipango itayokubalika kwa pande zote.

Aidha Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hija, alitaka kujua kuhusu utaratibu wa bidhaa zilizokamatwa na askari wa Manispaa. Namuomba kumueleza kwamba bidhaa zote zilizokamatwa hupelekwa Mahakama ya Mwanzo ya Baraza la Manispaa na wenyewe hushtakiwa kwa mujibu wa makosa waliyofanya ingawa kuna baadhi ya bidhaa huwa zinaharibika kutokana na maumbile yake na nyengine hutoweka kutokana na purukushani za kukimbia kwa jina jengine wenyewe wanasema ngawira.

Mhe. Naibu Spika, tunamshukuru Mhe. Salmin Awadh kwa ufafanuzi mzuri. Naomba kwanza nisisitize hapo kwamba ile purukushani inapotokea askari kulikuwa na malalamiko mengi kwamba wanachukua bidhaa zile. Ushahidi tunao wa kutosha, kama itatokea *incident* ni bahati mbaya lakini askari wetu wana nidhamu ya hali ya juu kabisa, hawajishughulishi na hayo, tatizo linalotokezea ni kwamba wale askari wanapokwenda kuwaondoa wao wanakimbia, wanapokimbia sasa hapo ndio matatizo tena watu kila mmoja tena ndio inakuwa mchafukoge, ndio hayo niliyosema ngawira yeye anaviacha anakimbia kukamatwa akashtakiwa, ndio tatizo linapotokea, lakini tumefuatilia maaskari wetu kwa kweli huwa hawashughuliki na kuchukua. Nasema tunajitahidi maaskari wetu kuwapa nidhamu ya kazi na wana nidhamu kabisa na hayo kwa kweli hawayafanyi, kama itatokezea mtu kaona mmoja au wawili wanafanya tunaomba turipotieni na sisi hatutanyamaza tutachukua hatua za kinidhamu, lakini kabisa hatuwatumi hilo kama wakanyang'anye watu kama wanavyosema baadhi ya Waheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mhe. Salmin Awadh kwa ufafanuzi mzuri alioutoa kuhusu kufanya kwa mikutano ya kisiasa na utoaji wa vitambulisho. Kuhusu ushauri wake wa ving'ora katika eneo la Hospitali ya Al-Rahma tumeupokea na tutauwasilisha kwa wahusika. Hata hivyo ving'ora vya misafara zaidi inahusiana na usalama wa viongozi hawa ili kuhakikisha kwamba wanapita katika maeneo kwa haraka. Aidha tunamuahidi kwamba ule mkataba wa mshauri elekezi kuhusu ujenzi wa misingi ya maji machafu nitampatia. Kuhusu mradi wa taa za *Solar* za barabarani mradi huo bado upo katika majaribio na Serikali bado haujakabidhiwa rasmi hii ni *pilot project*,

matatizo yote ya kiufundi aliyoyasema na Waheshimiwa wengi waliyasema yameonekana na yatapatiwa ufumbuzi ikiwemo kuondosha vivuli vya miti vinavyozuia jua.

Mhe. Naibu Spika, suala la kufungua barabara katika eneo la Forodhani linahusiana zaidi na utekelezaji wa masuala ya Mji Mkongwe na utendaji ambao tumeugundua ambao unashirikisha ile hoteli iliyopo katika nyumba ya zamani ya watoto. Ni kweli hilo tumeliona na tutafuatilia tuone kwamba suala lile tunalirekebisha. Kuhusu ufafanuzi wa aya 156 ni kwamba ilikosewa inachotakiwa ni kwamba kuwepo na mashirikiano na Kamisheni ya Utumishi wa Umma, hii namshukuru Mhe. Waziri Haji Omar ameliweka sawa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Salma Mohammed aliulizwa kwa nini Sheha anaingizwa katika Serikali za Mitaa. Kweli Sheha ni Serikali Kuu ambayo imefika mbali sana ukilinganisha na Serikali za Mitaa, kumbe tunaliangalia hili na ndio maana Serikali za Mitaa tunataka tuzipeleke katika ngazi ya chini kabisa ili kazi hizo ziweze kutenganishwa. Kukosa cheti kwa mwanawe, mtoto amesajiliwa taarifa nilivyozipata na kitambulisho ameshapatiwa. Ujenzi wa *stand* ya Michakaeni inasubiri mshauri elekezi ambaye anatarajiwa kuwasili wakati wowote, hakuna miradi mengine miradi haitekelezwi na mikoa isipokukwa mkoa unahamasisha tu. Miradi mengine tuliambatanisha katika kiambatanisho nambari 15. Vitanda katika kikosi cha Zima Moto na Uokozi tayari vimeshapelekwa. Fedha za mshauri wa Wilaya ya Micheweni, fedha nyengine zipo na taratibu za zabuni zimeshakamilika, tunachosubiri ni ufunguzi wa zabuni hizo mara baada ya bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, pia alizungumzia kuhusu Mkoa kushirikiana na polisi jamii kwani iliyokuwepo haisaidii chochote, tumesikia ushauri wake na tutauhimiza mkoa kushirikiana nao. Madarasa ya kufundishia vyama vya ushirika fedha hazikutiwa na tuko tayari kutekeleza hilo. Kuhusu ujenzi wa kituo cha magari Chake Chake kituo hicho kinatarajiwa kujengwa na kwa sasa mshauri elekezi ameshaajiriwa kutoka Kampuni ya *MECCO* ambayo imeshaanza kazi hiyo tokea mwezi wa Juni na mwezi wa Julai tunategemea inshallah kazi hiyo kukamilika.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Bikame ana wasi wasi kuhusu fedha hizi sh.13,000,000/= zilizotengwa kutumika kwa upimaji wa eneo lililojengwa kwamba sahihi kwa ujenzi wa ukumbi wa mikutano ni sh.15,000,000/= ambapo fedha zilizotumika ni sh.1,432,000/= kwa kazi ya upimaji na kiwanja yaani *site plan*, uchoraji wa ramani na *bill of quantity*. Aidha kazi ya kutangaza zabuni zmeshafanyika na tayari zabuni zimesharejeshwa ambapo tarehe 27/6 zabuni hiyo imepangwa kufunguliwa na mara tu baada ya kumpata mzabuni wa ujenzi, kazi hiyo itaanza mara moja kwa vile fedha za

ujenzi huo zipo. Pia alitaka ufafanuzi kwenye kasma 211011 mshahara kwamba hakuna uwiano, lakini nafikiri akiangalia kwamba posho zote hasa katika kifungu cha 21000 mishahara tunasema inakuwa *based* kwenye *payment* ya mwezi wa Mach, mwezi huo hasa ndio tunachukuliwa mishahara ile tunapoi-*calculate* kwa mwaka huu ujao, tunatarajiwa *salary adjustment*, kwa hivyo inawezekana hapana uwiano lakini sio mkubwa. Posho zote zipo hapa katika 21104 alitaka nacho kifungu hichi maelezo, kuna *siting allowance*, posho la mafuta, chakula, nyumba na nyenginezo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kulikuwa na michango iliyokuja jioni, hii nilioleza ni michango mpaka tulipoondoka hapa. Sasa mimi sitaki niwachoshe sana naomba nitoe *summary* tu kwa michango iliyokuja mchana wa leo na zaidi utakuta tulikuwa tunarejea yale yale, zaidi kusisitiza suala la vitambulisho na waliochangia ni:-

1. Mhe. Saleh Nassor Juma
2. Mhe. Salum Abdalla Hamad
3. Mhe. Hassan Hamad Omar
4. Mhe. Abdalla Moh'd Ali
5. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
6. Mhe. Abdi Mossi Kombo
7. Mhe. Farida Amour Moh'd
8. Mhe. Subeit Khamis Faki na
9. Mhe. Assaa Othman Hamad

Mhe. Naibu Spika, suala la Manispaa Darajani pia walizungumza:-

1. Mhe. Salim Abdalla Hamad
2. Mhe. Saleh Nassor Juma
3. Mhe. Panya Ali Abdalla
4. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
5. Mhe. Hassan Hamad Omar
6. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
7. Mhe. Abdi Mosi Kombo
8. Mhe. Subeit Khamis Fakin na
9. Mhe. Assaa Othman Hamad

Mhe. Naibu Spika, waliozungumzia kuhusu maslahi ya vikosi ni:-

1. Mhe. Panya Ali Abdalla
2. Mhe. Hassan Hamad Omar
3. Mhe. Abdi Mossi Kombo
4. Mhe. Rufai Said Rufai

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Jaku, alitaka kujua ile baa ya Saateni, pale ile baa hasa si kwa jamii ya watu, ile ni kama mesi ya kambi na iko ndani ya kambi na haiko nje wale raia wanaruhusiwa lakini kwa nidhamu maalum kuingia mle ndani. Kwa hivyo ile niseme haiko kama mitaani lakini kama kuna kero za mitaani basi tutalifuatilia tuone kweli tunaweza kurekebisha na si lengo letu kukera jamii.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema sasa nikianza michango ya wachangiaji walioanza leo Mhe. Saleh, utakuta ni yale yale tu kwa kweli mimi nimshkuru sana na niseme yote aliyoyasema tumeyachukua, najaribu kuona alikuwa na *issue* gani niweze kujibu, lakini kwa jumla nimefuatilia nimeona mambo mengi ambayo yameguswa na Mhe. Salah, nimeyazungumza.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Salum Abdalla Hamad, na yeye pia alizungumza mengi yale yale nafikiri sina haja hasa kuyarejea. Isipokuwa naomba nisisitize kwamba suala la msingi sana lazima kuamini ndugu wa *ZID* wa vitambulisho vya Uzanzibari kazi kubwa wanayoifanya, kwa kweli wanaifanya na tuseme nakubaliana na Mhe. Bi. Panya kwamba elimu kwa watu wengine haijafika. Kwa hivyo tuwasaidie elimu na wafahamu na hasa kwamba umuhimu wa kitambulisho hichi cha Mzanzibari Mkaazi kwa wote, ni suala la msingi kabisa wote lazima tuwapatieni na wao wapate, si kwa uchaguzi tu lakini hiyo ni kama suala la msingi kwa kila mtu kulipata.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Bi. Panya na wewe tunakushukuru kwa michango yako yote uliyoyazungumza tumesikia, nimezungumza suala la ukuta kule wa Mkokotoni tutalifuatilia na ulizungumza suala la Kiwanda cha Ushoni kule, hili tumelizungumza kwenye ukurasa wa 65 ya hotuba yangu ibara ya 200 kwamba unasimamiwa na Idara Maalum na kiwanda kipo Sebleni. Umewapongeza Wakuu wa Mkoa tunachukua pongezi. Mhe. Mwanajuma Faki na yeye pia alizungumzia juu ya kiwanda hicho na kama nilivyosema kipo Sebleni kule.

Kulikuwa na wazo kwamba Mhe. Abdalla alizungumza hili na Mhe. Mwanajuma kwamba tuunde tume kwenda kuangalia vitambulisho ambavyo havijachukuliwa. Mhe. Naibu Spika, nafikiri hakuna haja ya kuunda Tume mambo yako wazi kabisa na wala si siri kwamba tumeshapiga kampeni vya kutosha kila Wilaya mtu akavichukue, sasa hawa waliokuwa hawavichukui mawili, pengine hawapo nchini au wamedanganya, wanaogopa kwenda kuchukua watakamatwa, maana ile *system* itakukamata, huo ni ukweli ulio wazi. Sasa mawili kwamba wanaogopa kwenda kuchukua au hawapo nchini na *system* ile ni nzuri kabisa. Tulifanya ziara na Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais kwenye Makao Makuu hapo ya vitambulisho na yeye alivyoikubali

ile *system* akasema waziwazi hakuficha mawazo yake pale, kasema hata *system* hii vitambulisho hivi tunaweza kutumia kwa kupiga kura, kwa sababu huwezi kudanganya kabisa, sura yako pale ukenda kama mara mbili umejiandikisha itakukamata tu, kwa hivyo Mkurugenzi akamwambia basi ushauri huo tunauchukua lakini mambo ya uchaguzi kuna taasisi yake. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, nataka kusisitiza tu kwamba ule ukweli wa kitambulisho cha Uzanzibari haikubaliki Zanzibar tu, kimataifa pia na kila mwaka wapo wakaguzi wanakuja wanakagua na tunapasishwa killillahi kwamba kweli sasa kitambulisho kile bado kiko kwenye *standard*.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mhe. Mlinde sana kwa maoni yake na lile wazo la Fungu Mbaraka mnara ule unaojengwa kule sio wa KMKM, nasikia mnara unajengwa na Wizara ya Mawasiliano, tutafuatilia hili tuweze kuweka sawa. Lakini rai uliotoa kwamba tutoe kama kumbukumbu kwa Muasisi wa KMKM Marehemu Meja Mlinde, tunalichukua wazo na tutaona vipi tunaweza tukafanikisha tukaona kweli tunataja kambi moja au chochote kumuenzi mzee wetu ambaye alikuwa mstari wa mbele katika uanzishaji wa kikosi hichi cha KMKM hapo mwanzoni.

Mhe. Naibu Spika, ndugu yangu Mhe. Hassan Hamad alizungumza kwa jazba kweli kweli, naomba nimuhakikishie yote aliyosema asiseme kwa uchungu, yeye anasema kwa uchungu, naomba usiseme kwa uchungu cha msingi kwamba tufanye kazi pamoja kama kuna matatizo tuyaondoe, sote ni ndugu sisi tuende pamoja lakini yale ambayo yanapaswa kufanywa yafanywe na yale ambayo yanakataliwa basi tuyaache, hatusemi bure bure, na sisi tunasema kama yapo matatizo tuambieni tuyarekebishe. Halafu ulisema *block No. 7,* ni kweli tunakiri kuna matatizo, Baraza la Manispaa wenyewe walifanya mikutano pale miwili lakini ajabu watu wengine wako maghorofani, mkutano uko chini wameteremka watu saba au wanane tu na bado wanawatupia mapakacha ya taka. Sasa ninataka kushauri sana waheshimiwa mtusaidie hii *attitude* kwenye usafi tuibadili, sisi kama Manispaa ni kazi yetu kweli kuondoe lakini wewe unaondoa mtu anakupopoa anasema kazi yako Manispaa hiyo, hivyo sivyo tuwaelimishe wenzetu, kwa *Block No*. 7 tunakubali kidogo hali yake hakujakaa sawa, tutafanya kazi pamoja lakini tusaidiane kuwaelimisha wananchi wajue kwamba hii ni dhima yetu sote.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu *GSO*, Mhe. Abdalla Mohammed Ali, alizungumza kwa ufasaha kabisa na kazungumza suala zima la *GSO* kwamba nafikiri nililizungumza kwa urefu na kazungumza kwamba kwa nini hawakutimiza lengo lao, nafikiri nimeshatoa sababu za msingi. Hata hivyo nataka kusema kwamba lazima tukubali kwamba *GSO* wanafanya kazi zao kwa uadilifu mkubwa na wanajitahidi kuona kwamba yale yanayopaswa kufanywa na

hakuna upendeleo wowote, *GSO* wanajitahidi kupata maelekezo ya Serikali waende vipi na wakamilishe malengo yao.

Mhe. Naibu Spika, mwengine alikuwa ni Mhe. Abdalla Juma, yeye alizungumza kuhusu Sheha yule wa Kilindi tumefuatilia ni Sheha wa Ndagoni tumegundua kwamba tatizo hasa ni uuzaji wa ununuaji wa ardhi. Yeye hana tatizo lakini yule aliyemuuzia nimepata taarifa kwamba ndio yeye aliyekwenda kuuza, halafu kukawa na matatizo kati ya wao wenyewe, nilipata taarifa lakini maelezo kidogo nimeya-*misplace* hapa. Lakini hata hivyo mimi nitafuatilia huo utendaji mzima wa Sheha huyu na tuone kama kuna matatizo vipi tutalirekebisha hilo suala. Nakuahidi hata wewe tutakuomba kidogo uje utusaidie.

Mhe. Naibu Spika, kapteni Abdi Mossi na wewe umezungumza mengi tunakushukuru ushauri wako lakini nakuomba sana kapteni utusaidie, vijana hawanyanyaswi wanatakiwa wapate riziki zao. Mhe. Farida, ametoa pongezi Kaskazini Pemba kwa ufuatiliaji wa kazi za maendeleo tunashukuru kwa hayo yote yaliyopo na ufuatiliaji wa Baraza la Wete na Konde, pia amesema kuwa fidia bado hazijalipwa mpaka zimalizwe kujengwa barabara. Hili si kweli labda mwenyewe Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano baadae au siku nyengine atakuja kutoa ufafanuzi zaidi. Lakini nakumbuka Mhe. Waziri alikujibu swali alizungumza kwamba kitu cha mwanzo wanapoanza kujenga barabara ni kutoa fidia ili baadae mambo yasije yakaharibika.

Utanuzi wa Soko Kuu la Mji wa Wete. Tayari mfadhili keshapatikana kupitia *ZUSP* na *consultant* naye ameshapatikana. Anasema pia yule Katibu wa Halmashauri, nafikiri hili limeshashughulikiwa hakuna matatizo na tumeona tusikorogane. Haifai kumfungia ndani ya chumba Mheshimiwa mzima, ndio bora tukaona tumpeleke kule na kule nako kuna matatizo, lakini naona kule anafanya kazi vizuri sana, amepandisha mapato kutoka shilingi 52 milioni mpaka 80.8 milioni, posho maalum za Madiwani ameshaanza kuwalipa kwa 50, lakini sasa tukaona basi tusikilize ushauri wenu ili tuepuke matatizo na shari.

Mhe. Asaa Othman Hamad tunashukuru *wisdom* yako na mambo mengi uliyozungumzia, nafikiri yote ni ya msingi na tutayasikiliza. Lakini nakuomba sana na wewe utusaidie tuwaelimishe wenzetu hakuna ubadhirifu. Mkurugenzi wa Manispaa ulizungumza kwamba hajachukuliwa hatua, nimeshasema kwamba ripoti ile tutaileta serikalini imeshafanywa uchambuzi wake tutaipeleka kwenye Baraza la Mapinduzi halafu italetwa kama si kikao hiki basi kijacho ile ripoti iko tayari.

Mhe. Subeit Khamis Faki na wewe tunakushukuru sana kwa maelezo yako na michango yako. Hatuna matatizo tunajitahidi sana watu wa Darajani kwenda nao sambamba wanatusaidia sote, nakujua Mheshimiwa mle kuna baraza zako unakwenda basi tusaidie kuwaelimisha wale vijana.

Mhe. Salma na wewe umetoa pongezi nyingi pia tunakushukuru. Mhe. Fatma Mbarouk na wewe umechangia mambo mengi madogo madogo lakini usiwe na wasi wasi mengi ya ushauri na tunauchukua tutaufanyia kazi.

Mhe. Rufai Said Rufai umeeleza na wewe mengi lakini kubwa umenishtusha uliposema kwamba miaka 50 najiandaa kusherehekea, unasema hakuna maendeleo miaka 50. Mhe. Rufai hebu tizama tulipo katika Baraza la Wawakilishi jengo hili tena yule Bwana Al-Youseif alitukopesha, lakini alitukopesha kulikuwa na mkopo, kulikuwa na mengine ni msaada lakini huo msaada kidogo, pesa nyingi za mkopo na ilikuwa kwa miaka 16 sijui 17 lakini tumeshazilipa zote.

Mhe. Rufai nakuomba wewe mtu mzima una umri mkubwa kaitizame Ofisi ya *LEGICO* iliyokuwa ya zamani, nakupa *home work*, najua unajua ilipo. Ofisi hiyo ya *LEGICO* ilivyo halafu ulinganishe na jumba hili la Baraza la Wawakilishi. Halafu utizame pale unapotoka Pemba najua unapanda ndege yako ya Al-Salaam, najua unaipenda wewe na unapenda kiti cha mbele kile, ukikaa kiti cha mbele kile hebu tizama chini kidogo utizame hizi nyumba zilivyotandawaa, hayo yote ni maendeleo. Mbali ya hayo lakini tizama na vijana wetu upenda wa elimu, afya, miundombinu.

Mimi juzi nilikwenda barabara ya Mtambwe nikakuta inavyochongwa niliwatania Mhe. Abubakar na Mhe. Salim Abdalla nikawaambia barabara ya Mtambwe kama milima ya kitonga kule Iringa milima ilivyochongwa, leo unasema hakuna maendeleo. Naona Mheshimiwa lazima tuseme Mapinduzi Daima.

Mhe. Rufai alizungumza suala la sare za kiaskari. Ile ni gadi moja tu ya askari 120, najua tunaiandaa na sherehe, kwa hivyo ile ni gadi ya askari 120 na hakuna wasi wasi wa matumizi yake. Sasa KVZ alizungumza wana mishahara midogo. Kwa kweli hiki kikosi mwanzo kilikuwa na matatizo ya uanzishwaji wake. Sasa kimeshatulia na tunaendelea nacho vizuri na kinafanya kazi nzuri sana ya ulinzi. Kwa hivyo, naomba tuvi-*suport* na *Inshaallah* kadri itavyokuwa *ceiling* yao wataongezewa.

Mhe. Mussa Ali Hassan tunakushukuru sana kwa ushauri wako, yote uliyotueleza haya tutayazingatia. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa

Umma na Utawala Bora nakushukuru sana sina la kuongezea kwa uliyoyazungumza.

Na mwisho Mhe. Machano Othman Said (Waziri asiye Wizara Maalum) na yeye pia tunamshukuru sana kwa mchango wake. Waheshimiwa ningependa wote hawa nichambue kama nilivyochambua pale mwanzo lakini muda nafikiri mtanipa masaa mengine mawili. Sasa naomba tena kwamba ushauri mliotupa, maelekezo yote tutayachukua tutayafanyia kazi hasa hii ni wizara ya wananchi, hii ni wizara ya watu, ni *community* na jamii pamoja na sisi Waheshimiwa Wawakilishi. Kwa hivyo, naomba sana tufanye kazi pamoja wizara yetu bila ya nyinyi hatwendi, bila ya Madiwani hatwendi, bila ya Masheha hatwendi huko ndiko kwenye jamii na jamii ni watu. Kwa hivyo, naomba haya tufanyeni kazi pamoja tushirikiane, tubadilishane mawazo, tupeane, tuambizane sisi hatuna matatizo kama watendaji wenu tuko tayari kukosolewa, kuelekezwa ili tufanikishe malengo yetu. Wizara, vikosi havina ubaya na mtu sote nia safi wenyewe kwa wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri ametoa hoja sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 17 – JESHI LA KUJENGA UCHUMI

Kifungu 0201 Utawala Unguja	25,000,000/-
Jumla ya Fungu	**25,000,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 18 – CHUO CHA MAFUNZO

Kifungu 0201 Idara ya Vituo cya Mafunzo	41,000,000/-
Jumla ya Fungu	**41,000,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 29 – KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO

Kifungu 0201 Utawala	15,830,000/-
Jumla ya fungu	**15,830,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 32 – KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Kifungu 0201 Utawala Unguja	10,000,000/-
Jumla ya Fungu	**10,000,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 43 – AFISI YA USAJILI NA KADI ZA UTAMBULISHO

Kifungu 0201 Utawala Unguja	16,500,000/-
Kifungu 0301 Afisi Kuu Pemba	6,000,000/-
Jumla ya Fungu	**22,500,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 07 – OFISI YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA NA URATIBU WA WAZANZIBARI

Kifungu 0601	Uratibu wa Uchumi na Ushirikiano wa Kimataifa	873,000,000/-
Jumla ya Fungu		**873,000,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 08 – OFISI YA RAIS BARAZA LA MAPINDUZI

Kifungu 0501

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia suala hili nilitegemea sana kupata maelezo mazuri kwa Mhe. Waziri, lakini kwa bahati nzuri nilipokuwa hapo nje nimemsikia Mheshimiwa ambaye amenijibu yeye hana hata meza, kiti wala bajeti; amenijibu suala hili. Kwa hivyo, ningeomba sana sasa nimsikie mwenyewe anieleze kuhusu fungo hili kasma yake ya 220201 ya Ikulu shilingi 303 milioni za vyakula. Naomba Mhe. Waziri anieleze ili niweze kumuachia.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nilieleza lakini Mhe. Makame Mshimba madhali ametaka maelezo ya ziada basi naomba niyatoe.

Kuhusu mchanganuo wa vikao vya Baraza la Mapinduzi kwanza idadi ya vikao kwa mwaka ni 48, kwa kila kikao kimoja shilingi 2,400,000; kwa ujumla gharama kwa mwaka ni shilingi 115,200,000.

Halafu tunakuja vikao vya Makatibu Wakuu, kwa kila kikao shilingi 1,500,000, vikao 48 shilingi 72,000,000. Halafu vikao vya kamati za Baraza la Mapinduzi shilingi 800,000 kwa kila kikao, idadi ya vikao 12 jumla ya gharama kwa mwaka shilingi 9,600,000.

Mikutano ya Mhe. Rais na wizara mbali mbali maarufu Bangokitita kila kikao kimoja shilingi 1,400,000; idadi ya vikao ni 57, jumla ya gharama kwa mwaka ni shilingi 79,800,000. Vikao vya dharura vya Baraza la Mapinduzi na Makatibu Wakuu kwa kila kikao shilingi 2,400,000 inategemea dharura itavyojitokeza kwa hivyo, tumetia kama shilingi 26,400,000. Ukijumlisha hizo Mhe. Mwenyekiti, unapata shilingi 303,000,000 na ushei.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba kidogo Mhe. Waziri wangu anifahamishe kitu kimoja. Kwa sababu hapa kuna neno viburudishaji ina maana chakula na vinywaji, unajua Kiswahili kina tafsiri nyingi Mhe. Mwenyekiti. Sasa ningemuuliza ni ulaji mtupu au pamoja na posho wanalopewa hawa watu. Ningeomba kidogo anifafanulie, akinambia kama ni ulaji basi ningemuomba kifungu hiki anibadilishie sentensi kwa sababu itakuwa si vizuri kutamka vinywaji kwa shilingi 303,000,000 watu watatafsiri vyengine. Hebu mimi nimuombe Mhe. Waziri anieleweshe vizuri, kwa sababu mtazamo wa watu wengine na mimi unakuwa ni tofauti. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana sitaki Mhe. Waziri nimuinue ndio *practice*

yenyewe ya leo kuwa anifahamishe vizuri kuwa pamoja na posho, vinywaji na chakula.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumhakikishia Mhe. Makame Mshimba kwamba humu hamna posho hata senti moja, hizi ni makulati tu na vikao vile kama mimi na yeye ni mawaziri hapa mpaka saa nane usiku, saa nane usiku vikao tunafanya, yaani *average* wakati wetu saa sita saba, sasa usipokuwa *active* unakula kula na kunywa utafanyaje kazi. Kwa hivyo, nakuhakikishia Mhe. Mwenyekiti, kwamba humu hamna posho hata moja. Ndio hakuna ruhusa tu lakini Inshaallah tutakuja kumualika baada ya vikao Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kutoa nyongeza ndogo kuhusu taarifa aliyoulizia Mhe. Makame Mshimba kuhusu mchango wa Mhe. Machano Othman, MBM ambaye pia ni Waziri asiye na Wizara Maalum.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Machano wakati alipokuwa anatoa mchango wake alitoa mchango kwa niaba ya serikali kwa kuwa yeye ni Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi anaelewa fika mambo ya vikao vile na ndiko anakofanyia kazi. Kwa hivyo, kumwambia kwamba hana kiti na meza na haelewi sio vizuri. Mhe. Machano ana kiti, ana meza na ana ofisi yake na anayajua anayoeleza. Kwa hivyo, alitoa ufafanuzi ule kwa niaba ya serikali na kwa kuelewa kabisa. Sasa ningependa tu kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba huyu ni Mhe. Waziri na ni Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi analolisema lolote hapa pia analisema kwa niaba ya serikali.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nishataka kusema kuwa tuachie, lakini na mimi nasemaje, Mheshimiwa ukitamka neno waziri asiyekuwa na ofisi maalumu hakuna mtu asiyejua tafsiri yake ina maana kuwa wewe huna *special* ambayo….

Mhe. Mwenyekiti: Sio ofisi maalum asiyekuwa na wizara maalum.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Wizara asiyekuwa na ofisi maalum au sio? Sawa nimekuelewa Mhe. Mwenyekiti, ndio hivyo hivyo. Sasa tafsiri yake inaonesha kuwa hana wizara maalum ndio maana yake, sasa ndio maana nikasema kama wewe ukiwa huna wizara maalum hata na bajeti utakuwa huna. Siko huko sasa ningemuomba sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kumwambia sikuwa na tafsiri mbaya kwa sababu nikimuuliza ofisi yake iko wapi atanambia hana, meza yake siijui wala kiti chake.

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Waziri mhusika kuwa kifungu hiki mimi sasa namwambia tuendelee.

Kifungu 0501

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi na nimshukuru waziri kwa ufafanuzi wake wa mambo ambayo tumeyachangia hapa. Katika mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, niligusia suala la bajeti inayohusu ujenzi na matengenezo ya majengo yaliyokuwa katika Ikulu na Ofisi ya Rais kwa jumla. Sasa sitaki kuyagusia kila pahala lakini nitaomba niulizie hapa na baadae niulizie nikifika katika Ofisi ya Rais Ikulu. Kwa sababu hata hapa kwenye Baraza la Mapinduzi ni sehemu ya Ikulu au Ofisi ya Rais kwa pamoja katika ukurasa wa 47 fungu la matengenezo ya ofisi nyumba, fungu Nam. 220700 liko ukurasa wa 47 pale inaonekana kwamba kwa miaka kadhaa sasa kila mwaka kunakuwa na fungu si dogo la matengenezo madogo ya ofisi na matengenezo makubwa ya majengo.

Ili nifahamike Mhe. Mwenyekiti, mwaka 2010/2011 fedha hasa zilikuwa shilingi 62,930,347/-; mwaka 20112012 ilikuwa shilingi 156,998,000; mwaka uliomalizika 2012/2013 makisio ni 192,200,000 na mwaka huu imeombewa shilingi 145,509,000. Nilikuwa naomba kujua haya matengenezo ni ya nini ambayo hayamaliziki kila mwaka.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Ismail Jussa alitaka kujua matengenezo haya ambayo kila mwaka yapo. Kwa ujumla Ikulu zetu zote na nyumba za wageni wa serikali hazipungui 15 Unguja na Pemba. Sasa mwanzo zilikuwa kidogo nyengine tumeziacha, lakini tumeona kwamba tukiziacha tunazidi kuteketea kama ule mfano mliotoa wa Kibweni kwamba nyumba mbona haipendezi. Nyumba ndani nzima lakini inataka chokaa tu. Kwa hivyo tunamhakikishia kwamba hii *volume* anayoiona ni kweli hizo *figure* na matengenezo yameongezeka Dodoma, Dar es Salaam, Pemba Zanzibar, Mkokotoni mpaka sasa tupande zaidi twende mpaka Micheweni tuimalize.

Kwa hivyo, *volume* kama nilivyosema ni nyumba hizo, Ikulu kubwa na hizo *State Lodges*, sasa ndio zote zinatengenezwa na hatuzipati zote. Nafikiri akiangalia mle kwenye ile *grade* ataona ile *flow* yenyewe.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba waziri aniwekee sawa kwa sababu hili fungu la matengenezo linaonekana katika maeneo mengine vile vile katika Ofisi ya Rais Ikulu. Sasa hili la Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi nilikiuwa nataka kujua hili linahusu matengenezo ya majengo yepi hasa, haya ndio majengo ya Ikulu mbali mbali alizozitaja au

haya kuna majengo ambayo yako chini ya Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi. Hilo moja.

Lakini pili katika majibu yake kasema kwamba fedha hizi mara nyengine wanakuwa hawazipati zote, naweza kuelewa kwa ile ya mwaka jana kwa sababu bado inaambiwa ni makisio, *approved* haijafika mwisho wa mwaka. Lakini ile miaka miwili ya mwanzo Mhe. Mwenyekiti, hii ni hasa yaani *actually* kilichopatikana, kilichoingizwa katika wizara. Kwa mwaka wa 2010/2011 ilikuwa shilingi 62,930,347; kwa mwaka 2011/2012 ilikuwa shilingi 156,998,000. Hii ni hasa Mheshimiwa sio kile kimepitiwa katika miaka iliyofuata. Sasa hapa nilikuwa nataka maelezo ili yanikinaishe na tuweze kuendelea.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli alivyozungumza Mhe. Jussa lakini nataka kumhakikishia kwamba ya mwaka jana ni makisio *approved,* lakini kazi yenyewe hasa tuna matengenezo makubwa sana nyumba ya Migombani. Nyumba ya Migombani Mhe. Rais Mstaafu alipoondoka yeye alikuwa hatumii sana nyumba ile, kwa hivyo Mhe. Dr. Shein alipokuja tulifanya *major repair* ambayo yana *qualify* kabisa na hicho kifungu, mle hata ukuta unaouona umebadilika ule, tumetengeneza *park* zile, vifaa vile tumebadilisha.

Kwa kweli hiyo kazi Mheshimiwa nasema imefanywa pale lakini hata Ikulu ya Mnazi Mmoja pia ilikuwa inavuja na *Laiboni* vile vile, Dodoma halikadhalika. Kwa hivyo, utakuta Mhe. Jussa kwamba hizo kazi za *major maitenance* kweli zimefanyika na zime-*qualify* hiyo pesa aliyosema na mwaka huu tumeikisia 1.5. Unajua Ikulu siku zote iwe *to the standard*, kila siku lazima iwekwe sehemu nyumba ya wageni, vumbi lisianguke kwa hiyo pesa kwa kweli sisi tungeomba zaidi lakini ndio tunapata hizi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 0501 Baraza la Mapinduzi	1,379,000,000/-
Jumla ya Fungu	**1,379,000,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 10 – OFISI YA RAIS IKULU

Kifungu 0301

Mhe. Mbarouk Mussa Wadi: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi nipate ufafanuzi wa ziada kidogo kutoka kwa Mhe. Waziri. Nilikuwa naomba ufafanuzi katika fungu 0220702 Matengenezo Makubwa ya Majengo, shilingi 33,000,250 nilikuwa naomba ufafanuzi wake. Kwa sababu na huku nyuma tunakotoka ameeleza tena kwamba ni ukarabati wa Ikulu, ingawa na huku kuna mradi wa ujenzi wa Ikulu, lakini na hapa sasa naona kuna shilingi 33,000,250 nilikuwa naomba ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kifungu hiki hapa tuna ofisi yetu ya Afisa Mdhamini Pemba. Kwa hivyo, tume-*plan* kuanza ujenzi mpya, lile jengo ni kongwe. Kwa hiyo tunatarajia tuanze Ofisi yetu ya Pemba. Kwa hiyo, kazi za michoro na kazi za mwanzo yaani awali ndio gharama hizi.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee

Kifungu 0301 - Afisi Kuu Pemba 645,805,000/=

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilimuuliza Mhe. Waziri kwamba kuna kiwanda hichi cha ushoni na katika majibu yake alionijibu alinambia kiko Saateni. Lakini jibu ninalolitaka zaidi ni kwamba mradi wa Zanzibar uliidhishiwa milioni mia mbili na hamsini na sita nukta ziro. Hadi kufikia Machi 2013 mradi uliingiziwa shilingi milioni tano nukta nane ambazo ni sawa na asilimia mbili nukta tatu ya makadirio ya matumizi na kutelekeza yafuatayo.

Kugharamia shughuli za uendeshaji wa kiwanda zikiwemo ununuzi wa vifaa vidogo vidogo kama mikasi na nyuzi za kushonea. Hapa nilimtaka Mhe. Waziri anieleze shilingi milioni mia mbili na hamsini na sita, kilichonunuliwa ni nyuzi na mikasi ambazo zina thamani ya shilingi milioni tano nukta nane.

Halafu vile vile kifungu cha 201 kwa mwaka wa fedha 2013/2014 mradi wa kuimarisha kiwanda cha ushoni umetengewa shilingi mia tatu na hamsini nukta ziro milioni. Utatekeleza kazi zifuatazo ununuzi wa vifaa pamoja na kutafuta mali ghafi za uzalishaji. Jengine kujenga uwezo wa watendaji wa viwanda. Hapa nataka Mhe. Waziri anieleze ni kigezo gani ambacho kimetumika shilingi mia mbili na hamsini na sita na zikatumika shilingi milioni tano nukta nane na huku kukatengewa shilingi mia tatu na hamsini. Hapa naomba ufafanuzi zaidi Mhe. Waziri anieleze. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, napenda kumfahamisha Mhe. Mwanajuma

Faki Mdachi kwamba huu ni mradi wa maendeleo na huu mradi angesubiri kwenye mradi wa maendeleo. Lakini si neno nitamjibu kabisa.

Kwa mwaka jana hizo pesa alizoziona zimewekwa hapo kwa kweli hatukuzipata tumetumia hizo kama alivyosema shilingi milioni tano nukta nane kwa uendeshaji tu na fedha hizo zilizotoka kwenye mikopo au misamaha. Sisi hatukuwa na pesa yetu yoyote mle. Sasa mwaka huu ndio tunajaribu kuomba hizo pesa ili tuweze kununua hivyo vifaa na kutafuta mali ghafi pamoja na kujenga uwezo wa watendaji wa kiwanda, hilo ndilo lengo letu.

Mwaka jana kwa kweli kama umesoma hotuba yangu ukurasa wa 65 imeelezea wazi wazi mradi uliingiziwa shilingi 5.8 milioni ambazo ni sawa na asilimia 2.3 za makadirio na kutekeleza moja tu kugharamia shughuli za utekelezaji wa kiwanda na ununuzi wa vifaa vidogo vidogo alivyosema kama mkasi na nyuzi za kushonea. Kwa kweli haukuwa na pesa mwaka jana.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, naona kwanza milioni mia mbili na hamsini na sita ambazo ni za kununua mikasi tu hiyo mikasi na nyuzi ni shilingi milioni 5.8 Mhe. Waziri mimi naona kidogo inanipa mashaka Mhe. Mwenyekiti, naomba ufafanuzi zaidi hapa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, sio kununua mikasi tu kile ni kiwanda kamili kuna watu kuna kila kitu. Kwa hiyo, shughuli za uendeshaji ndio pesa hiyo iliyotumika, shilingi iliyopatikana milioni 5.8. Kwa hiyo sawa sawa na asilimia 2.3 tu, kwa hiyo ni pesa kidogo mno.

(Baraza lilirudia)

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Kwa kuwa muda wetu unakaribia kumalizika na kazi yetu hatujaimaliza namuomba Mhe. Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais aweke utaratibu ili tuweze kuendelea na shughuli zetu hadi mwisho.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda ulioko mbele yetu hautoshi kumaliza kazi ilioko mbele yetu. Hivyo naliomba Baraza lako tukufu liweke kando kanuni ya muda ili tupate nafasi ya kumaliza shughuli yetu. Sasa naomba kutoa hoja Mhe. Naibu Spika, Baraza liridhie kuongeza muda mpaka tutakapomaliza

muda mpaka tutakapomaliza shughuli hii kwa muda utakaowezekana. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naafiki**.**

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba Mhe. Waziri anisaidie kuniwekea *hansard* sawa kwa sababu nilimpelekea mchango wa maandishi. Lakini najua binadamu alidharurika, hilo baadae najua ataniwekea sawa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niendelee na hoja yangu, niliyomuandikia kwa maanidishi moja kuhusu suala la maslahi ya wafanyakazi wa Idara ya Vitambulisho vya Mzanzibari. Mhe. Mwenyekiti, hoja hii tumeizungumza karibu miaka miwili kwenye kamati kutokana na ugumu na unyeti wa ile kazi yenyewe.

Naishukuru sana Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais baada ya safari hii kuona kwamba kuna wafanyakazi ambao wanastahiki posho nyeti na walikuwa kwa muda mrefu hawajapatiwa na ile ni haki yao. Kwa sababu wanafanya kazi na Serikalini tena kwa uadilifu mkubwa sana. Sasa ukiangalia sitaki kutofautisha ugumu wa kazi lakini unyeti wa wafanyakazi katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Idara ya Vitambulisho, mimi nadhani tutangalia ule umuhimu wetu.

Sasa hili naamini kuwa Mhe. Waziri alipitikiwa, kwa hivyo naamini hili anaweza kutekeleza ndani ya bajeti hii. Najua Mhe. Waziri safari hii tumempa mashirikiano makubwa sana na ndio maana akaleta vitabu vinne ili tuweze kupata ufafanuzi wa kutosha. Kwa hivyo, naamini na hapa atanipa jawabu nzuri ili niendelee kumpa mashirikiano kama mwanzo. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba radhi sana kwa mwenyekiti wangu najua aliponiletea ule mchango wake alisahau jina kidogo na mimi nilighafilika kama binadamu. Kwa hiyo nakiri kwamba katika waliochangia kwa maandishi Mhe. Hamza Hassan Juma Mwakilishi wa kuchaguliwa wa Jimbo la Kwamtipura. Kwa hiyo, kuhusu suala lake nakiri na nasema kwamba

sasa hivi wanapata, iko asilimia shilingi ishirini milioni kwa hivyo tunataka iende hamsini. Kwa hiyo hiyo ya posho nyeti tutaishughulikia mwaka huu wa fedha kikamilifu kama alivyoshauri yeye na tumeshamjulisha katika kamati tutaishughulikia.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi ndio ninavyompenda Mhe. Waziri siku hizi anausikia sana ushauri tunashukuru sana kwa hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia asubuhi hii ya leo nilikuwa nalia na Sheha wangu wa Mchangani na Mchangani yenyewe sio kama shamba Sheha huyo alikuwa akifanya kazi kwa ubaguzi na kuwabagua watu. Je, Mhe. Waziri nilipokueleza mara ya kwanza ya pili utaendelea na kutuwekea Sheha yule yule au utatuondolea.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, mimi niliacha hii hoja kwa makusudi kidogo tuna mambo mengi sana dhidi ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub katika Shehia ya Mchangani, na kama ni Mwakilishi nilisema nichukue muda nije nikae nae tuzungumze. Kidogo vipi ashirikiane na Sheha yule.

Salamu tulizozipata Sheha hana matatizo yoyote lakini Mhe. Jaku Hashim Ayoub tokea yupo *Kikwajuni Sport Club* ana matata na chenga chenga vile kidogo pale hawasikilizani na Sheha yule haendi naye vizuri kidogo. Sheha hana matatizo kwa hiyo mimi ningemuomba sana mheshimiwa atwachie tukimaliza tuje kukaa pamoja yeye yuko Mchangani na Sheha yuko Mchangani na wote tunawataka kudumisha amani kuendeleza maendeleo. Kwa hiyo, mimi naomba tuje tukae tuzungumze haya mambo kwa faida yetu sote.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Mwenyekiti, mimi nitampa ushahidi wa kutosha mpaka kwa wafanyakazi wake wa Baraza la Mji jinsi anavyowanyanyasa yeye. Maana yake Sheha amekuwa na maamuzi kuliko watendaji wa Baraza la Mji kwa ushahidi tosha. Mimi namheshimu mzee wangu tulikuwepo sote katika timu ya Kikwajuni. Kwa hiyo nitamletea ushahidi tosha tu akesha kuridhika mimi sina tatizo. Akubali kupokea ushahidi huo atajua kama mimi ni mkweli au wananchi ndio wanao matatizo maana mpaka jana kapelekewa barua agonge muhuri kakataa kukonga muhuri wa mwananchi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. mwenyekiti, nimekubali kuupokea ushahidi kwa moyo mkunjufu kabisa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti 522,434,000/=
KIfungu 0701

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nimeliuliza pale katika fungu la Ofisi ya Rais na Baraza la Mapinduzi. Gharama za majengo inapokuja Ikulu au Ofisi ya Rais.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu iko ukurasa wa 57 fungu namba 220700 Matengenezo ya Ofisi na Nyumba. Mhe. Mwenyekiti, jumla ya fungu hili au kijifungu hiki kilichoombewa mwaka huu ni 19 milioni. Lakini muelekeo wake kwa miaka minne iliyopita ni kama nilivyosema katika Baraza la Mapindizi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2010/2011 fedha na sio makisio au walioomba hawakupata hasa imeingizwa katika kifungu hichi ni mia moja thamanini na saba milioni laki tano na elfu sita mia tano arubaini na nane. Mwaka 2011/2012 Ofisi ya Rais Ikulu Idara ya Faragha fungu hasa fedha iliyoingizwa katika matengenezo ya Ofisi ni mia moja sabini na nne milioni laki tisa sitini na saba elfu. Mwaka jana ndio hayo ambayo hayajamalizika ni makisio yamewekwa sabini milioni na mwaka huu 19 milioni.

Suala langu lilikuwa kule mwanzo katika Baraza la Mapinduzi katwambia kuwa ni matengenezo ya Ikulu kuanzia Mnazi Mmoja, Dodoma, Chake Chake, Mkokotoni. Sasa nataka kujua hizi kwa miaka hii mfuliluzo na zinaendelea kuombewa zinafanya matengenezo yepi naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kama nimemfahamu vizuri sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu anazungumzia kifungu 220701 ambapo matengenezo ya Ofisi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Hiyo jumla yake iliokuweko hapo chini kwa sababu matengenezo madogo na makubwa ukijumlisha unapata jumla kifungu hasa ni Matengenezo ya Ofisi kwa ujumla. Kwa hivyo, nakizungumzia kwa ujumla wake.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Nataka kusema Mhe. Mwenyekiti, hiyo jumla ya kifungu lazima uiangalie *breakdown* yake ili tutape mtiririko mzuri. Sasa tukienda kwenye taa, mifreji mambo yote yale na kwa Ikulu zote zile mwaka huu ndio tumeweka 19 milioni. Sasa kwenye matengenezo yale makubwa pale kuna ziro kabisa hatukuyagusa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, majibu wa Mhe. Waziri yananipa utatanishi kwa sababu kama matengenezo madogo anayoyazungumza yeye yanahusu Ikulu basi yalipaswa yakae kule kule alipotufafanulia kwenye Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi kwa sababu hata kule kuna matengenezo makubwa na madogo na kuna mafungu katika maeneo yote mawili. Sasa kule amenipa maelezo na yameingia katika *hansard record* kwamba inahusu matengenezo yale aliyoyataka yote.

Sasa kule ni yale, huku hayawezi kuwa ni yale hatuwezi kuyaweka pamoja vifungu viwili tofauti vya Ofisi ya Rais ikawa anahudumia tena majengo yale yale. Lakini zaidi hapa Mhe. Mwenyekiti, tunapopitisha vifungu tunapitisha vifungu tunavyoviombea mwaka huu tukilinganisha na ndio maana huwa tunaekewa na miaka iliyopita, tunalinganaisha na ile fedha iliyoidhinishwa katika miaka iliyopita na kuona ufanisi wake na uhalisia wake.

Sasa ninachosema kule kuna mamilioni kuanzia sitini na mbili milioni, laki tisa thalathini elfu mia tisa na arubaini na saba, zikaja mia moja hamsini na sita milioni laki tisa tisini na nane elfu na laki mbili kwa miaka mitatu mfululizo. Huku kuna mia moja thamanini na saba milioni laki tano elfu sita mia tano arubaini na nane, halafu kuna mia moja sabini na nne milioni laki tisa sitini na saba elfu halafu kuna sabini milioni. Sasa nasema haya matengenezo yote ni matengenezo hayo hayo naomba aniweke sawa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimfahamishe Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba lile fungu la mwanzo lile lilikuwa ni la Ofisi za Baraza la Mapinduzi. Hili la sasa ni fungu la Ikulu kwa ajili ya kutia rangi kila mwaka. Lakini mimi nataka kumuomba sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu usiende nyuma sana. Tizama hiyo *total* iliyopungua halafu mpaka tumefikia sabini na mwakani tumeomba kumi na tisa tu, naona ilivyopunguka. Kwa hiyo haturudii tena yale matengenezo makubwa kama anavyoyasema yeye. Lakini kubwa hili fungu la mwanzo ni Baraza la Mapinduzi kama nilivyosema hili sasa ni fungu la Ikulu hasa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, napata tabu kwa sababu mimi nachukua maelezo aliyonipa yeye, mimi si waziri. Kwa hivyo, siwezi kujua mafungu haya ya kazi gani. Yeye anavyonijibu ndivyo ninavyopokea, sasa la mwanzo yeye ndiye aliyenitolea ufafanuzi wote wa Baraza la Mapinduzi kwamba matengenezo ya Dodoma na Mnazi Mmoja, Migombani, Mkokotoni na Chake Chake kanipa yeye, mimi siyajui. Mhe. Mwenyekiti, mimi siko Ikulu wala sitegemei kwenda *inshaallah*.

Mhe. Mwenyekiti, sasa katika maelezo nimesema yale kanipa katika ukurasa wa 47 kwenye matengenezo ya majengo ni maelezo yake wala hajayakanusha ingelikuwa kanambia kule nimekosea sio ningesema basi ningetaka maelezo tu. Lakini sasa inakuwaje mafungu mawili yanapanda na kushuka yanahusu matengenezo ya majengo yale yote yanahitaji mabilioni ya fedha, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, labda niseme binadamu ulimi uliteleza wakati ule. Sasa hii ndio sahihi. Lile fungu la mwanzo ni la Ofisi ya Baraza la Mapinduzi na hili suala la sasa ni fungu la Ikulu tu kwa matengenezo ya Ikulu kama kutia rangi mara mbili. Kwa hivyo, naomba radhi kwa kuteleza ulimi. Lakini huu ufafanuzi zaidi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sasa ningeomba anisaidie halafu tupate kuendelea. Namshukuru kwa kurekebisha kauli yake kama nilivyosema tunasaidiana tu hapa. Naomba utaratibu wako kama ukinambia nikae mimi nitakaa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe umeshasema mara nne labda tuamue kwa kura sasa. Kwa hivyo, Wajumbe niwahoji kifungu waliokubali wanyoshe mikono, waliokataa. Waliokubali wameshinda tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia hapa nilimuomba Mhe. Waziri amshauri Rais kuhusu kuweko na Wizara Maalum ya Vikosi peke yake kuliko kuchanganywa na Tawala za Mikoa. Lakini suala hilo sikumsikia Mhe Waziri kunijibu naomba sana Mhe. Waziri kwa upendo kabisa anijibu ili tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Makame Mshimba alipochangia alilizungumza hili suala na si hapa tu hata kwenye kamati analiona hili suala na ananihurumia sana ule uzito anauona wa wizara hii. Kwa hivyo, mimi ushauri wake tunauchukua tutaupeleka kwa Mhe. Rais kama alivyoshauri yeye na mapendekezo yetu *inshaalla* anaweze akamuona kwa jicho la huruma.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na yeye Mhe. Waziri na atakapopeleka huko basi awe *special request* niwe mimi ndiye waziri wa vikosi vyenyewe.

Kifungu 0701 - Ofisi ya Faragha 2,197,216,000/=
Kifungu 0801 -

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru ingawa nimesikitika tu kwamba kifungu kilichopita umepigisha kura bila ya mimi mwenyewe mwenye hoja kuomba kura. Lakini baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti naomba nirudi katika kifungu 0801 Tawala za Mikoa ya Serikali za Mitaa.
Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu na Mhe. Waziri mwenyewe kakiri naomba na najua katoa ufafanuzi. Mhe. Mwenyekiti, mimi sikuridhika na ule ufafanuzi wake. Sasa ikiwa atanipa kauli ya kulifanyia kazi na nikaona matokeo sina tatizo.

Katika mchango wangu nilisema na nikifanya marejeo juu ya ripoti ile ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi iliyokwenda kuchunguza utendaji wa Baraza la Manispaa. Nikasema moja kati ya mambo yanayojulikana mle ni Sheria, Baraza la Manispaa kuna suala linalohusu kuwepo kwa jedwali ambayo ingeonesha ramani na maeneo ya Manispaa ya Zanzibar akasema sheria hiyo haina tangu wakati huo mpaka leo, na nimpongeze sana Mhe. Salmin Awadh kwamba yeye ndiye aliyetutanabahisha katika kamati ile wakati ule akiwa mwenyekiti wetu.

Sasa nilimuuliza hapa Mhe. Waziri kwamba nilipomuhoji wakati ule katika kamati alitwambia kwamba alikuwa halijui na atalifanyia kazi na ikatangazwa ile ramani iingie kwenye jadweli. Lakini leo katika majibu yake hapa kanambia kwamba kwa sababu wanakuja kufanya mapitio ya jumla, kwa hivyo suala tulitegemee huku. Sasa mimi naona si utaratibu mapitio ya jumla yatakuwepo tu.

Lakini tumeshaona kwa mfumo wa serikali yetu inaweza ikachukua miaka mitano tunasubiri mapitio tu hapa kwa sababu sera za Serikali za Mitaa miaka mitatu kila siku tunaambiwa tangu nimeingia Baraza hili itakuja haijaja mpaka leo. Sasa nilikuwa nasema naisubiri lakini kama sheria inaendelea kutumika inataka kuwepo kwa jadweli ambalo linaonesha mipaka na maeneo ya Manispaa, nilikuwa nataka anambie tu kwamba atalifanyia kazi na baada ya muda atatuletea mipaka na maeneo ya Manispaa ili tuweze kujua kwamba zile sheria za Manispaa kwa sababu inahusu haki za watu ni yepi na yanafanyiwa kazi vipi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu vizuri sana Mhe. Ismail Jussa na vile nilivyosema na unajua lile suala halipo moja kwa moja kwa Baraza la Manispaa. Ni kweli mawaziri ndio dhamana wa kukata mipaka. Lakini sasa kuna *master plan* ya mji wetu wa Zanzibar, sasa hujui unaishia wapi kwa sababu mfano tu Shehia yangu ya Tomondo leo ina wakaazi ishirini elfu Shehia moja.

Lakini sasa imeshakuwa si upande wa Magharibi ile Tomondo, Mbweni humo mote zamani ilikuwa ni Wilaya ya Magharibi. Lakini *Municipality* imeshafika huku. Kwa hivyo nilisema katika jimbo langu kuna programu hiyo ya kufanya *master plan* ndio inashughulikiwa pamoja na watu wa mipango miji.
Kwa hiyo, nakubali ushauri wake lakini kumwambia lini hasa tutafanya nafikiri hapo naomba aniridhie hivyo hivyo na mimi maelezo yangu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na yeye anayatambua hayo matatizo kwa sababu ndio hayo ambayo sisi tulikumbana nayo wakati kufanya kazi ya uchunguzi wa Kamati Teule na hata katika maeneo ya mapato tunagombana baina ya Manispaa na Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi hasa katika baadhi ya barabara hizi. Kwa hivyo, nasema hili linaleta matatizo kwa sababu kwanza kuna usumbufu katika masuala ya utawala.

Lakini kuna usumbufu kwa mfano waliotoa huduma na maeneo haya mawili kila mmoja anapotaka kutoza fedha au ada anakimbilia kuwa hili eneo lake. Kwa hivyo, nashukuru kwamba kaliona na nasikitika kwamba kasema hawezi kunambia lini atakamilisha kwa sababu nategemea kwamba Serikali inajua kwamba lini kazi yake hii imepangwa ikamilike. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 0801 - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa 643,620,000/=
Kifungu 0802 - Baraza la Manispaa

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia hotuba ya Mhe. Waziri nilizungumzia suala barabara iliyofungwa Forodhani ambapo nilimueleza Mhe. Waziri kwamba barabara ile aliahidi kuifungua katika wiki na baadae akaifungua na watu wakawahi kupita siku mbili tatu. Lakini cha kusikitisha ni kwamba kumbe alikuwa anatimiza tu kwa kutuondosha njiani yale yaliyokuwepo hapa, baadae akaifunga tena.

Sasa kwenye kitabu chake ametueleza kwamba ametekeleza kwa kuyanyanyua yale madude aliyokuwa ameyaweka, lakini kayaondosha tu

lakini njia ile bado inaonekana imefungwa na wale wanaopita wanakamatwa. Kwa hivyo, mimi nataka anipe ufafanuzi zaidi pamoja na kwamba ametoa maelezo kwamba atashirikiana na taasisi nyengine ili kupata mashauri ya jambo lile.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, nataka kujua ni lini suala lile watalimaliza pamoja na taasisi zake na juu ya umuhimu wenyewe, lakini pia atueleze ni taasisi gani ambazo atashirikiana nazo kwa sababu bado kuna bajeti huko mbele nyengine zinakuja.

Mhe. Mwenyekiti, swali jengine ni kwamba kwa nini barabara ile inayopita pale mbele waliifunga mpaka ikafika pahala sasa haipitiki tena. Tukipata maelezo mazuri basi tutaendelea mbele, ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mhe. Salmin Awadh aliuliza hilo swali na pia tulizungumza hata nje kuhusu utatuzi wa mahali pale. Nafikiri aliuliza hizo taasisi zinazohusika.

1. Wenyewe sisi Baraza la Manispaa.
2. Wizara kwa jumla ya Miundombinu na Mawasiliano na
3. Taasisi ya Mji Mkongwe

Hizo ndio taasisi kubwa hasa zinazoshughulika pale lakini labda nimuambie tu karibu pale na nyumba ile ya watoto ya zamani kuna hoteli pale na wale kwa kiasi kikubwa wanachangia. Kwa sababu yale matofali aliyosema sisi tuliyaondoa muda mrefu tokea mwaka jana. Lakini hata mimi hupeleleza nikipita nakuta wameweka kama kamba kuzuia *movement* ya gari upande ule.

Kwa hivyo, nasema tutashirikiana na hao ili tuweze kuona kwamba hilo suala tunaliondoa. Kwa sababu sio peke yangu na hizo taasisi nyengine. Kwa hivyo, ningemuomba atuachie kama miezi mitatu hivi ili tuone hili suala tunalizungumza na tunalipatiaa ufumbuzi wa kudumu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kule Mji Mkongwe tujaribu sana kuona kwamba kuna *master plan* ya Mji Mkongwe ambayo inajaribu kukataza magari makubwa na pia kuzistiri nyumba na hasa *authority* wanajaribu sana kuzitunza zile nyumba. Wanajaribu hata kusema mwenendo wa magari upungue. Kwa hivyo, tusione tabu kuelekezwa. Unajua wenzetu wengine wanafika kwenye miji mikubwa kama ile unaweka gari mbali kidogo, sio mbali unaweka gari pembeni unafanya shughuli zako unarudi.

Kwa hivyo, mimi niseme Mhe. Mwenyekiti, ushauri wake nimeupokea, tutakaa na hizi taasisi nilizozitaja ili tuone vipi tunaweza kulitatua hili suala lakini kwa kuzingatia haya masharti ya Mji Mkongwe, ahsante.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Basi Mhe. Waziri baada ya ufafanuzi mzuri na tunategemea kwamba hizi taasisi utakaa nazo ili kutatua jambo hili na muone umuhimu wa eneo lile na usumbufu wanaoupata wananchi wakati wa kupitisha yale magari yao. Kwa sababu kuna usumbufu mkubwa basi nimuombe Mhe. Waziri akae na taasisi zinazohusika, ili tuone kwamba njia zile zinafunguliwa kwa maslahi ya wananchi, sio kwa maslahi ya mwenye hoteli, ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru baada ya mara sita kunyanyuka ukaniona. Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia hotuba hii niliipongeza sana Baraza la Manispaa kwa kuendesha mradi ule wa taa. Lakini nikahoji zaidi kwamba uzuri ule sasa unachafuliwa na vijana wetu ambao wanapata tabu sana katika kufukuzana na vikosi vyetu katika suala zima la biashara ndogo ndogo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu alikiri kwamba vijana wale wanavunja sheria baadhi ya wakati kwa kupachika nguo kwenye madirisha ya skuli ya Vikokotoni. Kama hilo lipo basi itakuwa wanavunja sheria lakini nategemea vijana wakivunja sheria basi na serikali ilinde sheria, kwa maana ya kuwakamata na kuwapeleka mahakamani. Lakini vijana wanavunja sheria kwa kupachika nguo kwenye madirisha na serikali inavunja sheria kwa kuwapiga na kuwachukulia mali zao. Nikahoji je, mali ambayo inachukuliwa iko wapi, angalau tuambiwe, imehifadhiwa ghala gani. Naombo Mhe. Waziri atuambie.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri nilisema sana kwamba sio lengo la Baraza la Manispaa, askari wake kwa kushirikiana na ulinzi wa polisi na vikosi kuwapiga wananchi. Nilisema sana kwamba sio lengo letu hata kidogo. Nilishauri sana kama viongozi tusaidiane kuwaelimisha wale watu, kama alivyosema Mhe. Hija Hassan wasitundike bidhaa kwenye madirisha.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na ushauri wake kwamba hiyo kupiga wala hatufanyi, tukubali kwamba na wao wasiwarushie mawe au kuwapiga wale walinzi. Tukubaliane, unakuja unaombwa. Maana yake tunawaomba hasa, tafadhalini ondokeni hapa sio pazuri, wekeni biashara huko. Kwa sababu tunaujua umuhimu wao, kwa hivyo tunaomba sana tuwaelimishe na sisi kabisa hatuna lengo. Nilizungumza vizuri sana kwamba sisi ni wenyewe kwa wenyewe. Mimi nakuja nampiga bakora mwanawe

sithubutu, sisi ni wenyewe kwa wenyewe pale lakini na wao wafuate zile taratibu zilizowekwa basi hatuna ugomvi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, sijafahamu vyema kwa sababu leo kuna baridi. Nataka nielimishwe kwenye swali langu la kwanza kwamba ikiwa vijana wanarusha mawe maana yake mtu katika utawala wa sheria unakamatwa na kupelekwa mahakamani. Kama wale ambao wanatumia nguvu kuwapiga vijana. Mimi nilikwenda hospitali nikawakuta vijana wanne wamelazwa. Kwa hivyo, yule aliyerusha jiwe akamatwe na yule aliyekuwa hospitali atafutwe aliyefanya kosa lile akamatwe ndio utawala bora. Lakini pia nikamuuliza Mhe. Waziri vitu ambavyo mmevikusanya viko wapi. Hilo ni *simple* tu, aniambie viko ghala gani tujue.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, mali zilizokamatwa ziko wapi ndio swali lake zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa nilizonazo kwa maaskari wetu sisi, kwa kweli hakuna mali zilizokamatwa. Kama nilivyosema, unajua inapotokea purukushani tokea lile neno tunalotumia sio zuri, lakini tena wale wanakimbia. Nakubaliana na ushauri wake na wale wanatoroka kwa sababu wanaogopa kukamatwa na kufikishwa mahakamani, wanakimbia na wanapokimbia zile mali wanaziwacha, unajua siku nyingine zinaharibika, wanaacha machungwa na vyakula vyengine watu wanakula na vitambaa si unajua tena kwenye ghasia kama hizo hutokezea.

Lakini ninachosema tutajitahidi twende kwa njia ya maelewano na masikizano na wao tuwafanye watii sheria zilizowekwa, tusikurupushane, hivyo mpaka mali zao kuharibika. Tutajitahidi lakini kwa taarifa niliyonayo, sio kuwa hizo mali ziko Manispaa hazipo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima zote na taathima sikubaliani na jibu la Mhe. Waziri. Mimi nina hakika Mhe. Waziri anajua kuwa mali zinachukuliwa na mimi nimefanya utafiti. Juzi nilisema kwamba ninayo majina karibu 300 ya vijana na mali zao kwenye majimbo tofauti Unguja na Pemba, na wako tayari kuja kwa waziri kuthibitisha kuwa mali zimechukuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, hii nchi siku hizi imejaa hasa mitandao watu wanapiga picha mpaka za simu. Sasa Mhe. Waziri akiniambia kwamba hakuna mali zilizochukuliwa mimi sikubaliani naye, kwa heshima kubwa na ninamuheshimu sana. Ningetaka tuendelee, lakini ningeomba maelezo ya Mratibu wa Serikali Mhe. Mohamed Aboud atuambie kwa sababu wananchi

kila Mzanzibari anajua kuwa mali zinachukuliwa mchana kweupe hakuna siri, na humu nina hakika Wawakilishi wengi wanaona. Sasa Mhe. Waziri akituambia mali hazichukuliwi basi labda atuambie kuna Abunuasi anachukua, lakini mali inachukuliwa na kila mtu anaona. Mimi nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, labda atupe kauli hii mali iko wapi. Pengine ilipotea atuambie lakini akisema kwamba mali haichukuliwi sikubaliani naye, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alilitolea maelezo na Mhe. Hija amezidi kulielezea na kwa kweli sio nia ya serikali kumuonea mwananchi yeyote. Lakini kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba taratibu na sheria za kuweka mji wetu katika hali ya usafi. Sasa madamu Mhe. Hija anasema anao ushahidi wa malalamiko ya namna ambavyo mali hizi zilivyopotea. Lakini nataka nikubaliane pia na Mhe. Waziri anaposema kwamba panapotokea vurugu kweli inawezekana wakati mwengine mali hizi kupotea kutokana na vurugu. Lakini kwa kuwa Mhe. Hija anao ushahidi basi ni vyema tukakaa naye Mhe. Hija Hassan na hao wahusika wengine ili tulitafutie ufumbuzi tatizo hili. Katika ufumbuzi wake mkubwa ni kwa vijana wetu hawa kuwatafutia mahala pa kufanya shughuli zao za kibiashara, maana wanajitafutia maisha wanapofanya shughuli pale.

Kwa hivyo, tatizo liliopo ni eneo lile ambalo kwa kweli kujazana kwa namna ile hakuweki mazingira mazuri ya mji wetu. Lakini bado upo umuhimu wa kutafakari kwa kina kuona mahala ambapo tutakapojenga tukaweka misingi mizuri kwa vijana wetu hawa waweze kufanya shughuli zao za biashara bila ya kubughudhiwa. Kwa msingi huo mimi ningemuomba Mhe. Hija Hassan baada ya kikao hiki tutafute muda tukae pamoja, tujue kilichopotea kilikuwa ni cha nani, madhali *list* anayo tufanye kazi ili jambo hili tulitafutie ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kutoa wito kwamba askari wetu na vyombo vyengine vinavyofanya kazi vifuate utaratibu wa kisheria, pale wanapomuona mtu kavunja sheria basi zile mali zichukuliwe kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria na ziwekwe vizuri kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria ili taratibu zote zifuatwe na isitokee kwa mwengine kuchukua mali ya mtu mwengine bila ya kufuata taratibu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Hija Hassan akubali tuendelee tulitafutie jambo hili ufumbuzi wa kudumu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina tatizo na Mhe. Waziri fungu hili natetea wananchi wafanyabiashara, fungu lijalo nitatetea vikosi. Huu ndio wajibu wangu kila anayedhulumiwa mimi namtetea. Lakini Mhe. Waziri anasema kwamba tukae. Mimi ni mtetezi wa wananchi, nimuombe kuwa mimi na wale ambao ni Jumuiya ya Wafanyabiashara wadogo wadogo

pale Darajani, basi tuko pamoja mimi na wale vijana ambao ndio wanaojua hasa maelezo. Mimi haya nimeyachukua kwao, kuna wengine wa Matemwe, Wapemba wa Kiwani, Wamakunduchi, lakini pale hachaguliwi mtu kwa msingi mwengine. Vijana wetu wanaathirika.

Kwa hivyo, labda Mhe. Waziri akubali kwamba mimi nisaidie na wale Jumuiya ya Wafanyabiashara wadogo waje wakae. Ni jambo la busara kwamba serikali inakaa na vijana wake kuhusiana na mazungumzo ya amani ni jambo la busara, hili suala lisitokezee tena. Mhe. Waziri akilikubali hilo mimi nitamsaidia kumtafutia na nitamletea ili waje wakae na wazungumze, naamini wakizungumza wakielewana basi kutakuwa na amani kwa upande wa vijana na kutakuwa na amani kwa serikali. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri akikubali hilo mimi nitamtafutia vijana lakini aniwekee muda, isijekuwa danadana ya miaka mitatu. Naomba tupeane muda ili isije kuwa mpaka bajeti ya mwaka 2014.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa niliwahi kukaa na vijana wa pale tukazungumza vizuri na tulipata ufumbuzi mzuri, kwa hivyo kwangu sio tatizo hata kidogo kukutana nao tena tukazungumza. Maana wale ni ndugu zetu, tuna wajibu wa kuwasaidia na kushirikiana nao kufanya kazi na kwa vyovyote vile ni wajibu wa serikali kuwezesha kwa namna moja au nyengine kwa vijana wake kupata shughuli za ajira.

Kwa hivyo kwetu sio tatizo hata kidogo na haitochukua muda mkubwa kwa sababu pale tunaponafasika tuko pamoja hapa Barazani, haiwezekani kwamba tunakaa muda mrefu bila ya kukutana. Tuna shughuli za kibajeti tunaweza kuona siku ambayo ipo nafasi basi tukakutana tukazungumza. Yeye anatafuta ufumbuzi wa kuwasaidia vijana wetu, hakuna katika serikali anayependa kusumbua vijana, lakini pia tujenge utamaduni wa kuheshimu sheria zetu, kuweka miji yetu safi, kuheshimiana wenyewe kwa wenyewe ili mambo yende vizuri kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Mhe. Waziri kasema ataweka muda na mimi sina sababu ya kutokumuamini, namuamini sana hatonidanganya. Naomba tuendelee nasubiri huo muda, nina imani kwamba haitofika Ramadhani tutalimaliza hili suala.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia asubuhi hii ya leo, kulikuwa kuna kilio cha wafanyabiashara wa Forodhani, kulipishwa kwa meza shilingi 90,000 kwa kweli hizo pesa kwa muda huu ni nyingi na biashara zao hazitoki. Namuomba waziri angalau kutoka shilingi 90,000 japo ziwe shilingi 50,000 mpaka shilingi 40,000, zile

biashara zinapigwa moto, tunafuatiwa sisi tunauziwa tena na maisha ni magumu, utamkuta mtu ana wake watatu na watoto sita. Kwa hivyo, Mhe. Waziri kwa heshima na hili sio suala la Sheha, wala halihusiani na Sheha hili.

Pia Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa kuna kilimo cha msingi wa Gongoni. Nilichangia asubuhi kuwa ule msingi una hatari kwa maisha ya watoto, kutokea Gongoni hadi Kisiwandui.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, hoja iwe moja, mbili zimeshasemwa. Kwa hivyo, utajibiwa hoja moja. Mhe. Waziri kuhusu shilingi 90,000.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuhusu lile punguzo, suala hilo inabidi wacha tukakae, kwa sababu mimi sina mamlaka, ijapokuwa ni waziri ndio lakini lazima kuna Baraza linakaa na ni lazima tuyazingatie na kuweza kuyafanyia kazi. Kwa hivyo, nasema ushauri wake tunauchukua, wacha tukakae na wenzetu tuone tunaweza kulifanikisha vipi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kikao kinaweza kuchukua muda. Mimi aniambie tu, kama ni kesho au keshokutwa au baada ya wiki, anipe muda tu ili niweke kumbukumbu sawa, najua kikao kinaweza kuchukua muda au ukaambiwa serikali iko mbioni, uzoefu huo tumeuona humu Barazani.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nashauri tukutane baada ya wiki moja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sawa, hakuna tatizo, tuendelee.

Kifungu 0802 Kifungu 0901	Baraza la Manispaa	1,200,000

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia niliuliza swali moja ambalo sikulisikia Mhe. Waziri akilitolea ufafanuzi, inawezekana kwa sababu kama alivyosema mwenyewe hoja zilikuwa nyingi. Kwa hivyo, kajitahidi kuchukua zile alizoziona yeye ni nzito. Nilikuwa naomba anisaidie tu, niliuliza juu ya suala zima lile la mgawanyo wa bajeti za vikosi mbali mbali kwamba ukitizama kwa mfano fungu la jumla la JKU, lilikuwa ni shilingi 7,457,000,000. Fungu la Kikosi cha Mafunzo lilikuwa ni shilingi bilioni 6,099,000,000. Fungu la KMKM lilikuwa ni shilingi bilioni 9,452,000,000. Lakini vikosi viwili naviona kama kidogo ukivilinganisha na vyengine viko chini sana.

Kwanza Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ambacho katika huduma kinatoa huduma kubwa sana shilingi bilioni 3,113,000,000 na Kikosi cha KVZ ni shilingi bilioni 3,258,000,000. Sasa nilitaka kujua kwamba ni vigezo gani, niliwahi kuuliza pale katika mchango wangu ambavyo vinapelekea kwamba vikosi hivi viwili vya Zimamoto na Uokozi na kile cha Valantia vikawa na mafungu yake yako chini sana ukilinganisha na vifungu vya vikosi vyengine vitatu nilivyokuwa nimevitaja pale mwanzo. Naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mhe. Ismail Jussa Ladhu alipochangia alilizungumza hili suala. Ni kweli kwamba lazima tukubali kuwa hivi vikosi viwili hasa KMKM na JKU ambavyo ni vikosi vikubwa kwa shughuli zao na vijana ni wengi zaidi. Lakini pia Kikosi cha Valantia ni kidogo na kipya ndio kwanza, halikadhalika kuna vijana kule wanakwenda kwa lile jina lao la Valantia, wako wale wa kudumu na wako wale wa kujenga taifa kwa jina hilo la Valantia, lakini na wao bado hawajaajiriwa tunakwenda nao kidogo kidogo.

Lakini kubwa zaidi Mhe. Mwenyekiti, tunategemea na *ceiling*. Sisi kutokana na hizi kazi zilivyokuwa harakati nyingi hasa za ulinzi kwa viongozi na kwenye mabiashara ya mabenki na kwengineko. Kwa hivyo, ningependa sana tuwaajiri wengi ili tuwe na kikosi kikubwa, lakini *ceiling* tunayopewa ni ndogo, hiyo hasa ndio sababu kubwa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 0901	Idara ya Uratibu wa Idara Maalum	144,753,000

Kifungu 1101

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, mimi katika Idara hii ya Utumishi na Uwezeshaji, niko katika kifungu hiki 020700 matengenezo ya ofisi na nyumba.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba ufafanuzi katika fungu 220701 na 220702 Matengenezo madogo ya ofisi na matengenezo makubwa, hayo mafungu mawili nilikuwa nataka maelezo kwa sababu Mhe. Waziri hapa tangu tunakotoka huko haya mafungu yanaonekana yamenona na alijaribu kuyatolea maelezo, lakini bado tunaona yanajitokeza tena. Sasa nilikuwa naomba maelezo ya ziada katika mafungu haya.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki hasa kinagusia lije jengo la zamani ambalo tunaliita jengo la *ZIPA* pale Ikulu jengo la pili, kwa hivyo tumeshauriwa na

watu wa Mji Mkongwe tulifanyie matengenezo haraka, kidogo hali yake sio nzuri, tulishauriwa na ndio maana tukaomba pesa hizo ili tuweze kulifanyia matengenezo. Ukweli hasa tuliomba shilingi milioni 300,000,000 lakini tulichopata ndio hicho. Kwa hivyo, tunaanza mwaka huu kwa pesa hizo, lile jengo kidogo hali yake hata ukilipanda, tumuombe Mwenyezi Mungu, lakini hali yake kwa kweli sio nzuri ndio maana watu wa Mji Mkongwe wametushauri tufanye kazi haraka iwezekanavyo.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi kidogo sijafahamu, maana tuko kwenye Ofisi ya Rais Ikulu, kwa hivyo jengine lile tunalihesabu limechanganywa na Ikulu nalo, kwenye yale matengenezo ambayo alikuwa akiyaelezea Mhe. Waziri nafikiria analigusia. Lakini hata kama haligusii huko atakavyosema kwamba sio la Ikulu, lakini hapa kuna matengenezo madogo kuna fungu la fedha, sasa kipi kinahitajika hapa, matengenezo madogo au haya matengenezo makubwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, matengenezo makubwa ndio zile shilingi milioni 110,000,000 *major maintenance* ndio hayo niliyoyasema. Lakini kuna matengenezo madogo madogo ya kila siku, kama kutia rangi, mifereji mibovu, jengo la zamani lile, au dirisha limekaa vibaya, ndio hayo matengenezo madogo madogo. Lakini matengenezo makubwa ndio ukitaka kufanya kazi ushirikiane na watu wa Mji Mkongwe mshauriane kwa kutumia hizo pesa nyingi. Kwa hivyo, ni vifungu viwili vidogo tofauti, vyote vina *qualify* hapa.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya Mhe. Waziri mimi kidogo yananitatiza. Maelezo ya vifungu haya yanajitosheleza, maana yake tukiangalia haya matengenezo madogo Mhe. Mwenyekiti, yapo siku zote yanaonekana. Lakini kwa sababu yametokezea haja ya kufanya matengenezo sasa ndio haya matengenezo makubwa, maana yake matengenezo makubwa hata hiyo rangi itakuwemo kwenye hayo matengenezo makubwa, maana yake huwezi ukalijenga jengo au ukalifanyia matengenezo na kulitoa saruji ile ya juu, ukaipiga plasta yote halafu usipige na rangi.

Hebu Mhe. Waziri atupe maelezo ya kutosha kidogo katika mafungu haya. Kwa nini lisiwe fungu moja tu la matengenezo ya majengo, akalitengeneza lile jengo. Lakini haya mafungu yanaonekana kama yamebaguliwa mawili tofauti. Mimi hoja yangu nilikuwa nataka kujua hasa, hayo madogo anayotaka kuyatengeneza ni yepi na makubwa ni yepi, wakati kama kuna haja ya kufanya kutengenezo makubwa, yale madogo ndio hayapo kwa sababu yataletwa na yale makubwa. Kwa sababu matengenezo madogo kama alivyotueleza anasema anataka kupiga rangi na mambo madogo madogo.

Lakini unapojenga lile jengo kwa matengenezo makubwa hivyo vitu vyote vinajumuishwa pamoja. Sasa nilikuwa naomba maelezo ya ziada Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa ufafanuzi zaidi labda niseme kwamba naomba alitizame Mhe. Mtando hilo fungu kubwa na kama nilivyosema ile *major maintenance* hasa lilitaka shilingi milioni 300,000,000 na kwa mwaka huu tumezipata hizo, lakini atizame jumla ya fungu lote. Naomba nimpe maelezo ya ziada kwamba hii iko kwenye kasma ya uendeshaji na zaidi kwenye jengo lile ambapo kuna ofisi za wakurugenzi wetu, wawezeshaji wa mipango na kadhalika ni kama ofisi ndogo ya Ikulu.

Kwa hivyo, kama nilivyosema narudia tena, kuna tofauti kabisa. Hizi shilingi milioni 110,000,000 zilizowekwa ni makubwa na kuna sehemu tofauti mule na kuna ghorofa kama tatu mule Mhe. Mwenyekiti. Mimi ningemuomba kwa ufahamu mzuri wa lile jengo Mhe. Mtando nimualike kesho tukijaaliwa aje alikague lile jengo, halafu atanihurumia kwa hii pesa iliyowekwa hapa, ni pesa ndogo sana hii.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na namshukuru Mhe. Waziri kwa mualiko wake wa kwenda kulitembelea jengo lile nipate kuliona. Lakini Mhe. Waziri mimi ningekushauri kitu chengine hapa kwamba unapokuwa unafanya matengenezo makubwa, basi haya matengenezo madogo ni bora ungeyaweka kwenye matengenezo tu ya jengo tukaona kuwa una matengenezo makubwa kwa mwaka huu na unaziomba kiasi hiki, kuliko kuweka vifungu viwili tofauti. Hii inafanya kutia shaka sisi kidogo, maana yake inaonekana matumizi yake pia yatakuwa yanakwenda tofauti.

Mhe. Waziri nilikuwa nakuomba sana ujaribu kukaa na hawa watendaji wako, mnapokuwa na matengenezo makubwa kama haya ni vyema mkaomba fedha hizi kwa pamoja tukaweka katika fungu moja hili la matengenezo makubwa. Kwa sababu hapo unapotuambia umeomba shilingi milioni 500,000,000 sisi hatujaziona hapa, hatujui huko ulivyoomba Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, lakini sisi tunaona hiki ambacho unakiomba kiidhinishwe na Baraza hili. Kwa hivyo, sisi tunakiangalia hiki ambacho tunataka tukuidhinishie na sababu zake za kuidhinishiwa kwake, ndio maana tumepata shaka hapa nimeona niulize kidogo.

Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri mara nyengine utuwekee katika ufafanuzi uliokuwa mzuri kidogo. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia pia nilihoji maslahi ya askari wetu na nikatishika kwamba askari wetu wa vikosi vyote vitano kama sikosei vinapata maslahi madogo sana. Lakini sambamba na hilo tumekuwa tukiona kwamba kwa malalamiko ya matumizi mabaya ya fedha. Nikanukuu hapa ripoti ya *CAG* na nikanukuu na barua moja ambayo kuna askari pengine anaambiwa ni mstaafu kumbe hajastaafu na kumbe yuko hai.

Mhe. Mwenyekiti, wasi wasi wangu ni kwamba fedha kule zitakuwa zipo lakini zinatumika vibaya na tutasababisha askari wetu kuwalipa mshahara mdogo. Naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti. je, Mhe. Waziri atafanya vipi ili kuwadhibiti wale ambao wanatumia fedha vibaya, sambamba na kuwaongezea posho na mshahara mzuri wale wanaofanyakazi kwa maslahi ya umma. Naomba maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na ushauri wa Mhe. Hija Hassan Hija. Lakini tatizo ni mshiko, sisi tunapenda sana maafisa wetu, vijana wetu tuwape na wao wajisikie hasa, isipokuwa tunakwenda hatua kwa hatua kwa sababu ya matatizo ya fedha na huo ndio ukweli wenyewe, kwamba fedha na *ceiling* tunayopewa na *first charge item* ni mishahara. Kwa hivyo, siku zote kwanza mishahara tunahakikisha inatimia kwa vijana wetu na halafu ndio tuje kwenye *OC* nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, anayosema mimi nakubaliana nayo kabisa na tutajitahidi na Mhe. Rais mwenyewe amesema, ameelekeza na Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora amezidi kusisitiza kwamba kadri maslahi yetu yatakavyokuwa mazuri basi na vijana wetu nao tutawaongezea maslahi yao yawe mazuri zaidi. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Mjumbe kwamba sisi tunalo na ndio tumeanza hii *step* za kuweka *scheme of service*, yaani wale wenye miaka pamoja na ujuzi basi wazawadiwe na ujuzi wao, ili yote zamani ule ujuzi ulikuwa hauthaminiwi na leo tunauchukua pamoja ili tuwasaidie katika kuboresha maslahi yao.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, natamani nimuachie Mhe. Waziri lakini nashindwa na hasa hapa ndipo kwenye mshahara, yaani nikizuia hapa ndio ataona uchungu hasa wa kukosa mshahara. Mhe. Mwenyekiti, mimi siamini kwamba tatizo ni fedha kwa sababu ingelikuwa tatizo ni fedha basi kusingekuwa na mwanya wa fedha kutumika vibaya.

Taarifa ambazo zipo kwenye Ofisi ya *CAG* kwa mujibu wa ripoti ni kwamba *files* 1000 ndizo zilizochukuliwa na kesi 78 mpaka 80 zimekutikana. Je, *files* zote za askari na nadhani tatizo si fedha, isipokuwa kuna matumizi mabaya na

Mhe. Waziri ameshindwa kudhibiti na kama kukosa haki ni vizuri basi na yeye akose mshahara wake leo tuone.

Mhe. Mwenyekiti, nilimwambia kwamba posho ambalo lilikubaliwa na chakula kwa ajili ya askari nadhani kama sikosei ni shilingi 5,000/= nikamwambia askari wetu wanapata mkate mmoja wa Mikunguni shilingi 150/= na hiyo nimekwenda mimi mwenyewe katika vikosi na kuhoji. Kwa mfano, unamuweka mtu saa 12 asubuhi mpaka saa 12 asubuhi siku ya pili unampa mkate mmoja asubuhi na jioni na huku wengine wanatumia fedha vibaya kwa matumizi yasiyostahili. Kwa hivyo, si tatizo la fedha, isipokuwa ni udhibiti mbovu wa matumizi ya fedha.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri aniambie sasa atafanya nini ili anihakikishie kwamba hakutakuwa na udhibiti mbovu laa ameshindwa basi fedha na yeye tumnyang'anye aone uchungu wa kukosa fedha na wala siamini kwamba ni tatizo la fedha, isipokuwa ni matumizi mabaya ya fedha za umma ambapo yeye itakuwa ameshindwa kuyasimamia vizuri.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, *concern* ya Mhe. Mjumbe nimeiona na niseme wazi kwa suala la matumizi mabaya sasa niseme limepungua sana au halipo kabisa, kwa sababu taratibu zote za manunuzi, matumizi pamoja na Idara yetu Maalum wanafuata, wanakaguliwa katika *accounts* zao. Kwa hivyo, sasa kwa kweli taratibu zinafuatwa na wala hakuna tatizo hilo, labda tutasema mishahara pengine inapitishwa Wizara ya Fedha kwamba watatiliwa na wataziweka haipo.

Kwa maana hiyo, utendaji wa Vikosi vyetu au Idara yetu Maalum ni mzuri sana na hilo suala la *mismanagement* halipo hivi sasa na nidhamu tumeirudisha, tunafuatilia na wao pia Kamati za Baraza la Wawakilishi wanakwenda na kuwakagua, wanawatizama. Kwa hivyo, kama kuna matatizo ya ubadhirifu wa fedha tutabaini sote.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kumuomba Mhe. Mjumbe kwamba suala la *mismanagement* sasa halipo katika vikosi vyetu na wanakwenda kinidhamu na kitaratibu za kazi na pia Kamati zetu za Baraza zinawakagua, tunakaa nao pamoja Kamati ya *PAC* inawachunguza na tayari fedha zile wanazokusanya kuna makubaliano maalum na Wizara ya Fedha na wao wanawakagua. Kwa kweli napenda nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba hilo limeondoka kwa kiwango kikubwa kabisa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, sikubaliani na majibu ya Mhe. Waziri na sikubaliana hasa kwa nia safi kabisa na wala sio kwa ubishi, kwa

sababu mimi imani yangu askari wanafika kufanya yale wanayofanya kwa sababu hali yao ya maisha ni ngumu. Kwa mfano, ukimwambia mkamate Mhe. Ali Abdalla Ali basi anakamata na anakupiga kwa sababu hali yake ngumu na hiyo ndio imani yangu na hayo wanatuambia wenyewe kwamba hali yao ni ngumu sana.

Mhe. Mwenyekiti, nilitoa mfano hapa kwamba askari wanamtoa mjini kumpeleka Hanyegwa Mchana kujenga gereza kwa shilingi 1,500/= kwa mwezi sawa na shilingi 50/= kwa siku, basi hata hii kumpa nauli ndio hali ngumu. Sasa askari huyu akiona yeye hapewi nauli, lakini mwengine fedha anatumia ovyo ovyo na hata hao maafisa Mhe. Mwenyekiti, bado hali zao ni ngumu, kwa kweli huwezi kumlinganisha afisa wa cheo cha juu wa vikosi vyetu na askari mdogo wa Jeshi la Wananchi au Polisi.

Kwa hivyo, mimi nasema kwamba Mhe. Waziri anihakikishie sasa, ili nimpe nafasi kwamba hadithi hii ya hali ngumu itamaliza lini na hiyo *scheme* ambayo wanayotayarisha pamoja na uwazi itamaliza lini, kwa sababu kuna malalamiko kwamba askari wengine huwa wanadai kuona uwazi pia hawauoni na Mhe. Waziri yeye anajibu kisiasa.

Lakini sisi tunafanya utafiti kwamba askari hata uwazi wa maslahi yake haupati, kwa hivyo si suala la kisiasa na tunatetea kwenye askari wetu kwamba wana hali ngumu na kuwataja tu hairuhusiwi kwa sababu wanaweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu. Kwa kweli na hali ngumu, yaani hali ambayo inapelekea kukosa imani na wananchi wao.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora hebu hii hadithi ya *scheme of service* inarekebishwa lini, ili niweze kuachia mshahara la si hivyo kama hakuna lini itarekebishwa, basi tupige kura na yeye tumnyang'anye mshahara aone uchungu wa kosa maslahi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, kwa kweli Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, alitoa kwa urefu labda akuongezee. Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mhe. Mjumbe kwa nia yake njema ya kutaka askari wetu wa Vikosi vya SMZ wapewe maslahi kwa mujibu wa kazi wanazozifanya.

Wakati nilipokuwa nikitoa ufafanuzi juu ya suala hili sina hakika nitamuwia radhi kama alikuwa yupo au hayupo. Lakini nataka niungane na Mhe. Waziri

kwa majibu yake aliyoyasema kwamba hivi sasa yale mambo ya matumizi mabaya yamepungua sana au yameondoka kabisa katika Vikosi vyetu vya SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, labda nije kwenye hii hoja ya pili ambayo amesema Mhe. Mjumbe, kama nilivyosema Mhe. Rais kama Kamanda Mkuu wa Idara Maalum ametambua kuwepo kwa maslahi bora ya watumishi wa vikosi vyetu vya SMZ na nilisema hata tulipofanya marekebisho pale mwaka 2011 Oktoba, basi kulikuwa na tofauti kati ya maslahi ya watumisi wa kawaida na watumishi wa Idara Maalum hasa askari wetu wa wapiganaji wetu.

Hivi sasa ninavyotoa kauli hii ni kwamba tayari Tume ya Utumishi Idara Maalum imepitisha mapendekezo ya marekebisho ya mishahara ya Idara Maalum na iko Kamisheni inafanyiwa kazi. Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 64 cha Sheria ya Nam. 2 cha Utumishi wa Umma, Kamisheni wameshamaliza mapendekezo hayo, baada ya kufanya *consultation* na Wizara ya Fedha na Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma, wanatakiwa mapendekezo haya wayapeleke kwa Mhe. Rais na hivyo ndivyo sheria inavyosema.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Mhe. Rais yeye ni Kamanda Mkuu na anaelewa hali halisi ya ugumu wa maisha kwa askari wetu, basi bila ya shaka Mhe. Rais atakubaliana na mapendekezo ambayo yatafikishwa kama yalivyopelekwa na Tume ya Utumishi ya Idara Maalum. Kwa hiyo, mapendekezo haya yanafanyiwa kazi ndani ya bajeti hii tuliyonayo ya mwaka huu.

Kwa maana hiyo, niseme kwamba serikali inayafanyia kazi na itaweza kulipatia ufumbuzi suala hili la maslahi madogo ya watumishi wa Vikosi vya SMZ ndani ya mwaka huu wa bajeti. Mhe. Mwenyekiti, ikishakamilika kazi hii waifikishe kunakohusika kwa mujibu wa sheria, maana ndivyo sheria inavyosema na Mhe. Rais kwa anavyowapenda askari wake, basi atahakikisha maslahi mazuri kwa askari wa Vikosi vya SMZ yanakuwepo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nimuombe sana ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija auachie mshahara wa Mhe. Waziri ili aturuhusu sisi tuyafanyie kazi na halafu tumpelekee mwenyewe, ili aweze kutoa idhini na kuwatengenezea maslahi mazuri watumishi wa Idara Maalum.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa mwakani si mbali tukijaaliwa, basi nimueleze Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwamba ahadi hii ambayo imetolewa na Mhe. Waziri ambaye ndiye mwenye dhamana ya utumishi wa umma.

Kwa hivyo, tukijaaliwa tukifika na roho mwakani na sio mbali mwakani na wala tusifikiri mwakani ni miaka 500, basi tukifika na roho kama sijafariki hii ndio *first point* yangu ambayo itakuja kuhoji. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri afuatilie kauli hii, ili limalizike kwa sababu nina wasi wasi kwamba huo utumishi wa umma wenyewe ndio mambo yanapochelewa hapo.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, afuatilie na amuhimize Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ili tukifika na roho mwakani kama sijarogwa au kusahau, basi hili ni jambo langu nitakalohoji mwanzo kwamba imekamilika *scheme of service* ya askari. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 1101	Idara ya Utumishi na Uendeshaji	1,274,626,000/=
Kifungu 1601	Kitengo cha Ofisi ya Usalama SMZ	61,626,000/=
Kifungu 1801	Kitengo cha Mawasiliano na Habari	242,672,000/=
Kifungu 1802		

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Wakati nilipokuwa nikichangia nilizungumzia suala hili la taratibu za upandishaji vyeo katika Idara Maalum na nikatoa mfano mahsusi kwa Kikosi cha KMKM.

Sasa katika majibu yake Mhe. Waziri naona amekimbilia zaidi katika suala la barua na utaratibu wake na hilo nitamuachia na utaratibu wake, kwa sababu mimi nilitaka maelezo kwani ile hoja yangu ya msingi hasa haikujibiwa ni kwamba hivi kwa taratibu za Utumishi wa Idara Maalum, kwa sababu ninavyoamini ni kwamba suala lililoguswa kwanza ni la kawaida, yaani ni suala la upandishaji vyeo kama katika taasisi nyengine yoyote ya serikali.

Kwa hivyo, nataka kujua kwamba je, inakubalika katika taratibu kwamba kwa watu wa nafasi za mfano nilioutoa wa *LS* au *OP* kuwavuka wale wa *CPO* ambao walikuwa wameachwa na kupandishwa vyeo hawa na kuachwa hawa *CPO* ambao walikuwepo na hilo lilikuwa ni swali langu. Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya katika zile hamasa za Mhe. Waziri lile swali lenyewe hasa hakulipatia jawabu na ninaomba anipatie jawabu.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Mjumbe hayo aliyozungumza hapa na ile barua aliyoileta ya orodho ni *Non Commission Officers (NCO)*. Sasa hizi *courses* ziko tofauti na hata mimi nyengine zisijui. Lakini kwa hapa kama hii barua yake inasema ni *NCO* na ametaja cheo chengine hivi sasa. Kwa hivyo, ziko *categories* tofauti na wakati tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba kuna sifa mbali mbali kwanza uzoefu, halafu nidhamu, utendaji wako kwa ujumla na sio kama umeshakaa miaka miwili una-*qualify* kwa *further training*, kwa ajili ya kupata mambo fulani. Kwa hivyo lazima kidogo utendaji wako uridhishe na mkuu wako ndio anapendekeza.

Kutokana na hali hiyo Mhe. Mwenyekiti, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba hakuna upendeleo wowote na mimi hii *list* sijaifuatilia, lakini ni imani yangu kuwa hawa wamechukuliwa katika sehemu tofauti za Unguja na Pemba.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, unajua mara nyengine ukitoa maelezo unaweza kusema kitu hata hakipo kwenye hoja, kwa sababu mimi katika maelezo yangu wala sikugusa masuala ya Upemba na Unguja, sasa nashangaa kwamba anasema wametoka Pemba na Unguja.

Kwa kweli mimi nilipozungumza nilizungumza kadhia ya kwamba askari wanalalamika juu ya upendeleo kwamba wakubwa wanawaacha watu wenye sifa wanawachukua wengine ambao wako chini ya sifa zinazotakikana kwa sababu ni jamaa zao, si suala la Unguja wala Upemba ama ukabila au wapi mtu anatoka.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema yeye mwenyewe ikiwa yeye waziri mwenye dhamana anasema hajui nini zaidi. Masuala haya kama alivyosema Mhe. Hija Hassan Hija kwamba sisi ni watetezi wa wananchi na askari wa vikosi ni sehemu ya wananchi wetu, kwa hivyo wanapotupa hoja zao tunayo haki ya kuziwasilisha hapa na zipate majibu.

Sasa ningeweza kuelewa ule msingi wa hoja yake Mhe. Waziri na mimi namfahamu aliposema kwamba kwa sababu inataka *logic* ya kawaida tu kuelewa, ili upandishwe cheo kuna mambo mengi ya kutazamwa ikiwemo haya aliyoyataja kama nidhamu pamoja na mambo mengine. Lakini nasema haya ni kwa kiwango ambacho wapo wanaofikilia kupandishwa cheo. Kwa hiyo inakubalika katika taratibu zao na mimi sijui nataka anieleze yeye kwa sababu yeye ndiye mwenye kusimamia wizara hii.

Je, inakubalika katika taratibu zao kwa watu ambao hawajafikia ile nafasi ya juu wakarukishwa vihunzi kupelekwa katika ngazi nyengine, basi akinijibu hilo na akiniambia inakubalika nitamuachia Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu vizuri Mhe. Mjumbe, tunajua kama nilivyosema sio kama sijui lakini unajua mambo ya vyeo haya lazima uwe na

uhakika hasa, ndio maana kama nilivyosema kuna vyeo vyengine labda mimi sivijui na wala sivibaya. Kwa hivyo, kama nilivyosema kawaida mtu kupanda cheo kwenye vikosi lazima siku hizi ukasome na unasoma kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa, yaani ngazi kama vile unaweza kuwa koplo, *sergeant* na mote kuna mafunzo yake.

Mhe. Mwenyekiti, hawa kama nilivyosema wanachaguliwa kwa mujibu wa sifa zenyewe ulivyotumika, yaani utumishi wako, miaka yako mingapi, uadilifu wako. Kwa mfano, mtu anaweza kukaa miaka minne au mitano hajenda *course* kwa sababu pengine amekosa sifa moja.

Kutokana na hali hiyo, nataka kumhakikishia tu kwamba wenyewe makamanda wanajitahidi na lazima upate *approval* upite kwenye taratibu na suala la upendeleo kwa kweli halipo. Mhe. Mwenyekiti, kwa hilo nazidi kumhakikishia kwamba tunajitahidi kuona kuwa watu wanakwenda mafunzo ndipo wapate vyeo na hiyo ndio hali halisi na ile kuchupishwa ilikuwa zamani na sasa haipo ile.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru na laiti Mhe. Waziri angekuwa msikivu na mwenye kuzingatia hoja zetu, basi nafikiri mara zote tungekuwa tunakwenda vizuri sana.

Mimi nakata kumuomba suala moja tu Mhe. Mwenyekiti, nimelileta hapa kwa sababu ya uzito wake, katika pahala ambapo ni nyeti na yeye mwenyewe amesema ni vikosi kama hivi. Lakini haya masuala niliyoyazungumza mengi yanayohusu manung'uniko yakipokelewa katika mfanyakazi wa kawaida, basi tunaweza kulichukulia kikawaida, lakini kunapokuwa na manung'uniko kwenye vikosi vyetu kama hivi Mhe. Mwenyekiti, inaweza kuleta hali ya kutokupendana na kutokuaminiana humu ndani.

Kwa hivyo, nadhani hili badala ya kuendelea kutoa hoja na yeye akanijibu na baada ya ile kauli kali aliyokuja nayo hapa, basi mimi nafikiri ingelikuwa ni nzuri zaidi, nilitegemea Mhe. Waziri *appreciate* kwamba Mwakilishi mimi nimekuwa *responsible* wakati nilipoisoma barua ile sikusoma nani amesaini na wala sikusoma yale majina ya watu, isipokuwa nilisoma tarehe pamoja na kuelezea maudhui yake, kwa sababu ya kuheshimu kwamba kile ni chombo ni *sensitive*.

Sasa nafikiri baada ya maelezo yake aliyokuja nayo hapa, mimi nadhani kama ni waziri mwenye dhamana ya kuwasimamia hawa vijana wetu, kwa sababu yeye humu ndani ya Baraza hili yeye ndiye mwenye kumuwakilishi huyo Kamanda Mkuu ambaye ni Rais, kwa sababu yeye ni Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa hivyo, akubali kulichukua suala

hili akalifanyie kazi badala ya kwamba mtetezi tu, kwanza ajiridhishe kwanza suala hili lipo.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili asiishie kuzungumza na wale makamanda tu, apate nafasi kama Mhe. Waziri ya kuzungumza na hawa askari wenyewe na pengine kwa nidhamu za kijeshi anazijua yeye pengine hawa watakuwa wazi zaidi akikutana nao peke yao kuliko mbele ya mabosi wao.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri ule utaratibu aliokuja nao hapa katika majumuisho amelichukua zaidi kwa kauli za kwenda kulifanyia kazi na kuchunguza uhalisia wa suala lile kama halipo sawa kama lipo na linakiuka taratibu basi achukue hatua za kurekebisha, lakini akinijibu hilo basi sina matatizo na nitamwambia tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana ushauri wake na nimshukuru sana kulileta hili suala kwa hofu ya upendeleo, kwamba tutalichukua na tulitendee haki kwa wale maofisa au wapiganaji wahisi wapate fursa ya masomo labda wengine wameachwa. Mhe. Mwenyekiti, ushauri wake tunauchukua na tutaufanyia kazi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimepokea na imani yangu tu na ni utaratibu, kwa sababu inaingia katika maagizo ya Baraza kwamba baadaye yatakuja kuripoti juu ya matukio ya kazi ambayo atakuwa ameifanya. Baada ya hayo, nashukuru na ninasema tuendelee.

Kifungu 1802	Tume ya Utumishi Idara Maalum	53,247,000/=
Jumla ya Fungu		**6,986,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU LA 17 – JESHI LA KUJENGA UCHUMI

Kifungu 0201 Utawala Unguja

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika mchango kwenye maelezo niliyoyatoa kujenga hoja juu ya kuweka taratibu nzuri za kusimamia haki za vijana wetu hawa wanaofanyakazi za ulinzi nilizungumzia masuala mawili kuhusiana na Kikosi cha JKU na hilo moja pia lina-*appear* kwenye vikosi vyengine, pengine likijibiwa hapa na itakuwa tayari nimeshapata majibu na kule kwengine.

Mhe. Mwenyekiti, la kwanza na haya nafikiri kwa sababu ya wingi wa zile hoja Mhe. Waziri hakupata nafasi ya kuzijibu pale, naamini hivi sasa atanipa maelezo na yatanitosheleza. Vile vile nimuombe kabla sijamuhoji kwamba mambo mengine tukimpa akafanyakazi ya kuyafuatilia na halafu aje atupe majibu. kuliko kuwa mtetezi wa zile hoja

Jambo la kwanza nilitoa kadhia kwamba vijana wa JKU walichangishwa shilingi 2,000/= kwa ahadi kwamba zitakusanywa na baadaye zitafanyiwa kazi ya *SACCO's* au mfumo fulani. Lakini jumla baada ya kuchangishwa kila mmoja ni shilingi 42,000/= na wengine walipoona hazina maelezo na hakuna kazi iliyofanyika basi waliomba warejeshewe fedha zao. Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwenye mchango wangu kwamba inasemekana kama asilimia 25 hivi robo moja wale wamerejeshewa fedha zao na wengine wakaahidiwa hazikutolewa mpaka leo.

Sasa Mhe. Waziri punde tu alipokuwa akijibu hoja ya Mhe. Hija Hassan Hija alisema, kwamba serikali inapenda iwahudumie vizuri, lakini hali ya uchumi mbaya sana, basi angalau hichi chao kiwafike na Mhe. Waziri anaweza kusema shilingi 1,000/= au 2,000/=. Mhe. Mwenyekiti, kwa mtu mwenye kupata mshahara shilingi 140,000/= au 150,000/=, shilingi 2,000/= ni nyingi hiyo na hasa ikeshakuwa imekusanywa na ikafika shilingi 42,000/= ni nyingi.

Kwa hivyo, nasema na kwa sababu tunakwenda kwenye mwezi mtukufu wa Ramadhani na watu wanatayarisha Siku Kuu, basi pengine si vibaya Mhe. Waziri akanipa kauli kwamba suala hili atalisimamia kwa ajili ya kulipatia ufumbuzi.

Pili hapo hapo pia niliuliza kuhusu fedha za michezo Mhe. Mwenyekiti. Katika bajeti anayotuletea Mhe. Waziri kwenye kila kikosi kuna fungu la michezo, ambalo ni *sub vote* 220515 katika ukurasa wa 82 pale. Lakini bado unapokuwa na vikosi vile vina fungu kubwa tu na bado wanaendelea kukatwa hawa.

Sasa hoja sio aliyosema Mhe. Waziri kwamba pengine wanakatwa shilingi 1,000/=, isipokuwa hoja yao vijana wetu walinzi ni kwamba tayari kikosi kina fungu la kuhudumia shughuli hii. Sasa kwa nini wao waambiwe wachangie na hoja yao si kuchangia shilingi 1,000/= kwamba hii shilingi 1,000/= ya kila askari baadaye inaishia katika shughuli nyengine ile ambayo imekusudiwa wakati shughuli iliyokusudiwa ina fungu lake. Kwa hivyo, naomba maelezo katika hoja hizo mbili Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa majibu ya ziada kama nilivyosema kweli wanakatwa.

Kwa mfano, *KMKM Sport Club, JKU Sport Club, Chuo cha Mafunzo Sport Club*. Mhe. Mwenyekiti, kuendesha mchezo ni gharama sana wachezaji wale kuwa-*maintain* ni kazi mno utaona na tukitizama hata hizi klabu zetu za mipira za uraiani zilivyokufa kwamba hawana fedha za ku-*maintainance* ya timu na kwa wachezaji.

Sasa kwa fedha na kwa hili fungu lililotengwa humu tu hazitoshi Mhe. Mwenyekiti, zaidi hivi sasa KMKM ni bingwa anaiwakilisha Zanzibar na kwa bahati mbaya hakwenda kule kwenye Kombe la Afrika Mashariki la *CECAFA*. Lakini kuna Kombe la Afrika la kushiriki lile, basi tunahitaji fedha zaidi ya mara nne zilizotengwa pale kwa ajili ya tiketi pamoja na mambo mengine.

Kwa hivyo, nataka kumfahamisha Mhe. Mjumbe, kwamba tunajitahidi sana kwamba hawa wapiganaji wafahamu kwamba hawakatwi kwa ulazima na wala hawalazimishwi, lakini ile ni *Sport Club* na sharti moja wapo mwanachama uchangie.

Jengine alosema la JKU kuhusu shilingi 42,000/= nafikiri hilo nitalichukua kwa sababu sijalipata bado, basi tutalichukua kwa ajili ya kwenda kulifanyia kazi na kuona uhalali wake au ukweli wake undani ukoje na tuweze kurekebisha. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hili la michezo mara nyingi Mhe. Waziri ameshatuambia kwamba ni michango ya hiari na mimi sitaki kuendelea kumsumbua. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, alichukue na kwenda kulisimamia kama yale mengine machache aliyarekebisha, basi na hili alisimamie liwe la hiari kweli kwa sababu ikiwa hiari sidhani kama kutakuwa na malalamiko tena.

Lakini tuna utaratibu wa kufanya kila kitu cha kikosi kikawa cha maagizo tu kwamba *obey*. Kwa hivyo, na Mhe. Mwenyekiti kwa bahati nzuri ameshawahi kuwa waziri wao na unayajua mambo haya basi nadhani hilo alifanyie kazi.

Mhe. Mwenyekiti, hili la pili amesema nimuachie akalifanyie kazi na niko tayari kumuachia. Kwa kweli naomba Mhe. Mwenyekiti ajitahidi Mhe. Waziri na isiwe kama tulivyomzoea Dkt. Mwinyi kwanza huwa tunafanya masihara huku nyuma akituahidi pale inakuwa sio ahadi ya Dkt. Mwinyi. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri alifanyie kazi kwa sababu hii itamsaidia hata kujenga imani ya wale vijana anaowaongoza kule.

Mhe. Mwenyekiti, athari ya hili ni moja kwamba unapokuwa unao wengi na halafu kuna kama robo moja umeshawapa na wengine hujawapa, basi

inajenga picha kuona kwamba wengine wamepata na wengine hawakupata. Kwa maana hiyo, ndipo pale ninaposema si vizuri mambo kama haya yakabakishwa katika vikosi vyetu. Kwa hivyo, hili naomba ile aliyoichukua aifanyie kazi na halafu aje watupe maelezo baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, nasema tuendelee.

Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, mimi ilikuwa sina haja ya kusimama lakini nimesimama kwa ajili ya kupata ufafanuzi zaidi. Wakati nilipokuwa nazungumzia kuhusu askari wetu wa vikosi askari wetu wa Serikali ya Mapinduzi ambao wamesajiliwa kihalali kabisa na wanafanyakazi kwa ajili ya kutekeleza maagizo ya serikali.

Sasa nikasema kwamba askari wetu kwenda kufanya kazi zao wanavaa ninja ni kujidhalilisha na kuidhalilisha serikali. Kwa hivyo, nataka Mhe. Waziri anieleze kwamba kuna sababu gani ya askari ambao ni halali wakavaa ninja wakati wa kwenda kufanya kazi zao. Je, kuna sheria yoyote ile ya serikali inayoruhusu kwamba askari wavae ninja.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kweli Mhe. Mjumbe alilizungumzia hili suala lakini ninachotaka kusema unajua wakati wa harakati kila *uniform* na mahala pale. Kwa mfano, mimi nimepiga suti niko Barazani na yule pale yupo kazini kama kwenda kushughulikia mambo yale ya kufuatilia, basi si vizuri najua mwengine anavaa kofia lile anaacha macho na nguo ya kijani na kila nguo na mahala pake. Sasa ili ninja kwa pale ndio mahala pake. Kwa hivyo, kama haipendezi basi tutawaambia vijana wasivae. *(Makofi).*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuwa mnaona kama mimi nafanya maskhara, lakini mimi sifanyi maskhara, nasema kitu ambacho ni halali kabisa. Wanaovaa ninja kwenda kuiba ni majambazi, majambazi wanapokwenda kumdhuru mtu ndio wanavaa ninja. Sasa askari wetu kwa nini wavae ninja na wanafanya kazi zao za serikali yao halali. Sasa mnalaumu vijana kwamba wanarusha mawe, sasa anakuja mtu kavaa ninja asipigwe mawe vipi na wakati wanaona kama wale wanaokuja ni majambazi na wakati kumbe ni askari wetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nisaidiwe kama kuna sheria inayoruhusu kuvaa ninja pamoja na kuwa mimi nikija Barazani navaa suti na Mhe. Waziri anavaa suti kwa sababu anakuja Barazani ni sawa. Na wao askari wetu tumewapa *uniform* kwa ajili ya kwamba wakenda sehemu waonekane hawa ni askari fulani na kuna zaidi ya askari Polisi wana na vibao hapa kila mmoja ana namba yake na jina lake. Sasa hawa askari wetu wana nembo zao ambazo ni

zile *uniform* zao kwa nini wavae ninja na wengine askari wanakwenda hawana *uniform* halafu wamevaa ninja.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe nimewaona kwa macho yangu, hawana *uniform* halafu wamevaa ninja. Ni makosa Mheshimiwa, kwa hiyo kama kuna sheria inayoruhusu niambiwe sheria fulani inayoruhusu kwamba wavae ninja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Subeit Khamis Faki kwa maelezo yake. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwenye hili itabidi tulifanyie utafiti ili tuhakikishe kwanza kama ni kweli askari wetu ndio wanaovaa ninja ili tulifuatilie zaidi. Maana wakati mwengine Mhe. Mwenyekiti, watu huko mitaani wana mbinu nyingi wanaweza kutumia mambo mbali mbali kwa kuwasumbua wananchi kumbe sio askari wetu. Kwa msingi huo wacha tulipokee hili analosema Mhe. Subeit, tukalifanyie kazi tuone uhakika wake na taarifa tutamuwasilishia Mhe. Subeit baada ya kujihakikishia kwamba ni kweli askari wetu walivaa ninja.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Waziri alivyozungumza lakini sasa Mhe. Mwenyekiti, kama wale wanaokuja wakavaa ninja sio askari wetu kwa nini wakubali askari wetu kupanda gari moja na waje wafanye kazi pamoja na wengine wakiwa wana bunduki hasa wale waliokuwa hawana *uniform* na wamevaa ninja, kwa nini wakubali kushirikiana nao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema hivi kwa sababu mambo mengine tukifanya tunaidhalilisha serikali yetu, mambo mengine tusifanyeni. Mimi naomba Waziri anihakikishie kwamba mambo ya kuvaa ninja askari itakuwa hawavai tena, watakuja kihalali kama askari wetu wanavyokuja kwa kufanya kazi zao kama wanavyofanya kikawaida. Lakini kuwavalisha ninja si vizuri. Narudia tena kama wanaovaa ninja ni majambazi, wanapokwenda kumdhuru mtu akija nyumbani anataka anavaa ninja na masizi na uso anajificha asijulikane uso. Lakini wao ni wafanyakazi wetu halali wa serikali kwa nini wavae ninja.

Mimi nipo hapo na naomba niambiwe kwamba hili tutalichukulia hatua kwamba askari wetu hawatovaa tena ninja. Nipo tayari kama nikiambiwa hivyo na ikiwa jambo hilo litachukuliwa hatua tuendelee. Lakini ukinambia kwamba akija mtu amevaa nija katika kazi hali ya kuwa wanazo *uniform* na hali ya kuwa wewe ukija hapa unavaa suti, yeye avae ninja akaaa! Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba tukishahakikisha kwamba ni askari

wetu nataka nimuhakikishie kwamba tutafanya utafiti wa kutosha na ikigundulika ni askari basi tunamuhakikishia kwamba jambo hilo kwa askari wetu hatoliona.

Lakini vile vile kwanza tujiridhishe kuwa baadae tutachukua hatua zinazofaa.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, kama Mhe. Waziri anasema tumuache alifanyie kazi hili suala basi tuendelee.

Kifungu 0201	Utawala Unguja	7,457,000,000
Jumla ya Fungu		**7,457,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU 18 - CHUO CHA MAFUNZO

Kifungu 0201

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia niliviponge za sana vikosi vyetu hivi vya Mafunzo kwa kufanya maboresho, vimejirekebisha kufanya maboresho ya kuondoa mtondoo katika baadhi ya magereza. Hili nililitaka liendelee lisimalizie tu pale Ubago lakini liendelee mpaka Wete kule mambo yawe yametengemaa. Lakini kwa masikitiko makubwa inaonekana kwamba serikali yetu bado haijawa makini katika kuboresha hivi Vyuo vya Mafunzo.

Tunazungumzia Chuo cha Mafunzo Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba *three in one* ni hawa watumishi wa Magereza au wa Chuo cha Mafunzo, kuna wanafunzi na kuna hawa wa mahabusu, ni *three in one*. Inasikitisha sana kuona kwamba bajeti ya KMKM *about nine billions*. Hawa ndugu zetu wa JKU wana *seven billions* lakini hawa Mafunzo tumewawekea *six*. Ni vigezo gani vilivyotumika wakati ukizungmzia JKU unawazungumzia wale watumishi.

Lakini ukizungumzia hawa jamaa zangu wa Mafunzo, unazungumzia watumishi, unazungumzia mwanafunzi na mahabusu. Kwa nini bajeti yao iko hivi na wakati hawa wana lengo la kuboresha Magereza pamoja na kutoa maisha mazuri kwa hawa mahabusi pamoja na hawa wanafunzi. Ukitilia maanani sasa hivi mpaka televisheni wanataka kuwawekea katika Vyuo

vyetu. Kwa nini bajeti yao iwe ni bilioni sita tu hawa KMKM wawe 9 na hawa JKU wawe 7, *that is one?*

Mhe. Naibu Spika, hii bajeti ya bilioni 6 kuwekewa mafunzo ni kuwaonea kwa sababu hawa wana mkakati wa kuondosha umasikini katika nchi yetu, wana mabonde mazuri, juzi wakati nachangia nilisema hapa kama wanataka wawekewe miundombinu ya umwagiliaji maji kwa bajeti kama hii sidhani kama wanaweza kufanikisha hilo. Sasa nilikuwa nataka Mhe. Waziri anifafanulie hii azma ya kuiboresha Mafunzo ikiwa ni pamoja kuondosha mitondoo, sasa kuwawekea televishen pamoja na kuboresha kilimo itafanikiwa kwa bajeti hii.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana ndugu yangu Mhe. Saleh Nassor Juma, ukweli hata sisi hii bajeti ni ndogo kwetu. Lakini kama nilivyosema ndio keki iliyopo, *ceiling* tuliyopewa ndiyo hii. Tumeona majengo tuliyonayo mengi kazungumza alivyokuwa akichangia Kangagani na kwengineko, tunajenga wenyewe kidogo kidogo, *ceiling* hasa tuliyopewa ni ndogo mambo yetu ni mengi.

Kubwa nataka kumwambia Mhe. Saleh Nassor kazungumza vizuri kwamba na wao hawa wana mipango yao ya kujiendeleza hasa ya kilimo cha umwagiliaji. Huo ni mchango mmoja mkubwa sana katika suala zima la chakula wanajisaidia sana katika suala zima la chakula katika makambi yote. Unajua chakula nacho kinachangia sana. Mimi nataka kusema sababu hasa ni mbili. Kwanza hiyo ya chakula kuzalisha wenyewe na imara zaidi lakini pia tutizame na hizi kazi zao za hawa Chuo cha Mafunzo wanazofanya, tofauti na KMKM au JKU, huku matumizi ya askari ni kidogo zaidi ukilinganisha na kule. Nafikiri mimi nitoe sababu hizo tatu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Unapokuwa na familia unatakiwa usiwe na *double standard* unatakiwa uwe *intention*. Mhe. Waziri anatetea kwamba hivi hivi lakini mheshimiwa bado mimi niko pale pale kwamba ndugu zetu hawa, vijana wetu hawa wa Vyuo vya Mafunzo wana matatizo mengi na bajeti ni ndogo wanasaidia sana katika suala zima la kupunguza umasikini, hata makaazi ni tatizo.

Mimi nadhani Mhe. Waziri anambie ni lini serikali itahakikishakwamba inaboresha miundombinu ya kilimo katika magereza yetu na katika vyuo vyetu hivi vya mafunzo sambamba na kuwapatia makaazi. Kwa sababu sasa hivi wale vijana saa 24 wana kazi ngumu, wana *deal* na watu lazima tukubali wakirudi wanatakiwa wapate, *shelter* nimekwenda katika vile vijumba wanavyokaa pale niliona huruma sana.

Mimi nadhani hii bajeti ya Mhe. Waziri tukubali tu kwamba bajeti hii ya Magereza haitoshi ni ndogo. Mimi nadhani kama kungekuwa kuna kasma nyengine huku zilizokuwa zipo katika hivi vikosi basi wakaondoshewa wakapelekewa. Kwa sababu hawa Mahabusi na wao wahahitaji haki za msingi ikiwa ni pamoja na kupata hayo. Nashukuru kwamba Kamishna keshaanzisha kuanzisha televishen pale.

Tunategemea baadaye apeleke magazeti, apeleke la televishen Wete, apeleke kila pahala tu kwenye gereza. Sasa hii bajeti haitoshi Mhe. Waziri. mimi nadhani kama kutakuwa na sehemu tuangalie kuwaongeza hawa ndugu zetu wa mafunzo, tuwaongeze kasma kwa sababu wanaongezeka leo na 50 kesho unawakuta 100, keshokutwa unawakuta 150, hawana *stability*, hawana *stability* ya watu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mimi nafikiri Mhe. Saleh Nassor nakubaliana na yeye, simpingi hata kidogo kwamba bajeti ndogo huo ni ukweli. Sasa mimi nilichukue kama sehemu ya serikali niombe zaidi, Inshallah kwa bajeti ijayo kutokana na hizi shughuli zetu na zaidi kule tuna mahabusu wengi ukilinganisha na wanafunzi ambao wameshapata vifungu, nao wanachangia zaidi kwa sababu hawatumiki. Siku zote *proportion* ya Mahabusi na wengine ni tofauti sana. Kwa hivyo mimi nakubaliana na yeye kabisa simpingi kwamba bajeti tuliyoekewa ni ndogo. Hilo acha nilichukue na kiongozi wetu hapa yupo analisikia hilo tutalifanyia kazi kwa pamoja kwa mwaka ujao.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mimi nazungumza kwa *experience* kwa sababu mimi ni mzoefu katika mambo ya jela kwa hivyo sitoi kitu tu hivi hivi, ni mzoefu katika mambo ya kufungwa. Kwa sababu waziri ameshaeleza hilo. Kwa hivyo nadhani tuendelee.

Mhe. Naibu Spika: Niseme kwa ufupi, mmekuwa kama mnachangia upya, nenda kwenye hoja tumalize.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Sawa sawa Mhe. Mwenyekiti, nafikiri mimi nina taarifa naibua hoja tujadili upya bajeti. Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu wala hapa sikutaka maelezo makubwa kwa sababu linafanana na lile nililolizungumza. Lakini kwa sababu na hapa pia lipo. Nilizungumzia kadhia kama niliyoitaja ya vijana wa Chuo cha Mafunzo kuchangishwa kwa ahadi kwamba kunauzwa *SACCOS* ya Chuo cha Mafunzo na waliambiwa baada ya fedha kukusanywa zingetumika kuzalisha baadaye walirejeshewa fedha zao halafu lile faili lilipatikana lilitumika kuendelezea miradi.

Sasa na huku vile vile kuna kama asilimia 20 ninavyoambiwa wamerejeshewa, lakini inakuwa inafika asilimia 80 badi hawajarejeshewa fedha zao na kila wakiuliza bado wazungusha zungusha. Lakini nilikuwa nataka hili pia Mhe. Waziri kama ni la mwanzo kama nilivyosema sitegemei kwa sasa hivi atakuwa na jibu lakini kama ni la mwanzo na hili pia alichukue awafuatilie haki zao vijana wetu awarejeshee haki zao.

La pili Mhe. Mwenyekiti, suala la fedha za likizo suala hili linalalamikiwa katika vikosi vyote. Fedha zile wanapokwenda likizo hasa huwa hawapewi na wengine wanaweza wakapewa zaidi ya mwaka baada ya kwamba wameshakwenda likizo wakati fedha ile imekusudia waitumie wakati ule kwa shughuli za mapumziko wao na familia zao. Nataka maelezo katika haya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, lazima nikubali kulifuatilia hili suala alilozungumza la mgao wa wale ambao hawajapata katika *SACCOS* ile. Nitalifuatilia kuona kwamba haki inatendeka ili wale ambao hawajapata kuona wanapata. Kuhusu suala la fedha za likizo Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kila kikosi kwa mwaka huu tumeweka kabisa pesa zake. Tunatarajia labda milioni 85 au milioni 90 ukigawa kwa laki moja utaona pale ni wangapi wanatarajiwa kwenda.

Sasa kama nilivyosema zaidi kwamba kwanza tutahakikisha kwamba wanapatiwa pesa kama tulivyoambiwa. Kweli nakubali tumekuwa tunapata malalamiko ya hapa na pale kwamba hazipati kwa wakati. Hili tunalisimamia tuone kweli kila anayekwenda likizo kwa kipindi kile maana ni *rotation* ya miaka miwili. Kwa hivyo kama kipindi chake kimefika basi apewe haki yake. Tutalisimamia vizuri hili Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimepokea ahadi ya Mhe. Waziri na nimuombe kama zile alivyosema kwenye JKU kwamba akishakulifanyia kazi atuletee ripoti ya hatua aliyokuwa kaifikia.

Kifungu 0202	Idara ya Vituo vya Mafunzo	6,099,000,000
Jumla ya Fungu		**6.099,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU 29 - KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO

Kifungu 0201 Utawala

Mhe. Saleh Nassor Juma: Wakati nachangia nilisema sana kuhusiana na hawa vijana wetu wa KMKM kwamba kuboresha KMKM sio kwamba tunawasaidia hawa vijana. Vile vile itakuwa tunawasaidia Wazanzibari kwa ujumla kutokana na kazi zao wanazozifanya za uokozi. Vile vile nikasema kwamba hawa vijana wana changamoto nyingi ya kukosa vifaa. Kuna vifaa muhimu kwa mfano, *dehydration chamber, lifting bags, diving uniform* mambo kama hayo yanakosekana kwa vijana wetu hali ya kuwa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, yaani kijana akimalizikiwa na pumzi kule chini lazima akiletwa juu apate kitu kinachoitwa *dehydration chamber* aingizwe ili aweza ku-*regain*, kinyume na hivyo anapoteza maisha kabisa na wala hakuna hospitali yoyote ya kumtibu. Je, katika hii bajeti aliyotuletea Mhe. Waziri ya bilioni tisa mambo kama haya ya *dehydration chamber, lifting bags*, pamoja na *diving uniform* zimo?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Saleh akiangalia kifungu Nam. 220802 kinaelezea *spare* au zana tumetenga pale shilingi milioni mia sita na sitini kwa kununua. Hivyo vitu alivyozungumza lakini kwa kweli hicho kitu alichozungumza ni ghali mno. Hata hivyo tutajitahidi tuone kiasi gani tunaweza tukachangia kupata hizo *lifting bags* na zana nyengine lakini tumewapa bajeti nzuri sana kwa zana na kuthamini hilo alilolisema. Mhe. Saleh kwamba vijana wetu hawa wanashiriki katika kazi mbali mbali za uokozi na kuzamia Naona hii kazi pawe na zana za kisasa kabisa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakubaliana na yeye kabisa kwamba kweli ipo haja ya tumetenga bajeti nzuri sana kwa kulizingatia hilo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Sijamfahamu amekubaliana na mimi vipi, kwanza kuna bajeti anasema imo lakini halafu anasema kwamba vitu hivi ni ghali sana. Sijui kama imo hii au haimo anieleze kama katika hizi bilioni tisa katika huo ununuzi wa zana hii mambo ya *dehydration chamber*, kama haimo haoni kwamba hili ni tatizo. Kwa sababu hawa vijana meli zote Mwenyezi Mungu tunusuru wanazama ajali tunazozitegemea sana ni meli za hapa. Sasa ikiwa mambo kama haya hayamo hawa vijana wetu watakufa, wakija kutuokoa na sisi tutaendelea kufa.

Je, kitu hichi cha msingi, juzi serikali ilikata kata fedha katika bajeti zaWizara zote hapa kutaka kununua meli, washindwe kununua chombo hichi cha kuwasaidia wale vijana wetu kutuokoa tutakapopata ajali. Kama hakuna basi tubanane hapa hapa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, azma yetu na hayo masuala yawemo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, sitaki nipingane na Mhe. Waziri kwa sababu tumeshazoea hapa kwamba serikali haijajipanga, tuko mbioni, azma ipo, jamani mambo haya hayatufiki tunakokwenda. Mimi nadhani kama azma mnayo fanyeni kama mlivyofanya kwenye meli, kateni manyofu ya hapa, mnyofoe na pale, mtuletee hii. Hii itatusaidia sisi tutakapozama baharini kuja kutuokoa na vile vile kuwasaidia wawekezaji kuja. Watu wanawekeza katika mambo ya kuzamia hawawezi wanaogopa ni moja tu iliyopo ya mzungu na ni huko Kaskazini. Sasa kama tukipata hii *D-hydration chamber* ya serikali hata wawekezaji watakuja serikali itapata pesa. Kwa hiyo Mheshimiwa tuendele bwana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilipokuwa nikichangia katika kikosi hichi nilimuomba Mhe. Waziri kuzingatia kwa kuwaongezea boti katika kambi ile ya Mkokotoni kutokana na bandari iliyojitokeza na inakuwa kwa kazi pale. Mara nyingi huwa vyombo vinatoka Tanga hutokezea matatizo ya kuzama na pale ndio kituo kinategemewa katika maokozi. Tukizingatia tunasikia jirani na Tumbatu ambapo watu wanasafiri mara kwa mara na hutokea matatizo mara kwa mara. Namuomba Mhe. Waziri kuzingatia kuwaongezea boti, boti iliyokuwepo ni ndogo na ipo moja tu na inakuwa ina majukumu mengi.

Kwa hivyo hili nilikuwa namuomba Mhe. Waziri aweze kulizingatia kwa maslahi ya watu wetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na ushauri wa Mhe. Bi. Panya kuhusu ombi la kuongeza boti nyengine pale Mkokotoni. Ni kweli kazi wanayofanya vijana wetu ni nzuri na wanakaa muda wote kama *stand by* kwa watu wanaokwenda Mkokotoni na sehemu nyengine. Nakubaliana na yeye moja kwa moja kwamba tutalizingatia hilo tuone kwamba tunaongeza boti pale.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu naomba kwa upande wa vikosi nizungumzie hoja yangu ya mwisho kabisa. Katika mchango wangu nilitaka maelezo, hili nalo nafikiri Waziri ni katika yale mambo yalikuwa mengi akaamua asubiri tumuulize hapa ili ayatolee ufafanuzi wake.

Mhe. Mwenyekiti, ni suala KMKM lakini pia lipo kwenye JKU sijui na viko viwili kama lipo, lakini mimi sikuwa vikosi viwili nimepata malalamiko kwamba vijana walinzi wamekuwa wakifanya kazi. Kwa mfano katika

shughuli za ujenzi kupitia vitengo vya ujenzi vya vikosi hivi ni kwamba fedha zake ambazo zinapatikana huwa hazina *record* na inavyosemekana hata hazina *accounts,* mara nyingi zikiulizwa huambiwa zinaingia katika *canteen* wakati *canteen* kwenyewe chakula hapa bajeti yake kuanzia mwaka jana tuliiongeza sana kwa vikosi vyote.

Sasa nilikuwa nataka Mhe. Waziri anisaidie, sijui kama ni yeye hata kama Waziri mwenye dhamani anaweza akanijibu yeyote kwamba fedha hizi zinaingia katika *account* gani na matumizi yake yanatazamwa vipi kulingana kwamba yanatumika kwa ajili ya shughuli za kiserikali na hazitiwi katika mifuko ya watu, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Ismail Jussa alizungumza hilo suala na nakiri kwamba nilimjibu kwamba wanapata asilimia 20 ya mapato yanayopatikana katika kazi wanazozifanya wapiganaji wetu.

Kimsingi hasa yale ni mapato ya serikali na yanawajibikia kuingia kwenye mfuko mkuu wa serikali huko kuna makubaliana maalum kati ya Wizara ya Fedha pamoja na kwa kila kikosi *percentage* fulani wanayowaweka kama *retention* kwa kusaidia baadhi ya kazi zao. Hiyo nambari ya *account* sina lakini ninachosisitiza tu kwamba zinaingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Utaratibu huu tunataka tuuboreshe zaidi ili kuwe na uwazi kabisa kwa kila kazi wanayofanya na mapato yanayopatikana. Ahsante

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, sina matatizo nimuombe tu Mhe. Waziri hili alifuatilie halafu baadae aje atwambie ikiwa kwake ikiwa Waziri mwenye dhamana ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu kwamba hizi zinaingia, sitaki nambari ya *account*. Nataka kujua tu kama zimeingia katika *account* gani kwa sababu huko kuna malalamiko kwamba hizi zinashughulikiwa mara nyingi na Mkuu wa Kikosi husika na mhasibu wake lakini haziko hasa katika fedha zilizoingia panapohusika.

Sasa kuweka majibu yake kwamba zinaingia katika serikali na zinatumika wanapata mgao wao, nilikuwa nataka aje aturidhishe kama zinaingia katika mfuko gani. Lakini kwa sasa hivi nasema nashukuru tuendelee, mheshimiwa.

Kifungu 0201	Utawala	9,452,000,000
Jumla ya Fungu		**9,452,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU 32 - KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Kifungu 0201	Utawala Unguja	3,113,000,000
Jumla ya Fungu		**3,113,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU 34 - KIKOSI CHA VALANTIA

Kifungu 0201	Utawala	3,258,000,000
Jumla ya Fungu		**3,258,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU 37 MKOA WA MJINI/MAGHARIBI

Kifungu 0401	Mpango na Sera	599,601,000
Kifungu 0501	Wilaya ya Mjini	473,956,000
Kifungu 0601	Wilaya ya Magharibi	381,443,000
Jumla ya Fungu		**1,455,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 38 MKOA WA KUSINI UNGUJA

Kifungu 0401	Mipango na Sera	365,444,000
Kifungu 0501	Wilaya ya Kati Unguja	420,282,000
Kifungu 0601	Wilaya ya Kusini Unguja	361,274,000
Jumla ya Fungu		**1,147,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 39 MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

Kifungu 0401	Mipango na Sera	362,968,000
Kifungu 0501	Wilaya ya Kaskazini A	416,836,000
Kifungu 0601	Wilaya ya Kaskazini B	365,120,000
Kifungu 0701	Wilaya ndogo Tumbatu	102,076,000
Jumla ya Fungu		**1,247,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 40 MKOA WA KUSINI PEMBA

Kifungu 0401 Mipango na Sera 463,864,000
Kifungu 0402 Baraza la Mji Chake Chake

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Mwenyekiti wakati nachangia jana leo hii asubuhi wakati ninachangia nilizungumzia sana kuhusu Baraza langu la Mji wa Chake-Chake jinsi walivyowahamisha wafanyabiashara pale juu *stand* na kuwateremsha Qatar, kwa kweli pale soko la samaki ambapo panaitwa Qatar wafanyabiashara wale wako katika mazingira magumu, na kwa masikitiko makubwa asubuhi nilitoa hisia zangu kwamba mazingira yale hayaridhishi kwa sababu hawajapelekewa miundombinu ya maji na hata lile *shelter* ni *temporary,* yaani wameweka magunia tu ikinyesha mvua biashara zao zinaharibika, magonjwa yanatokea. Sasa Waziri katika hili wale wafanyabiashara ambao umewaondosha kule na kuwalazimisha waje huku Qatar lini utawafikishia miundombinu ya maji pamoja na masuala ya *shelter* ya uhakika pamoja na kuwaondosha wale wauzaji samaki pale barabarani ambapo wengi wanagongwa na magari siku hizi pamoja na mapikipiki ili wapate pahala pazuri pa kufanyia biashara.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Saleh alichangia kuhusu Baraza la Mji Chake-Chake na hizo *observation* zake ni kweli alisema. Nataka kusema tu kwamba soko la matunda la Qatar linategemea kujengwa upya kupitia mradi wa kilimo unaitwa Mivam. Upimaji wa eneo hilo tayari umeshafanyika na muda wote kuanzia mwezi Julai ujenzi unaweza kuanza.

Hali ilivyo hivi sasa choo kipya kimeshajengwa Mhe. Mwenyekiti, na kimeshaanza kutumika. Mahodhi mawili ya kuhifadhia maji pia yamejengwa na yanatumika. Pia umeme upo tayari pale. Kwa hivyo nakubalina na wazo lake tunajitahidi kuiboresha au kuiendeleza miundombinu ya pale ili soko lifanye kazi na lilete tija bila ya usumbufu kwa wauzaji na watumiaji wa pale.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakaa Vitongoji umangani soko ninalotumia ni la Qatar pamoja na majibu ya Mheshimiwa sitaki niseme kama kanidanganya lakini ile sehemu hairidhishi. Ikinyesha mvua kuna tope nyingi na lile soko liko barabarani, kuna barabara pale ni bidhaa na madimbwi ya maji. Kwa hivyo mimi nilikuwa nataka tu Waziri kwamba kwa sababu ameamua kupeleka soko pale, soko liko barabarani na barabara yenyewe ina madimbwi na matope pale karibu na lile soko kiasi ambacho magari yanaweza yakateleza mara nyingi na kukosa kuwagonga wafanyabiashara pamoja na wateja pale. Ninataka waziri anieleze ni lini ataweka alau kifusi katika sehemu ile na ikiwa si lami kabisa pamoja na mule

sehemu ya biashara kuweka saruji, kwa sababu hali ni mbaya na magonjwa nyemelezi kila wakati hasa yanayozaliwa na maji kama vile malaria na matumbo yanaweza yakajitokeza sana pale Qatar.

Kwa hivyo mimi nataka waziri pamoja na maelezo yake ambayo kwa kiasi fulani hayakidhi haja anieleze ni lini yale mashimo yaliyopo pale kwenye soko yanawekwa sawa ili wafanyabiashara waweze kufanya biashara zao uzuri na hawa wauza samaki waliopo kwenye barabara kuondoshwa na kupatiwa sehemu nyengine kwa kujaza, kwa sababu sehemu ile imejazwa ile ilikuwa ni bahari ikafukiwa. Sasa yeye atatufanyia mpango gani ili ile bahari iendelee kufukiwa na hawa wafanyabiashara wakae vizuri wauza samaki wasigongwe na gari kila wakati.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Mwenyekiti, kama nilivyosema ule mradi upo na mfadhili tumeshampata na hayo anayozungumza yote Mhe. Saleh yatashughulikiwa na mradi huu yote hayo hakuna wasi wasi wowote, michoro imeshafanywa kwa kushirikiana na hilo suala la mazingira na wenzetu wa Idara ya Mazingira yote yatashughulikiwa. Lakini kama kutakuwa labda na *delay* yoyote basi ninamuahidi alau tutaziba viraka kidogo kabla ya mvua za Vuli tutaziba viraka japo kwa fusi kama alivyosema. Ninamuomba sana tushirikiane lakini anatumia soko lile tushirikiane kulifanikisha suala hili. Nachukua ahadi kwamba ndani ya miezi mitatu alau tutaziba ziba viraka kabla ya mradi haujaweka sawa mambo yote.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti najua mara nyingi tendo hukidhi haja maridhawa kuliko neno, haja ikishughulikiwa kwa matendo hupatikana wepesi lakini ikishughulikiwa kwa maneno huchelewa kama sadaka. Mhe. Mwenyekiti, iliyoko mbele yetu ni Ramadhan pale pataongezeka maradufu wateja. Sasa mimi naomba tusizozane na Mhe. Waziri ni mwenzangu wa siku nyingi na tuna *history background* moja. Sasa mimi nadhani katika hii basi afanye matendo ili watu wale uhondo na asiseme maneno watu wakaendelea kula uvundo siku zote. Vile vile ashughulikie na ile *car park* kwa sababu pale Chake-Chake hakuna *car park*. Milioni 80 wanachangisha nimeona katika kitabu kimoja kwamba karibu milioni 80 wanachanga Baraza letu la Mji pale. Lakini kazi yao ni kukusanya kodi tu wao lakini gari iki-*park* wameshafika wanachukua pesa lakini hakuna maegesho ya gari. Je Mhe. Mwenyekiti, katika hili utanambia nini ili niweze kukuruhusu kuendelea katika mambo hayo.

Mhe. Mwenyekiti: Hoja ya mwanzo umekubali naona unaleta mpya, useme umekubali unatoa nyengine. Ya mwanzo umekubali?

Mhe. Saleh Nassor Juma: Kwa heshima kubwa na taadhima ya hali ya juu Mhe. Mwenyekiti, nadhani hii akishafanya matendo mimi sina tatizo. Afanye matendo tu asiseme kila wakati afanye matendo. Kwa hivyo hii twende lakini na hii *car park* naomba lini watawajengea pale ili wale wafanyabiashara wasipigwe tena na magari ipatikane *park* nzuri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru Mhe. Saleh kwanza kwa kukubali ushauri wangu huo aliosema tutashirikiana na hili. La pili alilozungumza ninafikiri ndio ile hutumia kauli hiyo kwamba tuaminiane kuwa atuamini na yeye tunamuamini yeye ni Makamu Mwenyekiti wangu wa Kamati yangu, sasa naamini atakuwa anafuatilia ule utendaji wetu naona atuamini.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, tuendelee.

Kifungu 0402	Baraza la Mji Chake Chake	370,000,000
Kifungu 0403	Baraza la Mji Mkoani	211,000,000
Kifungu 0501	Wilaya ya Chake Chake	430,728,000
Kifungu 0601	Wilaya ya Mkoani	395,408,000
Jumla ya Fungu		**1,871,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 41 MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Kifungu 0401	Mipango na Sera	430,375,000
Kifungu 0402	Baraza la Mji Wete	280,000,000
Kifungu 0501	Wilaya ya Wete	414,775,000
Kifungu 0601	Wilaya ya Micheweni	372,308,000
Kifungu 0701	Wilaya ndogo ya Kojani	59,542,000
Jumla ya Fungu		**1,557,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 43 AFISI YA USAJILI NA KADI ZA UTAMBULISHO

Kifungu 0201

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, leo mchana baada kuahirisha kikao cha mchana tulikuwa na semina ndogo ya viongozi wa kiroho kwenda

kutuaidhi namna gani tunaweza kama Wawakilishi kaondokana na mizozo katika jamii.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia hoja hii nililieleza bahati nzuri Mwenyezi Mungu katukubalia dua ya kupata viongozi hawa. Nilitaka kujua kwamba kuna wananchi wengi ambao wamenyimwa haki yao ya kupewa vitambulisho. Hoja yangu kwa Mhe. Waziri nilitaka kujua hatma ya wale ambao wanafika na ambao hadi sasa hawajapata haki yao. Kwa hivyo naomba Mhe. Mwenyekiti, sasa anipe jawabu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nilimjulisha Mhe. Omar Ali Shehe kwamba hakuna tatizo lolote kama wana sifa basi watapatiwa haki zile za *ZID* vitambulisho vya Mzanzibari. Ningemuomba arudi kwa *DC* wa Wilaya ya Kaskazini 'A' ndio yuko *field* tushirikiane na Masheha katika sehemu zile mbali, alileta huyu mwengine yuko Nungwi, Kidoti wapi, orodha mkubwa watu 500 kama alivyosema. Sasa mimi ninachomuomba tu ile orodha turudi kwa wale Masheha wathibitishe hakuna tatizo watathibitisha tu kweli huyu ana sifa zote atatoa ruhusa na *ZID* watampa kitambulisho hakuna tatizo Mhe. Mwenyekiti. Lakini sasa kuuchukua ule orodha ukaniletea mimi Waziri hapa nitoe kauli ninayotoa tushirikiane turudi kwa *DC* wa Wilaya ya Kaskazini 'A' na Kaskazini 'B' basi tufanye taratibu hizo, mwenye haki yake atapewa ambaye hana haki pale ataelekezwa. Bwana hapa wewe hustahiki unastahiki huku twende huku hakuna tatizo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, suala hili hadi kufikia katika ukumbu huu kwamba tayari huko halijapata ufumbuzi ndio maana sasa wananchi hawa wakalazimika kutafuta viongozi sisi Wawakilishi kuja kulizungumza hapa. Nasema hivi kwa sababu sheria imeeleza kwamba chochote kinachofanywa huko na Mkurugenzi ni kwa sababu ya maelekezo ya Waziri ndio sheria ilivyosema, kwamba Mkurugenzi atafanya hivi kwa maelekezo ya Waziri lakini hoja nyengine ni kuwa itakapofika hatua ya kukwama kama ambavyo sasa ipo ni Waziri ndiye atakuwa na *final decision*. Kwa hivyo Mhe. Waziri kunirudisha kwa Sheha akaturudisha kwa *DC* itakuwa kwa kweli hatujafanya sheria, inasema sasa watu wa-*appeal* kwake na kwa sababu wananchi hawawezi kumpata yeye ndio maana sasa sisi kama Wawakilishi vyenginevyo kama ikiwa ana uwezo wa kutuletea Sheha akaja akatujibu sasa atuletee Sheha. Kwa sababu sasa ni wakati ambao tunahitaji kupewa maelekezo kama Wawakilishi. Sasa sisi msemaji wetu katika *level* hii ni yeye, kwa hivyo sheria inasema kwamba baada ya hilo lote litakalotokea huko Mhe. Waziri katika hili ndiye atakuwa ana *final decision*, ndio maana suala kwake yeye kwamba tunataka muongozo wake yeye kauli yake ndio muhimu hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Mhe. Mwakilishi Waziri yuko muwazi na katoa maelezo vizuri yeye kwanza kapokea hoja yako anakwambia kwa kuwa yeye hapa hana wale wahusika mtoke shirika mwende kwa Sheha, huko Kidoti, Nungwi, Tumbatu wakaangaliwe sifa wanazo watapewa, hawana sifa ataelekezwa wapi kwa kwenda. Yeye kakubali kapokea au hukumfahamu.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, kama laitani Waziri angelisema kama hivyo unavyosema wewe wala nisingelikuwa na matatizo hiyo ndio kauli ambayo ninahitaji kwamba sasa mimi na yeye au sisi na yeye hilo hatuna tatizo. Lakini hiyo ilikuwa ni hoja moja, kama ikiwa kishalikubali hilo mimi nadhani sasa ni kitu cha kupanga.

Hoja ya pili ambayo niliitoa sambamba na hii kwamba kuna watu ambao hadi sasa wameshapigwa picha na katika kikao cha Mhe. Waziri tulichokifanya Pemba Mkurugenzi wake ametuthibitishia kwamba mtu atakapopigwa picha hatozidi wiki mbili kabla hajapewa kitambulisho. Sasa hivi kuna watu zaidi ya miezi 2 wamepigwa picha na hatma yao wanaambiwa wasubiri Disemba. Hoja yangu iko hapa kwamba uandikishaji hasa Kaskazini kwa Jimbo la Nungwi unamaliza leo na majimbo mengine vile vile utamaliza ndani ya siku tatu kila sehemu. Je, ambapo hapa ninataka sasa serikali itoe msimamo, nini hatma ya watu hawa ambao tayari watakuwa wameshapitiwa na uandishi katika daftari la kudumu la wapiga kura. Je, maana yake ikiwa daftari limeshapita hapa imani yetu inavyotupa, sasa wakati wa serikali kuhakikisha kwamba kabla ya uchaguzi daftari litarudia tena ili na wale wapate haki yao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Omar kama ifuatavyo kuhusu suala la daftari. Suala la daftari ni endelevu. Sasa hivi shughuli itaendelea na itaendelea kufanyika tena hasa wakati utapokabiria uchaguzi mkuu vile vile tunajipanga kufanya shughuli kama hii ya kuandikisha wale ambao watakuwa wameshafikia umri na sifa ili waweze kuandikishwa katika daftari. Kwa hivyo nataka nimuhakikishie Mhe. Omar kwamba suala la daftari la kudumu ni endelevu hata kama ikiwa sasa hivi mtu ameshindwa kuandikishwa katika eneo lake na anayo sifa basi vile vile wakati watakaporudia utaratibu ule utakuwepo ambapo kwenda katika Ofisi zao za Wilaya wataandikishwa katika daftari la kudumu la wapiga kura. Ushakuwa umetimiza vigezo hakutokuwa na tatizo kwa nini usiandikwe katika daftari la kudumu.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, baada ya kupata majibu sahihi kwa hoja zangu mbili na tuendele.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Naomba unikubalie kwamba kila mtu ana uwezo wake wa kufahamu na anaweza mmoja akaridhika mwengine ikawa bado, kwa hivyo naomba unipe ruhusa ya kuendelea na suala hili hili.

Mhe. Mwenyekiti kwa mujibu wa sheria yetu kama alivyoeleza Mhe. Omar kuwa kazi za Mkurugenzi wa Vitambulisho ni kutokana na sheria hii na maelekezo ya Mhe. Waziri atamuandikisha kila Mzanzibari Mkaazi katika Zanzibar ambaye ametimia umri wa miaka 18 na kuendelea.

Pili, kwa ushauri huo wa Mhe. Waziri Mkurugenzi atatoa vitambulisho kwa kila Mzanzibari aliyeandikishwa kuwa ni mkaazi wa hapa na sehemu ya tatu ni kuwa ataweka rekodi ya hao Wazanzibari waliopatiwa vitambulisho, yote haya yanafanywa kutokana na maelekezo ya Mhe. Waziri. Hapa hakutajwa Sheha, wala hapa hajatajwa Mkuu wa Wilaya. Mhe. Mwenyekiti, kwa uzoefu Mhe. Waziri sasa ni moja suala kama hili ilibidi atembee Zanzibar nzima na Wilaya ya Wete alikuja akatoa hotuba kali. Hata Mkuu wetu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba jamani tumeshabadilika sasa huu wakati mwengine. Sheha yeyote atakayekwenda kinyume na mambo haya kwa hapa hatusameheani. Mimi nikamwambia Mhe. Waziri nikifika nikiwa hai nataka nikusifu mpaka mwenyewe ushangae. Lakini mambo yenyewe yaliyotokea ni makubwa kama haya na *registration* haijesha bado, kuna watu mia saba na tena wenye vyeti vya kuzaliwa ambao haikuandikwa humu na halafu washatimia umri na kuna 71 hao mpaka hivi sasa. Tukisema warudi kule kule kwa Sheha wakati Sheha kafanya kwa makusudi na Mheshimiwa anajua ni kujihangaisha bure na kupoteza wakati na daftari lende sehemu nyengine. Kwa nini Mhe. Waziri kama kweli ana nia safi hasemi tu kuwa kwa wote wale waliokuwa wameshatimia umri na wanakoseshwa tukaja tukaona kuna mtu kakosea akamchukulia hatua badala ya kusema wende tena kwa Sheha na Mkuu wa Wilaya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ninafikiri kama ulivyosema kwamba tumejitahidi kutoa ufafanuzi na sisi umetusaidia pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais lakini pia kuna fursa nyengine kwamba kwa mujibu wa sheria kama mwananchi hakuridhika basi anapaswa kukata rufaa, nayo *element* hiyo ipo, mbali ya ushauri nilioutoa wa sisi kwenda kwa Mkuu wa Wilaya lakini mwananchi mwenyewe anaweza kukata rufaa hiyo ipo kwenye sheria kabisa. Mhe. Mwenyekiti, mimi silioni tatizo Mhe. Salum tumeshalimaliza hili.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza tujue kuwa kupewa kitambulisho cha Mzanzibari ni haki ya kila raia akishatimiza hayo masharti na kusema mwananchi akakata rufaa si jambo rahisi, kuna wengine hata

kuelekea kwenye rufaa hawataki japo kuwa ni haki yao si kwahala kuzuri kwa kwenda. Mhe. Mwenyekiti, anaowaadhibu ni Wazanzibari wetu, watoto wakikosa vitambulisho hivyo hawapati kuendelea kusoma, mtu hapati kusafiri, mtu hapati kupiga kura, mtu haki zote za uraia amezikosa kwa makusudi kabisa.

Mimi siwezi kuzuia kuwa kisiendelee kifungu lakini nasema Mhe. Mwenyekiti, ajue tu kuwa hivi sasa anawadhalilisha Wazanzibari tena anawakosesha haki zao kwa makusudi au atamke kuwa hawa watu kama wana sifa wapewe. 738 si kidogo wakati *registration* inaendelea, kuna uzito gani kusema hivyo au ndio kule tulikozungumza sheria namba 12 (5) kuwa watu wanafanya mambo haya kwa makusudi kujinufaisha kisiasa kwa kuwakosesha watu kupiga kura bure kwa uchaguzi wa 2015 pengine watu wanategа hapo. Hebu Mhe. Mwenyekiti, tuambie hasa ugumu uko wapi mpaka akaona sisi hawezi kutwambia ukweli kwa suala hili nyeti. Huu ugumu hasa uko wapi asiweze kutamka kuwa wapewe haki zao watu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mimi nakubaliana naye kama alivyosema kama anazo sifa wanastahiki watapewa ninafikiri mwenyewe kaungama kwamba wanazo sifa na mimi ninazidi kusisitiza, kama anazo sifa kwa eneo lile hakuna matatizo Mhe. Salim mimi sioni tatizo na wala sioni huu mvutano uko wapi. Mimi nitalichukua hilo tupe orodha tutakwenda kila Sheha atuthibitishie huyu mkaazi halali wa hapa, katimiza sifa, atapewa hamna tatizo lakini kama hana sifa basi hiyo ni haki kweli ya kila Mzanzibari lakini akachukulie kule ambako anastahiki kama pale hana sifa, kama ana sifa pale hakuna tatizo ruhusa apewe, hilo nasisitiza Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: nashukuru Mhe. Waziri, kazungumza vizuri lakini sasa basi kwa kulipa uzito suala hili ninaomba apange yeye na Mkurugenzi wa Uenezi katika Chama cha Wananchi *CUF* aliyendika hoja hii kwa maandishi na kupeleka barua kwake na kuwapa watu wa Serikali waaminifu wanaohusikana na shughuli hizi ili waende pamoja kwa kushuhudia kuwa yale mambo ni ya kweli na Sheha atakapofanya ukorofi iwe hatua ichukuliwe kuliko kumwambia aende peke yake, kuwe na mtu hasa wa kufuatana naye na hili suala lifuatiliwe kwa sababu limeshapelekwa kwake kwa maandishi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, namkaribisha Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Salim tushirikiane kulifanikisha hili suala.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Nashukuru Mhe. Waziri kazungumza jambo zuri tuendelee.

Kifungu 0201	Utawala wa Unguja	1,773,000/=
Kifungu 0301	Afisi Kuu - Pemba	

Mhe. Farida Amour Mohammed: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilivyokuwa nikichangia katika kifungu hichi nilimtaka Mhe.Waziri anipe ufafanuzi wa juu ya wale watu aliosema kama yeye wale watu atawafanyia uchunguzi wa kina ili kujua kama watu hawa ni wangapi na wachukuliwe hatua na kwa bahati mbaya sikusikia maelezo yoyote kama wale watu wamefikia idadi gani na wamechukuliwa hatua gani na wamekuaje, wamepata hivyo vitambulisho wakati wao sio wahusika wa vitambulisho.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ukifungua katika hotuba yangu ya bajeti nimejaribu kuangalia ukurasa ule kuna hesabu kamili ya vile alivyouliza Mhe. Farida. Mhe. Mwenyekiti, hizo *figures* ninazo kamili kwa wale ambao walihalifu sheria hiyo ya vitambulisho na ni wageni na nilizungumza Commoro, Zambia na nchi nyengine sikumbuki, nitajaribu kuitafuta halafu nitampatia.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Waziri lakini kutokana na idadi kubwa aliyoitaja ya vitambulisho vilivyokuwa vimo ndani ya mawilaya, lakini hawa aliosema Commoro, Zambia ni watu wangapi mbona hanipi ile hesabu sahihi. Sasa hivyo tutakuwa tunababaishana, vitambulisho vilivyokuwepo ni vingi na yeye kasema vile kafanya uchunguzi ni wageni ambao hawahusiki, sasa hawa Wacommoro, Wazambia wangapi hasa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni 98(1)(b) naomba ninukuu.

> "98(1) (b) Hairejeshi mjadala juu ya jambo ambalo limejibiwa kikamilifu katika mkutano uliopo au mkutano uliotangulia bila ya sababu za msingi, na kwa kuwa Mhe. Waziri wakati akijibu hoja alieleza kuwa majina kitakwimu kwa wale wageni wa kila nchi"

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kurudia mambo ambayo tayari yana majibu inakuwa ni kurudisha nyumba kikao chako hichi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, kutokana na kanuni iliyosomwa kwa hivyo tunaomba tuendelee.

Kifungu 0301	Afisi Kuu - Pemba	282,000,000/=
Jumla ya Fungu		**2,055,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa
na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU NO. 10 OFISI YA RAIS IKULU

Kifungu 01

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nipate maelezo ya kina kwa sababu tangu nilipoanza kule nilijikita sana juu ya hoja yangu moja juu ya suala la gharama kubwa za ujenzi na matengenezo ya Ikulu na nyumba mbali mbali ambazo ziko chini ya Ofisi ya Rais.

Sasa kule kulikuwa na mamilioni mengi kwa miaka mitatu iliyopita lakini bado katika fedha za maendeleo fungu nambari 750000 kifungu kidogo cha 750002 uimarishaji wa nyumba za viongozi wa nyumba za Serikali, lakini katika kiingereza imeandikwa *program for construction and rehabilitation of state and state lodging* pana milioni mia sita. Sasa nilikuwa nataka anieleze zile zilizokuwa kule katika fungu la *OC* katika Wizara ya Mhe. Waziri, zinafanya nini na hizi mia sita milioni zinafanya nini.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, uimarishaji wa nyumba za viongozi na nyumba za Serikali *program for construction and rehabilitation of state and state lodging* milioni mia sita, huu ni mradi, ndio ule ujenzi wenyewe tuliosema ujenzi mkubwa, uimarishaji wa nyumba za viongozi na nyumba za Serikali.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikiliza mimi Mhe. Waziri, bado maelezo yake nimeona ni ya jumla mno kwa sababu kama alivyosema kule tulipouliza katika fungu la *other charges* au gharama nyengine za utawala na uendeshaji, kuna mafungu mbali mbali ambayo Mhe. Waziri ameyatolea maelezo kwamba lengo lake ni kufanya matengenezo makubwa na madogo ya Ikulu na nyumba mbali mbali na ofisi ambazo ziko katika chini ya Ofisi ya Rais. Sasa humu kuna mradi wa maendeleo milioni mia sita na kule ukenda ukizichanganya zinaweza zikakaribia hizi hizi milioni mia sita, ukenda ukachukua na Idara ya Utumishi na Uendeshaji, ukazichukua za Ofisi ya Faragha, ukazichukua za Baraza la Mapinduzi, ukazichukua za Ofisi ya Rais Ikulu kwa ujumla wake. Sasa nilikuwa nataka kuwasaidia huu

mradi huu una tofauti gani na ule ambao upo katika mafungu yale moja moja ambayo kwa maelezo yake mwenyewe zinafanya kazi hiyo ya utengenezaji na uimarishaji wa nyumba zilizokuwa chini ya Ofisi ya Rais ambazo ni Ikulu kubwa ya Mnazi Mmoja, Ikulu ya makaazi Migombani na Ikulu nyengine mbali mbali ambazo zinatumika, sasa hizi mia sita aje atusaidie.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Jussa afungue ukurasa wa 62 mpaka 63 wa kitabu cha bajeti, tumeeleza miradi ya maendeleo ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na tumeueleza huu mradi wa sasa kule nyumba tumemaliza, sirudi nyuma mradi wa uimarishaji wa nyumba za viongozi na nyumba za Serikali na tumeeleza malengo yake kazi iliyofanywa na iliyotengenezwa mwaka jana na utekelezaji na tumeomba kwa mwaka huu na kazi zinazotaka kufanywa, naomba afungue kurasa hizo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, maelezo yake yaliyokuwemo katika kitabu cha bajeti nimeyasikiliza, alipokuwa akiwasilisha bajeti juzi hapa nilimsikiliza kwa makini sana na ndio lililozaa suala langu hasa katika mchango wangu kwamba huu mradi umekuwa haumaliziki na tukasema na haya mafungu yako mengi, na ndio maana nikauliza kwamba kwa sababu ukitizama haya yaliyokuwa yametajwa hapa, kwa mfano *summary* yake yametajwa kwamba tunafanya ukarabati, kuanza ujenzi wa nyumba za walinzi, kujenga ukuta wa nyumba, hii ni matengenezo ambayo ungeweza vile vile kuacha fungu kwamba ni matengenezo makubwa katika yale mafungu ya *other charges*, ndio maana ikawa suala langu kwamba kule kuna fedha ambapo maelezo yake aliyotupa hayatofautiani sana na haya. na tatizo linakuja katika hoja yetu ni kwamba kwa sababu kule hakuwa *specific*, katupa maelezo ya jumla kwamba ni matengenezo ya nyumba, hizi zilizotajwa hapa katika miradi ya maendeleo pia zimetajwa kule, ndio maana nauliza kwamba vipi ingekuwa matengenezo madogo madogo ningelielewa kwa sababu ningejua kwamba haya kama ulivyosema matengenezo ya *pipes*, umeme lakini kuna matengenezo makubwa yana mafungu yake hatuyahoji na Mhe. Mwenyekiti, wewe ni shahidi kwamba yalikuwa yamenona, halafu na huku kwenye mradi wa maendeleo milioni mia sita. Sasa mimi nikasema kule matengenezo yepi na huku ni matengenezo yepi, anisadie.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimemuelewa vizuri Mhe. Jussa. Mhe. Jussa anataka ufafanuzi wa yale mafungu yaliyooneshwa katika hotuba na Mhe. Waziri, alieleza hapa kwamba kwa yale mafungu ya mwanzo yaliyogusa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi yalikusudiwa ni matengenezo ya majengo ya Ofisi ya Baraza la Mapinduzi na lile fungu jengine lilikuwa linahusu Ofisi ya Faragha, kwa maana ya Ikulu

pale Mnazo Mmoja sehemu ile ofisi. Lakini hili fungu ambalo Mhe. Jussa analohoji limeelezwa vizuri sana, inaeleza naomba kunukuu:-

"Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/14, mradi wa uimarishaji wa nyumba za viongozi na nyumba za viongozi na nyumba Serikali umetengewa milioni mia sita na umepanga kutekeleza kama hivyo ifuatavyo:

1. Kuanza ujenzi wa nyumba ya walinzi katika Ikulu ya Labon Dar es Salaam.
2. Kufanya ukarabati wa Ikulu Chake Chake
3. Kufanya matengenezo katika Ikulu ya Mnazi Mmoja kuweza kubadilisha madirisha ya zamani.
4. Kujenga ukuta wa nyumba zilizokuwa Posta katika Ikulu ya Migombani.
5. Kujenga ukuta wa kuzuia mmomonyoko wa nyumba katika Ikulu ya Mkoani
6. Kujenga ukuta Ikulu ndogo Mkokotoni na
7. Kuendeleza ujenzi wa nyumba za mapumziko ya Micheweni

Sasa hizi Mhe. Mwenyekiti, ndio tulizokusudia kama mradi milioni mia sita na zile nyengine zimewekwa kama *OC* kulipia Ofisi ya Baraza la Mapinduzi na zile za Faragha. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Jussa akaturuhusu tuendelee kwa sababu ufafanuzi wa milioni mia sita unajieleza vizuri katika ukurasa huu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naruhusu tuendelee kwa sababu moja kwamba baada ya kupitishwa na Kamati zetu, jukumu lake ni kwenda kusimamia na kwa sababu Kamati hii ina mwanamapinduzi kijana na mwenyekiti wake Mhe. Hamza Hassan Juma, lakini pia ina mwanapinduzi muasisi aliyeshiriki 1964 mstari wa mbele hasa kuingia katika boma Mhe. Saleh Nassor Juma naamini kwamba atasimamia vizuri fedha za walipa kodi. Ahsante sana.

Kifungu 0401	Idara ya Mipango,Sera na Utafiti	1,250,000,000/=
Jumla ya Fungu		**1,250,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 17 - JESHI LA KUJENGA UCHUMI

Kifungu 0201

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilipokuwa nachangia hotuba ya Mhe. Waziri, nilionesha wasi wasi wangu juu ya kuombwa tena kwa fedha hizi. Fedha hizi kama utakumbuka mwaka jana nilizizuia na nilizizuia kwa maelekezo ya kwamba wakafanye utafiti wawasilishe ripoti hapa tukubaliane Baraza likubali ama likatae ripoti yao, likikubali fedha zile zitatumika, likikataa fedha zile tutazuia. Lakini ninasikitika sana kwamba mpaka tumeingia kwenye bajeti nyengine hii ripoti ile haikuwasilisha, lakini leo Mhe. Waziri anaomba tuziidhinishe fedha nyengine hapa, wakati hili la mwanzo ambalo tulilizungumza halijamalizika. Hivyo nilikuwa naomba maelezo kwa nini mpaka leo ripoti ile hakuiwasilishwa kwenye Baraza na kama maelezo hayakunitosheleza Mhe. Mwenyekiti, tufupishe muda tusiwe na mlolongo mrefu, fedha hizi tuendelee kuzizuia mpaka tukapoipata ripoti hiyo itakapowasilishwa Barazani tena tutazingatia.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, anavyosema Mhe. Mtando ni kweli na mwaka jana fedha tulizuiliwa kwa wasi wasi wake kwamba labda hazitumiki ipasavyo, na Baraza likakubali hoja ikaagiza kwamba Wizara ya Fedha waunde Tume ya kulichunguza hili suala na Wizara ya Fedha imefanya kazi hiyo na ripoti ndio ile niliyompa Mhe. Mtando. Kwa hivyo ninataka kuhakikisha tu kazi ile iliyoagizwa imefanyika na hii ndio ripoti kamili na mapendekezo yake imetoa, baada ya kutoa mapendekezo yake tukaletewa sisi mapendekezo. Lakini sasa, bahati mbaya imechelewa kutoka mwezi April mwaka 2013 juzi tu hapa ndio imetolewa na tukaipata sisi na nafikiri wa kuwajibika kuileta hapa waliyotayarisha ripoti Wizara ya Fedha ndio waliofanya hii kazi na wakatoa ripoti. Sasa isingekuwa busara mimi mwenyewe mwenye kesi tena niwasilishe ripoti hii.

Sasa mimi nataka kusema Mhe. Mwenyekiti, kazi iliyoagizwa na iliyosababishwa fungu lizuiliwe imefanyika, uchunguzi umefanyika na mapendekezo yametoka na *summary* ya mapendekezo hayo nimeisoma hapa ndani ya ukumbi wako ambapo kwa kweli imeeleza kwa ufasaha kabisa matatizo yaliyopo na nini *findings* zake. Kwa hiyo mimi sioni sababu tena kuutia hasara mradi kama nilivyosema kwa kutokana na fedha mwaka jana nerika tani 18 zimeharibika kwa kukosa vipoza hewa. Sasa wenzetu Misri ilibidi wapewe fedha zao wamenunua gari na hizo harakati ndogo ndogo. Kwa hivyo nafikiri kidogo busara hapa lazima itumike, sio kwamba kuzuia tu aah! lazima busara itumike na mantiki yenyewe. Suala la msingi narudia tena

imefanyika. Sasa labda ingelikuwa Wizara ya Fedha wenyewe wapo tungesema kwa nini wamechelewa lakini nasema ripoti ndio hii na mapendekezo yametoka kazi imefanyika, ndio maana tukaona sisi tuombe tena mwaka huu ili tuweze kuendeleza mradi.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi napingana na maelezo ya Mhe. Waziri, kidogo maagizo ambayo yalitoka hapa Barazani hayakuiagiza Wizara ya Fedha, maana Wizara ya Fedha sio waliokuwa wanaomba fedha, aliyeagiza Wizara ya Fedha kwamba asiwape hizi fedha. Sasa wailete hapa Barazani ikubaliwe na nitakusomea *Hansard* Mhe. Mwenyekiti, ya mwaka jana maagizo ambayo yaliyotolewa na Mwenyekiti. Ninaomba ninukuu. Mwenyekiti, alizungumza alisema hivi:-

"Maamuzi tunayoyataka kupitisha hapa tutapitisha fedha hizi lakini fedha hii isitumike mpaka baada ya utafiti, baada ya utafiti huo na taarifa yake kuja hapa tukaipokea".
Mhe. Mwenyekiti, hayo ndiyo maelezo ya Mwenyekiti, sasa taarifa hapa haijaletwa wala hatujaipokea, kwa hivyo fedha hizi hatuwezi kuzitumia.

Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kuziidhinisha tena, tuwache kwanza walete ripoti ipokelewe Barazani, ndio maagizo ya Baraza. Hichi chombo Mhe. Mwenyekiti, kinaenda kwa mujibu wa kanuni na sheria, tuliagiza hivyo na tulikubaliana, wakafanya utafiti walete ripoti, tuipokee ama tuikatae ndio halafu fedha zile tuidhinishe. Mimi ninasema kwamba tusiende mbali sana tukubaliane tu na Mhe. Waziri kwamba basi hoja yangu iko pale pale tuendelee kuzizuia tena hizi, alete ripoti tukubaliane nayo tumruhusu ndio utaratibu. Kwa sababu haya tuliyanzungumza na hii ndio hoja na haya ni maamuzi ya Baraza kwamba wafanye moja, mbili, tatu hawajafanya. Sasa sijui wanachelea kitu gani, kama ripoti anayo, anayo yeye Mhe. Waziri hajaiwasilisha Barazani, alichotakiwa ailete na hapa ameagiza vizuri kabisa baada ya utafiti huo na taarifa yake kuja tukaipokea, ndio ndipo fedha zile zitolewe, sasa leo akirudi anaziomba tena hizi maana yake bado tuendelee kuzizuia.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Kwanza Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema kilichoombwa cha mwaka 2012/13, yeye anavyosema kwamba na mwaka huu tunaomba aah! ule ni mwaka jana na huu ni mwaka leo, *activities* tofauti zimewekwa hilo akumbuke, ni vitu viwili tofauti, *point* ya kwanza lakini *point* ya pili sasa itakuwaje mimi ndiye mwenye kesi nijihukumu mwenyewe, nafikiri hiki kitu kiko wazi kabisa, hii ripoti wamefanya Wizara ya Fedha na Uchumi, sasa nitafiti mwenyewe au nitafute matatizo mimi mwenye, mimi ndiye mwenye kesi, hebu Mhe. Mtando kidogo atumie *logic* atumie akili kidogo samahani

kusema neno hilo. Mhe. Mwenyekiti, mimi ndiye mwenye kesi sasa nitajitathmini mwenyewe, waliopewa kazi hii ni Wizara ya Fedha na hii ripoti tayari, sasa awahoji wao kwa nini hawakuileta hapa, sio mimi. Sasa mimi ananihukumu kwa kosa sio langu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake na pia nimshukuru Mhe. Mtando, anayoyasema Mhe. Mtando sahihi kabisa. Sasa kwa kuwa ripoti tayari ipo hapa Mhe. Mwenyekiti, na kwa kuwa sasa utaratibu uliobaki ni kuwasilishwa rasmi katika kikao hichi na kwa kuwa kikao hichi ndio chenye maamuzi ya matumzi ya fedha, kwa hivyo tumuombe Mheshimiwa akubali kuliidhinisha fungu hili lipitishwe, matumizi yaanze pale tu tutakapoiwasilisha rasmi ripoti hii ili utekelezaji uendelee. Maana tunamsikia Mhe. Waziri hapa akieleza namna ya athari zinavyojitokeza kwa sababu ya kutokuwa na fedha na sisi ni Wawakilishi wa wananchi ambao kwa kiasi kikubwa cha Wazanzibari wanategemea kilimo, maana kama alivyosema athari zilizotokea katika mbegu na mambo mengine na kwa sababu kilimo hichi ni cha mboga mboga inatoa sura na taswira nzuri kwa ajili ya kuendeleza kilimo nchini na zaidi ya asilimia 70 ya Wazanzibari wanategemea kilimo, nilikuwa namuomba Mhe. Mtando atukubalie na atusamehe kwa kutokuwasilisha ripoti hii kwa wakati lakini ninamuhakikishia kesho ripoti hii itawasilishwa rasmi na Serikali ili tumpe nafasi Mhe. Waziri, aendelee kufanya kazi zake.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kusema hayo na Mhe. Mtando atuhurumie tuendelee na shughuli yetu hii.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, nimeyasikia maelezo ya Mnadhimu wa Serikali pale nilikuwa nataka na mimi kidogo nieleze mawili matatu.

Kwanza nimtake Mhe. Waziri kwanza aliombe radhi hili Baraza kwa kutokutimiza ile ahadi ambayo aliiahidi katika Baraza hili. Hichi ni chombo kitukufu sana tena cha wananchi unapotoa ahadi lazima uitimize. Kwa hivyo Waziri hakuwa ametimiza ahadi ya kuleta hapa, hivyo kama leo anatuambia kwamba wako tayari sasa kuileta ile ripoti basi kwanza angalau angetuomba radhi chombo hichi, pili ningeomba Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mnadhimu pale wa Serikali kwamba tuziidhinishe hizi fedha, tuzizuie matumizi yake, iletwe ripoti tuijadili hapa ama tuikubali ama tuikatae, tukikubali basi fedha hizi zianze kutumika, tukiikataa fedha hizi hazitatumika, maana yake itakuwa hatujaridhika na matumizi ya fedha hizi kutokana na ripoti ambayo iliyowasilishwa. Tukikubaliana hayo Mhe. Mwenyekiti, mimi sina tatizo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba radhi kwa Mhe. Mtando kwa kuchelewesharipoti hii na akubali kwamba ripoti hii itawasilishwa rasmi kesho na namuomba Mhe. Mtando, akubaliane nasi kwamba mara itakapowasilishwa ripoti hii basi aruhusu matumizi haya yaendelee.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilikuwa nataka nimsahihishe kidogo Mnadhimu pale pale, asiniombe radhi mimi aliombe radhi Baraza, Baraza ndio lililokosewa sio mimi, mimi sina tatizo, mimi nimekuja hapa kwa niaba ya wananchi na hili ni Baraza, kwa hivyo kama anaomba radhi aliombe radhi Baraza kwa niaba ya Serikali kwamba amekosea.

Mhe. Mwenyekiti: Likishaombwa radhi Baraza tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Makamu wa Pili wa Rais: Naomba radhi Baraza zima.

Kifungu 0201	Utawala wa Unguja	250,000,000/=
Jumla ya fungu		**250,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 18 CHUO CHA MAFUNZO

Kifungu 0201	Idara ya Vyuo vya Mafunzo	300,000,000/=
Jumla ya Fungu		**300,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 34 KIKOSI CHA VALANTIA

Kifungu 0201	Utawala Unguja	70,000,000/=
Jumla Fungu		**70,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko, naomba sasa kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masomo: Mhe. Naibu, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji waliokubali bajeti ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka 2013/14 wanyanyue mikono, waliokataa, waliokubali wameshinda.

Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa kazi kubwa tuliyoifanya tangu asubuhi hadi sasa hivi saa 4.40 usiku. Kwa hivyo nawashukuru sana kwa mashirikiano na nashukuru kwa kuipitisha bajeti ya Waziri wetu aweze kufanya kazi tuliyomkabidhi. Baada ya maelezo hayo naakhirisha Baraza letu hadi kesho siku ya Jumanne tarehe 2/7/2013 saa tatu za asubuhi.

(Saa 4.30 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 02/07/2013 Saa 3.00 Asubuhi)